# USAWIRI WA MWANAMKE KATIKA NDOA: MIFANO KUTOKA *UTENDI WA MWANAKUPONA*, *UTENDI WA AYUBU* NA MATINI TEULE ZA KIDINI

**NA**

**ANGELA SAWE**

**Tasnifu hii Imewasilishwa ili Kutimiza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamifu katika Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika**

**Chuo Kikuu Cha Moi**

**Oktoba, 2018**

# IKIRARI

Hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote ili kutimiza mahitaji ya shahada yoyote. Hairuhusiwi kuitolesha au kuichapisha bila ruhusa ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret.

**Mzamifu**

................................................... Tarehe.............................

**SAWE ANGELA**
SASS/D.PHIL/KIS/06/13

**Wasimamizi**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa ridhaa yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Moi.

................................................... Tarehe.............................

**DKT. SAMUEL M. OBUCHI**
Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika
Chuo Kikuu cha Moi
Eldoret

................................................... Tarehe.............................

**DKT. VIFU S. MAKOTI**
Idara ya Isimu na Lugha
Chuo Kikuu cha Machakos
Machakos

# TABARUKU

Kazi hii naitabarukia wanangu Lemuel na Leticia kwa uvumilivu wao katika umri wao mdogo niliposhinda usiku wote nikiandika tasnifu hii. Ninawatakia mema maishani, Mungu mwenye rehema awamiminie baraka zisizokuwa na mipaka.

*Na ladhati sharibina*
*Utunyweshe Subhana*
*Ni haqi taha amina*
*Utunyweshe kwa umoya*
(UWA, ubeti 400)

## SHUKRANI

Shukrani zangu za moyo zimwendee Mungu Muumba wa vyote, aliyeniongoza katika kazi hii. Mwenyezi Mungu alinipa uwezo na njia ya kusoma hadi kufikia kiwango hiki cha shahada ya uzamifu.

Naam, ni dhahiri shahiri kuwa kukamilika kwa tasnifu hii kumewahusisha waja wengi mno. Ni muhali kuwataja wote. Hata hivyo, nitakuwa mkavu wa fadhila endapo sitawataja wafuatao: Dkt. Vifu Makoti na Dkt. Samuel M. Obuchi, kwa usaidizi, uongozi, mlahaka na uelekezi katika mchakato mzima wa kuandika tasnifu hii. Waama, wamekuwa mithili ya mboni ya jicho langu. Maulana awajalie maisha marefu yaliyojaa siha njema. Pia, namshukuru Prof. N. Ogechi kwa kuwa kielelezo kwangu tangu mwaka wa kwanza kutafuta shahada ya kwanza chuoni leo.

Aidha, namshukuru mkuu wa idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Dkt. Mosol Kandagor kwa kuwa zaidi ya kiongozi. Mbali na kunishauri katika maandalizi ya tasnifu hii, alinifunza mengi maishani hasa kumtegemea Mwenyezi Mungu. Mawaidha yake na uelekezi wake ulinifungua macho zaidi katika safari ya kiakademia. Vile vile, nawashukuru walimu wengine katika Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi. Namshukuru Prof. Iribe Mwangi (Chuo Kikuu cha Nairobi), kwa kuniazima vitabu na makala nilizozihitaji katika uandishi wa tasnifu hii. Aidha, nawashukuru wazazi wangu Bw na Bi Sawe kwa kunizaa, kunilea na kunionyesha njia mwafaka ya kufuata maishani. Pia, namshukuru mume wangu Bw. Kemboy kwa kuwa rafiki wa dhati, mume aliyewajibika na kunipa nafasi yangu kama mke kudhihirisha hulka za mwanamke, ninakuheshimu. Ahsante wanangu Lemuel na Leticia kwa kuyashika mashauri yangu alivyoyashika bintiye Mwanakupona. Nawashukuru wote hata wale nisiowataja walionisaidia kwa kazi hii, Mungu awajalie mema siku zote.

# KIFUPISHO CHA MANENO

Khj - kama hapo juu

Mha .- mhariri

Uk - ukurasa

Waha .- wahariri

EAEP - East African Educational Publishers

KCM - Kitabu cha Methali

TUKI - Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

UWA - Utendi wa Ayubu

UWM - Utendi wa Mwanakupona

WUB - Wimbo Ulio Bora

## IKISIRI

Utafiti huu unahusu usawiri wa mwanamke katika kazi teule za fasihi na jinsi maandiko ya kidini yanavyomwangalia mwanamke katika jamii. Kazi hizi teule za fasihi ni *Utendi wa Mwanakupona* (1858), *Utendi wa Ayubu* (1723) na maandiko ya kidini ya 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora' katika *Biblia Takatifu, Agano la kale* (1921). Katika utafiti huu, tumelinganisha mwanamke anavyosawiriwa katika kazi hizi mbili za fasihi na maandiko matakatifu yanavyotarajia tabia na uhusiano wa mwanamke na mwanamume katika ndoa. Waandishi wengi kwa kuathiriwa na Ufeministi na usawa wa kijinsia, wamemsawiri mwanamke aliyedhalilishwa na kunyanyaswa katika ndoa. Katika utafiti wetu, tumechunguza miongozo inayotolewa katika tendi hizi na kulinganisha na mwongozo wa kidini unaotolewa kupitia 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora'. Mwanamke anaposimamia nafasi yake katika ndoa sio ukandamizaji bali utekelezaji wa majukumu yake katika ndoa. Kwa hivyo, tumechunguza iwapo yapo manufaa katika *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu,* ''Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora'' katika kukuza na kuujenga uhusiano madhubuti katika ndoa. Ili kuendeleza utafiti huu, tuliteua sampuli ya kimakusudi iliyoafikiana na malengo yaliyoongoza utafiti huu. Malengo kwenye tasnifu hii ni kuchanganua taswira ya mwanamke kutoka kazi hizi teule za fasihi na matini za dini, kutathmini uhusiano wa mwanamke na mwanamume katika *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu,* ''Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora'', na kubainisha dini kama kigezo muhimu katika uthabiti wa ndoa. Maktabani, utafiti huu ulipata data katika kazi teule za *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu,* 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora'. Data hii ilichanganuliwa kwa kutumia takwimu fafanuzi. Fasiri na mitazamo mbalimbali imetolewa na waandishi wengi kuhusiana na kazi zetu tulizozichagua na kuhitimisha kuwa mwanamke amekandamizwa na kudhalilishwa. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Ufeministi na nadharia ya Udenguzi. Nadharia ya Ufeministi huangazia jinsi mwanamke amenyanyaswa katika jamii na mbinu zinazoweza kumkomboa. Nadharia ya Udenguzi inadai kuwa kila tamko lina sura mbili, sura iliyopo na sura ya kupangua wakati ule ule mmoja. Mahitimisho ya utafiti huu ni kuwa mwanamke ana nafasi yake maalum katika jamii kama mpenda amani, kielelezo bora kwa watoto na familia kwa jumla. Utafiti huu vile vile ulibainisha mihimili muhimu inayojenga familia kama vile kusameheana, kufurahishana n.k na kwamba mwanamke na mwanamume wanastahili kuishi pamoja licha ya changamoto na matatizo ya maisha. Ilibainika wazi kuwa Mungu ndiye mwanzilishi wa familia na angependa waliooana waishi kwa amani, na kwa hivyo dini ni kigezo muhimu katika ndoa. Kwa jumla, utafiti huu una mchango mkubwa katika taaluma ya Kiswahili na jamii. Katika utafiti huu tumeonyesha kwamba wosia katika *Utendi wa Mwanakupona*, taswira ya mwanamke katika *Utendi wa Ayubu* na matini ya kidini si ukandamizaji wa mwanamke bali ni njia ya kuujenga uhusiano mwema katika ndoa. Wafuasi wa dini hizi mbili wakiyazingatia maelekezo kutoka kwa kazi hizi, basi itakuwa ni mchango mkubwa katika kuimarisha ndoa. Aidha, umechangia katika fasihi ya Kiswahili, Waswahili kama jamii na jamii nyingine duniani, wasomaji na wahakiki wa fasihi ya karne hii, kuziangalia kazi hizi upya, na kwamba zina wosia bora zikijikita katika misingi ya kidini katika ndoa za leo.

## ABSTRACT

This study examines the depiction of women characters in selected epic works as well as religious texts. The study explicates the epics of *Mwanakupona* (1858), *Ayubu* (1723) and the religious texts, i.e. 'Proverbs and Songs of Songs' (Old Testament Bible, 1921). This research is comparative in nature with regards to the place of women in the family setting. The reseacher, through reading different works realized that the position of a woman in the society has been shown though many writers have been infuenced by feminism and gender equality. When a woman stands on her position to accomplish her roles, is not a sign of oppression or sufferings but a dedication towards her roles as a woman in the society.The need for this study based on the literary works of *Mwanakupona*, *Ayubu* and Biblical works of Solomon; 'Proverbs and Songs of Songs'. The data for this study was purposively selected from the specified texts as was found relevant to the fundamental objectives which guided this study. The main objectives of the study is to analyze in depth the real picture of a woman in relation to *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu* and biblical works of 'Proverbs and Songs of Songs', to evaluate the relationship between a husband and a wife and to find out if religion can be a rock of ensuring marriage abides by the divinely principles keeping its flame of togetherness. Descriptive analysis was employed to analyse the collected data. Various approaches and interpretations have been rendered on the selected texts to the extent that many writers have concluded from the texts that women have been depicted as the weaker sex whose place is in the kitchen. The study was underpinned by feminism theory and deconstruction theory. Feminism theory is all about a woman, showing how she has suffered in the hands of men and how she needs to fight for her redemption. Deconstruction theory posits an undecidability of meaning for all texts, and the critic doesn't undermine the text but the text itself dismantles bringing a different perspective all together. A major finding of this study is that a woman has a role to play as a peacemaker, a role model other than playing a major role in promoting the welfare of the family unit as well as the marriage institution. The study also found out that some of the fundamental ingredients that cement a marriage institution include forgiveness, appeasing each other among others. Further, a couple should always stick together even in the midst of extreme challenges. Another major finding of this study is that God is the author and promoter of the marriage unit. The text in reference are replete with textual material that clearly indicate that the marriage institution is largely dependent on the religious teachings. The outcome of the research has shown the tenets found in the *epic of Mwanakupona*, *epic of Ayubu* and the writings of king Solomon are not meant to make a woman a lesser human being but its a way of strengthening her marital relationship. As followers of the two religions, this outcome will help to establish marriages. It will also be put into writing thereby becoming a great treasure to the literature of Kiswahili, critics of literature in the 21st century and the scholars in general to look into these texts in a different way that it carries paramount principles basing on the religions for the stability of today's marriages.

# YALIYOMO

IKIRARI ..................................................................................................ii
TABARUKU...............................................................................................iii
IKISIRI ....................................................................................................vi
ABSTRACT...............................................................................................vii
YALIYOMO ..............................................................................................viii
**SURA YA KWANZA.....................................................................................1**
**MISINGI YA UTAFITI ..................................................................................1**
1.0 Utangulizi .............................................................................................. 1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti ........................................................................... 1
1.2 Suala la Utafiti ........................................................................................ 5
1.3 Malengo ya Utafiti .................................................................................... 7
1.4 Nadharia Tete........................................................................................... 7
1.5 Sababu za Kuchagua Mada ........................................................................ 8
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti .......................................................................... 8
1.7 Umuhimu wa Utafiti .................................................................................. 9
1.8 Hitimisho................................................................................................. 10
**SURA YA PILI.............................................................................................11**
**MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA.............................11**
2.0 Utangulizi ............................................................................................... 11
2.1 Mapitio ya Maandishi ................................................................................ 11
2.1.1 Mapitio Kuhusu Dhana ya Taswira..............................................................11
2.1.2 Maandishi kuhusu Taswira ya Mwanamke katika Ndoa ...............................12
2.1.3 Uhusiano kati ya Mwanamke na Mwanamume ...........................................18
2.1.4 Dini kama kigezo muhimu katika Uthabiti wa Ndoa.....................................24
2.2 Msingi wa Kinadharia................................................................................ 25
2.2.1 Nadharia ya Ufeministi ..............................................................................26
2.2.2 Chimbuko la Nadharia ya Ufeministi............................................................27
2.2.3 Tapo la Ufeministi Huru .............................................................................32
2.2.4 Mihimili ya Nadharia ya Ufeministi Huru .....................................................33
2.2.5 Nadharia ya Udenguzi.................................................................................38
2.2.6 Mihimili ya Nadharia ya Udenguzi ..............................................................40
2.3 Hitimisho.................................................................................................. 45

**SURA YA TATU** ........................................................................................ **47**
**MBINU ZA UTAFITI** ................................................................................ **47**
3.0 Utangulizi ........................................................................................ 47
3.1 Eneo la Utafiti ........................................................................................ 47
3.2 Ukusanyaji wa Data ........................................................................................ 47
3.3 Usampulishaji ........................................................................................ 48
3.3.1 Kuchanganua Taswira ya Mwanamke katika *UWM, UWA, KCM* na *WUB* ... 48
3.3.2 Kutathmini Uhusiano wa Mwanamke na Mwanamume kama unavyojitokeza katika *UWM, UWA, KCM* na *WUB* ................................................ 49
3.3.3 Kubainisha Wosia kutoka Dini kama kigezo muhimu katika Uthabiti wa Ndoa ........................................................................................ 50
3.4 Vifaa vya Utafiti ........................................................................................ 51
3.5 Uchanganuzi wa Data ........................................................................................ 51
3.6 Hitimisho ........................................................................................ 53
**SURA YA NNE** ........................................................................................ **54**
**TASWIRA YA MWANAMKE KATIKA NDOA** .............................................. **54**
4.0 Utangulizi ........................................................................................ 54
*4.1 Historia fupi kuhusu* Utendi wa Mwanakupona *(UWM),* Utendi wa Ayubu *(UWA), Kitabu cha Methali (KCM) na Wimbo Ulio Bora (WUB)* .................................... 54
4.1.1 Historia Fupi ya *Utendi wa Mwanakupona* .................................................... 54
4.1.2 Historia Fupi ya *Utendi wa Ayubu* ................................................................ 55
4.1.3 Maelezo Mafupi Kuhusu Methali na Wimbo Ulio Bora ................................ 56
4.2 Taswira ya urembo wa Mwanamke katika Ndoa ................................................ 57
4.2.1 Taswira ya urembo wa Mwanamke katika UWM ........................................ 58
4.2.2 Taswira ya urembo wa mwanamke katika UWA ........................................ 60
4.2.3 Taswira ya urembo wa mwanamke katika WUB ........................................ 63
4.2.4 Taswira ya urembo wa mwanamke katika KCM ........................................ 65
4.3 Taswira ya Mwanamke Mpenda Amani ........................................................ 66
4.3.1 Taswira ya Mwanamke Mpenda Amani katika UWM .................................. 67
4.3.2 Taswira ya mwanamke Mpenda Amani katika UWA .................................. 72
4.3.3 Taswira ya mwanamke Mpenda Amani katika WUB .................................. 73
4.3.4 Taswira ya Mwanamke Mpenda Amani katika KCM .................................. 74
4.4 Taswira ya Heshima ........................................................................................ 77

4.4.1 Taswira ya Heshima katika UWM .......... 78
4.4.1.1 Mwanamke kutobishana na Mume wake .......... 80
4.4.1.2 Mwanamke kuomba Ruhusa ya kutoka Nje .......... 82
4.4.2 Suala la Mwanamke Kumheshimu Mume katika UWA .......... 83
4.4.3 Suala la Mwanamke Kumheshimu Mume katika WUB .......... 84
4.4.4 Suala la Mwanamke Kumheshimu Mume katika KCM .......... 85
4.5 Mwanamke kama Mtunzaji wa Mume .......... 86
4.5.1 Mwanamke kama Mtunzaji wa Mume katika UWM .......... 87
4.5.2 Mwanamke kama Mtunzaji wa Mume katika UWA .......... 90
4.5.3 Mwanamke kama Mtunzaji Wa Mume Katika WUB .......... 94
4.5.4 Mwanamke kama Mtunzaji Wa Mume Katika KCM .......... 95
4.6 Mwanamke kama Mfanyikazi katika Ndoa .......... 97
4.6.1 Mwanamke kama Mfanyikazi katika UWM .......... 98
4.6.2 Mwanamke kama Mfanyikazi katika UWA .......... 99
4.6.3 Mwanamke kama Mfanyikazi katika WUB .......... 102
4.6.4 Mwanamke kama Mfanyikazi katika KCM .......... 103
4.7 Mwanamke kama mtekelezaji wajibu katika Ndoa .......... 107
4.7.1 Uwajibika wa Mwanamke katika UWM .......... 108
4.7.2 Uwajibikaji wa mwanamke katika UWA .......... 108
4.7.3 Uwajibikaji wa Mwanamke katika WUB .......... 109
4.7.4 Uwajibika wa Mwanamke katika KCM .......... 110
4.8 Taswira ya Mwanamke Asiyenung’unika, Mvumilivu na Mpole Katika Ndoa .......... 111
4.8.1 Taswira ya Mwanamke asiyenung’unika katika Ndoa .......... 111
4.8.1.1 Taswira ya Mwanamke asiyenung’unika katika UWM .......... 111
4.8.1.2 Taswira ya Mwanamke asiyenung’unika katika UWA .......... 113
4.8.1.3 Taswira ya Mwanamke asiyenung’unika katika KCM .......... 115
4.8.2 Taswira ya Mwanamke Mvumilivu katika Ndoa .......... 115
4.8.2.1 Taswira ya Mwanamke mvumilivu katika UWM .......... 115
4.8.2.2 Taswira ya Mwanamke mvumilivu katika UWA .......... 116
4.8.2.3 Taswira ya Mwanamke Mvumilivu Katika KCM .......... 117
4.8.3 Taswira ya Mwanamke Mpole katika Ndoa .......... 118
4.8.3.1 Taswira ya Mwanamke mpole katika UWM .......... 118
4.8.3.2 Taswira ya Mwanamke mpole katika UWA .......... 119

4.8.3.3 Taswira ya Mwanamke mpole katika KCM ........................................ 120
4.9 Hitimisho ........................................................................................ 122
**SURA YA TANO ........................................................................................ 124**
**UHUSIANO WA MKE NA MUME KATIKA NDOA ........................................ 124**
5.0 Utangulizi ........................................................................................ 124
5.1 Mwanamume na Mwanamke Kuheshimiana katika Ndoa ................................ 125
5.1.1 Mwanamume na Mwanamke Kuheshimiana katika UWM .......................... 125
5.1.2 Mwanamume na Mwanamke Kuheshimiana katika UWA .......................... 126
5.1.3 Mwanamume na Mwanamke Kuheshimiana katika WUB .......................... 129
5.1.4 Mwanamume na Mwanamke Kuheshimiana katika KCM .......................... 130
5.2 Mwanamume na Mwanamke Kufurahiana na kutumia Lugha nzuri katika Ndoa ........................................................................................ 131
5.2.1 Mwanamke na Mwanamume Kufurahiana na Matumizi ya Lugha nzuri katika UWM ........................................................................................ 132
5.2.2 Mwanamke na Mwanamume Kufurahiana na Matumizi ya Lugha nzuri katika UWA ........................................................................................ 133
5.2.3 Mwanamke na Mwanamume Kufurahiana na Matumizi ya Lugha nzuri katika WUB ........................................................................................ 135
5.2.4 Mwanamke na Mwanamume Kufurahiana na Matumizi ya Lugha nzuri katika KCM ........................................................................................ 137
5.3 Mahaba katika uhusiano wa Mke na Mume ................................................ 139
5.3.1 Mahaba kati ya Mume na Mke katika UWM ............................................ 140
5.3.2 Mahaba kati ya Mume na Mke katika UWA ............................................ 142
5.3.3 Mahaba kati ya Mume na Mke katika WUB ............................................ 143
5.4 Kuthaminiana katika Ndoa kati ya Mke na Mume ........................................ 144
5.4.1 Kuthaminiana katika UWM kati ya Mke na Mume .................................... 145
5.4.2 Kuthaminiana katika UWA kati ya Mke na Mume .................................... 147
5.4.3 Kuthaminiana katika WUB kati ya Mke na Mume .................................... 150
5.4.4 Kuthaminiana katika KCM kati ya Mke na Mume .................................... 151
5.5 Mwanamke kuwa Nadhifu ili kudumisha Mapenzi katika Ndoa ...................... 153
5.5.1 Unadhifu wa Mwanamke katika UWM .................................................... 153
5.5.2 Unadhifu wa Mwanamke katika WUB ..................................................... 156
5.5.3 Unadhifu wa Mwanamke katika KCM ..................................................... 157

5.6 Mwanamume na Mwanamke Kuvumiliana katika Ndoa ..... 159
5.6.1 Mwanamume na Mwanamke Kuvumiliana katika UWM ..... 159
5.6.2 Mwanamume na Mwanamke Kuvumiliana katika UWA ..... 160
5.7 Dini kama Nyenzo muhimu katika Ndoa ..... 163
5.7.1 Suala la Dini linavojidhihirisha Katika UWM ..... 164
5.7.1.1 Sheria za Ndoa katika UWM ..... 165
5.7.1.2 Suala la Sala katika UWM ..... 166
5.7.1.3 Suala la kupendana katika UWM ..... 167
5.7.1.4 Suala la Faida za dini katika UMW ..... 168
5.7.1.5 Suala la Unyenyekevu katika UWM ..... 169
5.7.2 Suala la Dini Katika UWA ..... 170
5.7.2.1 Kigezo cha Sala katika UWA ..... 170
5.7.2.2 Suala la kupendana katika UWA ..... 172
5.7.2.3 Suala la Kunyenyekea kama agizo la Kidini katika UWA ..... 173
5.7.3 Mafundisho ya Ndoa katika WUB ..... 173
5.7.3.1 Suala la kupendana katika WUB ..... 173
5.7.4 Mafundisho ya Ndoa katika KCM ..... 174
5.7.4.1 Kanuni za dini katika KCM ..... 175
5.7.4.2 Suala la Kusali Pamoja katika KCM kama Agizo la Kidini ..... 175
5.7.4.3 Wosia faafu wa Ndoa katika KCM kama Agizo la Kidini ..... 176
5.7.4.4 Suala la kupendana katika KCM kama Agizo la Kidini ..... 178
5.7.4.5 Kunyenyekeana katika KCM kama Agizo la Kidini ..... 179
5.7.4.6 Suala la Kuheshimiana katika KCM kama Agizo la Kidini ..... 180
5.8 Hitimisho ..... 181
**SURA YA SITA ..... 183**
**MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..... 183**
6.0 Utangulizi ..... 183
6.1 Muhtasari wa Tasnifu ..... 183
6.2 Matokeo ya Utafiti ..... 184
6.2.1 Taswira ya Mwanamke katika Ndoa ..... 187
6.2.2 Uhusiano wa Mwanamke na Mwanamume katika Ndoa ..... 187
6.2.3 Dini kama Kigezo muhimu katika Ndoa ..... 188
6.3 Mahitimisho ..... 188

6.4 Mapendekezo ya Utafiti ........ 190
6.5 Mchango wa Utafiti ........ 192
MAREJELEO ........ 193
**VIAMBATISHO ........ 198**
**TASWIRA YA MWANAMKE KATIKA NDOA ........ 198**
*Kiambatisho 1: Utendi wa Mwanakupona (UWM)* ........ 198
*Kiambatisho 2: Wimbo Ulio Bora (W U B)* ........ 199
*Kiambatisho 3: Kitabu cha Methali (KCM)* ........ 199
*Kiambatisho 4: Utendi wa Ayubu (U W A)* ........ 201
**UHUSIANO WA MWANAMKE NA MWANAMUME KATIKA NDOA ........ 202**
*Kiambatisho 5: Uhusiano wa Mwanamke na Mwanamume (UWM)* ........ 202
*Kiambatisho 6: Uhusiano wa Mwanamke na Mwanamume (WUB)* ........ 203
*Kiambatisho 7: Uhusiano wa Mwanamke na Mwanamume (KCM)* ........ 205
*Kiambatisho 8: Uhusiano wa Mwanamke na Mwanamume (UWA)* ........ 207
*Kiambatisho 9: Dini Kama Kigezo Muhimu katika Ndoa (U W M)* ........ 209
*Kiambatisho 10: Dini Kama Kigezo Muhimu katika Ndoa (KCM)* ........ 210
*Kiambatisho 11: Dini Kama Kigezo Muhimu katika Ndoa (U W A)* ........ 211

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii inahusu masuala ya kimsingi katika utafiti huu. Hivyo basi nimeelezea vipengele vifuatavyo: Usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia-tete za utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka na umuhimu wa utafiti. Kila kipengele kilijadiliwa kwa kuzingatia mada yetu ya utafiti, *Usawiri wa mwanamke katika Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu* na matini za kidini ambazo ni Methali na Wimbo Ulio Bora katika *Biblia, Agano la Kale.*

## 1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Katika miaka ya hivi karibuni, msisitizo mkubwa kwa wanataaluma wengi, hasa wanaharakati wanaopigania haki na usawa wa wanawake dhidi ya ukandamizaji unaodhaniwa kufanywa na wanaume, umekuwa ukidadisi mgao wa majukumu kati ya wanawake na wanaume. Kutokana na uchunguzi unaofanywa mara kwa mara na wataalamu wa masuala ya ndoa kwa mfano, Katola (2006), Maingi (2005) na Biersteker (1991), ilivyodhihirika katika mapitio ya maandishi, imebainika kwamba taasisi ya ndoa huwa na changamoto hasa katika karne ya 21. Masuala yanayowahusu wanawake yamezua mjadala mkubwa miongoni mwa wanajamii na hata kufikia kiwango ambacho wanawake wameanza kupigania usawa wa kijinsia.

Ulinganisho wa mwanamke wa kisasa na wa kijadi unadhihirisha mabadiliko mengi. Mabadiliko haya yamekuwa makubwa hadi kugusa asasi ya ndoa na nafasi ya mwanamke kwa jumla. Katika tamaduni na desturi za Kiafrika, mwanamume alitarajiwa kutimiza wajibu wake kama mume katika ndoa lakini mwanamke alikuwa na nafasi kubwa ya kuhakikisha kuwa ndoa na familia yake imejengwa katika misingi

thabiti na ya kudumu. Katika utamaduni wa aina hii, wasichana walifunzwa nyakati za unyago. Mafunzo haya yaliendelea kutoka kwa mama, nyanya na hata shangazi. Katika karne ya kumi na tisa, mafunzo haya yalihifadhiwa katika maandishi kwa mfano kwenye *Utendi wa Mwanakupona* (UWM).

Kutokana na kazi za kifasihi tulizozichagua na matini za kidini, mwanamke amepewa jukumu muhimu la kukuza ndoa. Jambo hili halina maana kuwa mwanamume hahusiki, bali mwanamke ana jukumu kubwa kuhakikisha kuwa ndoa yake imesimama na kunawiri licha ya changamoto zilizopo. Katika hali ya kawaida, kujenga ni kuimarisha au kuweka mazingira bora juu ya kile unachokithamini ili kuzuia madhara yanayoweza kutokea. Naam, nafasi hii inalenga kumsaidia mwanamke awe makini sana na kila kinachoweza kubomoa ndoa yake.

Miongoni mwa matini za kifasihi zilizoteuliwa kwa ajili ya utafiti huu ni, *Utendi wa Mwanakupona* (UWM) na *Utendi wa Ayubu* (UWA) ambazo zimebainisha malengo matatu tuliyotarajia kuyafikia katika utafiti huu. Vile vile tumefanya utafiti kutoka kwa matini za kidini ambazo ni, 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora' kutoka kwa *Biblia*. Solomoni ambaye ni mwandishi wa matini hizi anabainisha taswira ya mwanamke katika ndoa, uhusiano wa mke na mume katika ndoa na kudhihirisha dini kama kigezo muhimu katika uthabiti wa ndoa.

Katika *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu,* 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora' mwanamke amesawiriwa kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, katika *Utendi wa Mwanakupona*, Mwanakupona anamshauri bintiye awe mnyenyekevu na mtiifu kwa mumewe. *Utendi wa Mwanakupona* waonekana kudhihirisha uhusiano wa mke na mume katika ndoa. Utendi huu hufunza kuhusu masuala ya ndoa jinsi mwanamke anavyoweza kuishi na mume na maisha ya jamii kwa jumla. Mwanakupona

anamwonya binti yake, juu ya mambo kadhaa ya kiutamaduni kama vile; adabu na heshima kwa mume wake, kuepuka umbeya, kuepuka fitina, kuepuka uchoyo miongoni mwa masuala mengine. Mafunzo haya yako katika mila na desturi za ndoa kwa jamii nyingi nchini Kenya, kwa mfano katika jamii ya Wanandi miongoni mwa Wakalenjin ambapo mwanamke anatarajiwa kumheshimu mume wake na kumtii kila mara.

Mwanamke anajitokeza kama msaidizi wa mumewe katika *Utendi wa Ayubu* na anayekubali kupoteza kila kitu chake cha thamani, kwa ajili ya mumewe. Wosia huu katika fasihi ulikuwa na maana kwa kuwa wanajamii walifahamu changamoto ambazo zinaweza kutokea katika jamii husika. Kwa hivyo, kwa kusoma maadili na mafunzo haya katika *Utendi wa Ayubu*, wanajamii waliweza kupata uponyaji katika masuala ya jamii, hasa changamoto kama za magonjwa na uhusiano kati ya mume na mke.

Dini ni kigezo muhimu katika uthabiti wa ndoa yoyote na wanandoa wanastahili kulifahamu jambo hili kwa kurejelea yaliyoagizwa na Mwenyezi Mungu katika *Biblia*. 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora' zimebainisha umuhimu wa imani kwa Mungu kama nguzo muhimu katika ndoa. Aghalabu, jamii nyingi huamini kuwa Mungu ndiye huwaelekeza maishani. Kutokana na maandishi haya ya 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora', Mungu ametoa maelekezo kupitia maandishi ya Mfalme Solomoni kuhusu jinsi mwanamke anaweza kuishi na mumewe kwa njia ya kuelewana na kuwa na uthabiti wa ndoa kati yao. Kwa mfano, wakristo wanapoozwa kanisani huambiwa watamke, 'hadi kifo kitutenganishe', 'kuishi kwa amani wakati wa shida na wakati wa furaha' n.k. Vile vile waandishi wa *Utendi wa Mwanakupona* na *Utendi wa Ayubu* ambao ni wa dini ya Kiislamu, wamedhihirisha umuhimu wa dini

katika ndoa. Katika Uislamu, tunaelezwa katika hadithi moja kwamba ‘watu wanapotalakiana, malaika wote mbinguni huwa na huzuni’, ‘kama kuna kitu anachochukia zaidi Mwenyezi Mungu kati ya mke na mume ni talaka’ n.k

Kwa hivyo, fasihi na dini imebainisha uhusiano wa mwanamke na mwanamume katika ndoa kwamba mke anapaswa kumtii mumewe na kunyenyekea iwapo angependa kufurahia ndoa na uhusiano wake na mumewe.

Vile vile, mwanamke anahitaji kuheshimika kutokana na majukumu yake katika jamii. Majukumu haya yanadhihirisha sifa zake za kuwa mwanamke bali si ukandamizaji. Baadhi ya waandishi na wanawake wa kisasa wameyachukulia majukumu na nafasi ya mwanamke katika jamii kuwa ni hali ya kunyanyaswa.

Ndoa katika jamii ya Kiafrika imebadilika kwa kiasi kikubwa. Ili ndoa ifanikiwe, isimame, iweze kuimarika na kudumu, jitihada ya mume na mke lazima iwepo. Mwanamke anatarajiwa kutekeleza majukumu yake kama mke na mwanamume vivyo hivyo anatarajiwa kuyafikia malengo ya mume. Kutokana na majukumu haya, wanawake wengi wa sasa wanadai kukandamizwa, kunyanyaswa, kuonewa na kudhalilishwa.

Wanawake wengi wamepigania usawa katika jamii na kudai kuwa wamenyimwa haki zao na jamii kwa jumla. Kwa kufanya hivi, mwanamke amebaki akilalamika ilhali ni majukumu yake ambayo kamwe hatakikani kulalamika kwa kuwa ni mojawapo ya hulka zinazomfanya kuitwa ‘mwanamke’ maadamu si mwanamume. Vile vile katika dini limeshadidiwa suala hili la unyenyekevu na utiifu wa mwanamke, kwa mfano ‘Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora’ katika *Biblia.*

Aidha, suala hili la uhusiano kati ya mke na mume katika ndoa limezungumziwa katika fasihi, kwa mfano katika *Utendi wa Mwanakupona* na *Utendi wa Ayubu*. Ingawaje huu ni ubunifu wa kifasihi, umeakisi utamaduni wa Waswahili na dini, vile vile umeangazia uhusiano wa mke na mume katika ndoa.

Sifa za mwanamke katika kazi teule za fasihi na matini za kidini, zimemfanya mwanamke kupata sifa nyingi kutoka jamii pana. Hulka hizi kwa mfano, utiifu, unyenyekevu na heshima zilimfanya mwanamke kuishi na mumewe muda mrefu bila kutengana wala kutalakiana, kinyume na taswira iliyopo katika jamii zetu kwa sasa ambapo wapenzi hugeuka maadui wa kuuana na kufanyiana unyama. Kwa mfano, mauaji ya Diana Chelele, mwimbaji maarufu katika jamii ya Wakalenjin aliyeuawa kwa kudungwa kisu, mshukiwa mkuu akiwa ni mumewe ambaye walikosana mara kwa mara (*Taifa Leo:* Januari 14, 2016). Vile vile habari za Bi Jackline Mwende kutoka kaunti ya Machakos aliyekatwa mikono na kujeruhiwa vibaya na mumewe Bw. Stephen Ngila, kwa madai ya kutoshika mimba, (*Taifa Leo:* Agosti 3, 2016)

Utafiti huu basi umechunguza wosia unaotolewa kwa mwanamke katika tendi za *Mwanakupona na Ayubu*, 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora'. Vile vile tumechunguza iwapo wosia huo ni ukandamizaji au ni wosia mwafaka katika ndoa za karne ya ishirini na moja.

### 1.2 Suala la Utafiti

Wanaharakati wanaopigania haki na usawa wa wanawake wamekuwa wakidai kuwa katika uhusiano baina ya wanawake na wanaume, wanawake wamekuwa wakinyanyaswa na kukandamizwa. Suala hili ndilo tumelichunguza, yaani iwapo kwa kweli mwanamke amenyanyaswa au ni kwa kutekeleza majukumu yake ndiko kunakoonekana kuwa ukandamizaji.

Katika utafiti huu tumeangazia usawiri wa mwanamke katika ndoa na jinsi unavyoelezewa na ulivyosheheni katika *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu*, ‘Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora’ katika *Biblia*. Kupitia kazi hizi teule za fasihi na maandiko ya kidini, uhusiano wa wanandoa ulikuwa wa heshima, upendo wa dhati, unyenyekevu na utiifu kutoka kwa mke bila kulalamika. Katika karne ya 21, mambo mengi yamebadilika jinsi inavyobainika katika vyombo vya habari ambapo wanandoa wengi hawaheshimiani. Ugomvi na vita vimejaa katika nyumba zao, kuachana na kutalakiana imekuwa ni hali ya kawaida katika kisingizio cha unyanyasaji.

Taswira ya mwanamke katika jamii mbalimbali imechanganuliwa na kuainisha kuwa mwanamke ametazamwa na jamii kama kiumbe duni na anayetumika tu na mwanamume katika kuendeleza kizazi chake. Wanawake wamesawiriwa kama wanaoteswa na wanaume, vile vile wameonyesha mikakati mbalimbali wanayotumia wanawake hawa kujikomboa kutoka kwa minyororo ya unyanyasaji. Utafiti huu unadhihirisha kuwa mwanamke hahitaji kujikomboa kwa kuwa kazi hizi zinazoonekana kuwa ni unyanyasaji ndizo zinazomtofautisha na mwanamume na kwamba ni majukumu na nafasi yake katika jamii. Kwa hivyo masuala yaliyoshughulikiwa hayakuangaziwa na tafiti tangulizi.

Katika utafiti huu, tumeyachunguza majukumu wanayoyatekeleza wanawake wa sasa katika ndoa na majukumu haya yanavyoonekana kuwa ni mateso katika ndoa zao. Kwa mfano, unyenyekevu, utiifu na kumtumikia mwanamume kwa hali na mali. Kwa hivyo, tulichunguza wosia na mwelekeo katika kazi hizi na kutathmini iwapo ni ukandamizaji au utekelezaji wa majukumu. Tumechunguza iwapo wosia na

maelekezo haya yanapozingatiwa katika ndoa, yanaweza kuimarisha ndoa katika karne hii ya ishirini na moja.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na malengo yafuatayo:

(i) Kuchanganua taswira ya mwanamke katika *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu*, 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora'.

(ii) Kutathmini uhusiano wa mwanamke na mwanamume, kama unavyojitokeza katika kazi teule za fasihi na matini za kidini na uzingatifu wa mielekeo hii inavyoweza kuimarisha ndoa katika karne hii.

(iii) Kubainisha wosia wa kidini kama kigezo muhimu katika uthabiti wa ndoa.

## 1.4 Nadharia Tete

Utafiti huu umeongozwa na nadharia-tete zifuatazo:

i) Taswira ya mwanamke katika *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu*, 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora' si ya ukandamizaji, bali inamjenga mwanamke katika majukumu yake katika asasi ya ndoa.

ii) *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu*, 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora' zina mwongozo bora katika uhusiano wa mwanamke na mwanamume katika ndoa.

iii) Dini ni kigezo muhimu katika uimarishaji wa ndoa, na mwongozo katika *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu*, 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora' unazingatia dini.

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Katika utafiti huu, tumechagua mada hii kwa kuwa watafiti wengi kwa mfano wa *Utendi wa Mwanakupona* wamesema kuwa tendi hizi ni ukandamizaji kwa jinsia ya kike. Utafiti huu unapinga haya na kuchunguza upya wosia huu kwa mtazamo mpya na hali halisi ya ndoa. Tulichagua mada hii kwa sababu, tafiti za awali nyingi zilifikia uamuzi wa ukandamizaji kwa kufuata dhana potovu za kimagharibi zinazouona wosia katika *Utendi wa Mwanakupona* na *Utendi wa Ayubu* kuwa ni ukandamizaji wa mwanamke.

Aidha, tumeteua mada hii ili kujua jinsi watunzi wa matini za kidini wanavyomsawiri mwanamke na iwapo ni tofauti na matini teule za fasihi (*Utendi wa Mwanakupona* na *Utendi wa Ayubu).* Tumechagua mada hii ili tuweze kusawiri nafasi ya mwanamke katika ndoa.

## 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Katika utafiti huu, tumejishughulisha na 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora', *Utendi wa Mwanakupona* na *Utendi wa Ayubu* pekee. Tumechunguza kazi za waandishi mahususi, dhima ya kila kazi na kisha tumechanganua beti zilizotufaa katika *Utendi wa Mwanakupona* ili tuweze kubainisha wosia uliotolewa na Mwanakupona kwa bintiye Mwana Hashimu. Tumechanganua, kimakusudi, *Utendi wa Ayubu* ili tupate taswira ya mwanamke katika ndoa, uhusiano wa mwanamke na mwanamume na dini kama kigezo muhimu katika uthabiti wa ndoa yoyote ile.

Tumechanganua kazi za Solomoni, 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora' zinazopatikana katika *Biblia*, kwa kukiangazia kila kifungu kilichochaguliwa kimakusudi na kuvilinganisha na *Utendi wa Mwanakupona* na *Utendi wa Ayubu*. Katika utafiti huu, tumejiwekea mipaka kwa kurejelea uhusiano wa mwanamke na

mwanamume jinsi wanavyozitekeleza shughuli zao katika ndoa yao. Kwa hivyo katika utafiti huu tumejikita tu katika uhusiano wa waliooana ili kuidhibiti ndoa yao.

Vile vile, tumejikita katika kubainisha taswira ya mwanamke katika matini ya kidini na za kifasihi tulizozichagua. Tumeteuwa tendi hizi mbili pekee, kwa sababu zina wosia mzuri kwa wanandoa. Tumechunguza usawiri wa mwanamke katika ndoa kwa kuwa tulitaka kubainisha iwapo wosia huu umepitwa na wakati au unafaa katika ndoa ya karne hii ya ishirini na moja. Vile vile, tumeangazia dini kama kigezo muhimu katika uthabiti wa ndoa, na kwamba ni kwa kumtegemea Mungu mwanzilishi wa ndoa ndipo wanandoa hunawiri katika uhusiano wao. Tumechagua kazi hizi kwa sababu tulitaka kujua iwapo wosia unaotolewa katika kazi za fasihi na matini za kidini una malengo sawa katika kusawiri ndoa. Kisha tumechunguza hali halisi ya ndoa katika karne hii ya ishirini na moja dhidi ya wosia huu.

**1.7 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu una umuhimu mkubwa sana kwa wasomi na wanafunzi watakaopata fursa ya kusoma kazi hii, kwani kazi hii itawasaidia kutathmini usawiri wa wanawake katika ndoa, kwa ajili ya uthabiti na kudumu kwa familia za karne ya 21 na zijavyo.

Pia utafiti huu utawasaidia wasomi, wanawake kwa wanaume ili kuwa na mtazamo chanya kuhusu mwanamke katika ndoa, kwani utawafanya wasiongozwe na tamaduni potovu zilizopitwa na wakati. Utawafanya wawe watu wa kuchuja maneno kabla ya kufanya uamuzi wa kusema kuwa wanawake wanadhulumiwa katika majukumu yao.

Familia nyingi, kwa njia moja au nyingine hupitia changamoto nyingi. Wapenzi wamebadilika maadui na hata kuuana jambo ambalo linaathiri watoto, jamii na hata taifa kwa jumla. Visa kama hivi vinaripotiwa katika redio, runinga, magazeti na hata mtandaoni. Kwa kubainisha taswira ya mwanamke katika ‘Kitabu cha Methali na

Wimbo Ulio Bora', *Utendi wa Mwanakupona* na *Utendi wa Ayubu*, tumetambua jinsi mwanamke alivyotarajiwa kutekeleza majukumu yake katika jamii. Kwa hivyo, utafiti huu utasaidia kuwa na jamii thabiti na kupata uhakika wa vizazi vijavyo. Vile vile utasaidia kuelewa taswira ya mwanamke katika ndoa, uhusiano wa mke na mume na dini kama kigezo thabiti cha wanandoa.

Kwa hivyo, katika utafiti huu umebainisha usawiri wa mwanamke katika ndoa kwa kuangazia matini ya kifasihi na kidini na utasaidia kuondoa dhana kuwa mwanamke ameonewa, amenyanyaswa na kudhulimiwa katika jamii. Katika utafiti huu tumedhihirisha kuwa majukumu haya ni mafunzo bora katika ndoa na hujenga uhusiano mwema kwa wawili waliooana. Kwa muda mrefu, waandishi na wataalamu wengi wameshikilia msimamo kuwa mwanamke katika kutekeleza wajibu wake katika jamii ni unyanyasaji, jambo ambalo limebainika kwamba sivyo.

## 1.8 Hitimisho

Utafiti huu unahusu usawiri wa mwanamke katika ndoa kwa kuangazia matini ya kifasihi na kidini. Utasaidia kuondoa dhana kuwa wosia unaotolewa katika kazi hizi ni unyanyasaji wa mwanamke. Kwa muda mrefu, waandishi na wataalamu wengi wameshikilia msimamo kuwa mwanamke katika kutekeleza wajibu wake katika jamii ni njia ya unyanyasaji, jambo ambalo tumeonyesha kwamba sivyo. Kazi za waandishi mbalimbali waliotanguliza mada ya usawiri wa mwanamke katika ndoa zimejadiliwa katika sura ya pili.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.0 Utangulizi

Katika sura ya kwanza, tumeangazia usuli wa suala la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia-tete za utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo wa utafiti na umuhimu wa utafiti. Katika sehemu hii, tumeonyesha yale tuliyoyadurusu kuhusiana na mada yetu ya utafiti na vile vile nadharia zilizotuongoza katika utafiti huu. Tumeeleza yale yaliyokwisha kuandikwa juu ya mada kwa kubainisha hoja zao, kutathmini jinsi hoja hizi zinavyoafikiana na kazi zetu na kisha kupambanua tofauti ya kazi zao na kazi hii yetu.

## 2.1 Mapitio ya Maandishi

Tumeyagawa maandiko haya katika sehemu tatu kuu: yaliyoandikwa kuhusu taswira ya mwanamke katika ndoa, yaliyoandikwa kuhusu uhusiano wa mwanamke na mwanamume na yaliyoandikwa kuhusu dini kama kigezo muhimu katika uthabiti wa ndoa. Kwa hivyo, tumefafanua dhana ya taswira na pia kuangazia maandishi mbalimbali yanayohusu taswira ya mwanamke katika ndoa. Vile vile tumefafanua nadharia iliyoongoza utafiti huu.

### 2.1.1 Mapitio Kuhusu Dhana ya Taswira

Dhana ya taswira imeelezwa na wataalamu mbalimbali kwa njia tofauti tofauti. Kimsingi, taswira ni istilahi ya kifasihi inayorejelea picha au mtazamo wa mambo fulani ambayo yanatokea katika kazi anuwai za fasihi kwa kutegemea tanzu husika. Kulingana na Senkoro (1987), taswira ni mkusanyiko wa picha mbalimbali ziundwazo na maelezo ya wasanii katika kazi za fasihi. Anaendelea kusema kuwa taswira ni lugha inayochora picha za vitu au mahali kwa kutumia ishara. Aidha,

Senkoro anaeleza kuwa taswira ni mbinu itumiwayo na mshairi kuumba picha kamili ya kitu, wazo au dhana, hali na uzoefu fulani wa mtu katika akili ya msomaji au msikilizaji wa shairi.

Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (1999), taswira ni mkusanyiko wa picha zinazotokana na ufundi wa msanii katika kuteua na kupanga maneno yake ya kazi fulani ya kifasihi. Vile vile, taswira ni mkusanyiko wa picha anazozipata msomaji au msikilizaji wa kazi fulani ya kifasihi. Picha hizi huwa na funzo au ujumbe fulani. Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2002), taswira ni picha ya mambo au vitu vinavyomjia mtu akilini mwake kama maono au picha anaposoma kazi fulani. Kwa muhtasari, neno hili taswira ni mkusanyiko wa picha zinazoundwa na maelezo ya msanii katika kazi yake ya fasihi.

### 2.1.2 Maandishi kuhusu Taswira ya Mwanamke katika Ndoa

Millet (1979) anazungumzia haki za wanawake kwa kupinga namna waandishi wanaume wanavyowasawiri wahusika wao wa kike. Anarejelea kazi za waandishi kama Henry Miller, Norman Mailer na Jean Genet. Kulingana na Millet, jamii pamoja na asasi zake zinashirikiana kumkandamiza mwanamke na hii ni sifa ambayo inajitokeza katika kazi ya wandishi tuliowataja. Pia anabainisha mikabala ya saikolojia changanuzi inayohusishwa na Sigmund Freud kwa kuwa na upendeleo. Anaeleza kuwa mtoto wa kike anaanza kujichukia mara tu anapotambua kuwa hana kiungo cha kiume.

Millet anakanusha madai ya Freud kwa kusema kuwa wivu uliopo ni wa uwezo alionao mwanamume kutokana na muundo wa kijamii, basi mwanamke anakuwa na wivu wa kinachoashiriwa na hilo zubu wala si kama kiungo cha mwili. Kazi yake Millet imetufaa kwa kuwa anaangazia masuala ya wanaume na wanawake na

ukandamizaji wa mwanamke kama unavyoanza tu pindi anapozaliwa. Tofauti na utafiti wake ni kuwa yeye ameufuata mrengo wa kisaikolojia lakini sisi tumezingatia kazi teule za fasihi na matini za dini.

Lugano (1989) anaonyesha picha ya mwanamke katika siasa na masuala ya kijamii kwa kumulika riwaya za Kezilahabi. Anaonyesha kuwa mwanamke anachorwa kama kiumbe anayetegemea mwanamume. Kauli hii ni muhimu kwetu kwa sababu imetusaidia kuchunguza na kubainisha uhalisia wake na athari zinazoibuka kutokana na taswira hii. Mirengo ya nadharia zote za kijamii humulika mifumo ya jamii na katika mfumo wowote ule, kipengele cha utegemezi hakiwezi kukosekana. Kipengele hiki kilitusaidia kuchunguza taswira ya mwanamke kwa kujikita katika usawiri wa mwanamke katika ndoa kutoka kwa kazi teule za fasihi na matini za dini. Lugano anaendelea kusema kuwa ni kupitia kwa ajira ambapo mwanamke ataweza kujinasua kutokana na hali ya unyanyasaji unaotokana na mila. Kule kumtegemea mwanamume ndiko mwanaharakati huyu anadai kuwa ni chanzo cha unyonyaji. Jamii haijaweka mikakati ya kutosha ili kuleta mabadiliko kuhusu hali ya wanawake kukandamizwa. Kazi yake ni tofauti na kazi yetu kwa kuwa tumeelezea kuwa mwanamke hajanyanyaswa wala kudhulumiwa katika harakati ya kusimamia nafasi yake kwenye ndoa. Mwanamke anafaa kuyatekeleza majukumu yake bila malalamishi yoyote.

Njozi (1990) anaelezea kwamba katika ulimwengu wa taasubi za kiume, Mwanakupona hakuwa na jingine ila kumuusia bintiye kujidunisha mbele ya mumewe ili kuepukana na matatizo ambayo yangetokea. Kule kumtumikia mume kama mjakazi na mtumwa ni mbinu mojawapo ya kuujenga uhusiano mwema baina ya mume na mke katika hali ya kudumisha ndoa.

Kazi yake Njozi imetufaa kwa kuwa Njozi anakubali katika nakala yake kwamba kuna majukumu muhimu katika ndoa ambayo wanandoa lazima wayatekeleze ili waweze kuishi kwa amani. Kazi yetu ni tofauti na kazi ya Njozi kwa kuwa anadai majukumu haya yanamfanya mwanamke kuwa mtumwa na mjakazi lakini katika kazi yetu, majukumu haya ndiyo nafasi ya mhusika mwanamke katika ndoa.

Biersteker (1991) anauchukulia *Utendi wa Mwanakupona* kwa bintiye kama kejeli kwa mwanamume. Anaeleza katika utendi huu kwamba mwanamume ni mtu mzima lakini binti anashauriwa kumtunza kama kijana na kumpumbaza. Anazidi kusema mwanamume anajitokeza kama mtu mpumbavu, asiye na thamani na ambaye hawezi kujitunza mwenyewe bila usaidizi wa mwanamke. Kazi yake Biersteker imetufaa kwa kuwa anazungumzia maoni ya Mwanakupona katika ndoa. Tofauti na kazi hii, yeye anamwona mwanamke kama kiumbe aliyedunishwa kwa majukumu anayopewa. Utafiti huu unaonyesha vile vile kuwa si kweli kwamba wanaume wanatazamwa kama watoto wachanga wanaopaswa kuchungwa na kubembelezwa, bali unaonyesha kuwa ni jukumu la mwanamke katika ndoa yake kumtunza mumewe.

Yule (1996) anaelezea kwamba utamaduni ni maarifa anayopata mtu kutoka kwa jamii, na kila jamii ina namna yake ya kuelezea mambo. Kwa hivyo ni muhimu kumfunza mtoto au mtu mzima itikadi za jamii, na kutenga nafasi ya kila mmoja. Kazi yake inatofautiana na kazi yetu kwa kuwa licha ya hawa watoto kufunzwa mila na tamaduni za jamii yao, wanaelekea kutozifuata wanapokuwa wakubwa. Kazi hii ina umuhimu kwa kazi yetu kwa kuwa imetuongoza kujua kuwa kila jamii ina mila, desturi, itikadi na imani yake kuhusu masuala ya jamii.

Simala (2000) alibainisha sitiari ya uana kwa kuiweka kwenye misingi ya jamii ya Waswahili. Simala aligundua kuwa masuala muhimu ya kiutamaduni yaliyoathiri

sitiari za uana ni ulezi, uchumba, ndoa na talaka. Kazi ya Simala inatupa mchango mkubwa katika tasnifu hii kwa kuwa aliegemea sana masuala ya uana na jinsi tunavyonuia kuufanya utafiti kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii kwa kuzirejelea kazi teule za fasihi na matini za dini. Tofauti na utafiti wa Simala, katika utafiti wetu tumejikita katika *Utendi wa Mwanakupona* na *Utendi wa Ayubu* na matini ya dini.

Maingi (2005) anaonyesha namna ambavyo mwanamke amewekwa pembeni kwa kutoshirikishwa katika maamuzi muhimu ya kijamii ilhali anasifiwa kwa mchango wake wa kuwalea watoto nyumbani. Kazi hii ina umuhimu kwetu kwani inatuangazia zaidi majukumu ya wanawake. Hata hivyo, tofauti ni kuwa mhakiki huyu ameangazia zaidi unyanyasaji wa mwanamke lakini sisi tuliangazia majukumu yanayodhaniwa na wengi kuwa ni dhuluma na kufinyiliwa chini kwa mwanamke wa sasa.

Katola (2006) ameshughulikia udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia nne za Kiswahili. Tamthilia hizo ni za waandishi wa jinsia tofauti ambao ni Muhando *Hatia* (1972), Mwachofi, *Mama ee* (1987). Hawa ni waandishi wa kike. Waandishi wa kiume ni Yahya na Mulwa, *Buriani* (1983) na Mohamed, *Kitumbua kimeingia Mchanga* (2000). Katika kazi yake hakuegemea upande wowote wa waandishi ila ameonyesha kuwa mwanamke anadhulumiwa na mifumo ya kiume katika taasisi ambazo zimejikita kwenye misingi ya ubabe-dume. Miongoni mwa dhuluma alizozitambua ni wanawake kutishwa, kutusiwa, kuozwa bila hiari, kupigwa, kunyimwa haki na kukataliwa na jamii miongoni mwa zingine. Matokeo yake ni mtazamo hasi kwa mwanamke katika jamii.

Aidha, Katola ametumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Kazi hii ina manufaa kwetu, kwa sababu mtazamo wake kuhusu dhuluma umetupatia mwanga kutambua

zile dhuluma kama changamoto ambazo zinaweza kutafutiwa suluhu mwafaka na kupunguzwa kwa sababu haziwezi kukomeshwa kabisa. Kazi yetu inatofautiana na kazi ya Katola kwa sababu sisi tumetumia tenzi za Kiswahili na matini za kidini. Mwelekeo wetu utatusaidia kugundua ikiwa madai mengine kama vile haki na usawa yanakubalika kulingana na kaida za kijamii au ni kwa jinsi gani mfumo wa kisheria utasaidia kuinua kiwango cha utekelezwaji. Pia tulichunguza sehemu ambazo dhana ya usawa haiwezi kuwa na uhalisia.

Wanawake wamekuwa kama walinzi wa itikadi za kiume. Wao wamezitilia maanani na kuzivuta vya kutosha mpaka zimekuwa sehemu ya maisha yao ya kila siku. Na si tofauti na jamii nyingine, jamii hii ya Waswahili kwa muda mrefu hutumia fasihi sanaa kutetea mfumo-dume kudumisha hali kama ilivyo. Holcombe (2007) anasema, wanawake wana maeneo yao wenyewe, na kwa utamaduni nyenzo hutumika na wao wenyewe. Kwa mfano, baadhi ya maeneo ya nyumbani, kama jikoni, imekuwa hifadhi ya wanawake katika jamii za Kiafrika na mahali pengine.

Matundura (2007) amejadili kuwa mkabala wa kiuana unahusu masuala ya kimahusiano katika jamii. Mahusiano yanajibainisha katika misingi mbalimbali kama vile kijinsia, kitamaduni na kiutenda kazi. Pia ametumia mkabala wa nadharia ya Ufeministi ambao ni mkusanyiko wa nadharia nyingi, ambao kimsingi lengo lake ni kuleta usawa kati ya wanawake na wanaume. Kazi hii imekuwa ya manufaa katika utafiti huu, kwani tumepata mambo muhimu ambayo yamejitokeza katika kazi yetu, ili kuangazia taswira ya mwanamke. Vipengele hivyo alivyovibainisha Matundura vimetusaidia kuchunguza mwelekeo ambao baadhi ya jamii huegemea na kuibua taswira mbalimbali za mwanamke. Matundura pia amefafanua dhana za uana na

jinsia. Anasema kuwa jinsia ni dhana ya kibayolojia na uana ni dhana ya kitamaduni. Dhana hizi mbili zimetusaidia kuangazia taswira ya mwanamke kwa misingi hiyo.

Uana ni dhana ya kisosholojia ambayo imezalika kutokana na nadharia ya Ufeministi inayodai kuwa kijamii mwanamke na mwanamume wanayo majukumu tofauti tofauti. Suala la dhana ya uana ni tata mno kwa kuwa ni suala lililo la misingi ya kijamii au kisosholojia. Kwa mfano, mtoto anapozaliwa katika jamii nyingi za Wanandi miongoni mwa Wakalenjin, hupewa jina ambalo litatambulisha jinsia yake kama vile, Jepkemboi ni jina la msichana aliyezaliwa usiku na Kipkemboi ni jina la mvulana aliyezaliwa usiku. Greer (1970) anasema kuwa jamii nyingi na haswa za Kiafrika, bado zinashikilia tamaduni au mfumo unaomwenzi na kumkweza mwanamume huku ukimtweza na kumdhalilisha mwanamke. Greer anazipinga asasi za kisiasa na za kiuchumi ambazo kwa muda mrefu zimekuwa zikitumiwa kumdhalilisha mwanamke katika jamii.

Kitali (2011) ameshughulikia fani na usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia ya *Pango* na *Mama ee*. Kuhusu tamthilia ya *Pango*, anasema kuwa tatizo kuu linahusu siasa, uchumi, uongozi na migongano ya wimbi la ukale na usasa. Kuhusu tamthilia ya *Mama ee*, anasema ni mchezo ambao mtunzi anayasawiri matatizo yanayoikumba ndoa ya Mwavita na mumewe Kinaya. Pia ameangazia mahusiano ya wanawake na wanaume katika jamii, nafasi ya mwanamke katika jamii, na ubabe-dume ambao umejikita katika jamii. Kazi yake imekuwa ya manufaa kwetu kwa kuwa tumeangazia nafasi ya mwanamke katika ndoa. Sisi tumeshughulikia nafasi ya mwanamke kwa kuangazia matini za Solomoni na *Utendi* wa *Mwanakupona* na *Utendi wa Ayubu.* Tumechunguza jinsi waandishi hawa wa kale walivyowasawiri wanawake katika jamii na jinsi akina mama hawa walivyofanikiwa na kusifiwa na waume zao.

Mirikau (2011) anabainisha istilahi *taswira* kwamba ni jinsi mtu anavyochorwa na kuweza kutoa picha kamili ya namna anavyoonekana. Mambo haya huweza kudhihirika kupitia matendo halisi anayotendewa. Kazi yake imetusaidia kufikia lengo la kubaini taswira ya mwanamke au mwanamume katika jamii yake. Hata hivyo, kazi yake ni tofauti na yetu kwa sababu kwa kurejelea makala ya Solomoni na Mwanakupona, mwanamke hujikuta amekabiliana na uamuzi unaomfanya atukuzwe au adhalilishwe na hata kujidhalilisha mwenyewe. Mawazo ya Mirikau yalitusaidia kuchunguza jinsi hali ilivyo ili tuweze kuyafikia malengo yetu kwa kumulika matendo anayotendewa mwanamke na kubainisha changamoto zinazomkabili katika mfumo wa kijamii na iwapo mwanamke huyu amechangia kwa hali hii tatanishi. Mirikau anaendelea kueleza kuwa taswira hii aghalabu hutokana na namna anavyofikiriwa akilinini mwa binadamu. Mambo haya huweza kudhihirika kupitia matendo halisi anayotendewa. Mwanamke hutendewa na hata mwenyewe huweza kujitendea mambo ya kushangaza katika jamii husika. Mirikau anaelezea kuwa taswira ni ngazi katika jamii ambayo mwanamke hujikuta amewekwa na kukubaliana na uamuzi huo unaomfanya aidha atukuzwe au adhalilishwe na hata kujidhalilisha mwenyewe.

### 2.1.3 Uhusiano kati ya Mwanamke na Mwanamume

Katika utafiti wetu tumepitia tasnifu kama vile ‘Tajriba za Uislamu Katika Utamaduni wa Mwanamke’ (Mwanakombo, 2011) ambayo inaangazia suala letu tulilokuwa tunalitafitia la usawiri wa mwanamke katika ndoa kwa kuongozwa na nadharia ya Ufeministi na nadharia ya Udenguzi huku tukizingatia malengo yetu.

Beauvoir (1952) naye anaeleza uhusiano wa mwanamume na mwanamke katika ndoa kwa kutaja unyanyasaji unaotokana na mfumo wa kijamii. Anaelezea kuwa

ulimwengu huu una baadhi ya sehemu ambazo zinadhibitiwa na mifumo ya kijamii ambayo huwakweza wanaume na kuwatweza wanawake. Ni wanawake wachache tu ndio ambao wana imani inayofungamana na misingi ya kisiasa na ambao wamechukua hatua ya kujiunga na kuunda vyama vinavyowasaidia kutetea haki zao.

Hali za wanawake, kwa mfano za kukosa kujihusisha na siasa na unyanyasaji kutoka jamii ndizo zilizochochea utafiti huu. Kazi yake Beauvoir inatufaa kwa kuweza kumwelewa mwanamke katika harakati zake za kujitambua na kuyatekeleza majukumu yake vilivyo. Kupitia kwa kazi yake, tulitambua majukumu ambayo yalichukuliwa kuwa yamemtweza mwanamke na yale ambayo yalimkweza mwanamume. Kazi yake inatofautiana na yetu kwa kuwa katika utafiti huu tumeyainisha majukumu ya mwanamke ambayo yanaonekana kumdhalilisha na majukumu hayo ndiyo yanayozitambulisha hulka zake kama mwanamke.

Khatib (1985) anapambanua katika kazi yake kuwa *Utendi wa Mwanakupona* ni shairi ambalo ni sumu kwa sababu linawatia wanawake moyo wa utumwa. Anaendelea kudai kuwa mtunzi wa shairi hili anamkandamiza na kumnyanyasa mwanamke wa sasa na halimfai. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa kuwa inazungumzia masuala ya wanawake na kwa hivyo tulitathmini hoja hizi anazozungumzia kama unyanyasaji. Kazi yake inatofautiana na kazi yetu kwa kuwa yale anayoyaona Khatib kama dhuluma, kwetu ni majukumu yanayoweza kusaidia ndoa kuwa thabiti.

Karne nyingi zimepita tangu utunzi wa *Utendi wa Mwanakupona* ulipotungwa, yakisiwa mwaka wa 1858. Utunzi huu umekuwa utendi maarufu sana, hasa kwa wahakiki wa fasihi na wanasosolojia kwa kurejelea swala la mwanamke katika jamii za Kiafrika. Huu ni utenzi ambao uliibua hisia mbalimbali kuhusiana na nafasi ya

mwanamke hasa mwanamke wa Kiislamu. Wengi walirejelea utenzi huu kama sumu kali ambayo inamdhalilisha mwanamke na kutompa hadhi anayostahili katika jamii.

Indede (2011) anauhakiki *Utendi wa Mwanakupona* kwa kumuunga mkono Biersteker (1991) kuwa Mwanakupona anamdhalilisha na kumdunisha mwanamume kwa kumlinganisha na mtoto mdogo. Mwanamume anajitokeza kama mtu anayetegemea mwanamke, asiye na thamani na ambaye hawezi kujisimamia mwenyewe. Kazi yake ni muhimu kwetu kwa kuwa anazungumzia masuala katika *Utendi wa Mwanakupona* na sifa za mwanamke katika utendi huu. Kazi yake Indede ni tofauti na kazi yetu kwa kuwa anamchora mwanamume kama mtoto mdogo anayehitaji usaidizi na kumwita mpumbavu na asiye na thamani. Kazi yetu imemchora mwanamume kama mhusika anayehitaji heshima zake kwa sababu ya nafasi yake na majukumu yake katika jamii.

Biersteker (1991) anachukulia *Utendi wa Mwanakupona* kama kejeli kwa mwanamume. Kwa mfano, katika beti hizi: "***Mtunde kama kijana, asiyejua kunena***" (ubeti 35); ***"Mpumbaze apumbae, amriye sikate"*** (ubeti 36). Mwanamume katika utenzi huu ni mtu mzima, lakini binti anashauriwa "kumtunza kama kijana na kumpumbazwa." Kazi yake Biersteker imetufaa kwa kuwa anazitaja sifa za kubainisha uhusiano wa mwanamke na mwanamume katika ndoa jinsi zinavyojitokeza katika *Utendi wa Mwanakupona*. Kazi yake ni tofauti na yetu kwa kuwa mtafiti huyu anaziona sifa hizi za mume kama hasi ilhali katika utafiti huu sifa hizi ni muhimu kwa uthabiti wa ndoa.

Wanjiku na Akinyi (1993) katika utafiti wao wanabaini kuwa jamii nyingi za Kiafrika humnasibisha mwanamke na maovu katika jamii. Kwamba nafasi za uongozi na za kiuchumi huthibitiwa na mwanamume. Mwanamke hashirikishwi katika uongozi

katika jamii nyingi za Kafrika. Wanaendelea kutoa pendekezo kuhusu suala la usawa wa kijinsia. Wanawake kwa wanaume wanastahili kujitahidi kwa ushirikiano katika kupiga vita ubabe-dume katika jamii. Wanaelezea kwamba maumbile hayawezi kubadilishwa lakini mfumo unaweza kubadilishwa kwa sababu ni tokeo la jamii la mazoea na desturi. Kazi yao ilitufaa kutathmini kwa undani na kutoa mifano maridhawa ili kutambua uhusiano kati ya mwanamke na mwanamume katika ndoa lakini kazi hizi zinatofautiana kutokana na vigezo muhimu vya uzalishaji wa mali katika jamii. Kazi teule za fasihi na dini tulizozichagua humdhihirisha mwanamke kama mfanyakazi mwenye bidii.

Kwa mujibu wa Mulokozi (1996), tabia ya mwanamke kama ilivyodhihirishwa na Mwanakupona ni ile ya unyenyekevu, na chombo kwa ajili ya kuridhisha tamaa ya mume. Mulokozi anasema kwamba umaarufu wa *Utendi wa Mwanakupona* miongoni mwa Waswahili ni ishara ya wazi ya jinsi mfumo-dume umeingilia maisha ya wanawake, hasa wale walio katika daraja la juu. Anaendelea kusema kuwa wakati wa kuwahudumia waume zao, mwanamke anafundishwa kukandamiza hisia zinazoonyesha nguvu au hata hasira, kwa maana nguvu ni mume, na hivyo ni kitu ambacho mwanamke lazima akiepuka. Kazi hii imetufaa kwa kuonyesha kuwa kihistoria, kitamaduni na kijamii, mwanamke alikuwa anaonyeshwa jinsi ya kuishi katika mazingira ambayo alichukuliwa kama vyanzo vya faraja na furaha kwa waume. Kazi yake Mulokozi inatofautiana na kazi yetu kwa kuwa Mulokozi anayaona majukumu ya mwanamke kama ukandamizaji lakini utafiti huu unayachukulia kama nafasi na hulka ya mwanamke katika jamii husika.

Kulingana na Ntarangwi (2004), mwanamke hawezi kupata ukombozi wa aina yoyote kama hajakombolewa kiuchumi. Kwa jumla, anaelezea kuwa katika jamii nyingi

ulimwenguni, nyenzo zote za kuzalisha mali zinatawaliwa na wanaume huku wanawake wakiwa wategemezi na watumishi wa wanaume. Hali hii huwakumba wanawake kwa sababu tangu zamani wanawake wamenyimwa nafasi ya kujiendeleza kiuchumi. Anapendekeza kuwa mwanamke apewe uhuru wa kiuchumi, ili aepuke unyanyaswaji na dhuluma. Kazi hii ilitufaa kwa vile tulichunguza nafasi ya mwanamke katika jamii na uwezo wake wa kutambua majukumu yake ya kuzalisha mali na uendelezaji wa uchumi katika jamii. Tofauti na kazi hii ya Ntarangwi, tumenuia kudengua imani potovu kuwa mwanamke ananyanyaswa au anadhalilishwa wakati anayatekeleza majukumu yake. Tumenuia kutambua kwa kweli iwapo mwanamke ana uhusiano mzuri na mwanamume katika jamii katika kuyaendeleza maisha yao. Kulingana na 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora' katika *Biblia*, mwanamke anatarajiwa kuwa mleta riziki nyumbani, na anayetegemewa na jamii nzima.

Iribe na Mukhwana (2011) wamezungumzia jinsia na uana kama vigezo vinavyotumiwa na jamii kuleta ubaguzi. Dhana ya jinsia ni kigezo cha maumbile ambapo kibayolojia inadhihirisha kama mtu anayezungumziwa alizaliwa mke au mume, na hali hii haibadiliki kamwe jinsi inavyobainishwa na Mohamed na Mohamed (2002). Kwa upande mwingine, uana ni dhana ya kisoshiolojia ambayo imezalika kutokana na nadharia ya Ufeministi inayodai kuwa kijamii, mwanamke na mwanamume wanayo majukumu tofauti tofauti. Tunaafikiana na wataalamu hawa kwamba kila mmoja ana majukumu yake katika jamii, na kwa kutekeleza majukumu haya swala la ubaguzi na ukandamizaji halitakuwepo. Kazi yetu ni tofauti na kazi yao kwa kuwa tumechunguza taswira ya mwanamke katika jamii bila kuegemea sayansi na jinsi mwanamke na mwanamume wamekuwa wakihusiana.

Mnenuka (2012), anahoji kuwa majukumu mengi ya mwanamke ambayo wakati mwingine hutekelezwa bila usaidizi kutoka kwa mwanamume, husababisha mwanamke kupoteza uzuri aliokuwa nao kabla ya kuolewa. Mnenuka anaeleza kuwa mwanamke kwa kiasi kikubwa amekuwa ni mtu wa kukandamizwa. Kazi hii ya Mnenuka inatufaa mno kwa kuwa alimrejelea mwanamke ambaye tulichunguza usawiri wake katika ndoa. Tofauti na kazi hii yetu ni kwamba mwanamke anafaa kufurahia majukumu haya si kwa kuyaona kuwa mateso hata kufikia kiwango cha kupoteza urembo na uzuri wake. Solomoni amemchora mwanamke katika Wimbo Ulio Bora kama mrembo aliyeumbwa akaumbika na akatunukiwa uzuri wa maumbile.

Katika *Habari Leo* (Oktoba 9, 2015) tunaelezwa kwamba Anne-Marie Lewis anayefanya kazi ya urubani anatathmini kuwa wanawake Wa kiafrika wahamasishwe kujiunga na sekta ya usafiri angani. Pamoja na kwamba uwepo wa wanawake katika sekta ya usafiri wa anga bado ni mdogo, uwezo wa kuwa viongozi katika safari ya anga hauna mwiko. Wanawake barani Afrika hawapaswi kuogopa sekta ya urubani inayokua barani kote. Hayo ni maneno kutoka kwa rubani mwanamke wa kwanza kuongoza ndege aina ya Airbus katika mikoa ya Tanzania.

Wanawake wanapaswa kufahamu kuwa hakuna aina ya kazi ambayo ipo kwa ajili ya wanaume pekee, bali wanawake wana uwezo wa kuchangia katika sekta ya usafiri wa anga kwa uwezo wao wa kufanya kazi kwa bidii. Aliyasema hayo wakati wa-mahojiano maalumu na mwandishi wa *Habari Leo.* Kwa mujibu wa Lewis, wanawake wa Afrika wanahitaji kuelewa kwamba nia na uamuzi wao utaondoa hofu au hasara ya kiuchumi.

Bi Lewis anabainisha kuwa uwezo wa wanawake kufanya kitu kwa kuongozwa na malengo yao utazaa matunda ya kuridhisha. Anaelezea kuwa wanawake wanapaswa

wabaki kwa uasilia wao ili waweze kufanikiwa, waendeleze sifa za kipekee katika nafasi zozote, kwani wao ni wasikivu wazuri, walezi na pia wana ujuzi mkubwa wa kupanga mambo. Kazi ya Lewis imetufaa kwa kuwa rubani huyu anaelezea kuwa mwanamke ana uwezo mkubwa na nafasi nzuri katika jamii hasa ya kujiwasilisha na kutoa taswira nzuri ya hulka za wanawake wenzake. Msisitizo wa Lewis kuwa mwanamke anaweza kufanya kazi yoyote, unatofautiana na msisitizo wa utafiti huu. Lewis analenga kumwonyesha mwanamume kuwa mwanamke hastahili kunyanyaswa kwa majukumu ya nyumbani. Katika utafiti huu hatupingi mwanamke kuwa rubani, lakini anapopata fursa hii asiyasahau majukumu yake kama mwanamke.

### 2.1.4 Dini kama kigezo muhimu katika Uthabiti wa Ndoa

Dini ni kigezo muhimu sana katika masuala ya ndoa. Hii inatokana na nafasi kubwa inayotolewa na waandishi mbalimbali wa *Biblia Takatifu*. Mfano mzuri wa waandishi hao ni Mfalme Solomoni ambaye ni mwandishi wa Kitabu cha Methali. Swaleh (1992) kwa kushughulikia maudhui katika *Utendi wa Mwanakupona,* anatathmini kuwa maudhui ya dini yamejikita katika mafundisho ya dini ya Kiislamu yanayomtunukia mwanamke nafasi anayostahiki katika jamii yake. Swaleh anaendelea kutuelezea katika kazi yake kuwa mwanamke anastahili hadhi anayopewa katika jamii yake. Ingawa mtaalamu huyu amezungumzia nafasi ya dini katika *Utendi wa Mwanakupona* sisi tunaangazia usawiri wa mwanamke katika utendi huu. Kazi ya mhakiki huyu imetufaa kuhakiki nafasi ya mwanamke katika jamii ya sasa.

Qauyson (1997) anaelezea kuwa kila kazi ya sanaa ina mwelekeo wa kitamaduni, ambayo inaingiana na mambo mengine ya maandishi ya fasihi katika taaluma fulani muhimu. Kwa mfano, mada ya ndoa na masomo maalum kuhusu ndoa kama maadili na hofu ya Mungu huingizwa. Kazi yake Qauyson ilitufaa kwa kuwa alizingatia

maudhui ya dini katika utafiti wake na kwamba Mungu anastahili kujadiliwa katika kazi zote za fasihi. Kazi yake ni tofauti na kazi zetu kwa kuwa katika kazi yetu tunajadili dini kama kigezo muhimu katika uthabiti wa ndoa.

Nkata na Thody (2001) wanabaini kuwa nyimbo katika dini hutumika kwa madhumuni mbalimbali katika jamii. Kuingizwa kwa nyimbo hizi katika muundo wa utendi, huendeleza maendeleo ya mandhari, tabia na njia ya kupasha masomo kwa wasomaji. Kazi hii imetufaa kwa kuwa anazungumzia mafunzo maalum ya kidini kupitia kwa nyimbo ingawa ni tofauti na kazi yetu tunayozingatia *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu* na matini za dini zinazotoa wosia na maadili katika ndoa.

Renate (2008) anabainisha kuwa Mwanakupona Binti Msham (1810-1860) alichukuliwa kuwa mmoja wa washairi wa kike wa karne ya kumi na tisa. Binti Msham anaandika shairi la kumwandaa bintiye kwa ndoa. Katika shairi hili anaonyesha jinsi mtu anaweza kusema bila hofu kupitia mashairi kuhusu masuala ya jinsia na kujamiiana. Renate (2008) anauhakiki utendi huu kuwa mama anamfunza binti yake jinsi ya kuvaa ili kumvutia mumewe. Inaonekana kwamba Binti Msham kama mama amechukua sehemu katika kuhakikisha kuwa bintiye amekaa vizuri na mumewe. Kazi hii ya Renate imetufaa kwa kuwa imemchora mwanamke anayetoa ushauri kwa mwanawe kama mhifadhina. Anatambua masuala yote yanayomhusu mwanamke katika jamii yake, masuala haya yanajikita katika mafundisho ya dini ambapo yamejikita katika kanuni za Kiungu.

## 2.2 Msingi wa Kinadharia

Katika utafiti huu tumeongozwa na nadharia mbili ambazo ni; nadharia ya Ufeministi na nadharia ya Udenguzi. Utafiti wetu ni wa kifasihi na hivyo tumeongozwa na

nadharia za kifasihi kulingana na uamilifu wake katika utafiti wetu. Tuanze na nadharia ya Ufeministi:

### 2.2.1 Nadharia ya Ufeministi

Murungi (2013) anaeleza kuwa neno 'Ufeministi' linatokana na neno la kilatini 'femina' lenye maana ya 'mwanamke'. Dhana hii inarejelea uwakilishaji wa haki za wanawake kufuatana na imani ya usawa wa kijinsia. Huu ni mwamko wa wanawake unaolenga kupigania na kukomesha udhalimu dhidi ya mwanamke. Ufeministi ni nadharia inayohusu masuala ya wanawake na inayojaribu kufichua matatizo wanayoyapata wanawake. Ufeministi ni jina linalojumlisha aina nyingi za misimamo, itikadi na matapo tofauti tofauti yanayozitetea haki za wanawake dhidi ya ubaguzi wa jinsia uliotawala dunia kwa muda mrefu sana katika upande wa siasa, uchumi, utamaduni, dini na jamii kwa jumla. Wafuasi wa nadharia hii wanashikilia kwamba pana haja ya kuwa na usawa wa kijinsia licha ya kuwapo kwa tofauti za kimaumbile.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa nadharia ya Ufeministi ina lengo la kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kiutamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Mtaalamu huyu anaendelea kusema kuwa Ufeministi ni nadharia ambayo inasaili na kudadisi itikadi ya kiume ambayo imekuwepo katika jamii tangu jadi. Inadadisi pia fasiri za kiume za fasihi pamoja na mikabala ya kiubabe-dume.

Kwa jumla, nadharia ya Ufeministi ni nadharia iliyojikita katika kupinga ukandamizaji wa mwanamke katika jamii hususan katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, na kiutamaduni.

### 2.2.2 Chimbuko la Nadharia ya Ufeministi

Masuala ya kifeministi yalianza kuzungumziwa katika karne ya kumi na tisa ambapo yalishika nguvu miaka ya sitini na sabini ya karne ya ishirini. Hivyo basi nadharia ya Ufeministi inafahamika kuwa iliibuka katika muungano wa ukombozi wa wanawake uliopamba moto katika miaka ya sitini huko Marekani (Ntarangwi 2004). Katika kipindi hiki, wanawake hasa wa Kimagharibi walianza kuzungumzia matatizo yao kwa kuyaandikia. Hata kama masuala ya kifeministi yameanza kuzungumziwa miaka ya sitini, kulikuwa na jitihada mbalimbali za kupigania usawa baina ya wanaume na wanawake ingawa hazikuchapishwa kama anavyosema Onyoni (2012).

Kulingana na mtaalamu Onyoni, nchi ya Ufaransa kuanzia mwaka 1789 hadi mwaka 1795, kulikuwa na maandamano ya wanawake kutetea kushushwa kwa hadhi zao kwa kile walichokiita *'Msimbo* wa *Napoleon'*. Mtawala Napoleon alisema kuwa akili za wanawake ni dhaifu zikilinganishwa na za wanaume. Kwa hivyo, wanawake walifaa kupewa elimu ya kiwango cha chini kama ya ushonaji. Mnamo mwaka 1848 huko Marekani Kaskazini, kuna kundi la wanawake lililoungana katika juhudi za kuleta ukombozi wa wanawake. Kulifanyika mkutano jijini New York ambapo wanawake walitangazwa kuwa huru katika misingi ya kukubaliwa kupiga kura, kupewa elimu ya kutosha, kupewa nafasi sawa za kufanya biashara, usawa wa kupata fidia, usawa wa kisheria na kupata ajira (khj).

Ithibati za kimaandishi za kifeministi zenye utaratibu na zilizowekea msingi nadharia ya Ufeministi ni *A vindication of the Rights of Women* ya Wollstonecraft (1792) na *A Room of One's Own* ya Virginia Woolf (1929). Woollstonecraft anasemekana ndiye wa kwanza kuzungumzia masuala ya wanawake kwa utaratibu maalum. Beauvoir (1952) alichangia pakubwa maendeleo ya uhakiki wa kifeministi. Lengo kuu la

Beauvoir lilikuwa kubainisha, kukosoa na kupiga vita asasi zilizomdhalilisha au kumdunisha mwanamke. Asasi hizi ni dini, ndoa na utamaduni. Beauvoir anasema kuwa dini humkandamiza mwanamke kwa kumfundisha kunyenyekea. Ndoa nayo imejengwa kwenye misingi na imani ya uwezo mkubwa alionao mwanamume akilinganishwa na mwanamke. Anadai kuwa utamaduni humsawiri mwanamke katika tamathali hasi na duni.

Millet (1979) ameleta athari kubwa katika historia ya Ufeministi. Millet aliwashambulia waandishi wanaume kama vile Henry Miller, Norman Miller, Jean Gennet na D.H. Lawrence kutokana na jinsi walivyowasawiri wahusika wa kike. Kutokana na aliyoyagundua katika kazi hizo, Millet anabainisha kuwa miundo ya kijamii pamoja na asasi zake zinashirikiana kumkandamiza mwanamke. Millet aidha anaishambulia mikabala ya saikolojia changanuzi ya Sigmund Freud kwani ina mapendeleo makubwa kwa mfumo wa kiubabe-dume. Freud alisema kuwa mtoto wa kike huanza kujichukia mara tu anapotambua kuwa hana kiungo cha kiume.

Ogundipe (1994) ana maoni kuwa wanawake wamepewa majukumu duni na yanayosawiriwa kwa ubaya kama vile kuwa wachawi, na wanaume nao husawiriwa kuwa werevu, wenye nguvu na kuaminika na wenye uwezo wa uongozi kwa kuzaliwa. Ogundipe anasema hali kama hii huchangia katika kumdunisha na kumtesa mwanamke katika jamii. Kuna wataalamu wengine ambao wamechangia kutoa maoni yao kuhusu Ufeministi. Tuliowataja ni baadhi yao tu. Wafula na Njogu (2007) wanadai kwamba Ufeministi kama nadharia, hufumbata mikabala na mitazamo kadhaa. Matapo ya Ufeministi hubainishwa kupitia njia mbili kuu: kiitikadi na kimaeneo.

Mkabala wa kiitikadi unahusu mitazamo mitatu mikuu ya Ufeministi ambayo ni Ufeministi Huru, Ufeministi wa Kijamaa na Ufeministi wa Kimapinduzi (Wafula na Njogu 2007). Ufeministi Huru hutetea usawa kati ya wanawake na wanaume katika ngazi zote za maisha. Ufeministi wa Kijamaa hulenga kukosoa jamii na hivyo, huwahimiza wanaume kushiriki katika malezi ya watoto na kadhia nyingine ambazo kimapokeo zimechukuliwa kuwa kazi za wanawake. Ufeministi wa Kimapinduzi pia huitwa Ufeministi wa Kiharakati. Ufeministi huu humchukulia mwanamume kama adui mkubwa zaidi ya mwanamke. Kwa hivyo, Ufeministi huu huhusisha ukandamizwaji wa mwanamke na tofauti za kimaumbile.

Tapo hili hushikilia kuwa wanawake wanapaswa waitawale miili yao na hata wasiolewe. Njia ya kuainisha matapo ya Ufeministi kimaeneo huhusisha Ufeministi na maeneo ya kijiografia. Wataalamu wa kuainisha Ufeministi kimaeneo ni Eagleton (1991). Wanaugawa Ufeministi katika matapo manne: Ufeministi wa Kifaransa, Ufeministi wa Kiingereza, Ufeministi wa Kimarekani na Ufeministi wa Kiafrika.

Ufeministi wa Kifaransa unafafanua jinsi lugha hutoa maana ya mtumiaji wake. Tapo la Ufaransa linadai kuwa lugha kama inavyotumiwa ni zao la taasubi za kiume. Wanasema kuwa lugha inampendelea mwanamume kuliko mwanamke. Jazanda za kuelezea uwezo, nguvu na mamlaka ni za kiume ilhali zile zenye kusawiria ulegevu na kutoweza ni za kike. Ufeministi wa Kimarekani unahusishwa na kazi ya Ellmann *Thinking about Women (1968).* Ellmann aliangalia jinsi wanawake wanasawiriwa kwa namna mbalimbali katika kazi zilizoandikwa na wanaume na jinsi wanawake walivyoendeleza usawiri huo hasi wa wanawake katika kazi zao.

Friedan katika *The Feminine Mystique* (1963) anachunguza maisha ya mwanamke ambayo anasema ni jambo lisiloeleweka na wanaume na pia wanawake wenyewe.

Wengine waliochangia Ufeministi wa Kimarekani ni kama Freud (1950) pamoja na Millet (1979). Tapo hili linashikilia kwamba wanawake wana namna yao ya kipekee ya kuandika na kujieleza. Aidha, wanasema kuwa kuna dhamira zinazorudiwarudiwa katika tungo za wanawake. Wanashugulikia kazi za fasihi zilizotungwa na wanawake na pia wanaume maadamu zinaongea juu ya wanawake. Ufeministi wa Kiingereza huchukulia kuwa mambo ya kihistoria na siasa ndiyo huathiri matendo ya wanawake.

Beauvoir (1952) anafafanua kwamba nadharia ya Ufeministi inaangazia haki za wanawake na usawa kati ya wanawake na wanaume. Chanzo cha kuibuka kwa nadharia hii ni vuguvugu la kutaka kufuta kabisa uonevu wa mwanamume kwa mwanamke. Nadharia hii inadai kuwa chimbuko la uonevu na ukandamizaji unaofanywa na wanaume kwa wanawake ni uroho wa mwanamume katika kumtawala mwanamke. Lengo kuu la Ufeministi ni kuumaliza kabisa utawala wa mwanamume kwa mwanamke.

Chodorow (1989) anaelezea kuwa kuna njia mbalimbali za kufafanua nadharia ya Ufeministi, ikiwa ni pamoja na haki za huria za wanawake na haki za wanawake kiujamaa. Nadharia ya Ufeministi kwa njia nyingine ni upanuzi wa haki za wanawake katika mjadala wa kinadharia au falsafa. Inalenga kueleza asili ya usawa wa kijinsia. Inaangazia majukumu ya wanawake kwa jamii, uzoefu, maslahi na kazi za wanawake katika nyanja mbalimbali, kama vile anthropolojia na sosholojia, mawasiliano, uchunguzi wa kisaikolojia, uchumi nyumbani, fasihi, elimu, na falsafa.

Dworkin (1976) alitoa mapendekezo katika kukomesha utawala wa mwanamume kwa mwanamke. Dworkin anasema kuwa ili kufanikisha nadharia hii, tunahitaji kubomoa kabisa muundo wa mihimili ya utamaduni wa jamii kama vile sanaa, kanisa na sheria zinazodhibitiwa na baba, jamii na taswira zote za asasi, mila pamoja na desturi

ambazo zinamwona mwanamke kuwa mtu ovyo. Nadharia ya Ufeministi inaathiriwa na ajenda na mapambano ya wananadharia kama Wollstonecraft (1792), waliohusisha Ufeministi na harakati za kupigania haki za mwanamke. Harakati hizi zilianzishwa na wanawake wa rangi tofauti nchini Marekani katika karne ya kumi na nane.

Hata hivyo, kazi iliyokuwa na mchango mkubwa katika kuuweka msingi wa uhakiki wa Ufeministi ni kazi maarufu ya mwandishi wa Kifaransa, Beauvoir iitwayo, *The Second Sex* (1952). Katika kitabu hiki, mwandishi huyu anachukua mkabala wa kiharakati kwa kushambulia na kukosoa baadhi ya asasi zinazochangia katika kumdhalilisha au kumdunisha mwanamke. Asasi kuu anazozishambulia ni ndoa, dini na utamaduni.

Ntarangwi (2004) anadai kuwa upiganiaji wa haki za mwanamke ulitokana na azma ya wanawake weusi kutoka Marekani na ambao walipitia ukandamizaji mwingi chini ya tawala za ufalme za Waingereza. Utumwa na kutengwa kwa misingi ya rangi zilikuwa ni sababu maalum za kupigania ukombozi huu. Kutengwa kwa msingi wa rangi na kunyimwa haki za kibinadamu kuliwafanya wanaharakati kufahamu kwamba njia ya kipekee ya kupata uhuru wa kijamii, kisiasa na kiuchumi ni kwa mwanamke kujisimamia kupitia kwa rasilmali.

Kipindi hiki cha ukandamizaji Marekani kilisababisha wanaharakati wa kijinsia waanze kusaili kuhusu miundo misingi ya kitamaduni iliyoakisi haki za raia kulingana na rangi, mali na matabaka ya kijamii. Mawazo haya yalikuja kuwa msingi wa kampeni za kupigania usawa wa kijinsia katika sehemu mbalimbali za ulimwengu. Kuna tofauti kati ya Ufeministi wa Magharibi na wa Afrika. Ufeministi wa Magharibi, ulipigania haki za raia na Ufeministi wa Afrika ulipigania haki za kibinadamu na kijinsia. Kwetu sisi tunadai kuwa kabla ya kupigania haki hizi, ilikuwa

ni muhimu kutambua majukumu ya akina mama na nafasi yao katika jamii, kwa sababu ukandamizaji huu kulingana na utafiti wetu si ukandamizaji bali ni hulka za wanawake katika jamii husika.

### 2.2.3 Tapo la Ufeministi Huru

Mkabala huu wa Ufeministi ndio uliotuongoza katika utafiti huu wetu wa 'Usawiri wa mwanamke katika ndoa kwa kurejelea kazi teule za fasihi na matini za kidini'. Wafula na Njogu (2007) wanaeleza kuwa Ufeministi Huru hutetea usawa kati ya wanawake na wanaume katika ngazi zote za maisha. Mjadala unaoendelezwa na Wollstonecraft (1792) kuhusu Ufeministi unatokana na mawazo yanayoendelezwa na wanaharakati wenye mawazo huru kwamba kila binadamu ana haki za usawa. Mtaalamu huyu anasema kwamba jambo la busara ni kukubali kuwa mwanamke ana uwezo na akili sawa na mwanamume kwa sababu waliumbwa, na kila mmoja akapewa kipawa cha kipekee na Mola. Tapo hili la Ufeministi ndilo Ufeministi huru. Aidha, mzizi wa Ufeministi unapinga madai kwamba mwanamke anamtegemea mwanamume na kuendelea kusema kuwa mwanamke ana haki na nafasi yake. Mabepari wa Marekani, Ufaransa na Uingereza waliyatia nguvu mawazo haya kwamba mwanamke ana uwezo sawa na mwanamume.

Utafiti huu unadhihirisha kwamba ni jukumu la mwanamke kumtii mume wake katika ndoa na bali hawakandamizwi wanaposimamia nafasi hiyo spesheli ya kuwa mwanamke. Bressler (2003) anaeleza kwamba uhakiki wa Ufeministi unaofaa katika kazi yoyote ni ule unaojikita katika uhakiki wa usawiri wa mwili, lugha, akili na utamaduni.

### 2.2.4 Mihimili ya Nadharia ya Ufeministi Huru

Mihimili ya nadharia hii ilituongoza katika kuchambua usawiri wa mwanamke katika ndoa kwa kuongozwa na malengo ya kuchunguza taswira ya mwanamke katika ndoa, kutathmini uhusiano wa mume na mke katika ndoa na kubainisha dini kama kigezo muhimu cha uthabiti wa ndoa.

Kuna mihimili ambayo ni ya kimsingi katika nadharia ya Ufeministi na ambayo humwelekeza mtafiti. Kwanza nadharia ya Ufemenisti ni ya jamii ya mfumo dume na inatumia masuala ya jamii kama jukwaa la kuelezea hali ya mwanamke katika jamii. Hii ilitumiwa katika utafiti kuonyesha uhusiano kati ya mwanamke na mwanamume katika ndoa. Utafiti wetu unahusu usawiri wa mwanamke katika *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu* na matini za dini katika ndoa. Watunzi wa kazi hizi za kifasihi na wa matini za kidini wametumia jukwaa la ndoa kuainisha uhusiano wa mwanamke na mwanamume katika ndoa, ambapo mwanamke amebainishiwa majukumu yake huku mwanamume akionyeshwa nafasi yake kikamilifu.

Nadharia ya Ufeministi huru inashambulia asasi mbili za jamii zinazochangia ukandamizwaji wa mwanamke. Asasi hizi ni ndoa na utamaduni. Nadharia hii inasisitiza kwamba dini inamfunza mwanamke kuwa mnyenyekevu na kuwa inampa mwanamume uwezo mkubwa akilinganishwa na mwanamke. Nao utamaduni katika jamii ya Waafrika umemsawiri mwanamke katika njia iliyo hasi na duni. Nadharia hii inadai kuwa kila jamii ulimwenguni ina nguvu fulani inayoiongoza na pia ina utamaduni wake. Katika utafiti wetu kigezo hiki kilituongoza kutafitia ikiwa kweli ndoa na utamaduni umechangia katika ukandamizaji wa mwanamke. Utafiti wetu kuhusu usawiri wa mwanamke katika *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu* na matini za dini katika ndoa umejikita katika ndoa na tamaduni. Kwa hivyo, tulibainisha

iwapo asasi hizi zimemkandamiza mwanamke au ni jukwaa zuri la kuutekeleza wajibu wake.

Wafeministi huru hujaribu kukiuka mitazamo ya kiume ambayo yaelekea kutumiwa sana katika jamii. Mkondo huu kwamba wanaume wamepewa nafasi ya juu katika jamii ulitusaidia kubainisha ukweli huo na kuonyesha kuwa kuna kanuni katika maisha ya binadamu ambazo hazitatolewa bila kupatwa na madhara au changamoto katika maisha ya kawaida.

Nadharia ya Ufeministi huru hupigania kulinda haki za wanawake katika jamii ya ubabe-dume. Mihimili hii inadhihirisha kubaguliwa kwa wanawake katika jamii kwa misingi ya jinsia yao ya kike, na kwamba hali hii imekuwepo ulimwenguni tangu jadi. Mihimili hii ilitufaa katika utafiti wetu kuhusu usawiri wa mwanamke katika *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu* na matini za kidini katika ndoa kwa kutubainishia haki zinazodaiwa kuwa za wanawake ambazo kulingana na utafiti wetu ndizo nafasi rasmi za mwanamke katika ndoa.

Ufeministi ni nadharia ya fasihi ambayo inajishughulisha na utetezi wa haki za wanawake dhidi ya ukandamizwaji katika jamii yenye mfumo uliodhibitiwa na wanaume. Nadharia ya Ufeministi yenye msimamo mkali ilisaidia katika kufikia lengo la kubainisha taswira ya mwanamke katika jamii ya kale na ya kisasa. Hivyo basi, Ufeministi huru ni nadharia ambayo imewekewa msingi na msukumo mkubwa wa kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kitamaduni, kiuchumi, kidini, kijamii na kisiasa. Pingu hizi zimejengeka kwenye misimamo ya itikadi ya kiume. Mihimili hii ilifaa mada hii ya usawiri wa mwanamke katika *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu* na matini za kidini katika ndoa kwa kuwa

tulichunguza masuala ya wanandoa na kudhihirisha wazi nafasi ya mwanamke kiutamaduni, kiuchumi, kidini, kijamii na kisiasa.

Katika nadharia hii, usawa wa kijinsia na kitamaduni hukuzwa kupitia kwa miundo misingi inayopatikana katika jamii. Inapigania jamii mpya inayoheshimu jinsia ya kike kupitia kwa amali zake. Mtafiti hakubaliani na haya yote kwa kuwa majukumu ya mwanamke si ukandamizaji wala kufinyiliwa chini kwa vyovyote bali ni nafasi yake na ni lazima awajibike iwapo anataka uimarishaji wa ndoa yake.

Nia ya nadharia ya Ufeministi huru ni kuondoa unyanyasaji wa kijinsia hasa kwa mwanamke. Hivyo basi, malengo ya Ufeministi yalijikita katika kumnasua mwanamke kutoka minyororo iliyomfunga katika jamii. Malengo haya yanaleta ukinzani wa maisha halisi ya mwanamke yalivyokusudiwa tangu jadi na tamaduni hasa kwa kurejelea *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu* na matini za dini ambazo ni 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora'.

Miongoni mwa misingi ya kifikra ya Ufeministi huru ni kuwahamasisha na kuwalazimisha wanawake kufanya kazi nje ya nyumba. Wafeministi wanaamini kuwa mwanamke akibaki nyumbani na kutofanya kazi nje ya makaazi yake ndiyo sababu kuu ya dhulma za kisiasa, kijamii na kiuchumi zinazowapata wanawake.

Fikra ya kupinga suala la mwanamke kufanya kazi za nyumbani na wadhifa wake kama mama ni miongoni mwa misingi na nguzo kuu za Ufeministi huru. Wafeministi wanafanya jitihada za kupunguza nafasi ya wanawake na kudhihirisha suala la mama kufanya kazi nyumbani kuwa ni kudunishwa. Kwa msingi huo baadhi ya watafiti wanasisitiza kuwa lengo la nadharia hii ni kuanzisha vita dhidi ya familia. Kutokana na utafiti wetu, familia ni kiungo muhimu katika jamii na taifa kwa jumla na ni lazima

tuitetee kwa vyovyote vile. Wafeministi huru wanaamini kuwa kazi za mama nyumbani hazina thamani yoyote maadamu hazina kipato cha fedha licha ya kwamba zinatayarisha mazingira salama na ya utulivu kwa familia yake. Kwa maoni yetu, mwanamke anapoajiriwa nyumbani kufanya kazi kwa ajili ya kipato si ukandamizaji bali humfanya kudhihirisha sifa za mwanamke katika mazingira ya nyumbani na kwa hivyo atafanya kazi inayoridhisha tofauti na mwanamume anapoajiriwa kufanya kazi ya nyumba.

Beauvoir (1952) anadai kuwa mwanamke yeyote hapaswi kuruhusiwa kubaki nyumbani na kujishughulisha na malezi ya watoto wake. Jamii inapaswa kubadilika kabisa na isiwaruhusu wanawake kulea watoto tu. Kulingana na utafiti wetu, mwanamke ndiye mlezi bora kwa watoto wake na kwa hivyo maelezo haya hatukubaliani nayo kabisa.

Friedan (1963), anabainisha chuki yake kubwa dhidi ya nafasi ya mwanamke nyumbani na anawahamasisha wanawake kujikomboa kutoka kwenye tundu la nyumba zao za familia na kusisitiza kuwa nyumbani si mahala mwafaka kwa wanawake. Inasikitisha kuona kwamba wafeministi wanawalazimisha wanawake kuondoka mahali ambako kwa itikadi za watu wengi ni fursa kubwa zaidi na isiyo na kifani kwa ajili ya kulea na kumstawisha mwanadamu. Kutokana na utafiti huu tunagundua kuwa mwanadamu hawezi kuficha ukweli wa kupambana na fikra na maumbile yake asili katika kipindi kirefu.

Wanafeministi huru wengi hawakuweza kukabiliana na kupigana na hakika ya ndani ya nafsi zao kwa kuwa wao wenyewe pia walikuwa wake na mama watoto. Kwa msingi huo wanaharakati hao wengi katika kipindi cha muda mrefu walifanya jitihada za kutubu na kurekebisha matamshi na mitazamo yao isiyo sahihi. Kwa mfano, Betty

Friedan miaka kadhaa baada ya kitabu chake cha kwanza cha *The Feminine Mystique* alilegeza misimamo yake ya awali aliposema kwamba wanawake wanaweza kuambatanisha kazi za nje na zile za nyumbani, na kuziweza zote. Katika kitabu hicho Friedan anaeleza wasiwasi wake kuhusu mustakbali wa wanawake waliotanguliza mbele mafanikio ya kikazi kuliko kuunda na kuanzisha familia na sasa wamechanganyikiwa na kukosa matumaini, yote haya yamewatia wasiwasi magwiji wa fikra za kifeministi.

Katika utafiti huu, tunagundua kuwa kazi ni sehemu ya maisha na wadhifa mkuu wa mwanamke, ni kulea watoto. Hata hivyo, utamaduni wa kimagharibi umelifanya suala la kufanya kazi nje ya nyumba kuwa la kiasili na la kimsingi, na kazi ya mama ya kulea watoto na familia kuwa ni jambo la pembeni na lisilo la kimsingi. Lengo la nadharia ya Ufeministi huru lilikuwa ni kuondoa unyanyasaji wa kijinsia hasa kwa mwanamke. Hivyo basi, malengo ya Ufeministi huru yalijikita katika kumnasua mwanamke kutoka pingu za kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii. Malengo haya ndiyo yanayoleta ukinzani wa maisha halisi ya mwanamke wa Kiafrika.

Tulifanya uchunguzi wetu kwa kutumia mawazo haya kama kigezo cha kupimia iwapo waandishi wa Methali, Wimbo Ulio Bora, *Utendi wa Ayubu* na *Utendi wa Mwanakupona* wamempa mwanamke nafasi anayostahiki. Kulingana na maandishi haya ya kifasihi na kidini mwelekeo umetolewa kwa wanandoa ambao wangependa unawiri wa ndoa na maisha yao kwa jumla.

Baada ya kutathmini chimbuko la nadharia ya Ufeministi, tapo tulilolitumia katika utafiti huu na mihimili yake muhimu tulibainisha kuwa kuna haja ya kutumia nadharia ya Udenguzi ili kutuelekeza katika ubomozi wa dhana zilizokita mizizi kuhusiana na usawiri wa mwanamke katika ndoa.

### 2.2.5 Nadharia ya Udenguzi

Udenguzi ni nadharia ya uhakiki iliyoanzishwa na mwanafalsafa wa Kifaransa Derrida (1981). Yeye anasema kwamba ujuzi na maarifa si vitu vinavyoweza kueleweka moja kwa moja. Katika matini yoyote ile, ujuzi hutumika katika kuunda matini hiyo, kwa kuwa ujuzi si kitu kinachoweza kueleweka moja kwa moja na husababisha kuonekana kwamba ujuzi na maarifa kuwa ni kitu kisichoshikika, yaani chenye utelezi. Hivyo hata tafsiri ya matini kwa wahakiki haiwezi kuelezwa kwa namna moja, kila mtu ataieleza kwa namna yake. Hii ina maana kwamba maana zinaweza zikaendana au zikapingana.

Kwa hivyo, nadharia ya Udenguzi huzama katika ufafanuzi wa matini na kuyatazama kwa jicho la ndani kwa kuyadengua na kuyabomoa. Nadharia hii inadai kuwa uelewaji wa ndani wa matini unaweza kutupa mwanga kamili kuhusu jamii na kwamba si muhimu tuangalie muktadha wa jamii husika.

Mwamzandi (2013) anabainisha kuwa mbinu kuu na muhimu inayotumiwa na wanaUdenguzi ni ukinzani wa jozi za maneno. Mwamzandi anatueleza kuwa tasnifu ya Derrida kuhusu jozi hizo ni kuwa jamii za Kimagharibi zimejenga upendeleo wa wazi pale neno moja katika jozi husika daima linawakilisha utukufu au kile kinachopaniwa kufikiwa kama kitu adili huku dhana ya pili ya jozi hiyo hiyo ikiangaliwa kama ghushi, isiyo safi na ya daraja la chini. Kwa hivyo, kwa kutumia nadharia ya Udenguzi katika uhakiki wa usawiri wa mwanamke katika ndoa mintarafu *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu, Methali na Wimbo Ulio Bora,* tuliweza kubainisha jozi hizi za maneno na kuzifafanua ili kuweza kupata maana na dhana tofauti na zile za hapo awali au kazi tangulizi.

Schmitz (2007) anaeleza kwamba wanaUdenguzi husisisitiza kufuatilia maana ya maneno kama linavyotarajia zoezi la kidenguzi ili kubainisha kile kisichosemwa na athari yake katika uwanja mzima wa maana. Kulingana na Schmitz, ni kutokana na maneno kwenye matini ambapo tunaweza kufanya Udenguzi ili kupata kwa kweli maana iliyokusudiwa. Ubomozi huu wa kazi hufanyika ili kuweza kupata dhana mpya kabisa kwa wasomaji wa kazi husika.

Carter (2006) anatambua kuwa watu hupania tu kuweka mipaka kati ya vitu vya kufikirika na Udenguzi kwa upande mwingine hutuelekeza tuangalie kwa makini ukinzani unaojitokeza ndani ya matini. Kwa maoni ya Carter, tunaweza kuwa tulisoma kazi fulani na tukajiwekea mipaka na imani kuhusu kazi hiyo bila kufikiria zaidi nje ya kazi hiyo. Lakini kulingana naye, tunaweza kupata maana tofauti ya matini yenyewe na kwa hivyo tukabomoa mipaka na imani tuliyokuwa nayo kuhusiana na kazi husika.

Miller (1976) anasema Udenguzi ni juhudi ya kufikia nguvu na uwezo wa matini kama chombo kinachoweza kujifafanua. Miller anaelezea kuwa matini ni kazi ambayo inaweza kujieleza na kujifafanua kwa mapana. Kwa mfano, *Utendi wa Mwanakupona* na *Utendi wa Ayubu*, zinaposomwa tena, mawazo mapya ambayo hayakuibuliwa awali yanaweza chipuka kwa kuelekezwa na nadharia ya Udenguzi.

Kwa jumla, Udenguzi unachunguza lugha kama chombo cha mawasiliano chenye utata, na uwezo wa kujifafanua, hasa katika maandishi. Ni uchambuzi unaoweka wazi ukinzani wa fasihi na matini nyingine zisizo za kifasihi. Nadharia ya Udenguzi unapinga mgawo mkali wa hali mbili au zaidi zinazokinzana, na kuonyesha uwezekano wa hali kama hizo kuwa pamoja na kuchangiana kimaana. Nadharia hii ilitumika kuhakiki suala la usawiri wa mwanamke katika ndoa mintarafu kazi teule za

fasihi *Utendi wa Mwanakupona* na *Utendi wa Ayubu* na matini za kidini ambazo ni Methali na Wimbo Ulio Bora.

### 2.2.6 Mihimili ya Nadharia ya Udenguzi

Udenguzi au 'ubomozi' unahusishwa na usomaji upya na utazamaji wa kila neno katika matini kwa jicho pekuzi. Usomaji huu umependelewa sana na wadenguzi wanaodai kuwa aghalabu matini za fasihi huzungumzia mambo yasiyodhamiriwa. Hii ni mianya inayostahili kufuatiliwa na msomaji ili aweze kuidengua kikamilifu matini husika. Madhumuni ya nadharia hii ni kujenga maana kwa njia ya kubomoa maana na kujenga mvuto wa kisanaa. Mtu anaweza kujenga maana hata katika mwanya mtupu.

Nadharia hii ilifaa kazi hii kwa kuwa kupitia kazi tangulizi, mengi yamesemwa jinsi mwanamke amekandamizwa katika *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu* na matini za kidini tulizozichagua. Kwa hivyo, tulinuia kupata picha mpya ya mwanamke mkamilifu jinsi alivyokusudiwa tangu hapo jadi kutoka kwa mababu zetu na Mungu Muumba kupitia kwa *Biblia Takatifu*.

Nadharia hii ilifaa katika uchambuzi wa data tulizokusanya kuhusiana na taswira ya mwanamke katika ndoa, uhusiano wa mume na mke katika ndoa na kubainisha dini kama kigezo thabiti cha ndoa. Tulizisoma kazi zetu kwa jicho la ndani ili tuweze kubainisha malengo haya na kumtazama mwanamke kwa mtazamo mpya si wa unyanyasaji bali wa hadhi na heshima ya juu.

Rorty (1996) anabainisha kuwa Udenguzi ni ukiushi wa kaida za matini. Ukiushi huu utokeapo kwa mara ya kwanza huonekana kama ni usaliti, lakini utokeaji wa ukiushi si ajali bali hukusudia kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Maelezo hayo ya Rorty yanatupa picha halisi ya mabadiliko yanayoweza kutokea katika uundaji wa matini.

Mfano, uundaji wa mashairi ya Kiswahili hapo mwanzo ulikuwa ukifuata urari wa vina na mizani lakini baadaye yakaibuka mashairi ya kisasa ambapo wanajadi waliona kuwa ni usaliti wa ushairi wa Kiswahili. Vile vile maelezo hayo yanatupa mwanga wa kuelewa kuwa katika matini Udenguzi utokeapo unakuwa na lengo la kujifafanua zaidi.

Kutokana na maelezo hayo, ndipo Wafula na Njogu (2007) walipodai kuwa katika Udenguzi hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi. Hii ndio inayofanya wahakiki kutoa fasili tofauti tofauti za jambo moja. Fasili hizo zaweza kufanana au kutofautiana. Kwa hiyo Udenguzi unaweza kuboresha matini au kuumba upya kwa lengo la kukidhi upya mahitaji ya jamii. Mwelekeo huu ulitusaidia katika utafiti wetu wa kuchunguza usawiri wa mwanamke katika ndoa kwa kurejelea *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu*, Methali na Wimbo Ulio Bora. Mwanamke katika kazi hizi zote alichukuliwa kuwa amekandamizwa na kunyanyaswa kutokana na kazi tangulizi zilizofanywa, lakini katika utafiti huu, tunafanya ubomozi wa kazi hizi na tunagundua kuwa mwanamke ameheshimiwa mno katika kuyatekeleza majukumu yake kama mke. Taswira ya mwanamke katika ndoa ni chanya na mahusiano yake na mume yanatakikana kuwa ya heshima.

Mohamed (2006) anasema, msomaji wa matini fulani anaweza kimakusudi kupoteza maana kabisa kwa vivuli vya maana. Kwa maoni yetu, nadharia ya Udenguzi ilikuwa ya manufaa mno kuyasoma matini upya na kuirejelea maana iliyokusudiwa na waandishi wa kazi hizo. Mihimili hii ilituongoza katika utafiti wetu wa usawiri wa mwanamke katika *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu* na matini za dini ambapo tulisoma kazi hizi na hakiki zilizotolewa kwa kazi tangulizi kisha kuzidengua kazi hizi kwa kurejelea matokeo tuliyoyapata katika utafiti wetu.

Nadharia ya Udenguzi hulenga kufutilia mbali mipaka katika jozi za maneno kuwa ni mfano wa sarafu moja yenye pande mbili. Udenguzi hubainisha kuwa nuru na kiza ni vitu ambavyo wanafilosofia wa kijadi wangevitenganisha kwa kupendelea nuru kuliko kiza. Kwa wadenguzi, nuru sawasawa na kiza, zimetangamana na huwezi kukielewa kimoja bila kingine. Mihimili hii ilituongoza katika utafiti wetu wa usawiri wa mwanamke katika *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu* na matini za dini. Hatungeweza kumaizi kile tunachokifahamu kama nuru iwapo lugha tunayoitumia haingekuwa imeratibu ndani yake dhana ya kiza.

Udenguzi hushughulikia maneno yanayokinzana na wakati uo huo kubainisha itikadi kuu inayojitokeza na inayostahili kusailiwa upya. Kupitia uchanganuzi makini wa lugha ya matini, wanadenguzi hudhihirisha ukinzani na utepetevu wa matini hizo. Hili ndilo linalowafanya wanaUdenguzi kudai kuwa matini hujiumbua na kujibomoa yenyewe na wala sio wao wanaUdenguzi wanaofanya hivyo. Mihimili hii ilituongoza katika utafiti wetu wa usawiri wa mwanamke katika *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu* na matini za dini kwa sababu ilitubainishia sifa ya azali na iliyomo katika lugha kwani tangu jadi lugha imejengeka kama mfumo wenye ukinzani na unaotofautisha maana. Lugha katika yaliyoandikwa kuhusiana na mada ya utafiti imejengeka kiUdenguzi kwani hubainisha tofauti za kimaana na za kiitikadi. Vile vile katika kufikia lengo letu la tatu la dini kama kigezo thabiti katika ndoa. Kwa kusoma upya maneno haya tunabainisha wazi kuwa Mungu alichukuwa nafasi muhimu katika uimarishaji wa ndoa na uthabiti wake na bila Mungu hatupati raha katika ndoa.

Mawazo haya ya Udenguzi yamefaa kwa kuongoza na kuelekeza kazi zetu za usawiri wa mwanamke katika *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu* na matini za dini kwani ni dhahiri shahiri kuwa watafiti wa awali kuhusu usawiri wa mwanamke

katika ndoa waliegemea sana upande wa kunyanyaswa kwa mwanamke. Lakini sisi tunapinga mawazo haya kwa misingi ya nadharia ya Udenguzi. Tukirejelea *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu* na matini ya kidini ya Wimbo Ulio Bora na Kitabu cha Methali, tunagundua kwamba mwanamke alitekeleza majukumu yake kwa furaha. Aliyatenda haya yote kwa minajili ya kuhakikisha kuwa familia yake inabakia imara na haikuwa njia ya kudhalilisha na kunyanyaswa kama walivyonena waandishi wa awali.

Udenguzi au 'ubomozi' kama unavyorejelewa katika *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu,* matini ya kidini ya Wimbo Ulio Bora na Kitabu cha Methali unahusishwa na usomaji wa kutazama kila neno katika jozi kwa jicho pekuzi. Usomaji huu umependelewa sana na wadenguzi wanaodai kuwa matini za fasihi zina tabia ya kuzungumzia kile kilichodhamiriwa. Hii ni mianya inayostahili kufuatiliwa na msomaji ili aweze kuidengua kikamilifu matini husika. Kwa mfano, katika *Utendi wa Mwanakupona,* mama anamhimiza bintiye awe mtiifu, adumishe usafi na kuzingatia majukumu yake yote katika ndoa. Wosio huu wa mama kwa bintiye ulinuia kumfanya bintiye aishi vyema na mumewe ili ndoa yao idumu. Kwa hivyo mihimili hii ilifaa mno katika utekelezaji wa malengo tuliyojiwekea katika utafiti huu. Nadharia hii ilibainisha wazi taswira ya mwanamke katika ndoa kwa kutupa picha kamili jinsi mwanamume na mwanamke wanavyostahili kuhusiana katika ndoa.

Nadharia ya Udenguzi hushughulikia kwa pamoja jozi ya maneno yanayokinzana na wakati uo huo kubainisha itikadi kuu inayojitokeza na inayostahili kusailiwa upya. Tukirejelea *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu* na matini ya kidini ya Wimbo Ulio Bora na Kitabu cha Methali kwa kupitia uchanganuzi makini wa lugha

ya matini, kazi hizi zinadhihirisha ukinzani na utepetevu wa matini zilizoandikwa na wahakiki mbalimbali.

Hili ndilo linalowafanya wanaoshikilia nadharia ya Udenguzi kudai kuwa matini hujiumbua na kujibomoa yenyewe na wala sio wao wanaUdenguzi wanaofanya hivyo. Wanavyodai, hii ni sifa ya azali na iliyomo katika lugha kwani tangu jadi lugha imejengeka kama mfumo wenye ukinzani na unaotofautisha maana. Lugha yenyewe imejengeka kiUdenguzi kwani hubainisha tofauti zilizomo ndani yake za kimaana na za kiitikadi. Nadharia hii ilifaa kwa kuwa tuliweza kuumba upya kazi zetu teule za fasihi ambazo ni *Utendi wa Mwanakupona* na *Utendi wa Ayubu*, kwa kubainisha taswira chanya katika majukumu yake kwenye ndoa.

Udenguzi ni uhakiki unaokita na kuzingatia matini kama chombo kinachojitosheleza na kinachoweza kufichua maana mbili kwa kurejelea muktadha. Katika utafiti wetu wa usawiri wa mwanamke katika *Utendi wa Mwanakupona*,*Utendi wa Ayubu* na matini ya kidini ya Wimbo Ulio Bora na Kitabu cha Methali tulizingatia lugha na matini. Tulipasua matini mbalimbali katika vipengele vyake vyote ili kuweka wazi kilichofichika kuhusiana na yaliyoandikwa kuhusu *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu* na matini ya kidini ya Wimbo Ulio Bora na Kitabu cha Methali.

Ni nadharia inayotumika sana katika uhakiki wa ushairi wa Kiswahili, hasa tukizingatia muundo wa ushairi na matumizi yake ya lugha kwa namna ya ukinzani. Kwa hivyo nadharia hii ilituongoza katika utafiti kuhusu *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu* na matini ya kidini ya Wimbo Ulio Bora na Kitabu cha Methali. Vipengele vyake muhimu vilifaa mno katika utafiti huu wa kifasihi na kazi za matini ya kidini.

Udenguzi kwa jumla ni mkabala unaolenga katika kuingilia matini kati, kuihakiki ndani kwa kuipeperusha, kuipindapinda, na kuonyesha uwezekano wa kutokuwa na vidato vya vinyume. Lengo la wadenguzi ni kuvunja tofauti za kimaana.

Kwa kutumia nadharia hii ya Udenguzi tumepata mtazamo mpya wa mwanamke katika jamii na uhusiano wake na mwanamume. Hivyo basi wanawake na wanaume hawakinzani bali wanasaidiana. Jambo lililo muhimu ni kwamba usaidizi huo uwe hauna masharti ya kuwakataza uhuru wa kuchagua jinsi na maana sawa aitakayo mhusika awe mwanamume au mwanamke katika kuyaendeleza maisha na kumudu mazingira yake.

**2.3 Hitimisho**

Kutokana na yote tuliyoyapitia ni kuwa kuna mitazamo mbalimbali kuhusu wosia katika *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu,* Wimbo Ulio Bora na Kitabu cha Methali. Wengi wanaonelea kuwa wosia huu ni ukandamizaji na wachache sana wanaona si ukandamizaji. Utafiti wetu ulitaka kuchunguza iwapo wosia utolewao ni ukandamizaji au la.  Kulifikia hili, mihimili ya nadharia za Ufeministi na Udenguzi zilitumika. Kila nadharia ina mhimili mkuu, mfano Ufeministi unachukulia kuwa wanawake wanakandamizwa katika jamii. Udenguzi nao unadai kila andiko au tamko lina maana mbili, ile asili na nyingine ni kinyume cha maana asili. Kwa hivyo, nadharia hizi zilitufaa sana katika utafiti wetu.

Mapitio ya kazi za *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu*, Wimbo Ulio Bora na Kitabu cha Methali, yamebainisha wazi kwamba kazi hizi za kifasihi na matini hizi za kidini zimemsawiri mwanamke kama kiumbe wa thamani na wa majukumu yake mahususi. Nadharia ya Udenguzi ilitusaidia kubomoa na kuunda upya mielekeo mbalimbali inayohusiana na kazi yetu ya usawiri wa mwanamke katika ndoa. Kwa

kusoma upya *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu* na matini za kidini tulizozichagua kwa kazi hii, inabainika wazi kwamba maonevu, unyanyasaji na ukandamamizaji uliodhaniwa kwa muda mrefu kufanyiwa mwanamke yalikuwa ni majukumu yake yaliyokusudiwa tangu jadi. Hizi ni kanuni ambazo lazima zifuatwe kwa minajili ya uthabiti wa ndoa. Hivyo basi wanawake na wanaume hawakinzani bali wanasaidiana. Sura inayofuata imefafanua zaidi kuhusu mbinu na zana za utafiti.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Katika sura ya pili tumeeleza yale yaliyoandikwa kuhusu mada yetu na waandishi wengine na vile vile kuzibainisha nadharia zilizotuongoza katika utafiti huu. Katika sura hii tumeangazia mbinu za utafiti. Tulikusanya data kutoka kwa kazi zetu teule za kifasihi, *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu*, na matini za kidini, 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora'. Jambo lingine ni uchanganuzi wa data iliyokusanywa. Mchakato huu ulizingatia malengo mahususi ya utafiti huu na kuongozwa na nadharia ya Udenguzi na nadharia ya Ufeministi. Data hii ilibainisha usawiri wa mwanamke katika ndoa kutoka kwa kazi teule za fasihi tulizozichagua kimakusudi na matini za kidini.

## 3.1 Eneo la Utafiti

Uchunguzi ulifanywa maktbani ambapo tuliteuwa *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu* na matini za kidini, 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora'. Tulisoma kazi mbalimbali zinazohusu *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu,* na matini za kidini. Pia tulisoma magazeti na kuzuru mtandao kufahamu yaliyoandikwa juu ya tendi hizi na tahakiki mbalimbali. Malengo ya kuchunguza kwa makini na kutathmini kazi hizi za fasihi na za dini ni kubainisha usawiri wa mwanamke katika ndoa na majukumu mahususi ya mwanamke.

## 3.2 Ukusanyaji wa Data

Kwa kurejelea malengo yetu ya kuchunguza taswira katika kazi teule za fasihi na za dini, kutathmini uhusiano wa mwanamume na mwanamke katika ndoa na kubainisha dini kama kigezo muhimu katika uthabiti wa ndoa, tulikusanya data ili tupate picha

kamili ya mwanamke katika ndoa ya zamani na ndoa ya sasa ambapo tulinakili kutoka kwa *Utendi wa Mwanakupona*, vipengele muhimu vinavyoendana na utafiti huu. Pia, tulisoma kwa undani *Utendi wa Ayubu*, tukadondoa yale yote yanayohusu ndoa tukayanakili katika daftari. Vile vile tumerejelea matini ya kidini: Wimbo ulio Bora na Kitabu cha Methali, tukadondoa hoja zote zinazohusiana na usawiri wa mwanamke katika ndoa.

## 3.3 Usampulishaji

Utafiti huu ulikusanya sampuli kutoka kwa *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu* na matini za kidini: Wimbo Ulio Bora na Kitabu cha Methali. Usampulishaji huu ulifanywa kimakusudi kulingana na malengo ya utafiti huu. Tuliteuwa sampuli kutoka kwa kazi tulizokusanya katika *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu*, 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora'. Tuliteuwa sampuli kimakusudi kwa kurejelea mada ya utafiti. Pia, tumezichagua kazi hizi za kifasihi kwa kuwa ndizo zilizozungumzia masuala ya wanawake na dhana kwa wasomaji kuwa mwanamke amenyanyaswa katika kazi hizi.Vile vile waandishi wa kazi hizi za kifasihi waliaminika kuwa walitoka katika dini ya Kiislamu. Tulizichagua matini za kidini kutoka *Biblia Takatifu* kwa kuwa zilichukua imani za Kikristo. Malengo yaliyoongoza utafiti huu ni uchanganuzi wa taswira ya mwanamke katika ndoa, kutathmini uhusiano wa mwanamume na mwanamke katika ndoa, na kubainisha dini kama kigezo muhimu katika ndoa**.** Usampulishaji wa data ulifanywa kwa kuegemea malengo tuliyojiwekea katika utafiti huu.

### 3.3.1 Kuchanganua Taswira ya Mwanamke katika *UWM, UWA, KCM* na *WUB*

Beti mia moja na mbili (102), ziliteuliwa katika *Utendi wa Mwanakupona*. Kati ya beti 102, beti sitini na tano (65) zinazoakisi taswira ya mwanamke katika ndoa. Beti

hizo zimeambatishwa katika kurasa za viambatisho. Uchanganuzi wa *Utendi wa Ayubu* kwa kuzingatia lengo la kwanza la kuchunguza taswira ya mwanamke katika ndoa, tulichagua kimakusudi beti ishirini na saba (27). Beti hizi zilibainisha taswira ya mwanamke katika ndoa hasa kwa kumtumia mwanamke kielelezo, mhusika Rehema. Rehema anachorwa kama mwanamke mvumilivu, mfanyikazi, mnyenyekevu na anayemheshimu mumewe kwa hali zote.

Katika uchanganuzi wa Methali kwa kuzingatia lengo la kwanza la kuchunguza taswira ya mwanamke katika ndoa, tulichagua kimakusudi vifungu thelathini na mbili (32) ambavyo vimeambatishwa katika kurasa za viambatisho. Sura hizi zote zinazungumzia masuala ya wanawake na taswira yao katika ndoa.

Katika uchanganuzi wa Wimbo Ulio Bora kwa kuzingatia lengo la kwanza la kuchunguza taswira ya mwanamke katika ndoa, tumechagua kimakusudi vifungu (15) vilivyoambatishwa katika kurasa za viambatisho. Solomoni katika kazi hii ameyazungumzia masuala ya mwanamke kwa kumsifu na kumpa hadhi ya juu kutokana na uzuri wake na sifa zake za uke. Katika sura hizi anaelezea urembo wa mwanamke na jinsi mwanamke alivyo na thamani ya juu.

### 3.3.2 Kutathmini Uhusiano wa Mwanamke na Mwanamume kama unavyojitokeza katika *UWM, UWA, KCM* na *WUB*

Kwa kurejelea lengo letu la pili la kutathmini uhusiano wa mwanamume na mwanamke, tumechanganua data kutoka kwa UWM, UWA, KCM na WUB. Kutoka *Utendi wa Mwanakupona*, tumeteuwa kimakusudi beti ishirini (20) zilizoafikiana na uhusiano wa mwanamume na mwanamke katika ndoa. Beti hizo zimeambatishwa katika kurasa za viambatisho. Mwanakupona anamshauri bintiye anavyotakiwa kumfanyia bwanake. Miongoni mwa mambo hayo ni kutojibizana naye, kumpa kila

anachokihitaji, kumuaga vizuri kila anapoondoka, kumpokea vizuri kila anaporejea, kumpapasa na kumpepea usiku, kumkanda mwili, kumsifu kwa watu wengine, kumwandalia chakula, kumnyoa ndevu, kumpendeza kila mara, n.k.

Uchanganuzi wa *Utendi wa Ayubu* kama ilivyo lengo la pili kuhusu uhusiano wa mwanamke na mwanamume katika ndoa. Beti thelathini na nne (34) zilichaguliwa kama zilivyo katika viambatisho. Beti hizo zinaainisha uhusiano wa mwanamume na mwanamke katika ndoa, na kwamba mwanamume na mwanamke wanashauriwa wasiwaruhusu watu wa nje kuharibu uhusiano wao.

Katika uchanganuzi wa Methali kwa kuzingatia lengo la pili la kutathmini uhusiano wa mwanamke na mwanamume katika ndoa, vifungu arobaini na nne (44) viliteuliwa ambavyo vimeambatishwa katika kurasa za viambatisho. Sura hizi zilibainisha wazi uhusiano wa mwanamume na mwanamke katika ndoa, na Solomoni anasisitiza kuwa mwanamke ni lazima awe mtiifu na mwenye kumheshimu mumewe.

Tulichanganua Wimbo Ulio Bora kwa kurejelea lengo la kutathmini uhusiano wa mwanamume na mwanamke katika ndoa. Tulivichagua vifungu thelathini na saba (37) ambavyo vimeambatishwa katika kurasa za viambatisho. Solomoni anabainisha waziwazi mahusiano kati ya mwanamume na mwanamke katika ndoa kwa kuieleza nafasi ya mume na mke katika uhusiano wao.

### 3.3.3 Kubainisha Wosia kutoka Dini kama kigezo muhimu katika Uthabiti wa Ndoa

Katika *Utendi wa Mwanakupona*, tulizingatia lengo la tatu la kubainisha wosia kutoka dini kama kigezo muhimu katika uthabiti wa ndoa kwa kuteuwa beti kumi na tano (15) ambazo zimeambatishwa katika kurasa za viambatisho. Beti hizi zimebainisha

dini kama kigezo muhimu katika uthabiti wa ndoa. Zinaelezea wosia wa kumheshimu Mungu, kuwa mwaminifu, kuepuka umbeya, kushika dini kwa dhati n.k.

Katika *Utendi wa Ayubu,* tumezingatia lengo la tatu la kubainisha wosia kutoka dini kama kigezo muhimu katika uthabiti wa ndoa kwa kuteuwa beti kumi na nne (14) ambazo zimeambatishwa katika sehemu ya viambatisho. *Utendi wa Ayubu* unadhihirisha kupitia beti hizi kuwa Mungu ni mwanzilishi wa ndoa na kuwa wanandoa wanatakikana kumtii Mungu kwa kuwa kuna maisha baada ya haya ya ulimwengu.

Tumechanganua Methali kwa kuegemea lengo hili la tatu la dini kama kigezo muhimu katika ndoa. Vifungu saba (7) tulivyovichanganua vimeambatishwa katika sehemu ya viambatisho ambapo Solomoni anabainisha kuwa ni Mungu anayewasaidia wanandoa kudumu pamoja kwenye uhusiano wao.

Kazi teule za *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu,* Methali na Wimbo Ulio Bora zilitusaidia kupata usawiri wa mwanamke katika kazi hizi za zamani na tofauti zilizopo katika usawiri wa mwanamke wa karne ya ishirini na moja.

### 3.4 Vifaa vya Utafiti

Vifaa vilivyotumika katika utafiti huu ni tarakilishi, kalamu na vitabu ili kurekodia data iliyopatikana maktabani. Kwa kutumia vifaa hivi, data iliyozalishwa iliorodheshwa na kuwekwa katika vikundi kisha kunakili ruwaza iliyojitokeza ili kukimu mahitaji ya malengo ya utafiti.

### 3.5 Uchanganuzi wa Data

Data imechanganuliwa kwa mizani ya malengo yetu ya kuchunguza taswira ya mwanamke katika jamii, ya kutathmini uhusiano wa mwanamume na mwanamke

katika ndoa na kubainisha dini kama kigezo muhimu katika uthabiti wa ndoa ya leo. Tumechanganua data iliyokusanywa inavyoafikiana na lengo kuu la utafiti la kuchunguza taswira ya mwanamke katika jamii katika *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu*, 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora'. Vile vile tulitathmini uhusiano wa mwanamume na mwanamke katika ndoa kwa kuangazia *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu,* na kazi teule za Mfalme Solomoni katika *Biblia Takatifu.*

Tumechunguza beti mbalimbali kutoka *Utendi wa Mwanakupona*, tukazilinganisha na beti katika *Utendi wa Ayubu* kuangalia iwapo maoni yanafanana au la. Yale yaliyofanana tuliangalia ni kwa asilimia (%) gani. Kisha tukavilinganisha vipengele vyote vilivyojitokeza katika *Utendi wa wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu* na matini za kidini ambazo ni Methali na Wimbo Ulio Bora. Tukaangalia ni kwa asilimia (%) ngapi zinaoana na asilimia (%) ngapi hazioani. Uchunguzi huu ulibainisha iwapo maoni haya kutoka UWM, UWA, WUB na KCM ni sawa au yanatofautiana katika usawiri wa mwanamke katika taasisi ya ndoa. Tumebaini kuwa asilimia kubwa (70%) ya beti hizi zinabeba wosia uliokaribiana katika kubainisha majukumu ya mwanamke na mwanamume katika asasi ya ndoa. Haya yote tumeyatekeleza kwa msingi wa malengo yetu matatu kama yafuatavyo: Uchunguzi wa taswira ya mwanamke katika ndoa, kutathmini uhusiano wa mwanamke na mwanamume katika ndoa na kubainisha dini kama msingi thabiti wa ndoa. Baada ya kuzilinganisha, tukaeleza maoni yaliyomo na maoni yetu juu ya usawiri wa mwanamke katika ndoa tukizingatia tuliyoyapata katika data yetu.

Data iliyokusanywa kutoka maktabani ilichanganuliwa kwa kutumia takwimu fafanuzi. Festinger (2005) anabainisha kuwa uchanganuzi kifafanuzi ni aina ya

ufafanuzi ulio rahisi kuwasilisha matokeo kwa watafiti wengi bila kutatanisha data kutoka kwa sampuli iliyotumika. Kwa hivyo uchanganuzi kifafanuzi ulifaa utafiti huu kwa kuwa ulijumuisha maelezo ya uchanganuzi na uchambuzi wa hali ilivyokuwa wakati wa utafiti na kuyawasilisha matokeo ya utafiti kwa njia mwafaka.

### 3.6 Hitimisho

Tumejadili mbinu za utafiti zilizozingatiwa, ukusanyaji wa data wenyewe, na uchanganuzi wa data iliyokusanywa. Tulikusanya data kutoka kwa kazi zetu teule za kifasihi ambazo ni *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu*, kisha matini za kidini ambazo ni Methali na Wimbo Ulio Bora. Data kutoka kwa matini za kifasihi na kidini, ilitusaidia kufikia uamuzi wetu wa utafiti katika sura za Nne, Tano na Sita. Katika sura ya nne, mengi yataelezwa yanayohusiana na lengo la kwanza la utafiti huu la kuchunguza taswira ya mwanamke katika ndoa.

# SURA YA NNE

# TASWIRA YA MWANAMKE KATIKA NDOA

## 4.0 Utangulizi

Sura ya tatu ilihusu ukusanyaji wa data kutoka matini za kifasihi na matini za kidini. Jambo lingine lililoangaziwa ni uchanganuzi wa data iliyokusanywa. Katika sura hii, tumechunguza taswira ya mwanamke katika ndoa. Hivyo basi tumeangazia lengo la kwanza katika utafiti ambapo tumechanganua taswira ya mwanamke katika *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu,* 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora'. Pia, tumefafanua kwa ufupi historia ya UWM, UWA, KCM na WUB.

## *4.1 Historia fupi kuhusu* Utendi wa Mwanakupona *(UWM),* Utendi wa Ayubu *(UWA), Kitabu cha Methali (KCM) na Wimbo Ulio Bora (WUB)*

### 4.1.1 Historia Fupi ya *Utendi wa Mwanakupona*

Mulokozi (1999) anatueleza kuwa Mwanakupona binti Mshamu Nabhany alizaliwa Pate mwaka 1810. Mwaka wa 1836, aliolewa na Bwana Mohammed Is-Haq bin Mbarak. Lakini inasemekana kuwa alijulikana zaidi kwa jina la Mataka. Mwanakupona aliolewa na Bwana Mataka katika ndoa ya wake wengine watatu. Mataka alikuwa ni mtawala wa Siu na mpinzani mkubwa wa utawala wa Waarabu huko Zanzibar.

Mwanakupona alijaliwa wana wawili na Bwana Mataka, mke na mume, ambao ni Mwana Hashimu bint Shee Mataka (1841-1933) na ndiye alitungiwa utenzi huu, na Mohammed bin Shee Mataka aliyezaliwa baina ya mwaka 1856 na 1858. Kwa hivyo, Utendi huu umemchora mwanamke kwa njia ya kipekee na kuonyesha taswira ya mwanamke iliyo tofauti sana na ya mwanamume katika ndoa. Nafasi ambayo

Mwanakupona anapendekeza iwapo mwanamke atawajibikia vilivyo, ataweza kufurahia ndoa na kuepuka mikwaruzo na ugomvi kutoka kwa mumewe. Kwa muhtasari, utendi huu hutoa mafunzo kuhusu mambo ya ndoa, yaani namna mwanamke anaweza kuishi na mumewe, mavyaa, mawifi na maisha kwa jumla. Mtunzi anamwonya binti yake juu ya mambo kadhaa ya kiutamaduni kama vile; adabu na heshima, kuepuka umbeya, kuepuka fitina, kuepuka uchoyo n.k.

### 4.1.2 Historia Fupi ya *Utendi wa Ayubu*

Werner (1971) anasema kuwa mwandishi wa *Utendi wa Ayubu* alikuwa ni Shehe maarufu aliyeuandika Utendi huu kabla ya mwaka 1723. Utendi huu, unamhusu Mtume mwaminifu wa Mungu aitwaye Ayubu aliyebarikiwa na mali nyingi sana. Alikuwa mcha Mungu na aliyeimarika kwa imani yake. Kutokana na imani hii na baraka nyingi alizokuwa nazo, shetani anamwonea wivu. Shetani anamwomba Mungu ruhusa ili aweze kumjaribu Ayubu. Aliporuhusiwa na Mungu, shetani anamfilisi na kumdhuru kiafya lakini Ayubu anasimama imara katika imani yake na wala hakumkana Mungu.

Ayubu anatengwa na jamii nzima na hata kupelekwa mwituni kwa sababu ya ukoma lakini mkewe anasimama pamoja naye. Katika majaribu hayo, mkewe Rehema anapata ushawishi mwingi kutoka kwa shetani ili amtoroke mumewe lakini anakataa. Mateso haya ya shetani dhidi ya Ayubu na familia yake yanamwathiri sana Rehema ambaye anafanya uamuzi wa kuziuza nywele zake kisha kuzitumia pesa alizozipata kununua chakula cha kumlisha mumewe. Taswira hii ya mwanamke ni ya kujitoa kwa vyovyote alivyonavyo. Kwa maoni yangu kama mwanamke, wanawake wengi huthamini nywele zao sana, na iwapo yeyote ataamua kuziuza nywele hizo kwa ajili

ya mume wake, itakuwa ni ishara tosha kwamba mwanamke huyu amejitolea kwa moyo wote kumpenda mumewe.

### 4.1.3 Maelezo Mafupi Kuhusu Methali na Wimbo Ulio Bora

Solomoni alikuwa mwana wa Daudi aliyechaguliwa na babake awe mfalme wa Wayahudi. Ufalme wake ulitazamwa na Wayahudi kuwa na ustawi usio na mfano, kutokana na hekima yake na amani iliyotawala katika wakati wake. Ufalme wake ulistawi kuliko ule wa baba yake kutokana na msingi imara aliouweka. Kutokana na hekima yake, aliviandika vitabu vingi mno, miongoni mwavyo ni Methali na Wimbo Ulio Bora.  Katika matini hizi za kidini alizoziandika Solomoni, anatumia dini kama kigezo muhimu cha kudumisha ndoa.

Katika Methali na Wimbo Ulio Bora, mwanamke huthaminiwa, huheshimiwa, na kuaminiwa na mumewe kwa sababu ya kukubali kuwa mke na kutimiza wajibu wake. Solomoni hamkandamizi mwanamke wala kumwona kuwa wa hali ya chini bali anadhihirisha hulka za mwanamke zinazomfanya kuwa spesheli miongoni mwa binadamu. Solomoni anasema kuwa mwanamke mwema ni mfanyakazi mwenye bidii na ambaye hufanya biashara ya kuuza na kununua mashamba. Mwanamke hutengeneza mavazi na kuyauza. Pia mwanamke ni mwenye nguvu na bidii katika utendaji wake.

Isitoshe, maneno yake ya hekima na fadhili zake zenye upendo zinathaminiwa sana. Kwa sababu hiyo, yeye huheshimiwa sana na mume wake, wana wake, na jamii kwa jumla. Mawazo haya yanaoana na yale ya *Utendi wa Mwanakupona na Utendi wa Ayubu* ambapo sawia na ‘Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora’, mwanamke huchukua nafasi muhimu zaidi katika jamii. Kutokana na kazi hizi, mwanamke ni

ngao, ni msimamizi, ni mlezi, ni mfanyakazi, ni mshauri, hutegemewa miongoni mwa sifa zingine.

Baada ya kupitia historia fupi kuhusiana na UWM, UWA, KCM na WUB, tunaeleza kuwa taswira ni mkusanyiko wa picha anazozipata msomaji au msikilizaji wa kazi fulani ya kifasihi (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu, 2002*). Taswira ya mwanamke katika ndoa inajidhihirisha katika kazi zetu teule za kifasihi ambazo ni *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu* na matini za kidini tulizozichagua ambazo ni 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora' katika *Biblia*. Katika uainishaji wa kazi hizi, tunampata mwanamke aliyechorwa kama mrembo, mpenda amani, mfanyi kazi, mwema, mlezi, mtiifu, asiyenung'unika, aliye na tabia nzuri, mvumilivu, mkakamavu, jasiri huku akinyenyekea kwa heshima, jambo ambalo ni kinyume na mawazo ya Wafeministi kama vile Beauvoir (1952), Ogundipe (1994), Eagleton (1991) wanaodai kuwa mwanamke anapozingatia hulka hizi atakuwa anakandamizwa, anaonewa na kudhalilishwa katika jamii husika. Wanawachora wanawake katika hali hii ya unyenyekevu na utiifu kama watumishi wasioweza kuamua lolote kuhusiana na maisha yao. Basi tutajadili kila mojawapo ya sifa hizi kwa msingi wa data tulizokusanya kutoka UWM, UWA, KCM na WUB.

**4.2 Taswira ya urembo wa Mwanamke katika Ndoa**

Katika sehemu hii, tumebainisha hali ya mwanamke jinsi anavyodhihirishwa katika jamii yake. Ndoa njema hujengwa na mwanamke jinsi inavyojidhihirisha katika *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu,* 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora'. Mwanamke katika kazi hizi za kifasihi na matini za kidini tulizozichagua amechorwa kama mrembo na kuwa ni ua zuri la kutamanika. Mwanamke ametengewa nafasi yake teule tofauti na mwanamume. Al Farsy (1942: 6) katika dini ya Kiislamu

analijibu swali la Bwana Maaqil bin Yasar, “Mwanamke gani bora kumwoa?” Anasema, “Ambaye mume atafurahi akimtazama kila siku”. Kutokana na jibu hili, mwanamke anatarajiwa kuwa mrembo na wa kuvutia, awe tayari kujirembesha na kufanya hivi zaidi kwa mumewe. Katika kipengele hiki, tutazungumzia taswira ya mwanamke mrembo katika UWM, UWA, WUB na KCM.

### 4.2.1 Taswira ya urembo wa Mwanamke katika UWM

Mwanamke katika *Utendi wa Mwanakupona* amedhihirishwa kwa njia spesheli, na ni jukumu la kila mwanamke kujirembesha kwa ajili ya mumewe. Kwa mfano:

**MF 1**

Na kowa na kuisinga,
Na nyee zako kufunga,
Na yasimini kutunga,
Na firashani kutiya
(UWM ubeti 38)

Kutokana na maelezo tunayoyasoma katika MF 1, tunaelezwa kwamba mwanamke anapaswa kuwa safi wakati wowote, aweze kukoga na kujipaka manukato kwa ajili ya kumfurahisha mumewe. Tunasoma: ***Na kowa na kuisinga.*** Jukumu la mwanamke ni kuhakikisha kuwa amejirembesha na kujizatiti kubaki wa kuvutia kwa ajili ya mume wake. Urembo huu, humwezesha mwanamume kutaka kukaa karibu na mke wake. Mwanamke vile vile aweze kusuka nywele zake kwa ajili ya urembo na njia mojawapo ya kumvutia mumewe. Tunaelezwa kuwa: ***Na nyee zako kufunga.***

Kwa mujibu wa Mwanakupona, mwanamke anastahili kusuka nywele zake na kuzirembesha ili aonekane kama mwanamke aliyewajibika katika nafasi yake. Mwanamke vile vile anahimizwa kufunga maua pamoja na kuyaanika kitandani. Tunaelezwa kuwa: ***Na firashani kutiya***. Iwapo mwanamume hatafurahia kitanda

chake anaweza kukosa kutekeleza majukumu yake kama mume. Mwanamke anatekeleza haya kwa ajili ya mumewe ili mume afurahikie mandhari ya chumbani, hususan kitandani. Uswahilini, kitandani huwekwa maua (mara nyingi ya asumini) ili kunukia harufu nzuri. Mume avutike. Asisikie harufu mbaya. Mwanamke anahimizwa kujiwasilisha kwa njia bora na ya kuvutia mumewe. Mwanakupona anaendelea kumhimiza bintiye ajiwasilishe kwa jamii kwa njia ya kipekee inavyodhihirika katika MF 2 hapa chini:

**MF 2**

Nawe ipambe libasi,
Ukae kama ‘arusi,
Maguu tia kugesi,
Na mikononi makowa
(UWM ubeti 39)

Katika MF 2 hapo juu, mwanamke anahimizwa kujirembesha na kuhakikisha mavazi yake yanapendeza ili aweze kubaki kama bibi arusi kwa unadhifu na urembo wake wa kipekee: ***Ukae kama arusi.*** Mwanamke akae kama bibi arusi daima. Jukumu la mwanamke ni kuwa aonyeshe urembo huu kila mara ili mumewe ajivunie na kufurahia kuwa alimpata na kumwoa mke huyo. Anapofanya hivi, katu mume hatampuuzilia mbali bali atazidi kumpenda.

Mwanakupona anamhimiza mwanawe kuwa avae bangili kwenye miguu yake na herini na kila aina ya mapambo kwenye mwili wake: ***Maguu tia kugesi, Na mikononi makowa.*** Taswira inayobainika hapa, ni mwanamke aliyetumia muda wake kwa ajili ya upodozi na kuhakikisha kuwa anaonekana kama bibi arusi. Mwanamke kwenye ndoa anafaa kuishi maisha ya kujinadhifisha na kuyaelewa majukumu ya kimsingi katika ndoa yake, la sivyo, mumewe atashawishika kuwa na jicho la pembeni. Mwanakupona anaendelea kutoa wosia kwa mwanamke anavyotakiwa

kujiwasilisha katika ndoa. Maelezo hayo tunayapata katika MF3 kama tunavyosoma hapa chini.

**MF 3**

Pete sikose zandano
Hina sikome nyaani
Wanda siwate matoni
Na nshini kuitiya
(UWM ubeti 41)

Mwanakupona anaendelea kutoa wosia kuhusu mapambo ya mwili kuwa bintiye asivue pete: ***Pete sikose zandano,*** wala kukoma kujipaka hina kwenye kucha zake: ***Hina sikome nyaani***. Hali hii inaonyesha unadhifu na urembo wa mwanamke. Mwanamke anahimizwa kujipaka wanja kwenye kope zake: ***Wanda siwate matoni,*** ili adhihirishe ile sura nzuri ya mwanamke.

Mwanakupona anaamini bintiye asipojikwatua vilivyo, hadhi yake itashuka na kuwepo uwezekano wa kutowashawishi watakao mposa, na kuwa fedheha kwa wavyele wake. Mke mrembo alithaminiwa na mume wake hasa katika sherehe na tamaduni zinapofanywa katika ukoo na kijiji kwa jumla. Wanaume watampongeza mwanamume mwenzao ambaye mke wake ataonekana kuwavutia wengi.

### 4.2.2 Taswira ya urembo wa mwanamke katika UWA

Katika *Utendi wa Ayubu* tunapata taswira ya wanawake warembo: mkewe Ayubu pamoja na wasichana wake jinsi inavyodhihirika katika MF 4 hapa chini:

**MF 4**

Na watatu wanawake
Wenye nuru taambake
Jumla zijana zake
Ashara metimilia
(UWA ubeti 25)

Wasichana wa Ayubu walikuwa na nuru kama ya taa, kumaanisha kuwa wasichana hawa walipendeza na kuvutia macho ya waliowatazama. Rehema mkewe Ayubu vile vile alipendeza mno, licha ya changamoto alizozipitia. Ibilisi anamwuliza, ***U wapi uzuri wake aliopewa na Mwenyezi Mungu?*** Haya yanajidhihirisha katika ubeti wa 160:

**MF 5**

U wapi uzuri wako
Walopewa na Jabali
Uso umetahayari
Kamwe sikukutambua
(UWA 160)

Aya hii inaonyesha wazi kuwa Rehema alikuwa mrembo: ***U wapi uzuri wako? Walopewa na Jabali.*** Rehema pia alikuwa na mazoea ya kujirembesha ila matatizo yalikuwa yamemkumba mno hivi kwamba ibilisi hangemtambua kamwe: ***Uso umetahayari, kamwe sikukutambua.*** Haya yanajidhihirisha katika aya mbili zifuatazo:

**MF 6**

Hela upeo ni wewe
Na mwekevu ni kamawe
Hoyo kukuoa uwe
Ni aibu kusikia
(UWA ubeti 167)

**MF 7**

Mzuri mke huramu
Mwema mwenye tabasamu
Kutwaa mwenye juzamu
Ni aibu kusikiwa
(UWA ubeti 168)

Rehema alikuwa mwanamke wa kupendeza sana na pia mwelekevu: ***Hela upeo ni wewe, na mwekevu ni kamawe,*** kwa hivyo kulingana na ibilisi kuolewa na Ayubu

mwenye ukoma ni kama aibu na kwamba alikuwa anapoteza uzuri wake: ***Hoyo kukuoa uwe ni aibu kusikia.*** Rehema hakushawishika na shetani kwa kuwa aliendelea kumpenda Ayubu kwa dhati. Shetani anaendelea kumshawishi kuwa Rehema alikuwa mke mzuri na mwungwana mwenye tabasamu njema: ***Mzuri mke huramu, mwema mwenye tabasamu,*** na hivyo hafai kuridhika kuolewa na mume mwenye ukoma ni fedheha isiyohitajika, ***Kutwaa mwenye juzamu, ni aibu kusikiwa.***

Katika ubeti wa 172, tunaelezwa Rehema mwenye nasaba njema akaondoka kwa ghadhabu na alipomfikia Ayubu, akamsalimu.

**MF 8**

Rehema mwenye nasabu
Akenenda kwa ghadhabu
Akifika kwa Ayubu
Salamu akatongoa
(UWA ubeti wa 172)

Katika ubeti wa 172, tumepewa taswira ya mwanamke mwenye nasabu njema ambaye anapigania maisha ya mume wake aliyekuwa mgonjwa mahututi. Japo mwanamke huyu alikuwa salama na mrembo wa maumbile: ***Rehema mwenye nasaba***, lakini anaamua kujidunisha kuzunguka huku na kule akimtafutia mumewe chakula. Rehema alidhihirisha hali yake ya urembo kwa jinsi alivyojipamba katika ubeti wa 187:

**MF 9**

Nyee sura zikeeo
Mikili ilingeneo
Yali ikikoma nyao
Yalipokifumuliwa
(UWA ubeti wa 187)

Ubeti huu unadhihirisha urembo wake Rehema, shungi zake za nywele ziling’aa na zilipofumuliwa zilifika chini kwenye unyayo: ***Yali ikikoma nyao, yalipokifumuliwa.***

Wanawake wengi wangependa wawe na nywele kama za Rehema lakini hawataweza kuzitunza ndiposa tunaambiwa katika ubeti wa 198 kuwa Rehema achanapo nywele zake na kufunga mashungi, hung'aa kupita wanawake wote.

#### 4.2.3 Taswira ya urembo wa mwanamke katika WUB

Katika Wimbo Ulio Bora, nafasi ya mwanamke katika ndoa imefafanuliwa. Ameonyeshwa jinsi anavyotakikana kukaa katika ndoa ili kufanikisha maisha katika ndoa. Ndoa hutoa huduma ya hifadhi kwa kila mtu anayeishi kwani humfanya mtu kupata mwenzi wa maisha ambaye anaweza kushirikiana naye katika furaha na huzuni. Ndoa pia humtimizia mtu matamanio ya kawaida ya kijinsia. Kwa njia ya ndoa, binadamu wanaendelea kuzaana. Watoto ni matokeo ya ndoa na ni kipengele muhimu katika kuimarisha misingi ya familia na hali kadhalika kama chanzo cha furaha kwa wazazi wao. Katika Wimbo Ulio Bora, mwanamke amesawiriwa kwa njia hiyo hiyo kama tunavyosoma katika MF 10 hapa chini:

**MF 10**

> Mpenzi wangu, nimekulinganisha, Na farasi katika magari ya Farao. Mashavu yako ni mazuri kwa mashada, Shingo yako kwa mikufu ya vito.
> (WUB 1:9-10)

Kulingana na MF 10, Mfalme Solomoni anamsifu mwanamke kwa maumbile yake kwa kumlinganisha na farasi katika magari ya Farao: ***Mpenzi wangu, nimekulinganisha na farasi katika magari ya Farao.*** Anamlinganisha na Farao kwa kuwa alijulikana kwa utajiri na umiliki wa vitu vya kifahari na farasi wake alipambwa vyema daima kudhihirisha ufahari. Mwanamke amepewa nafasi ya kutamanika katika jamii jinsi alivyoumbwa na Maulana. Solomoni ameonyesha kuwa licha ya

majukumu ya mwanamke kwenye ndoa, yeye (mwanamke) ameheshimika na kupewa jukwaa la kudhihirisha hulka zake.

Mwanamke aliumbwa na Maulana akaumbika, mashavu yake yanapendeza na mashavu haya yanamfanya tofauti na mwanamume: ***Mashavu yako ni mazuri kwa mashada.*** Shingo yake vile vile inavutia anapoirembesha kwa mikufu, ***Shingo yako kwa mikufu ya vito.*** Kutokana na uchanganuzi huu, mwanamke amechorwa kwa njia ya kipekee na hii inamfanya kuwa na majukumu mahususi katika jamii. Nafasi hii, imetupa taswira ya mwanamke mrembo anayevutia kwa maumbile yake. Vile vile Solomoni anaendelea kutaja katika kifungu kifuatacho:

**MF 11**

> Mpendwa wangu ni kama kishada cha hina,
> Katika mizabibu huko Engedi.
> (WUB 1:14)

Tunaposoma MF 11 tunapata kwamba Solomoni kama *Utendi wa Mwanakupona* katika ubeti wa 41, anamchora mwanamke aliyerembeka katika maumbile yake na anamhimiza kuendelea kutumia mapambo kwa sababu anapendeza sana. Solomoni anasema kuwa mwanamke ni kama hina, matawi mazuri kwenye mizabibu yanayomfanya mrembo na wa kutamanika: ***Mpendwa wangu ni kama kishada cha hina.***

Mwanamke anahakikishiwa na kukumbushwa jinsi alivyo mzuri, wa kupendeza na kwamba macho yake yanavutia mno. Hii ni sifa mojawapo ya sifa za mwanamke na kuwa anastahili ajithamini na asijidharau wala kumruhusu yeyote kumkandamiza kwa kumwona kama kiumbe asiyefaa. Solomoni katika *Biblia Takatifu* alitajika kwa sifa

za hekima alizopewa na Mwenyezi Mungu, kwa hivyo maneno yake yaliyomhusu mwanamke yalitokana na mtazamo wa Mungu kwa kiumbe mwanamke.

Mwanamke analinganishwa na uzuri wa maua ambapo unapoyaona huna budi kupendezwa nayo. Katika mkabala huo tunaweza kudai kwamba mwanamke mrembo aliyejipaka marashi ananukia vizuri kama maua yaliyochanua maua yake. Maelezo haya yanaendelezwa katika WUB kama tunavyosoma katika MF12:

**MF 12**

> Tazama, u mzuri, mpenzi wangu,
> U mzuri, macho yako ni kama ya hua.
> (WUB 1:15)

Kulingana na Solomoni katika MF 12 hapo juu, mwanamke ameumbwa kupendeza macho: ***Tazama, u mzuri, mpenzi wangu***. Kwa hivyo tabia ya mwanamke na umbo lake latakikana kuvutia kwa kuwa ni maumbile yake. Anaelezea jinsi macho ya mwanamke yanavyovutia kutazamwa: ***macho yako ni kama ya hua***, kumaanisha kuwa macho ya mwanamke yanapendeza kama ya ndege aitwaye ninga au njiwa. Kwa hivyo hana sababu za kujidharau kwani Mwenyezi Mungu alimwuumba kwa njia spesheli ya kuwavutia viumbe wengine. Taswira hii ya urembo wa mwanamke katika ndoa, humpatia nafasi bora ya kumvutia mumewe na kuhakikisha kuwa ndoa yao inadumu.

### 4.2.4 Taswira ya urembo wa mwanamke katika KCM

Solomoni katika Kitabu cha Methali amemchora mwanamke mkamilifu na aliyewajibika katika sura alizomzungumzia. Kwa mfano katika sura ya 31:22

**MF 13**

> Hujifanyia mazulia ya urembo
> Mavazi yake ni kitani safi na urujuani
> (KCM 31:22)

Solomoni anamchora mwanamke mrembo ambaye anajifanyia mazulia yanayoongeza urembo nyumbani kwake: ***Hujifanyia mazulia ya urembo***. Mwanamke huyu ni mwenye bidii ambaye anafanya kazi kwa mikono yake ili kupata mavazi yaliyorembeka na safi ya kuvutia: ***Mavazi yake ni kitani safi na urujuani***. Mwanamke huyu huvisha jamii yake mavazi na mume wake anapotembea na wazee wenzake husifiwa kwa kumpata mke mwema anayemjali kwa kumvisha vyema. Tofauti na wanawake wengi wa sasa ambao wanajishughulikia wenyewe bila kuwajali waume zao na jamii kwa jumla. Solomoni anatufunza kuwa mwanamke anatakikana kuwa mrembo na kuhakikisha kuwa familia yake inapendeza siku zote.

### 4.3 Taswira ya Mwanamke Mpenda Amani

Kama ilivyokuwa katika hoja ya kwanza ya mwanamke kuwa mrembo katika ndoa, ndivyo inajitokeza katika kipengele hiki ambapo mwanamke anadhihirisha kuwa ni mpenda amani. Hii ni taswira inayomfanya mwanamke kuelewana na wanajamii na hasa mume wake katika udumishaji wa ndoa. Dini ya Kikristo inasheheni mwanamke mpenda amani na ambaye hujenga nyumba yake kwa maneno yake mazuri. Kwa mfano Methali 14: 1, Solomoni anasema kuwa kila mwanamke aliye na hekima hujenga nyumba yake mwenyewe, bali aliye mpumbavu huibomoa kwa mikono yake mwenyewe. Katika mfano huu, mwanamke akipenda kushirikiana na jamii yake vizuri ataweza kudumisha ndoa yake. Mwanamke anahimizwa kupenda amani ili aweze kufurahia maisha yake ya ndoa. Mawazo haya yanadhihirishwa na Al Farsy anaposema, 'Na pindi mwanamke akihisi kuwa mumewe hana shughuli naye na kumpuuza, hapana lingine la kufanya ila kupatana. Na kupatana ndiyo bora kuliko kugombana'. Mwanamke hapa amechorwa kama mpenda amani ambaye wakati kuna migogoro nyumbani, ni sharti ajifunze kuomba msamaha na kubaki wakiishi kwa amani.

Katika sehemu hii, tutachunguza sifa ya mwanamke mpenda amani kwa kuzingatia vifungu vya data inayotokana na kazi za kifasihi (UWA, UWM) na pia maandishi ya kidini (KCM na WUB).

### 4.3.1 Taswira ya Mwanamke Mpenda Amani katika UWM

Katika *Utendi Wa Mwanakupona*, mwanamke amehimizwa awe mpenda amani. Mwanakupona anaeleza kuhusu mwanamke mpenda amani katika MF 14 hapa chini:

**MF 14**

Mama sinoe ulimi,
Nioleza wako umi,
Naliowa nyaka kumi,
Tusitete siku moya
( UWM ubeti 51)

Katika ubeti huu, mama anamwambia bintiye achunge ulimi wake ndiposa ndoa yake idumu: ***nioleza wako ulimi.*** Mwanamke anashauriwa kuwa mwangalifu sana jinsi anavyotumia ulimi wake hasa katika mawasiliano yake na mumewe: ***Mama sinoe ulimi***. Anampa mfano wake mwenyewe kuwa amekuwa katika ndoa kwa muda wa miaka kumi lakini hakuwahi kufanya ugomvi wowote na mumewe: ***naliowa nyaka kumi, tusitete siku moya***. Kisa na maana, aliuchunga ulimi wake daima. Ulimi ndio chanzo cha maovu katika ndoa.

Mwanamke anapaswa kutumia ulimi wake vizuri, yaani awe na maneno matamu ili adumishe ndoa yake. Kwa mfano, mume wake anapomwonya anapaswa kunyama na kumsikiza kwa makini, wala asimjibu wakati huo bali anaweza kufanya hivyo wakati mumewe atakapokuwa na furaha. Katika KCM na UWM mwanamke anashauriwa aepukane na ugomvi nyumbani ili kuidhibiti ndoa yake. Kwa upande mwingine, wanaume wanapoelezwa mambo mema kwa lengo la kujenga familia zao wanapaswa

kuyapokea vizuri bila mabishano. Mwanakupona anaendelea kumwelekeza bintiye kutumia ulimi wake kusema mema bali si maovu kama tunavyosoma katika MF 15:

**MF 15**

Pili uwa na adabu,
Na ulimi wa thawabu,
Uwe kitu mahabubu,
Kulla utakapongiya
( UWM ubeti 13)

Katika ubeti MF15 mwanamke anahimizwa awe na adabu na heshima kwa mumewe. Tunasoma kwamba: ***Uwa na adabu***, na ayateue maneno yake kwa uangalifu na kwa kuzingatia hekima ya juu ili asije akamkosea mumewe kwa vyovyote vile: ***Na ulimi wa thawabu***. Ushauri huu unatolewa kwa mwanamke anayeipenda na kuiheshimu ndoa yake. Yaani mwanamke ambaye anastahili katika familia.

Mwandishi wa utenzi huu anatoa ushauri kwa wanawake wote wa dini ya Kiislamu kuipa ndoa zao kipaumbele ili waweze kuwatunza waume zao. Ingawa ushauri huu ni kwa mwanamke wa Kiislamu, unaweza kuwafaa hata wanawake wasio wa dini husika. Katika mkabala huo, tunaweza kusema kwamba jambo hili ni muhimu sana kwa kuwa wanawake wengi wamebomoa nyumba zao kwa kutumia ulimi wao na kutomheshimu mumewe. Iwapo mwanamke atatumia ulimi wake vizuri, kutakuwa na amani katika ndoa yake. Mwanakupona anaendelea kutoa wosia kwa bintiye kama ilivyo katika kifungu kifuatacho:

**MF 16**

Uonapo uso wake,
Funua meno uteke,
Akwambialo lishike,
Illa kuasi Jaliya
(UWM ubeti 50)

Katika MF 16, Mwanakupona anahimizwa aonyeshe meno yake huku akicheka kila mara amwonapo mumewe. Tunasoma kwamba: ***Uonapo uso wake, Funua meno uteke.*** Hali hii inaonyesha kuwa mwanamke anastahili awe chombo cha kufurahisha mumewe kila mara wanapokutana. Jambo lolote analomwambia, mwanamke anatakikana alishike na kulifuata bila malalamishi yoyote. Tunasoma kwamba: ***Akwambialo lishike.***

Mwanakupona anatoa wosia kwa bintiye kuwa ili kuweza kuishi na mumewe vyema, lazima atabasamu kila mara anapomwona mumewe. Ayashike yote aambiwayo na mumewe bila kupuuza neno hata moja ili waweze kuishi kwa furaha na kwa muda mrefu. Analoweza kuliasi, ni jambo ambalo litamwasi Mwenyezi Mungu mfano mume amwambie mke aibe, asisali au asiende kuabudu kama tulivyosoma katika MF 16.

Mwanakupona alikuwa na tajriba ya ndoa kwa kuwa aliishi na mumewe bila matatizo yoyote pia kwa kuisimamia nafasi yake kama mke bila kunung'unika wala kujuta kuwa mwanamke. Anaendelea kumpa bintiye wosia kutokana na tajriba ya ndoa katika ubeti 52:

**MF 17**

Naliowa na babako,
Kwa furaha na ziteko,
Tusondoleane mbeko,
Siku zot'e twalokaa
(UWM ubeti 52)

Katika ubeti wa 52, Mwanakupona anaeleza kuwa alifurahia maisha ya ndoa na mume wake. Tunasoma kwamba: ***Naliowa na babako, kwa furaha na ziteko.*** Kwa kuwa alizifuata kanuni za ndoa bila kubishana na mume wake. Aliyafurahia maisha

yao kwa kuwa kila mmoja aliyatekeleza majukumu yake bila kulazimishwa: ***siku zote twalikaa.***

**MF 18**

Siku moya tusitete,
Ovu langu asipate,
Na lake lisinikute,
Hatta akakhitariwa
(UWM ubeti 53)

Mwanakupona anamweleza bintiye kuwa hakuzungumza maovu kuhusu mumewe: ***Siku moya tusitete,*** naye mumewe hakumtesa bali waliheshimiana hadi mume wake alipochukuliwa na Mwenyezi Mungu. Tunasoma kwamba: ***Hatta akakhitariwa***. Mwanakupona anaendelea kumhimiza bintiye azingatie suala la amani katika ubeti wa 48 ambao umedondolewa hapa chini:

**MF 19**

Na bwanako mtukuze,
Sifa zake uzeneze,
Wala simshurutize,
Asoweza kutukuwa
(UWM ubeti 48)

Katika MF 19, ni dhahiri Mwanakupona anamshauri bintiye wahusiane vyema na mumewe kwa kumtukuza na kumpa sifa miongoni mwa wanajamii. Tunasoma kwamba: ***Na bwanako mtukuze, Sifa zake uzeneze.*** Mwanamke anastahili kuzungumza mema kumhusu mumewe na hata kutangaza mambo mazuri kumhusu na asimlazimishe mumewe kumfanyia mambo asiyoyaweza kifedha. Aombe tu yale ambayo mumewe anaweza kuyatenda kwa mujibu wa pato lake.

Mwanamke anastahili kumsifu mume wake, na kwamba sifa hizo za mumewe zienee kila mahali na hivyo mumewe atahisi furaha na kutimiza majukumu yake vilivyo.

Sifa hizi zinachangia amani kwenye ndoa kwa kuwa mume anapewa nafasi yake kikamilifu katika familia. Mwanamke anastahili kumsifu mume wake, na kwamba sifa hizo kwa mumewe zienee kila mahali na papo mumewe atahisi furaha na kutimiza majukumu yake vilivyo.

Mwanamke anaweza kuifanya nyumba kuwa jehanamu inayowaka moto kwa kukosa kumpa mume nafasi yake kama kichwa au kiongozi wa jamii. Anaweza akamfikisha mumewe kwenye kilele cha mafanikio au balaa isiyofaa. Mwanamke ambaye anatambua wajibu wake, anaweza kumfanya mume wake kuwa mtu wa kuheshimika hata kama alikuwa mtu wa chini sana kuliko wote.  Kwa mujibu wa ubeti huu, mama anamshauri bintiye kuwa anapaswa amtukuze bwanake, sifa zake azieneze wala asimshurutishe mambo asiyoweza kuyatekeleza: ***Wala simsharutize, Asichoweza kutoa***. Wanawake wengi wanapenda kujilinganisha na wenzao walioolewa na wanaojiweza kifedha, wanawalazimisha waume zao kununua bidhaa ambazo kwa kweli kulingana na hali yao ya kiuchumi, hawana uwezo wowote. Matokeo ni ugomvi, vita, utengano na hata talaka.

Mke anayemsimanga mumewe, huwa anamdhalilisha na mara mume anapojua mkewe ana mazoea hayo, upendo, amani na kutokuaminiana hujiri katika ndoa yao na mwishowe husababisha talaka. Mawaidha haya kwa mwanamke si mabaya, ni mazuri. Matakwa kama haya, yasitolewe kwa mume iwapo uwezo wake wa kiuchumi ni duni. Mawaidha haya si ya kumkandamiza mwanamke bali ni mawaidha bora ya kudumisha uhusiano mwema kati ya bwana na bibi katika ndoa. Mke lazima afahamu hali ya uchumi wa mumewe anapotoa matakwa yake. Mwanakupona anasisitiza furaha kwa mume kila mara anapoishi na bintiye. Kwa mfano katika MF 20:

**MF 20**

Naawe radhi mumeo,
Siku zot'e mkaao,
Siku mukhitariwao,
Awe radhi mekuwiya
(UWM ubeti 24)

Katika MF 20, mwanamke anapaswa kumkubali mume wake daima alimuradi bado wanaishi pamoja. Katika ubeti huu, Mwanakupona anamshauri bintiye kuwa ahakikishe mumewe ana radhi naye, yaani anamkubali na kumridhia siku zote katika ndoa yao, ***Naawe radhi mumeo.*** Na wakati mmoja wao wakiondoka ulimwenguni, mfano mume akitangulia, basi afariki akiwa bado anaridhika na mkewe.

Wosia huu ni muhimu sana hasa kwa minajili ya kudumisha amani daima katika maisha ya ndoa. Wawili hao wakubaliane au waridhiane katika yote wafanyayo. Wanandoa wanapewa ushauri ambao unalenga kuijenga na kuidumisha ndoa yao. Katika hali ya kawaida inatarajiwa kwamba mwanamke anapokubali kuingia katika ndoa ni sharti amkubali mume wake kama mpenzi wake wa maisha. Asipofanya hivyo, anahatarisha ndoa yake.

Kwa maoni yangu, mafunzo haya si mabaya wala si ukandamizaji. Waliooana wakiwa daima katika maisha yao ya ndoa wataridhiana, wataishi ndoa ya furaha na amani hadi kufariki kwao. Katika MF 20 tunapata taswira ya mwanamke mpenda amani, kwa kuwa ni jukumu lake kuhakikisha mwanamume anaishi kwa amani ili aweze kutekeleza wajibu wake kama mume.

**4.3.2 Taswira ya mwanamke Mpenda Amani katika UWA**

Katika *Utendi wa Ayubu* ubeti wa 124, mkewe Ayubu, Rehema amechorwa kama mwanamke mpenda amani, na anashtuka sana mumewe anapofukuzwa kwa sababu ya ugonjwa. Haya yanadhihirika katika MF 21 hapa chini:

**MF 21**

Mwema mzawa na wema
yakamuelea tama
mumewe  kumsukuma
kwa sababu ya kuwaa
(UWA ubeti124)

Katika MF 21, tunaelezwa kuwa Rehema alikuwa mwema kama wazazi wake, na kwamba aliwatendea wengine mema bila manung'uniko: ***Mwema mzawa na wema, yakamuelea tama.*** Alijawa na huzuni mumewe alipofukuzwa kwa ajili ya ugonjwa wake. Sifa hii ilimfanya awe kielelezo kwa wanawake wengine: ***yakamuelea tama, mumewe  kumsukuma kwa sababu ya kuwaa***. Taswira ya mwanamke mpenda amani imejidhihirisha katika ubeti huu jinsi Rehema alitamani wangeishi wote kama jamii kwa amani bila kumbagua yeyote kwa sababu ya magonjwa.

### 4.3.3 Taswira ya mwanamke Mpenda Amani katika WUB

Katika Wimbo Ulio Bora, Solomoni amemchora mwanamke anayependa amani katika familia yake. Mwanamke huyu ni mpole na hapendi ugomvi, muhimu kwake ni kumpenda na kudumisha amani na mumewe. Suala hili linajidhihirisha katika WUB 2:1

**MF 22**

Mimi ni ua la uwandani,
Ni nyinyoro ya mabondeni
Kama nyinyoro kati ya miiba,
Kadhalika mpenzi wangu kati ya binti
(WUB 2:1-2)

Katika MF 22, Solomoni anajifananisha na ua la kondeni na nyinyoro kati ya miiba, na kwamba mpenzi wake vile vile ni mpole na mtulivu kati ya binti wa Yerusalemu. Solomoni anamlinganisha mke wake na ua katikati mwa miiba. Tunasoma kwamba:

***Kama nyinyoro kati ya miiba***, kumaanisha kuwa ni mpole na mpenda amani. Ijapokuwa mwanamke amezingirwa na watu wabaya na wanaochukiza kama miiba, yeye (mwanamke) ametulia tu bila kukwaruza yeyote au kuchukiza. Hali kadhalika katika WUB 2:3

**MF 23**

Kama mpera kati ya miti ya msituni,
Kadhalika mpendwa wangu kati ya vijana,
Naliketi kivulini mwake kwa furaha,
Na matunda yake naliyaonja
Kuwa matamu.
(WUB 2:3)

Katika MF 23, Solomoni anamfananisha mpenzi wake na mpera kati ya msituni. Mshororo huu unadhihirisha upole na amani ya mwanamke, jinsi ***mpera unavyoweza kumea kati ya miti ya msituni*** na kuweza kuzaa matunda yanayoliwa na binadamu. Solomoni anaendelea kusema kuwa: ***Naliketi kivulini mwake kwa furaha,*** na ili mtu aweze kufurahi jambo lolote, lazima kuwepo na amani. Kwa hivyo, Solomoni anadhihirisha usawiri wa mwanamke kuwa mpenda amani. Kwa hivyo mwanamume anaweza kuishi kwa furaha mustarehe. Solomoni anaendelea kusema kuwa: ***Na matunda yake naliyaonja kuwa matamu.*** Mwanamke anayependa amani humfanya mume wake aishi miaka mingi kwa kuwa hatasumbuliwa na maradhi yanayoletwa na migogoro nyumbani. Vile vile, mwanamume atayafurahia maisha yake na kumfurahia mke wake kwa kuwa hapati usumbufu nyumbani.

### 4.3.4 Taswira ya Mwanamke Mpenda Amani katika KCM

Katika KCM, mwanamke amechorwa kama mpenda amani, na suala hili linamfanya kukwepa ugomvi wa kila mara katika ndoa. Majukumu ya mwanamke katika kumtunza mwanamume ni mengi na hayafai yalete ugomvi nyumbani. Kwa hivyo mwanamke awe mtu anayependa amani katika ndoa yake na kujiepusha na ugomvi

unaoharibu unyumba. Kwa mfano, tukirejelea Kitabu cha Methali 21:9, tunasoma kuwa:

**MF 24**

> Ni afadhali kukaa katika pembe ya darini,
> Kuliko katika nyumba pana pamoja na mwanamke mgomvi
> (KCM 21:9)

Katika MF 24, Solomoni anasema kuwa ni afadhali kuishi juu ya paa kuliko kuishi na mwanamke mgomvi: ***Afadhali kukaa katika pembe ya darini, Kuliko katika nyumba pana pamoja na mwanamke mgomvi***, kwa sababu kuishi na mwanamke kama huyu kwenye nyumba moja ni sawa na kujichimbia kaburi lako mwenyewe.

**MF 25**

> Ni afadhali kukaa katika nchi ya nyika;
> Kuliko na mwanamke mgomvi, mchokozi
> (KCM 21: 19)

Nyikani, hamna lolote la kufurahisha binadamu na hata uhai umehatarishwa mno, lakini mwandishi wa Kitabu cha Methali anaona ni heri kuishi nyikani kuliko kuishi na mke mgomvi: ***Afadhali kukaa katika nchi ya nyika***.

Katika MF 24 na MF 25, Solomoni anaeleza wazi kuwa mwanamke ambaye ni mgomvi husababisha majonzi na hata kifo kwa mumewe. Mke mchokozi ni sawa na mauti kwa kuwa wanaume hawapendi kupigiwa kelele wala kuonyeshwa madharau ya aina yoyote. Mwanamke mchokozi mara nyingi huachwa na wanaume na hata wengine kukosa kuolewa kabisa.

Mwanamke mgomvi na mchokozi wa aina hii huibomoa nyumba yake mwenyewe kwa mikono yake kwa kuwa anapozua ugomvi kila mara, humfukuza mumewe nyumbani na mwanamume huadimika nyumbani. Hakuna binadamu anayestahimili

ugomvi wa kila mara. Mke na mume huhitaji utulivu nyumbani unaoletwa na maneno mazuri na matamu. Hayo yakikosekana, ndoa hiyo hubomoka au kusambaratika.

Taswira ya mwanamke mpenda amani, ni mfano unaotuonyesha mwelekeo ambao mwanamke anastahili kuwa nao katika ndoa, ili aishi vyema na mumewe kwa kuifurahia ndoa yao na maisha kwa jumla. Kuepukana na ugomvi nyumbani ni wosia mwema wala si ukandamizaji wa mwanamke. Taswira ya mwanamke mpenda amani hujidhihirisha jinsi anavyowasiliana na mume wake, bila ugomvi na matata. Solomoni anaendelea katika KCM ambapo anasema:

**MF 26**

> Mke mgomvi ni kama
> matone yasiyokoma ya siku ya mvua
> Kumzuia yeye ni kama kuuzuia upepo
> au kukamata mafuta kwa kiganja cha mkono
> (KCM 27:15-16)

Katika MF 26 Solomoni anamfananisha mwanamke mgomvi na matone yasiyokoma ya siku ya mvua. Tunasoma kwamba: ***Mke mgomvi ni kama matone yasiyokoma ya siku ya mvua.*** Jinsi matone yanavyoanguka ndivyo mwanamke mgomvi amepigiwa mfano kwamba ni hali inayoghadhabisha sana.

Kutokana na maelezo haya tunapata funzo kwa mwanamume ambapo anashauriwa kuepukana na mwanamke mgomvi. Solomoni, anadai mwanamke mgomvi hana dawa, hawezi kudhibitiwa. Kwa hivyo wanaume waepukane naye kabisa. Funzo kwa mwanamke, ni afahamu ugomvi haufai, unaudhi. Katika jamii ya leo, nyumba iliyojaa ugomvi wanaume hukwepa kwa kujiingiza katika shughuli za kujisahaulisha kama vile kunywa mvinyo na mwishowe hata kujihusisha na uasherati na kusambaratisha familia yake. Chanzo cha mambo haya ni ugomvi nyumbani kwake.

Mwanamke anapaswa kuifanya nyumba yake iwe ya furaha na kutamanika ili mumewe ahisi yuko na amani na uhuru aingiapo nyumbani.

### 4.4 Taswira ya Heshima

Mwanamke anahimizwa kuwa mwenye heshima kwa mumewe. Jambo hili linajenga ndoa. Waliooana wasipoheshimiana, mafarakano hutokea katika nyumba. Kwa hivyo, heshima ni muhimu sana kati ya mke na mumewe. Dini ya Kiislamu na Kikristo husisitiza heshima katika ndoa, kwa mfano katika *Biblia*, inasisitiza kuwa wanawake waheshimu waume zao (Waefeso 5:22-24, 1 Petro 3:1). Mitume waliandika maandiko haya ili kuwaonya wanawake kutokana na mienendo yao mbele ya waume zao kitabia na hasa katika suala zima la heshima. Mwanamke, kutokana na maagizo ya Mwenyezi Mungu, anatakiwa kumheshimu mume wake na kumtambua kama kiongozi wa jamii na ndoa yake.

Katika Waefeso 5:22 tunaelezwa: ***Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu***. Hii ni amri iliyoandikiwa wanawake kwamba waume zao wanafaa heshima kama kumtii Mungu muumba wa vyote. La kushangaza ni kwamba si wote wanaoshikilia msimamo huu ulioandikwa katika *Biblia*, kwa kuwa wengi wanadai wamesoma na kwa hivyo kukombolewa kutoka kwa minyororo ya utumwa. Mtume Petro anawaonya wanawake akisema: ***Kadhalika ninyi wake, watiini waume zenu; kusudi, ikiwa wako wasioliamini Neno, wavutwe kwa mwenendo wa wake zao, pasipo lile Neno'*** (1Petro 3:1). Kwa maelezo zaidi, heshima ya mke kwa mume wake, utawafanya wengine kumwamini Yesu Kristo anayezungumziwa kwenye maandiko. Na upande wa pili, kukosa heshima kwa mume kutawazuia wengine kumwamini Yesu na kwa hivyo kupotoka na kuingia Jehanamu jinsi inavyozungumziwa na waandishi wa *Biblia*. Iwapo Wakristo wanapinga haya, ni dhahiri kuwa wanaasi

*Biblia* kitabu cha Mungu. Kwa hivyo kumheshimu mume ni maagizo yanayopatikana katika Kitabu Kitakatifu cha Wakristo.

### 4.4.1 Taswira ya Heshima katika UWM

Picha ambayo tunasawiriwa hapa ni kuwa ili mwanamke awe mlezi mwema katika jamii, sharti amheshimu na kumtii mume wake. Kazi zetu za kifasihi na za kidini zimedhihirisha mwanamke anavyostahili kumpa mumewe heshima na kumtii nyakati zote kama tunavyosoma katika *Utendi wa Mwanakupona*, MF 27:

**MF 27**

Moyowe alipendalo,
Nawe ufuate lilo,
Yambo limtukialo,
Siwe mwenye kumweteya
(UWM ubeti 43)

Katika MF 27, tunapata ushauri wa mama kwa bintiye kuwa ayatilie maanani yale yote yanayompendeza au anayoyapenda mumewe. Tunasoma kuwa: ***Moyowe alipendalo, Nawe ufuate lilo.*** Mwanamke anastahili kumheshimu mumewe kwa vyovyote vile bila kumdharau wala kuonyesha vitendo visivyoambatana na heshima. Vile vile, aepukane na yale ambayo kwayo hayamfurahishi na yanaweza kumletea ghadhabu na uchungu moyoni mwake. Tunaelezwa kuwa: ***siwe mwenye kumweteya.***

Kando na hayo, amsifu mbele ya watu wengine. Awape watoto msingi mzuri wa kumheshimu baba yao na awakaripie kama hawaonyeshi adabu kwake. Amheshimu mbele ya wageni na awe makini kwa mahitaji yake, na yale ya wageni. Kwa mfano, katika UWM (ubeti 50), Mwanakupona anamshauri bintiye awe mwenye tabasamu na ayazingatie yote anayoambiwa na mumewe. Katika kufanya hivyo anamshauri kuwa asiende kinyume na kanuni za Mungu.

Nguzo hii ni muhimu sana katika ndoa yoyote. Wanaume wote wanapenda kuheshimiwa, wanapenda kupewe nafasi zao katika ndoa. Mwanakupona anamshauri bintiye atabasamu kila mara anapomwona mumewe. Tunasoma kuwa: ***funua meno uteke,*** kwani ni muhimu kwa mke kuwa mtu wa furaha. Mwanamke anapomheshimu mumewe, humwongezea nguvu na mwelekeo kwenye harakati za kuyafanya maisha kuwa bora. Tunaelezwa kuwa: ***akwambialo lishike.*** Kila mara anatakiwa kumsalimia mumewe kwa sababu hayo maamkizi yatamfanya ahisi kuwa mkewe anamjali. Mke anafaa kuwa na adabu na upole anapozungumza na mumewe wala asimpigie kelele.

Mwanamke anapaswa kujua kwamba mumewe hukutana na watu wengi katika shughuli zake za kila siku. Baadhi ya watu hao wanaweza kuwa hawana utu na wanaweza kumfedhehesha na kumfanya kukosa furaha au amani moyoni. Ni wajibu wa mwanamke kumwonyesha heshima na ari akiwa nyumbani na kwa hali hiyo atampandisha hadhi ya nafsi yake iliyokanyagwa.

Vile vile, mwanamke anapewa wosia kuhusu jinsi ya kumuaga na kumlaki mumewe anapoondoka na kurudi nyumbani kama njia ya heshima kwa mume. Hayo tunayasoma katika MF 28:

**MF 28**

Kitoka agana naye,
Kingia mkongowee,
Kisa umtandikie,
Mahala pa kupumua
(UWM ubeti 30)

Katika MF 28 hapo juu, Mwanakupona daima alimjali sana bintiye. Anamshauri kwamba mumewe lazima amfikirie kila wakati. Hii ina maana kwamba ndoa hujengwa kwa kumwaza mwenzio wakati wote. Katika ubeti huu, mwanamke anapewa wosia kuwa kila mara mume anapotoka nyumbani lazima amuage na

anaporudi lazima apokelewe vyema: ***Kitoka agana naye, kingia mkongowee***. Mwanamke anastahili kumshughulia mume wake kwa kumtandikia malazi vyema ili aweze kupumzika arudipo. Anamweleza kwamba: ***Kisa umtandikie, mahala pa kupumua.*** Hali hii itawafanya wawili hawa waishi vizuri kwa amani na utulivu.

Vile vile, mume anapopokelewa vyema na mkewe, hatajihusisha na shughuli nyingi kule nje, bali atajitahidi kurudi nyumbani mapema ili apate muda mzuri na familia yake. Kwa hivyo, wajibu wa mwanamke ni kumshughulikia mumewe ili amfurahishe ndiposa uwiano uwepo ndani ya nyumba. Katika jamii nyingi za Kiafrika, mwanamke anastahili kuwa mwema kwa mumewe na kumwonyesha heshima kwa sababu mume ndiye kiongozi wa jamii.

#### 4.4.1.1 Mwanamke kutobishana na Mume wake

Katika *Utendi wa Mwanakupona*, Mwanakupona anatoa wosia kwa bintiye kuwa anastahili kumheshimu mume wake bila kubishana naye kama tunavyosoma katika MF 29 hapa chini:

**MF 29**

Fuata yake idhini,
Awe radhi kwa yakini,
Wala sikae ndiani,
Saa yane kasia ndiani
(UWM ubeti 45)

Katika MF 29 hapo juu, tunaelezwa kwamba mwanamke anastahili kumsikiza mumewe. Tunaelezwa kuwa: ***Fuata yake idhini,*** ili mume aridhike, na pia aweze kumwamini kwa kila hali. Kama mwanamke anampenda mumewe kwa dhati, atajitahidi na kujitolea kwa ajili ya ustawi wa familia yake. Anaponyimwa ruhusa ni

wajibu wake kumtii mumewe kwani kufanya hivi, wataishi maisha ya raha na mustarehe milele.

Mwanamume anamtegemea mkewe kupata urafiki na mapenzi, ambayo ni mahitaji ya kila mwanadamu. Kama mapenzi yanatoka sehemu zote mbili, msingi wa ndoa utakuwa na nguvu na hatari za kutengana zitaepukwa. Mapenzi yanayodumu ni yale yanayopitia katika wema na huba ya kudumu ndani ya urafiki wa karibu sana. Mwanamke anapoondoka kwenda shughuli zake ahakikishe kuwa anafika nyumbani kabla ya saa nne usiku ili adhihirishe heshima kwa mumewe: ***Wale sikae ndiani, saa yane kasia ndiani.*** Mwanamke ahakikishe anamhudumia mumewe kila mara anapomhitaji. Mwanamume naye anastahili pia amtendee mkewe wema.

Mwanamume anayefurahia mapenzi ya mkewe, huwa na changamoto chache sana za kiafya. Moyo huwa umetulia na usumbufu pengine wa kiuchumi ndio utampata, jambo ambalo ni la kawaida. Iwapo mwanamume hapati wema kutoka kwa mkewe, anaweza kukata tamaa na kuanza kuikwepa nyumba yake. Anaweza kujikuta anatumia muda wake mwingi sana katika kutafuta marafiki na watu wa kumjali.

Mwanamke anaweza kumpenda mumewe kwa uaminifu, lakini mara nyingi hayadhihirishi mapenzi yake. Haitoshi kuanzisha uhusiano wa kirafiki na kuchukulia kwamba hali hiyo ni sawa. Matamshi ya mara kwa mara miongoni mwa binadamu kama vile; "Ninakupenda, umepotea machoni mwangu sana! Ninafurahi kukuona" na kadhalika, huchangia katika kuendeleza uhusiano mwema. Mume anapokuwa safarini, ni muhimu mkewe amjulie hali kadiri inavyowezekana ili kuonyesha kwamba haoni raha bila kuwa naye au kumpigia simu mara kwa mara au kumtumia ujumbe wa mapenzi. Mahusiano kama haya si ukandamizaji, ni kujenga mapenzi na uhusiano mwema wa ndoa.

#### 4.4.1.2 Mwanamke kuomba Ruhusa ya kutoka Nje

Katika *Utendi wa Mwanakupona* ubeti wa 44, tunamwona mama akimpa bintiye ushauri kwamba mke mwema anahitaji kumheshimu mumewe kwa kumwomba mumewe ruhusa anapotaka kutoka nyumbani, pengine kuwatembelea marafiki zake na kuwajulia hali majirani. Baada ya kuomba ruhusa, mwanamke anatarajiwa kupata jibu kutoka kwa mumewe. Jibu lake laweza kuwa ndio au la. Ikiwa atanyimwa ruhusa ya kutoka nje, basi hatakuwa na budi bali atabaki nyumbani hadi atakapopata ruhusa wakati mwingine. Tunayapata maelezo kamili katika MF 30 hapa chini:

**MF 30**

Ukutiwapo kutoka,
Sharuti ruhusa taka,
Uonapo meudhika,
Rudi na kuiketiya
(UWM ubeti 44)

Mwanamke anapewa wosia kuwa ni vyema kuomba ruhusa kabla ya kutoka nyumbani. Tunaelezwa kuwa: ***Ukutiwapo kutoka,*** amwombe mumewe ruhusa: ***Sharuti ruhusa taka.*** Mwanamume anapewa nafasi yake ya heshima ya kuombwa ruhusa kabla ya mwanamke kufanya lolote. Iwapo mume atakataa: ***uonapo meudhika, rudi na kuiketiya,*** pengine kwa sababu fulani, basi asitoke. Mwanamke anapopewa ruhusa ni sharti azingatie kile alichotaka kufanya. Nionavyo mimi, huu ni mlahaka mwema nyumbani. Huu si ukandamizaji kwa sababu hata wanawake wa karne hii, wenye nidhamu, huomba ruhusa waume wao wakati wanataka kutoka kwenda kufanya shughuli zao. Aghalabu, waume hawakatai kwani kuomba ruhusa ni heshima ya ndoa. Huku si kukandamizwa bali ni njia bora ya kuishi na kuelewana. MF 31 hapa chini unatoa maelezo zaidi:

**MF 31**

Fuata yake idhini
Awe radhi kwa yakini
Wala sikae ndiani
Saa yane kasia ndiani
(UWM ubeti 45)

Katika MF 31 tunaelezwa kwamba mwanamke anastahili kumtii mumewe. Tunasoma kuwa: ***Fuata yake idhini,*** na mumewe aridhike na safari hiyo. Mwanamke anapopewa ruhusa, basi asiende kuzurura. Anapokamilisha haja yake, arudi nyumbani akae na mumewe: ***wala sikae ndiani.*** Kuzurura kwa mwanamke aliyeolewa si jambo jema hata leo. Katika nyakati za Mwanakupona, jambo hilo lilikuwa baya. Vivyo hivyo jambo hilo bado ni baya katika karne ya 21. Kwa hivyo, wosia huu ni mwafaka kwa mwanamke katika jicho la mtafiti huyu. Huu si ukandamizaji ni desturi bora za watu waliooana.

### 4.4.2 Suala la Mwanamke Kumheshimu Mume katika UWA

Kadhalika, katika UWA beti za 286 na 287, tunamwona Rehema akimwarifu mumewe Ayubu kuwa anamtii. Anamhimiza mumewe ale vipande vya mkate alivyokuwa amevileta. Ayubu pia anamshukuru mkewe na kumwambia kuwa nasaba yake ni njema. Beti hizi zinatuonyesha tu heshima na utiifu aliokuwa nao Rehema kwa mumewe, suala ambalo liliwafanya waishi pamoja bila ugomvi. Mawazo haya yanadhihirika vyema katika MF 32 na MF 33 hapa chini.

**MF 32**

Lo lote nikufuate
ili radhi niipate
bwana pokea nkate
usiiiudhi kwa ndaa
(UWA ubeti 286)

**MF 33**

Ayubu katakalama
Akamwambia Rehema
Nawe ni asili njema
Dhuria ya mursaa
(UWA ubeti 287)

Katika MF 32 na MF 33, tunaelezwa kuwa Rehema anamwahidi mumewe kuwa yeye atamtii kwa vyovyote vile ili aweze kupata radhi yake. Tunasoma kwamba: ***Lo lote nikufuate, ili radhi niipate.*** Mwanamke anatakikana kuamua kwa kweli kumtii na kumheshimu mumewe kwa hali zote bila kushurutishwa, matunda yake ni kuwa wataishi na mumewe kwa miaka mingi iliyojaa furaha. Mwanakupona anasisitiza umuhimu wa mke kumshughulikia mume wake hasa wakati wa shida. Anaeleza kwamba: ***Bwana pokea nkate,*** ili kuhakikisha kuwa amepata anachohitaji.

Matokeo ya utiifu na heshima kwa mume yanajitokeza katika ubeti wa 287 UWA, ambapo Ayubu anamwombea mkewe baraka kutoka kwa Mungu, anamwambia Rehema nasaba yake ni njema, yeye mjukuu wa mtume. Tunasoma kuwa: ***Nawe ni asili njema, dhuria ya mursaa.*** Mwanamke mzuri lazima awe mwangalifu asije akamfedhehesha mumewe, asizungumze naye kwa ukali, asimtukane, awe msikivu kwake na asimuite kwa majina machafu akimkosea kwa sababu yeye pia atafedheheka.

### 4.4.3 Suala la Mwanamke Kumheshimu Mume katika WUB

Solomoni anamchora mwanamke anayemheshimu mume wake kwa kila hali. Heshima hii kwa mume wake ndiyo inayomfanya mume wake kumpenda zaidi ya wanawake wengine. Mwanamke anayemheshimu mume wake anaitumia midomo yake vizuri bila kumkera mumewe. Kwa mfano katika WUB 5:16,

**MF 34**

> Kinywa chake kimejaa maneno matamu,
> Ndiye mzuri sana pia pia,
> Ni huyu mpendwa wangu,
> Ni huyu rafiki yangu,
> Enyi binti za Yerusalemu.
> (WUB 5:16)

Mwanamke huyu anamheshimu mume wake kwa kuwa anayatumia maneno mazuri kila mara anapozungumza na mumewe. Tunasoma kuwa: ***Kinywa chake kimejaa maneno matamu.*** Heshima hii inamfanya Solomoni kuwatangazia binti za Yerusalemu kuwa yeye (mwanamke) alikuwa mpendwa wake na rafiki yake milele.

### 4.4.4 Suala la Mwanamke Kumheshimu Mume katika KCM

Katika Kitabu cha Methali 31:12, Solomoni anatuhimiza kuwa mwanamke mzuri humtendea mumewe mema. Haya tunayapata katika MF 35 hapa chini:

**MF 35**

> Humtendea mema wala si mabaya,
> Siku zote za maisha yake
> (KCM 31:12)

Kutokana na kifungu hiki (MF 35), mwanamke anafanya uamuzi wake bila kushurutishwa kumheshimu mumewe, kumtendea mema wala si mabaya: ***Humtendea mema wala si mabaya.*** Mwanamke anachagua mambo mema ambayo mume wake atayafurahia, kumshughulikia bila kukumbushwa na kutomjibu au kutomtii hasa mbele ya watu wengine. Anayatenda mambo haya mema siku zote za maisha yake.

Solomoni anaendelea kubainisha kuwa kutokana na heshima alizonazo mke kwa mume wake, mume atajulikana kwenye miji na maeneo mbalimbali. Kila mara

anapoketi na wazee wenzake hutambuliwa kwa sababu ya heshima kutoka kwa mke wake kama tunavyosoma katika MF 36 hapa chini.

**MF 36**

> Mume wake hujulikana malangoni;
> Aketipo pamoja na wazee wa nchi.
> (KCM 31:23)

Kutokana na MF 36 hapo juu, Solomoni anamhakikishia mwanamke kuwa akiyatekeleza majukumu yake mume wake hujulikana na kuheshimika anapokwa pamoja na wazee wenzake. Tunaelezwa kuwa: ***Mume wake hujulikana malangoni.*** Nafasi hii amepewa mwanamume ambaye anaheshimiwa na mke wake, huyu mume atapewa hadhi ya juu na wenzake kumsikiza kila mara anapozungumza. Tunaelezwa kuwa: ***aketipo pamoja na wazee wa nchi***, yeye huheshimiwa. Iwapo Wakristo wanapinga haya, wajue wanaasi *Biblia*, kitabu cha maneno ya Mungu. Kwa hivyo kumtii mume ni maagizo hata katika Kitabu Kitakatifu cha Wakristo.

### 4.5 Mwanamke kama Mtunzaji wa Mume

Hii ni taswira nyingine aliyopewa mwanamke katika ndoa. Mbali na majukumu mengine, hili vile vile ni lake. Ingawaje mwanamume naye huwa mtunzi wa mkewe na familia, mke pia ana jukumu la kumtunza mumewe na watoto. Al-Amin (1936), anasema ni jukumu la mwanamke katika sharia ya Kiyahudi kumpikia mume, kushona nguo zake, za mume wake na watoto wake. Anasema kuwa ni kazi ya mwanamke kuhakikisha mume wake ameshughulikiwa vilivyo. Sifa hii imejitokeza katika matini ya kifasihi na kidini tulizozichagua, kuwa mwanamke ni mtunzaji wa mwanamume.

### 4.5.1 Mwanamke kama Mtunzaji wa Mume katika UWM

Jinsi tulivyomjadili mwanamke mwenye heshima kwa mume wake, mwanamke huyu kwa sababu ya tabia yake nzuri, humtunza mume wake ili asipatikane ameteseka kwa mambo ambayo mke wake angeweza kuyakimu. UWM ni wosia wa mwanamke katika karne ya 19 ambapo jamii nyingi za Kiafrika, Waswahili wakiwemo, kazi za nyumbani zilikuwa za mwanamke na kazi za sulubu zilikuwa za mwanamume. Kwa hivyo, Mwanakupona alisisitiza jukumu la kazi za nyumbani kwa mwanamke. Katika karne ya ishirini na moja (21), wapo wanawake ambao hawajaajiriwa na kwa hivyo hubaki nyumbani ili kuyatekeleza majukumu yao ya kila siku. Mawaidha kama haya yanawafaa, ingawaje tayari wanadumisha usafi nyumbani na kumpangia kazi mjakazi (yaya) iwapo anaye nyumbani. Huku si kukandamizwa bali kuwajibika kwa mwanamke. Iwapo anataka kukwepa majukumu yake, kama hili, atalalamika. Suala la utunzaji limejitokeza katika kazi za kifasihi na matini za kidini tulizozichunguza kama taswira mojawapo ya mwanamke. Katika *Utendi wa Mwanakupona*, suala la utunzaji limejitokeza katika MF 37, MF 38, MF 39, MF 40, MF 41 na MF 42 hapa chini:

**MF 37**

Keti naye kwa adabu,
Usimtie ghadhabu,
Akinena simjibu,
Itahidi kunyamaa.
(UWM ubeti 28)

**MF 38**

Enda naye kwa imani,
Atakalo simukhini,
We naye sikindaneni,
Mkindani huumiya.
(UWM ubeti 29)

**MF 39**

Kilala siikukuse,
Mwegeme umpapase,
Na upepo nasikose,
Mtu wa kumpepeya.
(UWM ubeti 31)

**MF 40**

Chamka siimuhuli,
Mwandikie maakuli,
Na kumtunda muili,
Kumsinga na kumowa.
(UWM ubeti 33)

**MF 41**

Mnyoe mpalilize,
Sharafa umtengeze,
Na udi umfukize,
Burukata wa ashia
(UWM ubeti 34b)

**MF 42**

Mtunde kama kijana,
Asioyua kunena,
Kitu changalie sana,
Kitokacho na kungiya.
(UWM ubeti 35)

Katika MF 37, MF 38, MF 39, MF 40, MF 41 na MF 42 hapo juu, mwanamke anashauriwa kumtunza mume wake kwa hali zote. Kwa mfano anapaswa kuketi naye, asimghadhabishe kwa kuwa ni mume wake. Tunaelezwa, ***keti naye kwa adabu, usimtie ghadhabu*** (MF 37). Vile vile anashauriwa kuwa mume wake akinena asimjibu kwa ujeuri ila asubiri hadi mambo hayo yatulie. Tunaelezwa kuwa: ***akinena simjibu, itahidi kunyamaa*** (MF 37). Mwanakupona anaendelea kumshauri bintiye kuwa atakalo mumewe apewe, asimnyime. Tunaelezwa kuwa: ***atakalo simukhini, we naye sikindaneni*** (MF 38). Vile vile mwanamke anashauriwa asiwe mgomvi bali awe mpole anapoongea na mume wake.

Mwanamke anapewa wosia wa kumtunza mume, hivi kwamba mume anapolala, mwanamke anashauriwa asiwe mbali naye bali amkaribie ili akihisi joto aweze kumpepea na vile vile kumpapasa asihisi upweke. Tunaelezwa kuwa: ***Kilala siikukuse, mwegeme umpapase*** (MF 39). Anapewa wosia kwamba mwanamume anapoamka awe tayari kumwandalia chakula na kumkanda mwili wake na hata kumwosha. Tunaelezwa: ***mwandikie maakuli na kumtunda muili*** (MF 40). Hii ndio njia nzuri ya kumtunza mume. Anaelezwa kuwa amnyoe na kumtengenezea sharafa na kumpaka manukato asubuhi na jioni. Tunasoma: ***mnyoe mpalilize sharafa mtengeneze*** (MF 41). Vile vile anashauriwa amtunze kama mtoto mchanga asiyejua kuongea. Tunasoma: ***mtunde kama kijana asioyua kunena*** (MF 42). Mwanakupona anapendekeza kuwa kwa kufanya hivi mwanamke hatapata shida kuishi na mume wake siku zake zote kwa raha mustarehe.

Katika MF 43 tunapata maelezo yafuatayo:

**MF 43**

Moyowe alipendalo,
Nawe ufuate lilo,
Yambo limtukialo,
Siwe mwenye kumweteya
(UWM ubeti 43)

Kutokana na MF 52, tunapata ushauri wa mama kwa bintiye kuwa ayatilie maanani yale yote yanayompendeza au anayoyapenda mumewe. Tunaelezwa kuwa: ***Moyowe alipendalo, nawe ufuate lilo***. Mwanamke anastahili kumtunza mumewe huku akimtii bila manung'uniko. Vile vile, asimchukize kwa kumletea mambo anayoyachukia. Tunaelezwa kuwa: ***Yambo limtukialo, siwe mwenye kumtweya***.

Kulingana na utafiti huu, mwanamke anapotekeleza majukumu haya ya kumtunza mume haina maana kuwa amenyanyaswa, bali amepewa fursa ya kudhihirisha hulka

zake za uuke. Ni jukumu lake kumtunza mumewe kwani wanaume wameumbwa katika hali ya kutaka kutumikiwa na kwa hivyo mke wake asipomtekelezea mahitaji haya yake anaweza kuelekeza mapenzi yake nje.

### 4.5.2 Mwanamke kama Mtunzaji wa Mume katika UWA

Katika *Utendi wa Ayubu*, mwanamke amechorwa kama ngao na msaidizi wa kweli kwenye ndoa. Haya yanadhihirika katika MF 44:

**MF 44**

Wote wakamsukuma
pasiwe alomwegema
illaye mwana Rehema
mke wake mfadhaa
(UWA ubeti 121)

Tunaelezwa MF44, jambo muhimu linalobainika ni kwamba mwanamke anaonekana kama rafiki wa kweli kwani wakati Ayubu aliposukumwa na kila mmoja katika jamii yake, ni mkewe tu ndiye aliyemvumilia na kubaki naye wakati wa majonzi: ***Wote wakamsukuma***. Rehema aliamua kusimama na mumewe (***illaye mwana Rehema)*** kwa kuwa alikuwa ameapa kuishi na mumewe hadi mwisho.

Kinachodhihirika hapa ni kwamba mwanamke ndiye anayeamua kubaki kwa machungu moyoni kinyume na mwanamume ambao wengi wao huwa wanaamua kuoa au kupata ‘mpango wa kando’. Ayubu alipokuwa ameteseka na hata kutengwa na jamii, aliyebaki naye ni Rehema mkewe aliyeamua kusimama na mumewe wakati wa mateso na dhiki. Tunaelezwa: ***mke wake mfadhaa.*** Mwanamke anabaki kuwa na nafasi spesheli katika ndoa ya kumsaidia mumewe na kuwa rafiki wa kweli.

Sifa hizi za Rehema ni mfano mzuri ambao unaweza kuigwa na wanawake wengine walio ndani ya ndoa. Pengine tunaweza kusema kwamba sifa hizo za Rehema

zilitokana na mfano bora alioachiwa na wazazi wake. Hii ina maana kwamba ni jukumu la mama mzazi kumrithisha bintiye tabia njema. Tunasoma: ***ni binti furahimu wa yusufu nisikie.*** Watoto wanaweza kuiga tabia ya wazazi wao katika maisha yao ya usoni. Iwapo wazazi wana tabia nzuri, watoto watakuwa wazuri na iwapo wana tabia potovu vile vile wataziiga na kuwa wasumbufu katika jamii. Kwa hivyo Rehema alitoka familia nzuri kama inavyodhihirika katika MF 45:

**MF 45**

Na yeye mwana Rehema
asiliye mbeu njema
ni binti furahimu
wa yusufu nisikie
(UWA ubeti 122)

Rehema alichukuwa nafasi ya mwanamke aliye na sifa bora: ***asiliye mbeu njema***, na sifa hizi ndizo zilizomvutia mumewe Ayubu kwake. Wema huu wa mwanamke ni taswira yake ya kumvutia mume na kuweza kudumu kwa ndoa.

Rehema alizifuata nyayo za wazazi wake waliokuwa na tabia nzuri katika jamii. Katika MF 45 tunapata kuwa: ***ni binti furahimu wa Yusufu nisikie,*** ambao walikuwa na wema na sifa bora. Kwa hivyo, Rehema aliyafuata maagizo ya wazazi wake na basi kuamua kuketi na kuishi na mumewe bila kujali ukoma wake, wakalala na kula pamoja. Kulingana na utafiti huu, wazazi wanatakiwa kuwa kielelezo kizuri kwa wanao ili watoto waweze kuwaiga katika maisha yao ya ndoa. Hii ni nafasi spesheli ya mwanamke kwa mume wake, aweze kuwa na hulka bora kwa ajili ya ndoa na ulezi wa watoto. Rehema alibaki amesikitika na kulia siku zote kwa mateso aliyoyapata Ayubu. Hayo yanadhihirika katika MF 46 na MF 47 kama tunavyosoma hapa chini.

**MF 46**

Mwema mzawa na wema
yakamuelea tama
mumewe kumsukuma
kwa sababu ya kuwaa
(UWA ubeti 124)

**MF 47**

Kaketi naye rijali
juzamu asiijali
walikilala wawili
na kuamka pamoya
(UWA ubeti 125)

Katika MF46 na MF47, tunaelezwa kwamba Rehema alikuwa mwema kama wazazi wake walivyokuwa wema. Tunapata kuwa: ***Mwema mzawa na wema,*** ambayo ina maana kuwa aliurithi wema wake kutoka kwa wazazi wake. Alipatwa na huzuni nyingi mumewe alipofukuzwa kwa sababu ya ugonjwa. Kutokana na uchanganuzi huu, tunabainisha kuwa Rehema alikuwa na moyo tofauti na wanawake wengi wa siku hizi kwa kuwa aliamua kumvumilia mumewe. Tunapata kuwa: ***mumewe kumsukuma kwa sababu ya kuwaa.*** Rehema aliamua kuishi na mumewe na kutekeleza majukumu yote ya mwanamke katika ndoa. Rehema aliamua kuketi na mumewe bila kujali ukoma wake. Tunasoma kuwa: ***Kaketi naye rijali juzamu asiijali,*** kwa sababu ya mapenzi ya dhati aliyokuwa nayo kwake Ayubu. Hii ni taswira ya mwanamke aliyeamua na moyo wake wote kudumu kwa ndoa yake bila manung'uniko wala majuto.

Wanawake wengi katika karne ya 21, hawawezi kustahimili changamoto kwa sababu ya usasa uliowaingia. Rehema aliamua kulala na mumewe na kuamka naye. Tunasoma kuwa: ***walikilala wawili, na kuamka pamoya.*** Hii ni taswira ya mwanamke aliyeamua kusimama kikamilifu katika nafasi yake. Rehema aliamua

kujivisha uchungu na maumivu ya mumewe katika ndoa, kwa mfano katika MF 48 hapa chini:

**MF 48**

Ayubu akasumbuka
Kwa ndwee yalomshika
Rehema kusikitika
Siku zote akilia
(UWA ubeti 126)

Katika MF 48 hapo juu, tunasoma kwamba Ayubu alisononeka kwa mateso yake kwa sababu, mwili wote ulikuwa unaumia. Tunasoma: ***Ayubu akasumbuka, Kwa ndwee yalomshika***. Hali hii ilimwacha kuwa pweke na mnyonge na alishindwa kujisaidia. Alibaki katika mateso na kutojua la kufanya, lakini Rehema aliamua kusimama na mume wake nyakati zote. Tunasoma: ***Siku zote akilia.*** Vile vile tunaelezwa kwamba Rehema alitambua nafasi yake kama mwanamke ndani ya ndoa. Katika hali ya kawaida taswira ya mwanamke yapaswa kuwa na uvumilivu. Rehema alimpenda Ayubu kwa moyo wake wote, wakati huu mgumu alishinda akilia na kusikitika moyoni: Tunasoma: ***Rehema kusikitika***, kwa sababu ya hali ya mume wake. Kwa hivyo beti hizi zimemsawiri mwanamke kama kiumbe mvumilivu.

Hali kadhalika katika UWA ubeti wa 286 tunamwona Rehema akimwarifu mumewe Ayubu kuwa atamtunza kwa njia zote. Tunaelezwa katika MF 49 kwamba:

**MF 49**

Lo lote nikufuate
ili radhi niipate
bwana pokea nkate
usiiudhi kwa ndaa
(UWA ubeti 286)

Katika MF 49, tunaelezwa kuwa Rehema anamwahidi mumewe kuwa yeye atamtii kwa vyovyote vile ili tu apate radhi yake. Tunaelezwa kuwa: ***Ili radhi niipate.*** Anamhimiza mumewe ale vipande vya mkate alivyokuwa amevileta, ***Bwana pokea nkate, usiiudhi kwa ndaa.*** Ayubu pia anamshukuru mkewe na kumwambia kuwa nasaba yake ni njema. Ubeti huu unatuonyesha hali ya utunzaji wa Rehema kwa mumewe Ayubu suala ambalo liliwafanya waishi pamoja bila ugomvi.

Mwanamke anatakikana kuamua kwa kweli kumtunza mumewe kwa hali zote bila kushurutishwa, na matokeo yake ni kuwa wataishi na mumewe kwa miaka mingi iliyojaa furaha.

### 4.5.3 Mwanamke kama Mtunzaji Wa Mume Katika WUB

Solomoni amebainisha mwanamke kama mlinzi katika WUB 4:15,

**MF 50**

> Wewe ndiwe chemchemi ya bustani yangu,
> Kisima cha maji yaliyo hai,
> Vijito vya Lebanoni viendavyo kasi
> (WUB 4:15)

Katika MF 50 hapo juu, Solomoni anamfananisha mpenzi wake na chemchemi ya bustani yake. Tunaelezwa: ***Wewe ndiwe chemichemi ya bustani yangu*** (MF 50). Ametumia bustani kumaanisha maisha yake, familia na mali yake. Bila chemchemi bustanini, mimea yote itakauka. Kwa hivyo, mwanamke amefananishwa na mlinda familia na pia kiumbe muhimu kwa mume wake, na kwamba bila mwanamke, mume atakosa kunawiri na kustawi maishani. Solomoni anaendelea kusema kuwa:

**MF 51**

Tukamatie mbweha,
Wale mbweha wadogo,
Waiharibuo mizabibu,
Maana mizabibu yetu yachanua
(WUB 2:15)

Katika MF 51 hapo juu, mwanamke anayezungumziwa hapa ni mtunzaji wa mume. Solomoni anamsihi awakamate mbweha wadogo wanaoaharibu mizabibu. Mwanamke amepewa jukumu hili kwa kuwa yu kwenye bustani, na kwa hivyo anaweza kufanya utunzaji wa hali ya juu. Tunasoma: ***Tukamatie mbweha, Wale mbweha wadogo*****.** Mwanamke ndiye mtunzaji wa mumewe kwa kuhakikisha kuwa wale maadui wadogo wadogo wanaofananishwa na mbweha hawamkaribii mumewe, kwa mfano, makahaba.

### 4.5.4 Mwanamke kama Mtunzaji Wa Mume Katika KCM

Licha ya kudumisha nguvu na hadhi, mwanamke anatakikana kuzingatia maongezi yake na kujiheshimu kwa mahusiano yake na wanajamii kama inavyojidhihirisha katika MF 52 na MF 53 hapa chini:

**MF 52**

Hufumbua kinywa chake kwa hekima,
Na sheria ya wema i katika ulimi wake
(KCM 31:26)

**MF 53**

Huangalia sana njia za watu wa nyumbani mwake;
Wala hali chakula cha uvivu
(KCM 31:27)

Katika MF 52 na 53, tunaelezwa kuwa mwanamke anapaswa kufahamu kuweka mipaka ya maongezi yake na aweze kufungua kinywa chake kwa hekima

anapowasiliana na wengine. Tunaelezwa: ***Hufumbua kinywa chake kwa hekima***. Mwanamke huyu vile vile anazifahamu sheria ya wema na kwamba sheria hizi zi karibu naye kila mara. Kwa sababu ya hekima aliyonayo huwashughulikia watu wa nyumbani mwake na hufanya kazi kwa mikono yake mwenyewe.

Katika maisha ya sasa, wanawake wengi wameshambuliwa kwa kutotumia midomo yao vizuri. Wengine wamevunja ndoa zao kwa kutoa maneno yasiyo na heshima wanapojibizana na waume zao. Mwanamke anatakikana azijue sheria za wema, na kanuni hizi zimwongoze katika matamshi yake. Tunaelezwa: ***Na sheria ya wema i katika ulimi wake***. Sheria hizi zimwongoze katika uteuzi wa maneno, na kwamba maneno haya yatawaliwe na wema na heshima.

Hivyo, inasisitizwa kuwa mwanamke atumie muda wake mwingi kuijenga familia yake ili aigwe na familia zingine na kuwa mfano bora kwa jamii. Siri ya nyumba yake na changamoto zimwezeshe kukua na kufikiria jinsi ya kukabiliana nazo bali isiwe fursa ya kutangaza kwa watu wengine kwani suluhu ni bidii yake wala sio kwa kuzianika changamoto hizi kwa umati.

Mwanamke anapotumia kinywa chake vizuri na kuongozwa na sheria mahususi ni lazima vile vile kuangalia njia na mapito ya familia yake. Taswira ya mwanamke katika jamii ni kuangalia njia za watu wa nyumbani kwake. Tunasoma: ***Huangalia sana njia za watu wa nyumbani mwake***, na kuhakikisha kuwa wameshughulikiwa vilivyo na kwamba wanapata amani katika makao yale. Ina maana ya tabia za watu wake (watoto). Halafu pia mwanamke huyu mzuri asiwe mvivu. Ana jukumu la kumhimiza kila mmoja katika familia yake kuwa na tabia njema.

Mke anafaa kuwa mfano bora kwa juhudi za kuzalisha mapato ya familia, kwani inapokumbwa na janga yeye ndiye atakayelaumiwa pakubwa kwa uzembe wala ni

nadra sana wanaume kulaumiwa: ***Wala hali chakula cha uvivu***. Kwa hivyo, mwanamke ajizatiti kutumia hekima yake katika usimamishaji wa nyumba yake ili asije akalaumiwa.

Solomoni anaendelea kusema kuwa kutokana na sifa hii ya mwanamke kumtunza mume wake, mume huyu atajulikana katika miji na maeneo mbalimbali. Kila mara mume anapoketi na wazee wenzake ataweza kutambuliwa kwa sababu ya heshima kutoka kwa mke wake. Tazama maelezo yafuatayo katika MF 54:

**MF 54**

> Mume wake hujulikana malangoni;
> Aketipo pamoja na wazee wa nchi.
> (KCM 31:23)

Katika MF 54, tunaelezwa kwamba mwanamke mwema humfanya mume wake kuheshimiwa na kupewa hadhi ya juu na wenzake kumsikiza kila mara anapozungumza. Tunaelezwa kuwa: ***Mume wake hujulikana malangoni,aketipo pamoja na wazee wa nchi.***

### 4.6 Mwanamke kama Mfanyikazi katika Ndoa

Katika hali ya kawaida, mwanawake katika jamii nyingi ulimwenguni hutarajiwa kutekeleza majukumu ya kimsingi ambayo humsawiri kama mfanyikazi ndani ya nyumba. Licha ya mwanamke kumtunza mume wake, amechorwa kama mfanyikazi anayependa kazi yake. Katika ndoa, mwanamke amechorwa kama mwenye bidii, anayefanya kazi kwa mikono yake bila kushurutishwa. Amesawiriwa kama mfanyikazi ili kumsaidia mumewe katika kukimu mahitaji ya familia. Kwa hiyo, kufanya kazi ni kwa wote wawili; mke na mumewe. Mchango huu husaidia majukumu kuwa mepesi.

### 4.6.1 Mwanamke kama Mfanyikazi katika UWM

Katika *Utendi wa Mwanakupona*, mwanamke amesawiriwa kuwa mwenye bidii na hujitafutia pato lake mwenyewe na kuezeka pesa hizo katika miradi kama ukulima. Je, mwanamke wa leo, hapendi kuezeka na kupata mali zaidi? Je, huu ni ukandamizaji? Wosia huu ni wa kumfanya mwanamke awe huru kiuchumi. Hii ni taswira ya mwanamke mfanyikazi. Katika ubeti wa 37, Mwanakupona anamhimiza bintiye vile vile kufanya kazi bila kudharau kazi yoyote ile katika kudumisha usafi. Wazo hilo linaelezwa katika MF 55 kama tunavyosoma hapa chini.

**MF 55**

Mwanangu siwe mkoo,
Tenda kama uonao,
Kupea na kuosha choo,
Sidharau mara moya
(UWM ubeti 37)

Katika MF 55, mwanamke anapaswa kuwa safi na asiwe mchafu. Mwanakupona anamweleza bintiye kuwa taswira ya mwanamke katika jamii ni kuweza kutekeleza wajibu wake bila kuelezwa na yeyote. Anasisitiza kuwa kila mwanamke azingatie unadhifu nyumbani. Tunaelezwa: ***Mwanangu siwe mkoo, Tenda kama uonao,*** na kwamba siku zote anapaswa kuzingatia usafi nyumbani. Hili ni jukumu la mwanamke na majukumu haya ayatekeleze bila kushurutishwa au kuogopa madhara ya kutotii. Mwanamke anahimizwa kuyatekeleza majukumu ya usafi, kuosha chooni bila kudharau kazi yenyewe. Tunasoma: ***Kupea na kuosha choo, sidharau mara moya***.

Vile vile Mwanakupona anamhimiza bintiye kufanya bidii nyumbani kwake ili mume wake amfurahie zaidi kama tunavyosoma katika MF 56:

**MF 56**

Nyumba yako i nadhifu,
Mumeo umsharifu,
Wakutanapo sufufu,
Msifu ukimweteya
(UWM ubeti 42)

Katika MF 56, Mwanakupona anamhimiza bintiye kufanya kazi kwa mikono yake mwenyewe, aifanye nyumba yake nadhifu na ya kupendeza kwa ajili ya mumewe. Tunaelezwa kwamba: ***Nyumba yako i nadhifu, mumeo umsharifu.*** Hivyo basi, ni jukumu la kila mwanamke kuhakikisha nyumbani kwake kunanadhifishwa vilivyo ili kila mara mume anapoingia ajihisi yu kwenye mazingira safi na ya kuvutia.

Rafikizo mumewe wanapokutana katika nyumba hiyo, mumewe atapewa sifa kwa kazi nzuri inayofanywa na mkewe. Tunaelezwa kuwa: ***Wakutanapo sufufu, msifu ukimweteya***. Sifa hizi anazopewa na rafiki wa mumewe ni dhihirisho tosha kwamba mume huyu alipata mwanamke mkomavu aliyetokota na akaiva kutokana na mafunzo mazuri kwa wanawake.

### 4.6.2 Mwanamke kama Mfanyikazi katika UWA

Mawazo kama haya yanadhihirika katika *Utendi wa Ayubu* pale ambapo Rehema mke wa Ayubu, anajitolea kwa udi na uvumba ili kuhakikisha kuwa mumewe anapata lishe alipokuwa anaugua, kwa sababu Ayubu mwenyewe hangeweza kufanya kazi ya kujikimu. Katika MF 57 tunasoma kwamba:

**MF 57**

Akawata masindizi
Rehema kitenda kazi
Ili kupata khubuzi
Kumpa wake rijaa
(UWA ubeti 127)

Katika MF 57 tunaelezwa kuwa *Utendi wa Ayubu* unadhihirisha kuwa Rehema alijinyima usingizi wake ili atekeleze majukumu yake. Jambo ambalo si rahisi kwa wanawake wa leo. Anaeleza kuwa: ***akawata masindizi, Rehema kitenda kazi.*** Rehema anajinyima usingizi ili mume wake aweze kupata mahitaji yake ya kila siku bila kupungukiwa wala kuombaomba kutoka kwa jamii yake. Tunaelezwa kwamba: ***ili kupata khubuzi, kumpa wake rijaa.*** Rehema alishughulika ili mumewe apate chakula cha kila siku. Sifa hii haipo kwa wanawake wengi wa leo ambapo wengi wanajifikiria tu bila kuwajali waume zao.

Katika *Utendi wa Ayubu* vile vile, Rehema anavumilia na kuingia kila nyumba na kusema kuwa yu tayari kuwatumikia. Anasema kuwa yu tayari kutumwa kwa shughuli zote za nyumbani, la muhimu kwake ni kutimiza mahitaji ya jamii yake kama tunavyosoma katika MF 58:

**MF 58**

Rehema asikasiri
Akingia kulla dari
Kawambia ni tayari
Taka kuwatumikia
(UWA ubeti 128)

Katika MF 58 tunaelezwa kuwa mwanamke ametunukiwa nafasi nzuri ya kufanya kazi katika jamii yake bila kulalamika kwa kuwa sifa hii ndiyo inayomtambua kuwa mwanamke mwenye bidii. Tunasoma kwamba: ***Rehema asikasiri, akingia kulla dari.*** Rehema alizunguka kutoka kwa nyumba moja hadi nyingine akitafuta kazi kwa uvumilivu, na alikuwa tayari kufanya lolote, muhimu ni kuwa mumewe apate mkate wa siku na kutojisumbua. Tunaelezwa kuwa: ***Kawambia ni tayari taka kuwatumikia.*** Hali hii inadhihirisha mwanamke aliyejitolea kufanya kazi ili jamii yake inawiri.

Pamoja na hulka mbalimbali alizonazo mwanamke katika jamii, kufanya kazi ni sifa kubwa na yenye hadhi ya juu hasa kwa wasichana wanaotaka kuolewa na hata wale walio katika ndoa tayari. Ni muhimu kwa mwanamke kuwa na bidii katika kazi, kwa sababu mara baada ya kuolewa, yeye (mwanamke) na mumewe wanapaswa kujitegemea wenyewe. Kujitegemea huko kunaongezeka zaidi ikiwa mwanamke huyo ameolewa katika ndoa ya ukewenza, au ameingia katika ukewenza baada ya mumewe kuamua kuoa mwanamke mwingine. Hivyo basi, ni muhimu kutambua kwamba ili mwanamke aweze kumudu maisha yake pamoja na ya jamii yake, hana budi kujibidiisha katika kazi.

Katika *Utendi wa Ayubu* vile vile, Rehema anajitolea kufanya kazi za aina zozote. Anaamua kutembea kutoka familia moja hadi nyingine huku akiomba ajira yoyote ili aweze kumlisha mumewe. Tunayasoma hayo katika MF 59 hapa chini:

**MF 59**

Nitumani kazi zenu
Zilo mayumbani mwenu
Kwamba ni kutwewa ngano
Mkinipa tawetea
(UWA ubeti 129)

Katika MF 59 hapo juu, tunaelezwa kwamba mkewe Ayubu alikuwa tayari kufanya kazi yoyote ile bila kuchagua. Rehema anasema kuwa wamtumie katika shughuli zao zote za nyumba. Tunaelezwa kuwa: ***Nitumani kazi zenu,zilo mayumbani mwenu,*** hata akitumwa kupepeta ngano kwa uteo, atairudisha. Tunaelezwa kuwa: ***Kwamba ni kutwewa ngano, Mkinipa tawetea***. Rehema anaamua kuwafanyia kazi wale ambao walijiweza kiuchumi ili hata yeye aweze kupata chakula cha familia yake.

Mwanamke anahimizwa kufanya kazi yoyote kusaidia familia inapobidi, si kumwachia mwanamume pekee. Hii ni taswira ya mwanamke katika kazi za kifasihi na matini za kidini tulizozichagua, kwamba mwanamke anaweza kujinyima raha zake kwa ajili ya familia yake.

### 4.6.3 Mwanamke kama Mfanyikazi katika WUB

Jinsi ilivyo katika UWM na UWA, mwanamke amechorwa kama mfanyikazi. Japo Solomoni ametupa taswira ya mwanamke mrembo kwelikweli, lakini vile vile ametupa picha ya shambani. Anamwalika mpenzie waende shambani waone iwapo mizabibu imechanua. Kwa mfano katika WUB 7: 12,

**MF 60**

Njoo, mpendwa wangu,
Twende mashambani....
Twende mapema hata mashamba ya mizabibu
Tuone kama mzabibu umechanua ,
Na maua yake yamefunuka,
Kama mikomamanga imetoa maua...
(WUB 7: 12)

Katika MF 60, Solomoni anamhimiza mpenziye waende shambani waone mizabibu iwapo imechanua. Mwanamke anahitajika kufanya kazi na kuhakikisha kuwa mimea shambani imetunzwa vizuri. Taswira ya mwanamke mfanyikazi ilibainika wazi katika UWM, UWA na KCM lakini Solomoni hajaizungumzia sana sifa hii katika WUB kwa kuwa amejikita katika urembo wa mpenzi wake. Amemchora mwanamke aliyerembeka na ambaye mume wake amejitolea kumtafutia lolote analojitakia bustanini.

### 4.6.4 Mwanamke kama Mfanyikazi katika KCM

Solomoni anatupa picha ya mwanamke mfanyikazi katika Kitabu cha Methali anapozungumzia mwanamke mwenye bidii ya mchwa. Haya yanajidhihirisha katika MF 61 na MF 62:

**MF 61**

> Hujifunga nguvu viunoni kama mshipi;
> Hutia mikono yake nguvu
> (KCM 31:17)

**MF 62**

> Huona kama bidhaa yake ina faida;
> Taa yake haizimiki usiku.
> Hutia mikono yake katika kusokota;
> Na mikono yake. Huishika pia
> (KCM 31:18)

Katika MF 61 na MF 62 hapo juu, Solomoni anasema kuwa mwanamke mwenye bidii hujizatiti kuleta mapato nyumbani. Tunaelezwa kuwa: ***hujifunga viunoni kama mshipi***, ili aweze kufanya kazi kwa bidii. Vile vile mwanamke huyu hutumia mikono yake vizuri kwa kufanya kazi. Tunaelezwa kuwa: ***hutia mikono yake nguvu.*** Hii ni taswira ya mwanamke mwenye nguvu aliyeamua kufanya bidii kwa ajili ya familia yake. Huyu ni mwanamke aliyeamua kutozembea bali kujitolea kwa mali ili kutafuta riziki kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya jamii yake.

Mwanamke wa aina hii ni yule ambaye ameamua kuishughulikia familia yake na kwamba taa yake haizimiki usiku wote, ***taa yake haizimiki usiku***, akifanya kazi ya kusokota nyuzi kwa mikono yake na kutumia cherehani kushona nguo kwa ajili ya familia yake. Kazi hii huifanya usiku kucha. Ni mwanamke mfanyibiashara shupavu, hukesha kufanya kazi ili apate pesa kukimu familia yake. Mwanamke mfanyikazi anatambulika katika jamii yoyote ile, hali hii si ukandamizaji bali humpatia

mwanamke nafasi spesheli katika familia yake. Mwanamke lazima ajitahidi kumsaidia mumewe katika mahitaji ya familia. Haya tunayapata katika MF 63 hapa chini:

**MF 63**

Hufanya nguo za kitani na kuziuza;
Huwapa wafanya biashara mishipi
(KCM 31:24)

Katika MF 63, tunaelezwa kuwa mwanamke katika kifungu hiki uhakikisha kuwa mume wake na watoto wamevaa mavazi mazuri na pia kuziuza zingine kwa ajili ya mapato. Tunaelezwa kuwa: ***hufanya nguo za kitani na kuziuza.*** Mwanamke huyu anafanya biashara ili aweze kuzipata hela za kuikimu jamii yake. Tunaelezwa kuwa: ***huwapa wafanya biashara mishipi.*** Dhana kuwa wanawake ni wavivu na wasioweza lolote ni potovu kwa kuwa wanawake katika *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu*, Methali na Wimbo Ulio Bora ni wakakamavu walioamua kufanya kazi kwa mikono yao kwa ajili ya familia zao. Wanawake kwa hivyo hawajakandamizwa wanapofanya kazi hizi bali ni hulka muhimu zinazomtambua mwanamke kuwa mkamilifu na aliyewajibika katika ndoa yake. Mwanamke anapowajibika, ndoa hudumu na mume atafurahia jitihada za mkewe kwamba anachangia katika mahitaji ya familia. Mume asiyetambua hili, basi ni katili asiyeweza kuishi na mke. Mwanamke anaonyeshwa zaidi katika Kitabu cha Methali 31:15-16 kuwa ni mfanyakazi anayerauka asubuhi na mapema. Katika MF 64 tunaelezwa kuwa:

**MF 64**

Tena huamka,
kabla haujaisha usiku;
Huwapa watu wa nyumbani mwake chakula;
Na wajakazi wake sehemu zao
(KCM 31:15)

Kwa mujibu wa MF 64, tunaelezwa kuwa Mwanamke huyu huamka mapema na kushughulikia jamii yake kama tunavyoelezwa katika kifungu kifuatacho: ***huamka kabla haujaisha usiku.*** Mwanamke huyu si mvivu bali amejitolea kurauka ili kuishughulikia jamii yake. Mwanamke katika KCM, huwapa watu wa nyumbani kwake chakula. Tunaelezwa kwamba: ***huwapa watu wa nyumbani mwake chakula,*** na pia kuwaonyesha wajakazi kazi zao za kufanya katika sehemu zao alizowatengea. Hivi ni kwamba hutayarisha chakula cha jamaa yake asubuhi sana kabla ya kupambazuka na vile vile kuwapangia wajakazi kazi zao za siku.

Kwa hivyo, mwanamke amesawiriwa kama mtu wa bidii, anayejua majukumu yake na kusimamia kazi za nyumbani. Hadi leo kuna wanawake wanafanya haya, si mashambani tu hata mijini. Iwapo mwanamke anafanya hivi, huwa anawajibika na si kukandamizwa. Hata wale wanawake wasomi au waliosoma, huwajibika katika kupanga kazi za nyumbani iwapo wana wajakazi. Hawawaachii tu waume zao wafanye. Na kuwajibika si makosa hata kidogo, ni jambo jema. Uchanganuzi huu unadhihirisha kuwa mwanamke anaweza kufanya kazi ili jamii yake ipate lishe na hii ndiyo taswira ya mwanamke katika MF 65:

**MF 65**

Huangalia shamba, akalinunua;
Kwa mapato ya mikono yake
hupanda mizabibu
(KCM 31:16)

Katika MF 65, tunaelezwa kuwa mwanamke hununua shamba na hupanda mizabibu ili jamii yake iwe na chakula cha kuwatosha. Katika kufanya kazi ya ukulima, tunaona mwanamke akinunua shamba. Tunaelezwa kuwa: ***huangalia shamba akalinunua,*** na kupanda mizabibu (***hupanda mizabibu),*** kwa ajili ya mapato ya jamii. Mwanamke hununua shamba kwa pesa zake mwenyewe alizozipata kwa kufanya kazi na katika shamba hilo, kwa jitihada yake mwenyewe, hupanda mimea ya mizabibu. Anapouza zabibu hizo, hupata pesa ambazo humwezesha kujimudu kimaisha. Mwanamke anatarajiwa kumsaidia mumewe katika majukumu ya kikazi nyumbani. Hayo tunaelezwa katika MF 66 hapa chini:

**MF 66**

> Afanana na merikebu za biashara;
> Huleta chakula chake kutoka mbali
> (KCM 31:14)

Katika MF 66, tunaelezwa kwamba wanawake Wakristo walio ndani ya ndoa wanahimizwa kufanya bidii ya mchwa kila uchao ili waweze kuzilisha familia zao. Katika ubeti huu, Mfalme Solomoni anatoa ushauri kwa mwanamke ambaye angependa kujenga familia yake; kwamba ni lazima afanye kazi siku zote ili aweze kuleta chakula mezani. Kwa jinsi hiyo mume pamoja na watoto wake wanaweza kumfurahia. Katika Methali 31:14, mwanamke anahimizwa kufanya kazi kwa bidii ili familia yake iweze kupata mahitaji ya kila siku: ***Huleta chakula chake kutoka mbali***.

Kutokana na maelezo haya, mwanamke anaweza kumsaidia mumewe katika shughuli ya kutafuta chakula cha wanajamii na kwa kufanya hivi, kutakuwa na amani katika familia yake. Mwanamke akitia bidii maishani, familia yake itanawiri na kufanikiwa. Ushauri kama huu unatolewa pia katika Agano Jipya. Katika kitabu cha Wathesalonike wa Kwanza 3:10, Mtume Paulo anawaeleza wathosolanike kwamba:

***Mtu yeyote asiyefanya kazi na asipate chakula***. Ingawa ushauri ni kwa watu wote kwa jumla, wanawake pia wamo ndani. Kwa jinsi hiyo ni lazima wafanye kazi ili waweze kulisha familia zao. Kwa mfano katika KCM (MF 67) tunasoma kuwa:

**MF 67**

> Hutafuta sufu na kitani;
> Hufanya kazi yake ya mikono kwa moyo
> (KCM 31:13)

Kitabu cha Methali 31:13, mwanamke amedhihirishwa kama mfanyikazi katika familia yake. Tunaelezwa kuwa: ***Hufanya kazi yake ya mikono kwa moyo***. Ubeti huu unadhihirisha mwanamke ambaye amejizatiti kufanya kazi kwa mikono yake mwenyewe. Maelezo yake Solomoni kumhusu mwanamke mfanyikazi ni kuwa yeye (mwanamke) hufanya kazi yake kwa moyo wake wote na kwamba hutafuta aina zote za vyakula hata kutoka mbali ili familia yake iweze kupata lishe bora. Hii ni taswira ya mwanamke katika ndoa, ufanyaji wa kazi hufanya ndoa kunawiri na kupata mapato ya kujimudu.

### 4.7 Mwanamke kama mtekelezaji wajibu katika Ndoa

Kama tulivyojadili katika kipengele cha tano, tumechorewa mwanamke aliye mwema kwa mume wake na jamii kwa jumla. Mwanamke huyu mwema pia anaweza kutekeleza wajibu wake bila kushurutishwa na yeyote. Taswira ya mwanamke anayewajibika inajidhihirisha katika kazi zetu teule za fasihi na matini za kidini. Al-Amin (1936) anaelezea kuwa ni wajibu wa mke kumtii mumewe katika mambo yaliyo halali na kukaa nyumbani wala asitoke ila kwa ruhusa ya mumewe, asimruhusu mtu yeyote asiyemtaka mumewe kuingia kwake. Fundisho hili la Kiislamu linaoana na matini tulizozichagua za kifasihi na za Kidini.

### 4.7.1 Uwajibika wa Mwanamke katika UWM

Kutokana na majukumu makubwa aliyonayo katika kufanya kazi, mwanamke anahitaji watoto wenye afya watakaomsaidia. Vile vile, watoto watamsaidia mama akiwa mzee. Kutokana na hilo, watoto wana umuhimu mkubwa katika ndoa kwa sababu wanaweza kuleta mchango wao mkubwa kwa familia yake. Vile vile, haitoshi kwa mwanamke kuwa na watoto, kwani anapaswa kuhakikisha kuwa watoto wanalelewa kulingana na mila na desturi za jamii inayohusika. Kwa kawaida, tabia mbaya aliyonayo mtoto inatokana na malezi mabaya aliyoyapata kutoka kwa mama yake kwa sababu mama huwa karibu na mtoto kwa muda mrefu. Haya yanajitokeza vyema katika *Utendi wa Mwanakupona*, ambapo Mwanakupona anamwita bintiye aje ili ampatie wosia wa maisha katika MF 68:

**MF 68**

Negema wangu binti,
Mchachefu hasanati,
Upulike wasiati,
Asaa ukazingatiya
(UWM ubeti 1)

Katika MF 68, Mwanakupona anamshauri bintiye kuzingatia wosia wake kuhusu uwajibikaji katika ndoa. Tunaelezwa kuwa: ***negema wangu binti,*** asikize wosia na kuuzingatia maishani mwake. Wosia huu utamsaidia kuishi vyema na mumewe. Kwa hivyo mama hapa anaonyeshwa kuwa mlezi anayemwadilisha mwanawe. Tunaelezwa kuwa: ***asaa ukazingatiya.*** Mwanakupona anasisitiza maelekezi mema kwa watoto nyumbani.

### 4.7.2 Uwajibikaji wa mwanamke katika UWA

Suala hili linajitokeza katika *Utendi wa Ayubu* pale ambapo Rehema mkewe Ayubu amechorwa kama mzazi kwani anafanya kila awezalo kuhakikisha kwamba familia

yake imepata mahitaji yake ya kila siku. Kwa mfano katika ubeti wa 288 ambao umeonyeshwa katika MF 69:

**MF 69**

Umekusa sumbuko
umezanya nywee zako
wala usiche ziteko
za wendo kukutekea
(UWA ubeti 288)

Kupitia kwa MF 69, Ayubu anamshukuru mkewe kwa kuwa mvumilivu. Tunaelezwa kwamba: ***umekusa sumbuko,*** na kwa kujitolea kwa vyovyote ili kuhakikisha kuwa familia yake inapata mahitaji yake. Rehema alivumilia taabu, akauza nywele zake na bila kuogopa vicheko vya wenzake. Tunaelezwa kwamba: ***umezanya nywee zako.*** Mwanamke huthamini nywele zake sana na anapoamua kuziuza huonyesha hali ya kujinyima na kujitolea kwa moyo wote katika enzi hizo huko Uyahudini. Rehema anaamua kuwa mzazi kwa kujinyima raha na starehe zake ili jamii yake iweze kufanikiwa. Wanajamii walimcheka kwa mateso yake: ***za wendo kukutekea,*** lakini aliamua kuwa mvumilivu.

### 4.7.3 Uwajibikaji wa Mwanamke katika WUB

Mwanamke katika Wimbo Ulio Bora ana wajibu wa kumpenda mume wake. Ni mwanamke aliyejitolea kumpenda mumewe siku zote.

**MF 70**

Nitie kama muhuri moyoni mwako,
Kama muhuri juu ya mkono wako,
Kwa maana upendo una nguvu kama mauti,
Na wivu ni mkali kama ahera...
(WUB 8:6)

Mwanamke kulingana na Solomoni anatakikana kumweka kama muhuri moyoni na kwenye mkono wake. Tunaelezwa kuwa: ***Nitie kama muhuri moyoni mwako.*** Mwanamke ana wajibu wa kumshughulikia mume wake kwa masuala yake yote, hasa ya mahaba. Solomoni anaelezea kuwa upendo una nguvu kama mauti, ***Kwa maana upendo una nguvu kama mauti***, na kwa hivyo mwanamume aliyejotolea kupenda ni lazima apendwe pia. Suala hili limeathiri wanawake wengi wa sasa kwa kuwa ni wajibu wa mwanamke kuwa mwaminifu na kumpenda mwanamume wake vilivyo. Wapenzi wengi wamefikia kujiuua au kuwaua wenzao iwapo mmoja wao hajawajibika katika safari ya mapenzi.

### 4.7.4 Uwajibika wa Mwanamke katika KCM

Katika Kitabu cha Methali, Solomoni anamwelekeza mke kuwa mzazi katika masuala muhimu ya jamii kama inavyojitokeza katika MF 71 hapa chini:

**MF 71**

> Wanawe huondoka na kumwita heri;
> Mumewe naye humsifu, na kusema,
> Binti za watu wengi wamefanya mema,
> Lakini wewe umewapita wote
> (KCM 31:28-29)

Katika MF 71, tunaelezwa kuwa mwanamke akiyatekeleza majukumu yake kama mama mzazi, wana wake watamfurahia na kumpa sifa huku wakimtakia heri. Tunaelezwa kuwa: ***wanawe huondoka na kumwita heri.*** Watoto wake humpa sifa hizi kwa kuwa amewalea kwa njia inayostahili. Watoto wengi hawana uhusiano mwema na mama zao kwa kuwa akina mama wengi hawafuati mkondo mwema wa kuwalea watoto wao. Mwanamke huyu anazipata sifa hizi kwa kuwa yeye aliamua kuwa mama mzazi, mume wake vile vile anamsifu kochokocho kwa kusema kuwa: ***Binti za watu wengi wamefanya mema, lakini wewe umewapita wote.*** Mume wake

anamlinganisha na wanawake wengine lakini anatambua kuwa hakuna mwanamke anayefanana na mkewe.

### 4.8 Taswira ya Mwanamke Asiyenung'unika, Mvumilivu na Mpole Katika Ndoa

Kutokana na kipengele cha saba kuwa mwanamke anatakikana kuwajibika katika ndoa, ni dhahiri kuwa akiwajibika hatakuwa na manung'uniko, atakuwa na uvumilivu na tabia yake itakuwa ya upole. Mafundisho ya Kiislamu kama anavyoeleza Al Farsy (1942), katika *Ndoa na talaka,* ni kuwa mwanamke aliyeoleka anatarajiwa kuwa na rai nzuri na kuwa mvumilivu katika ndoa ili kuepuka talaka. Mwanamke Asiwe mwepesi wa kunung'unika na kutotosheka kwa yale anayopewa na mume wake. Hii ni kwa sababu, ni jukumu la mwanamume kuyakidhi mahitaji ya mke au wanawake wake pasi wengine wanaweza kulalamika na kwa hivyo kutoridhika katika ndoa yao. Anaendelea kuzungumzia kuwa pana mtu na nusu mtu na si mtu. Anasema kuwa mtu ni yule mwenye rai nzuri na akataka rai za wengine pia ili azilinganishe na yake, atazame ipi iliyo bora zaidi. Na nusu mtu ni yule mwenye rai nzuri wala hataki kutazama rai za wengine-huyu huenda akakosa. Na si mtu ni yule asiyekuwa na rai nzuri wala hataki kusikiliza rai nzuri za wengine; akaona ndiyo nzuri.

#### 4.8.1 Taswira ya Mwanamke asiyenung'unika katika Ndoa

Huyu ni mwanamke aliyekubali hali yake ya maisha na kwamba anaridhika na chochote anachopewa na mumewe. Mwanamke huyu hamlinganishi mumewe na wanaume wengine labda waliojaliwa mali na vyeo katika maisha.

##### 4.8.1.1 Taswira ya Mwanamke asiyenung'unika katika UWM

Katika UWM (beti 51, 52) mama anamwelekeza bintiye kuwa ni vyema kama atauchunga ulimi wake, na kuiga tabia zake, kisa na maana kuwa alikaa kwa ndoa kwa muda mrefu bila ugomvi wowote. Mifano MF 72 na MF 73 inatoa maelezo zaidi:

**MF 72**

Mama sinoe ulimi,
Nioleza wako umi,
Naliowa nyaka kumi,
Tusitete siku moya
(UWM ubeti 51)

**MF 73**

Naliowa na babako,
Kwa furaha na ziteko,
Tusondoleane mbeko,
Siku zote twalokaa
(UWM ubeti 52)

Katika MF 72 na MF 73, tunamwona Mwanakupona akimpa bintiye wosia asitumie ulimi wake vibaya kwa kulalamika au kumtusi mumeo. Anamweleza kuwa: ***Mama sinoe ulimi,*** bali azifuate nyayo za wanawake waliokaa kwa ndoa kwa miaka kumi na hawakungombana na mumewe hata siku moja. Tunaelezwa kuwa: ***naliowa nyaka kumi, tusitete siku moya.*** Mwanakupona alijua jinsi ya kutumia ulimi wake kwa njia inayostahili kwa kusema tu yaliyo mema.

Mwanakupona anajivunia kuwa waliishi na mumewe kwa miaka mingi wakiheshimiana bila kugombana hata siku moja. Anasema kuwa: ***Tusondoleane mbeko, Siku zote twalokaa***. Haya yaliwezekana kwa sababu Mwanakupona aliacha kulalamika wala kunung’unika. Iwapo matatizo yoyote yatatokea, ni vyema mwanamke atafute muda unaofaa kisha atoe hoja ambazo ni za kweli, si kwa kulalamika, lakini afanye hivyo, kwa namna ya kushauriana na mume wake. Kwa njia hii, atamfanya mumewe kuanza kujenga hisia za upendo na mapatano na yatasababisha familia kubaki salama jinsi Mwanakupona anavyosema waliishi kwa furaha: ***naliowa na babako, kwa furaha na ziteko.***

Baadhi ya wanawake ambao wametawaliwa na fikra hasi na wabinafsi hawatambui kwamba waume zao wanachoka sana na fadhaa baada ya kazi ya siku nzima. Waume wao wanaporejea nyumbani, badala ya kuwapa muda wa kutosha wapumzike na kupata nguvu, wao huanza kuwashambulia kwa mfululizo wa malalamiko. Wanawake wa aina hii hudhani kwamba waume zao huenda katika shughuli ambazo ni kinyume na matakwa ya ndoa. Wao husahau kuwa waume wao hukutana na mamia ya matatizo kila wanapokuwa katika shughuli zao za hapa na pale. Kwa hivyo, wanaporejea nyumbani wasiwasilishe malalamiko yao yote kwa wakati mmoja wala wasiwafanye wajihisi kuwa wanahatia ya kuwa wanaume.

#### 4.8.1.2 Taswira ya Mwanamke asiyenung'unika katika UWA

Rehema anajitolea kumshughulikia mumewe bila manung'uniko yoyote, anawasihi wanajamii kumpa kazi ya kuikimu familia yake kama tunavyoelezwa katika MF 74

**MF 74**

Niwakatulie pete
Niwasinge niwapote
Mnipe name mkate
Mlapo ukisali
(UWA ubeti 130)

Katika MF 74, tunaelezwa kwamba Rehema anazungukazunguka kutoka nyumba moja hadi nyingine huku akiwaomba nafasi ya kuwang'arishia pete zao na kuwasuka nywele ili angalau aweze kujimudu kimaisha na kwa jinsi hiyo apate chakula cha kumlishia mumewe. Tunaelezwa kuwa: ***Niwasinge niwapote.*** Muhimu ni kuwa apate chakula hata kama ni masazo ya mkate wanapokula. Tunasoma kuwa: ***Mnipe name mkate***. Hivyo basi, Rehema alikuwa amefikia hali ya kujitolea kumsaidia mume wake. Anajitolea kufanya kazi zilizodunishwa ili aweze kupata chakula cha kumpa

mumewe. Rehema anaendelea kuomba kazi duni mno katika jamii kama tunavyosoma katika MF 75 na MF 76:

**MF 75**

Na tena msinikinde
Niyapoona kipande
Cha mkate nikitunde
Tiati nichangukia
(UWA ubeti 131)

**MF 76**

Wala hamna mashaka
Kikitunda kichanguka
Kwani kitakula paka
Enyi hakitowafaa
(UWA ubeti 132)

Katika MF 75 na MF 76, Rehema anaomba asikatazwe kuokota kipande cha mkate. Tunasoma kuwa: ***na tena msinikinde, niyapoona kipande,*** hata kama kimeanguka chini, na anawaomba wasijali aokotapo kilichoanguka kwani hicho kitaliwa na paka bali si wao, ***cha mkate nikitunde.*** Kwa hivyo wamruhusu kukiokota kuwa chakula kwake. Alifanya hivi kwa kuwa hakuwa na lingine au mtu wa kumtegemea ili kumsaidia mumewe aliyekuwa anaugua na mwenye njaa.

Rehema anasema kuwa wasimjali aokotapo kiangukacho. Tunasoma kuwa: ***kikitunda kichanguka,*** kwani hicho chafaa kuliwa na paka lakini badala yake kingemfaa. Rehema anajifananisha na paka anayeokota chakula kilichoanguka. Tunasoma: ***Kwani kitakula paka, enyi hakitowafaa.*** Rehema alikuwa tayari kuteseka kwa ajili ya mumewe, la muhimu kwake ni kuwa mumewe aweze kupata nafuu na shibe.

Kwa maoni yangu, hii ni taswira ya mwanamke aliyejitolea mhanga kuhakikisha jamii yake inadumu na kupata lishe licha ya matatizo wanayoyapitia. Rehema anatupa sura ya mwanamke mkakamavu aliye tayari kuipigania ndoa yake kwa kila hali na hivyo

ndivyo mwanamke anastahili kuwa katika ndoa. Mwanamke anastahili kujitoa mhanga na kufanya kazi yoyote iliyopatikana ili kuikimu jamii yake, hii si kukandamizwa bali kuishughulikia jamii.

#### 4.8.1.3 Taswira ya Mwanamke asiyenung'unika katika KCM

Katika Kitabu cha Methali 31:26, mwanamke anahimizwa awe mtu wa kuzungumza kwa hekima na mafundisho ya ulimi wake yawe ni mazuri kama tunavyosoma katika MF 77:

**MF 77**

> Huzungumza kwa hekima na mafundisho ya kuaminika
> yapo ulimini mwake.
> (KCM 31:26)

Maelezo katika MF 77, yanatuonyesha picha ya mwanamke mzuri kuwa ni yule ambaye anaepukana na hali yoyote ya manung'uniko kwa sababu huenda yakachangia kubomoka kwa nyumba yake. Mwanamke anastahili kutumia ulimi wake vizuri ili kuepuka matatizo yanayotokea kila mara katika jamii.

### 4.8.2 Taswira ya Mwanamke  Mvumilivu katika Ndoa

Sawia na mwanamke asiyenung'unika, tumechorewa mwanamke mvumilivu anayeishi kwa amani wakati wote. Mwanamke mvumilivu hawezi kuwa mwepesi wa kunung'unika.

#### 4.8.2.1 Taswira ya Mwanamke mvumilivu katika UWM

Mwanamke katika UWM anapewa wosia wa kumtunza mumewe na hali hii inahitaji uvumilivu, la sivyo wanawake wengine watashindwa na majukumu kama haya. Maelezo haya yanajidhihirisha katika MF 78:

**MF 78**

Kilala siikukuse,
Mwegeme umpapase,
Na upepo nasikose,
Mtu wa kumpepeya
(UWM ubeti wa 31)

Maelezo kutoka MF 78, yanaonyesha nafasi ya mwanamume jinsi anavyostahili kutunzwa na kupewa heshima zake kama mfalme wa familia. Kwa mfano, kutompigia kelele anapolala ili asisumbuke katika usingizi wake. Tunaelezwa kuwa: ***Kilala siikukuse.*** Mwanamke anashauriwa ampapase mumewe, ***Mwegeme umpapase***, na kunapokuwa na joto usiku, ampepee. Tunasoma kuwa: ***Na upepo nasikose, mtu wa kumpepeya.*** Badala ya kumheshimu mumewe, mwanamke anaweza kuamua kuzua ugomvi wa mara kwa mara unaoweza kusababisha hali ya mtafaruku kwenye familia na wanandoa husika kukosana kwa kila wanalofanya. Kwa jinsi hiyo, mume na mke hujikuta katika hali ya kutoelewana. Familia kama hiyo kwa kweli si nzuri.

Tukiangazia ubeti huu, hali kama hiyo inakataliwa kabisa. Tunamwona mwandishi akimjenga mwanamke ambaye hapendi ugomvi, yaani yule ambaye furaha yake iko kwa mumewe na daima anataka kumfurahisha mumewe. Kwa hivyo, tunaweza kusema kwamba mwanamke mkamilifu lazima awe mvumilivu na awe tayari kukabiliana na shida yoyote ambayo inaweza kutokea katika familia.

### 4.8.2.2 Taswira ya Mwanamke mvumilivu katika UWA

Katika ubeti wa 288 wa UWA, Rehema amechorwa kama mtu mvumilivu. Ushahidi huu unatolewa na mumewe Ayubu anapomwambia kuwa amevumilia taabu vya kutosha kwani hata aliuza nywele zake ili ampe mumewe lishe kama tunavyosoma katika MF 79:

**MF 79**

> Umekusa sumbuko
> Umezanya nywee zako
> Wala usiche ziteko
> Za wendo kukutekea
> (UWA ubeti 288)

Katika MF 79 tunapata kuwa kutokana na uvumilivu, Rehema anaamua kuuza kitu chake cha thamana ambacho ni nywele ili apate hela za kumshughulikia mumewe. Tunasoma kuwa: ***Umekusa sumbuko, umezanya nywee zako.*** Hii inaamanisha kuwa Rehema alikuwa tayari kupoteza lolote kwa ajili ya mumewe na hata hakujali wenzake ambao walimcheka au kumkebehi kwa matendo yake ambayo waliyaona kama ya kipumbavu. Tunaelezwa kuwa: ***wala usiche zitekoza, za wendo kukutekea.***

#### 4.8.2.3 Taswira ya Mwanamke Mvumilivu Katika KCM

Mwanamke katika KCM amepewa nafasi sawia na WUB. Kulingana na Solomoni katika Kitabu cha Methali, mwanamke anatakikana kufanya kazi kwa bidii ili familia yake inufaike na kunawiri vilivyo. Tazama maelezo yafuatayo katika MF 80:

**MF 80**

> Nguvu na hadhi ndiyo mavazi yake;
> Anaucheka wakati ujao
> (KCM 31:25)

Katika MF 80, Solomoni anabainisha picha ya mwanamke katika ndoa kuwa daima awe na nguvu na heshima yake. Vitu hivi viwili awe navyo kila wakati kama mavazi. Viwe kama mavazi anayoyavaa nyakati zote. Aya hii inasisitiza mwanamke afanye kazi na ajiwekee heshima yake daima. Tunasoma kuwa: ***Nguvu na hadhi ndiyo mavazi yake.*** Mwanamke vile vile anatakikana kutekeleza wajibu wake ili siku zijazo awe wa kucheka bali si wa kulia na kujuta kwa kutowajibika kama mwanamke

anayestahili. Tunasoma kuwa: ***Anaucheka wakati ujao.*** Mwanamke huyu ataucheka kwa kuwa alivalia mavazi ya heshima na nguvu kumaanisha hatajipata matatani kama wanawake wapumbavu ambao hawasimami katika nafasi zao vilivyo. Kufanikisha maisha ya familia ni wajibu wa mwanamke, kuhakikisha hata kama kipato ni kidogo anaitumia vizuri pasipo na uharibifu. Solomoni anasisitiza kuwa katika ufanisi wa familia, mchango mkubwa unamtegemea mwanamke.

### 4.8.3 Taswira ya Mwanamke Mpole katika Ndoa

Jinsi ilivyojitokeza katika kipengele hiki cha nane, kuchorewa mwanamke asiyekuwa na manung'uniko na mvumilivu, hali hii inamsababisha mwanamke huyu kuwa na tabia nzuri, tabia ya upole.

#### 4.8.3.1 Taswira ya Mwanamke mpole katika UWM

Mwanakupona, katika ubeti wa 28 na 29, anamhimiza bintiye kuwa mpole. Anamweleza kuwa aishi na mumewe kwa adabu na achunge asimghadhabishe, anapomkemea asimjibu na ajaribu awezavyo asimjibu mumewe. Hayo tunayapata katika MF 81 hapa chini.

**MF 81**

Keti naye kwa adabu,
Usimtie ghadhabu,
Akinena simjibu,
Itahidi kunyamaa
(UWM ubeti wa 28)

Katika MF 81 tunaelezwa kwamba mwanamke akiwa na imani na mume wake, chochote anatakachohitaji atapewa. Mamake anamhakikishia kilichomfanya adumishe ndoa yake kwa miaka mingi ni adabu nzuri kwa mumewe. Tunaelezwa kuwa: ***Keti naye kwa adabu.*** Mwanakupona anamtolea mfano wakati alipogombana na mumewe jinsi alivyonyenyekea: ***Akinena simjibu,*** hata kama hakuwa na kosa kwani mumewe

baadaye anatafakari na kujuta na hatimaye kuomba msamaha. Anamkumbusha kila mara kuwa mume ndiye kichwa cha nyumba, hana budi kuzifuata kanuni na sheria atakazopewa aolekapo. Katika MF 82 hapa chini tunapata maelezo zaidi.

**MF 82**

Enda naye kwa imani,
Atakalo simukhini,
We naye sikindaneni,
Mkindani huumiya
(UWM ubeti wa 29)

Iwapo mwanamke ataijali hali yake (MF 82) ya tabia na uhusiano alionao na mumewe, hatatenda kinyume na tabia njema. Mwanamke aishi kwa amani na mumewe na kila mume anachohitaji apewe. Tunaelezwa kuwa: ***Enda naye kwa imani, Atakalo simukhini.*** Awe dhahiri katika msimamo na tabia inayopendeza kwani nguzo bora zaidi ya kutegemea katika ndoa ni maadili mazuri ambayo yanaelekeza kwenye tabia inayopendeza. Mwanamke asigombane kwa kuwa hali hii inazusha hadhi ya mume, na kwamba anayegombana ndiye anayeumia. Tunasoma kuwa: ***we naye sikindaneni, mkindani huumiya.***

### 4.8.3.2 Taswira ya Mwanamke mpole katika UWA

Pia katika MF 83, mwanamke amechorwa kama mtu asiyependa kukasirika na awekaye ahadi bila kuivunja.

**MF 83**

Sidhani takasirika
Na nadhiri nimeweka
Upoapo uchinuka
Unipije mbati mia
(UWA ubeti 284)

Katika MF 83, tunaelezwa kwamba Rehema anapoambiwa atachapwa pindi tu atakapopata nafuu, yeye hakatai bali anaitikia wito wake kwani ni nadhiri aliyoiweka. Tunaelezwa kwamba: ***upoapo uchinuka, unipije mbati mia***. Katika ubeti huu, Rehema anadhihirisha sifa adhimu sana miongoni mwa wanawake wa leo ambao wako katika ndoa. Tunamwona mwanamke mtulivu anayependa amani. Yaani mkewe Ayubu anaonyeshwa kama mwanamke mwenye sifa za kutamanika na mume yeyote ambaye ameoa.

Tabia ya Rehema katika UWA ni ya kuvutia. Inadhihirisha mke aliyejitolea kumtii mumewe kwa hali zote kwa kuitambua nafasi yake na kwamba yeye ndiye kichwa cha familia. Mwanamke aliye na tabia nzuri huwa na shukrani tele kwa yale aliyofanyiwa.

#### 4.8.3.3 Taswira ya Mwanamke mpole katika KCM

Mtu yeyote mwenye tabia njema na inayopendeza, ni mtu ana mlahaka mwema na kila mtu maishani. Huyu ni mtu ambaye watu huvutiwa naye wakati wowote. Talaka nyingi hutokea kwa sababu ya tabia zisizolingana za mume na mke. Takwimu juu ya talaka zinaonyesha kuwa chanzo cha ugomvi na kutoelewana kwa wanandoa ni kwa sababu ya kutolingana kwa tabia na kanuni za maadili za wanandoa. Kukosekana kwa uzingatifu wa kanuni hizo basi husababisha ndoa nyingi kusambaratika. Maelezo haya yanabainika katika MF 84:

**MF 84**

> Mke mwenye sifa nzuri, ni nani awezaye kumpata?
> Yeye ni wa thamani sana kuliko majirani
> (KCM 31:10)

Kutoka MF 84 hapo juu, tunampata mwanamke aliyechorwa kama mtu mwenye sifa kuliko majirani. Katika maamrisho ya kidini, jirani ni mtu muhimu sana na atendewe vyema lakini mwandishi wa Kitabu cha Methali anasema mwanamke mwenye sifa nzuri ni bora kuliko jirani. Kwa maneno mengine, mwanamke anapaswa kutekeleza majukumu yake ya kindoa huku akionyesha utu wema na kudhihirisha sifa nzuri katika familia yake, yaani kwa mumewe na watoto wake. Mwanamke anapofanya hivyo, inatarajiwa kwamba ndoa yake itakuwa imara.

Mwanamke anafaa kuonyesha sifa nzuri kwa mume na jamii kwa ujumla. Mwanamke mwenye sifa nzuri ni vigumu kupatikana kwa sababu wanaume huwakimbilia. Mwanamke mwenye tabia nzuri ni wa thamani na wa kujivunia kwa hulka njema inayostahili akina mama kama hawa. Maelezo haya yanadhihirika wazi katika MF 85 hapo chini:

**MF 85**

> Afadhali kula ukoko mkavu ukiwa na amani na utulivu, kuliko kukaa kwenye nyumba ya karamu kukiwa na magomvi.
> (KCM 17:1)

Kulingana na MF 85 hapo juu, Solomoni anatupa taswira ya mama mwenye ugomvi ambaye hawezi kuishi na mumewe. Yaani, mwanamke anayependa kuzozana na mume wake kila wakati. Mwanamke wa aina hiyo anaweza kuiharibu ndoa yake na familia yake kwa jumla. Katika nukuu hili, Mfalme Solomoni anafahamu kwamba kuna uwezekano wa kuwa na mke ambaye huzua ugomvi kila wakati katika ndoa yake. Kwa jinsi hiyo, Solomoni anajaribu kuwatahadharisha kwa kuonyesha kwamba ugomvi ni chanzo cha migogoro katika ndoa.

Mfalme Solomoni kutokana na hekima yake, anatumia methali inayobeba ujumbe mzito kuhusu ugomvi. Anasema kwamba ni heri kuishi maisha ya chini yenye utulivu

na amani kuliko kuishi maisha ya juu yenye ugomvi. Kwa kweli amani ni suala muhimu ambalo ukosefu wake unalinganishwa na mtu kuamua kutupilia mbali iwapo anayechangia ni mwanamke mgomvi. Anadai ni heri kula ukoko au kuishi kwa taabu lakini nyumbani pana amani. Tunaelezwa kuwa: ***Afadhali kula ukoko mkavu ukiwa na amani na utulivu***. Solomoni anasisitiza sana kuepuka ugomvi ili wanandoa waishi kwa amani.

Solomoni hajabainisha wazi katika Wimbo Ulio Bora mwanamke asiyenung'unika, mvumilivu na mpole kwa kuwa mpenzi wake amechorwa kama malkia. Mwanamke huyu ni mrembo na wa kupendeza sana na kwa hivyo mume wake anashinda akimfuata na kumsifu kwa maumbile yake na hulka zake kama mwanamke. Hajakumbwa na mateso wala dhiki ya ndoa, na kwa hivyo hatumpati akinung'unika wala kuvumilia lolote. Solomoni ametupa taswira ya mwanamke mkamilifu anayependeza mume wake kwa kila hali na kumfanya mume wake ajihisi vizuri kama mfalme.

## 4.9 Hitimisho

Sura ya nne imeangazia lengo letu la kwanza la utafiti, 'Kuchanganua taswira ya mwanamke katika *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu,* 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora''. Tumefikia lengo hili kwa kuangazia data tuliyokusanya kutokana na kazi zetu teule za kifasihi ambazo ni *tendi za Mwanakupona na Ayubu,* na matini za kidini ambazo ni Methali, Wimbo Ulio Bora.

Tumeangazia kwa upana hulka zinazomtambulisha mwanamke na taswira yake katika ndoa. Ni matumaini yangu kwamba wanawake wakiyazingatia haya yote wataboresha ndoa zao na kuleta uthabiti katika familia. Kutokana na matini hizi, inabainika wazi kuwa kazi ya mke ni kumtunza na kumlea mume jinsi mtoto mdogo anavyolelewa. Si

kazi rahisi na ndiposa katika jamii ya leo, wengi wa wanawake, hasa waliopata kisomo cha juu, hukwepa jukumu hili ambalo ni muhimu kwa udumishaji wa ndoa. Ni jambo ambalo lina mvuto mkubwa katika ndoa na husababisha aidha ndoa isimame imara ama kuishia katika uwanja wa fujo.

Basi kwa jumla tunaweza kujiuliza swali hili, 'Mwanamke ni nani katika jamii?' Mwanamke ni msaidizi wa Mwanamume, taji la mwanamume, mjenzi wa mji wake na nyumba yake, ni kipenzi cha mume na watoto, ni mwalimu wa familia na pia ni mshawishi wa tabia njema kwa jamii inayomzunguka. Kwa hivyo mwanamke ana nafasi bora sana katika ndoa, na hii nafasi si ukandamizaji bali ni wajibu wake spesheli aliyompa Mwenyezi Mungu. Mambo haya yanawezeshwa na uhusiano mwema kati ya mke na mume katika ndoa jinsi yatakavyojadiliwa kwa mapana katika sura ya tano.

# SURA YA TANO

# UHUSIANO WA MKE NA MUME KATIKA NDOA

## 5.0 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia, tumefafanua taswira ya mwanamke kama inavyojitokeza katika kazi teule za fasihi na kidini. Katika sura hii, tumejadili uhusiano wa mwanamume na mwanamke katika ndoa kwa kurejelea kazi teule za fasihi: *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu* na matini za kidini; 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora' katika *Biblia*. Vile vile katika sura hii, tumechunguza dini kama kigezo muhimu cha kuidhibiti ndoa. Ndoa ni asasi muhimu katika jamii yoyote ile, na mwanamume alipewa nafasi maalumu katika jamii na majukumu yake yalitofautiana na ya mwanamke. Kwa mfano, dini na tamaduni nyingi za jamii za Kiafrika, zimempa mwanamume mamlaka katika ndoa, na maamuzi ya masuala mengi yanayohusiana na ndoa ni jukumu lake. Mwanamke kwa upande mwingine anatarajiwa kuwa msaidizi wa mwanamume katika jamii.

Katika sehemu hii, tumeshughulikia uhusiano wa mwanamke na mwanamume katika ndoa kwa kurejelea vipengele mbalimbali vinavyoweza kuujenga uhusiano wao. Kwa mfano, kigezo cha kufurahiana, kufarijiana, kuheshimiana, kusameheana, kufaana na kwamba uhusiano mwema humtegemea sana mwanamke. Kwa upande mwingine, tumeangazia vigezo muhimu kama vile utumiaji wa lugha nzuri wakati wa maongezi, mke kumuaga mume na kumkaribisha anaporejea, kupendana na kumjali mwenzake, kutimiza mahitaji ya kujamiiana, kutojihusisha na vimada, kumsaidia mke ama mume wakati wa shida kwa mfano wakati wa ugonjwa, maafa, kupoteza kazi n.k. Kwa hivyo, uchanganuzi wetu ni kwa kurejelea data za UWM, UWA, KCM na WUB.

### 5.1 Mwanamume na Mwanamke Kuheshimiana katika Ndoa

Kimsingi, heshima katika ndoa ni tabia njema na adabu anayokuwa nayo mhusika mmoja kwa mwenzio. Katika maisha ya kawaida, binadamu hutarajiwa kuonyesheshana adabu na heshima ili waweze kuwa na maisha mazuri yanayotamanika. Ingawa heshima ni muhimu katika maisha ya kila siku, sio kitu cha lazima bali hutokana na hiari ya mhusika. Hii ndio maana wavyele walidai kwamba *heshima si utumwa*. Methali hii ina maana kuwa hakuna mtu anayelazimishwa kuwa na heshima, yaani ni kwa hiari ya mtu. Al Farsy (1942) anashadidia suala la heshima anaposema kuwa mume na mke wakae kwa wema. Anawahimiza wanaume wasikae na wake kwa ajili ya sheria tu ya ndoa ili wasipite mipaka aliyowawekea Mwenyezi Mungu, lakini ni muhimu kutoa heshima ya ndoa.

Katika mkabala huo, heshima katika ndoa ni jambo muhimu sana kwani wanandoa wanapoheshimiana basi ndoa yao itadumu. Mwanamke anapokuwa kwenye ndoa anapaswa kuonyesha heshima kwa mumewe bila kulazimishwa kama vile alivyojipeleka kwa mumewe kwa hiari yake mwenyewe. Ni wajibu wa kila mmoja apatapo nafasi ampongeze mwenziwe mbele ya watu au hata wanapokuwa pekee yao. Kila mmoja ana jukumu la kumjengea mwenzake sifa mbele ya wengine na kukubali pongezi zote za mafanikio. Pia kila mwanandoa amruhusu mpenziwe ajue kuwa anaafikiana naye katika yote afanyayo. Kila mara wanavyowainua wapenzi wao ndivyo wanavyothaminiana na kunyanyuana wakati wa shida.

#### 5.1.1 Mwanamume na Mwanamke Kuheshimiana katika UWM

Heshima katika ndoa ni jambo muhimu sana. Wapendanao huheshimiana ili kudumisha mapenzi na ndoa. Iwapo heshima itakosekana katika ndoa, basi ndoa hiyo iko mashakani. Katika UWM, heshima imesisitizwa kwa binti katika unyumba wake.

Kwa mfano, katika MF 86, mama anamshauri bintiye aishi na mumewe kwa heshima, unyenyekevu na upole bila kumkasirisha wala kujibizana naye bali ajifunze kufunga kinywa chake au kutoropokwa. Anasema kuwa asiyemheshimu mwenzake, ameidhulumu mwenyewe nafsi yake.

**MF 86**

Keti naye kwa adabu,
Usimtie ghadhabu,
Akinena simjibu,
Itahidi kunyamaa
(UWM ubeti 28)

Katika MF 86 hapo juu, Mwanakupona anamshauri bintiye asimkosee mumewe bali aonyeshe adabu na heshima ili asimghadhabishe. Mwanakupona anasema kwamba: ***Keti naye kwa adabu, Usimtie ghadhabu.*** Katika mfano huu, bintiye Mwanakupona anashauriwa kumtii mumewe na asiwe na haraka ya kumjibu wala kujibizana naye bali waishi pamoja kwa kudumisha heshima na maelewano. Mwanamke anapodhihirisha heshima katika ndoa yake atakuwa na ndoa ya kutamanika na kila mtu. Mwanakupona anaendelea kusema kwamba: ***Akinena simjibu, Itahidi kunyamaa***. Hii ina maana kwamba mwanamke mzuri ni yule ambaye hawezi kujibizana na mumewe kwa vyovyote vile.

### 5.1.2 Mwanamume na Mwanamke Kuheshimiana katika UWA

Kama tulivyoeleza, suala hili linajitokeza katika UWA. Mawazo haya tunayapata katika MF 87 na MF 88 kama ilivyo hapo chini:

**MF 87**

Kurudi kwangu ndiani
Kamkuta insane
Naye umo sakarani
Sura alokiongoa
(UWA ubeti 220)

**MF 88**

Akaniambia mumeo
Hana mali hana cheo
Umeikusa upeo
Ntume atakuua
(UWA ubeti 221)

Kupitia beti hizi (MF 87 na 88), tunagundua kwamba baada ya Rehema kuhadaiwa na shetani, yeye hakuyatilia maanani maoni ya shetani. Tunaelezwa kuwa: ***kamkuta insane, naye umo sakarani,*** Rehema anaenda hadi kwake na kumweleza mumewe Ayubu yale yaliyotokea. Anafanya hivyo kwa sababu ya heshima aliyokuwa nayo kwa mumewe.

Shetani anamweleza Rehema kuwa Ayubu hana mali wala cheo chochote. Tunaelezwa kuwa: ***akaniambia mumeo, hana mali hana cheo,*** na kwamba asipotahadhari mtume atamuua: ***ntume atakuua.*** Lakini Ayubu anakiri kuwa atamwadhibu pindi tu atakapopata nafuu. Rehema naye alipokea mawazo ya mumewe kwa unyenyekevu na anakubali kusudio lake. Tazama MF 89 hapa chini:

**MF 89**

Nipoapo imi mja
Kwako usiweke huja
Sina shaka takupija
Mungu kinipa afia
(UWA ubeti 224)

Kwa mujibu wa MF 89 hapo juu, mumewe Rehema anamwambia kuwa atampiga kwa kuwa hakumtii alipoambiwa asizungumze na yeyote njiani. Tunaelezwa kuwa: ***Sina shaka takupija, Mungu kinipa afia.*** Rehema alikubali adhabu hiyo kwa kuwa alijua alikuwa amekosa. Alifanya haya kwa sababu ilikuwa njia mojawapo ya kumwomba mumewe msamaha na kutuliza ghadhabu zake kwa kuwa alimheshimu. Lakini

mambo yalibadilika, Ayubu anapopona, anajawa na msamaha hadi kufikia kiwango cha kutaka kuvunja nadhari yake kwa kuwa alimheshimu mkewe.

**MF 90**

Nipo mke wako nipo
Mbee zako hapo ndipo
Timiza chako kiapo
Ayubu walotongoa
(UWA ubeti 353)

Katika MF 90 hapo juu, Rehema anajitolea kuadhibiwa na mumewe kama njia ya msamaha kwa tendo lililotendeka. Tunaelezwa kuwa: ***nipo mke wako nipo***. Ayubu alikataa katakata hadi malaika alipotumwa na Mwenyezi Mungu mwenyewe ili amwamuru kutimiza kiapo chake. Tunaelezwa kuwa: ***timiza chako kiapo***, kama inavyodhihirika katika MF 91:

**MF 91**

Hukwambia Mola wako
Timiza kiapo chako
Ya nadhiri mke wako
Ipate kumwondokea
(UWA ubeti 358)

Maelezo haya yanadhihirisha heshima ya kweli ambapo japo Ayubu alikuwa ameghadhabika mwanzoni, lakini alipojirudia akaona kuwa hataweza kumwadhibu Rehema mke wake. Tunasoma kuwa: ***ya nadhiri mke wako ipate kumwondokea.*** Ayubu kwa kuwa alikuwa amemsamehe mkewe, alichelea kutimiza kiapo chake. Kutokana na beti hizi katika UWA, tunagundua kuwa mmoja wa wanandoa anapokasirika au kufadhaishwa, anaweza kushindwa kujizuia kumlaumu aliyemsababishia hali hiyo, hata kama mtu mwenyewe ni mwenzi wake wa maisha.

Kwa kawaida, wanandoa hujaribu kuelekezana hasa wanapohisi kwamba kuna udhaifu fulani. Hata hivyo, wanapojaribu kukosoana na kurekebishana, ni vyema

wafahamu jambo hili huenda likawa na changamoto katika ndoa yao kwa sababu litasababisha kila mmoja kuonekana kuwa anajitetea. Matokeo yake ni kwamba yule anayekosolewa hatabadilika na pengine atawacha kuwajibika. Kama kweli mwanandoa mmoja anataka kumpa kipaumbele mwenzake na kisha kutarajia mazuri kutoka kwake, yeye mwenyewe ajirekebishe kwanza iwapo ana upungufu fulani.

Pia, ni vyema kama wanandoa watawacha kukabiliana kwa maneno wakati wa mgogoro. Wanandoa wenye furaha ni wale ambao huepuka sana kutumia vibaya vinywa vyao dhidi ya wenzao. Hawa hufahamu jinsi ya kuzuia mazungumzo kulipuka na kuwa ugomvi. Iwapo ugomvi utatokea, wajaribu kubadilisha mada, waingize ucheshi, waonyeshane mapenzi ya ziada kwa kuwa heshima lazima idumishwe.

### 5.1.3 Mwanamume na Mwanamke Kuheshimiana katika WUB

Solomoni katika Wimbo Ulio Bora anaheshimiana na mke wake. Sura zote nane katika WUB, zinaonyesha wapendanao wawili ambao wanaheshimiana kwa kuonyesha mahaba tele. Suala hili linajidhihirisha katika WUB 5:3-5,

**MF 92**

Nimeivua kanzu yangu, niivaeje?
Nimeitawadha miguu:
Niichafuaje?
Mpendwa wangu aliutia mkono wake tunduni,
Na moyo wangu ukachomeka kwa ajili yake,
Nikaondoka nimfungulie mpendwa wangu,
Mikono yangu ilidondoza manemane,
Na vidole vyangu matone ya manemane,
Penye vipini vya komeo
(WUB 5:3-5)

Katika MF 92, Solomoni anaeleza alivyomheshimu mpenzi wake kwa moyo wake wote. Anatuchorea taswira alivyokuwa, ameivua kanzu yake na kuitawadha miguu yake. Anasema, ***Nimeivua kanzu yangu, niivaeje? Nimeitawadha miguu.*** Lakini

wakati alipomsikia mpenziye mlangoni, hakusita kumfungulia japo alikuwa na sababu tosha za kumzuia kuufungua mlango. Alimheshimu mpenzi wake na kwa hivyo ilimlazimu aamke na kumfungulia mlango wake. Tunaelezwa kuwa: ***Nikaondoka nimfungulie mpendwa wangu, Mikono yangu ilidondoza manemane.*** Iwapo Solomoni hangefungua mlango wake kwa mpenziwe, tungepata taswira ya kukosa heshima na kutojali mwenzake kabisa.

### 5.1.4 Mwanamume na Mwanamke Kuheshimiana katika KCM

Kwa upande mwingine, katika Kitabu cha Methali 12:4, Mfalme Solomoni anatueleza kuwa mke mwema huwa ni taji la fahari kwa mumewe, yaani hutekeleza kila suala kwa utu na upendo, lakini mwanamke mkorofi ni kama dondandugu kwa mumewe. Humfanya mumewe kuwa na huzuni na mashaka milele kama tunavyoona katika MF 93, ufuataao:

**MF 93**

> Mwanamke mwema ni taji la mumewe;
> Bali aaibishaye ni kama kuoza mifupani mwake.
> (KCM 12:4)

Maelezo haya katika MF 93, yanaonyesha kuwa mwanamke mwema ni taji la mumewe na kwamba mumewe humfurahia na kujivunia kwa wema wake. Tunaelezwa kwamba: ***Mwanamke mwema ni taji la mumewe.*** Kutokana na maelezo haya, mwanamke ambaye hana heshima kwa mumewe ni kama uozo katika mwili wake na hivyo ni vigumu kuishi naye. Tunayapata haya katika Methali: ***Bali aaibishaye ni kama kuoza mifupani mwake.***

Katika Kitabu cha Methali 11:16, Mfalme Solomoni anatueleza kuwa mwanamke aliye na hekima, heshima na busara, daima huwa na uhusiano mwema na watu, hali

ambayo husababisha watu wengine kumheshimu kuliko mwanamke mwenye kiburi, msaliti au anayekosa hekima. Maelezo haya yote yanarejelea tu heshima kama msingi wa mahusiano mema katika ndoa kama yanavyodhihirika katika MF 94:

**MF 94**

> Mwanamke wa adabu huheshimiwa daima;
> Na watu wakali hushika mali siku zote.
> (KCM 11:16)

Kwa mujibu wa mfano huu (MF 94), mwanamke anastahili kufurahia ndoa yake hata ikiwa na changamoto nyingi. Yaani, asiwe wa kujisema kwa watu bali afikiri atakavyoinua familia yake iwe imara ndiposa awe mfano mwema kwa familia yake**.**

Mwanamke asipojiheshimu, ni vigumu kuheshimiwa na watu wengine. Katika ubeti huo, tunaelezwa kwamba: ***Mwanamke wa adabu huheshimiwa daima.*** Ni furaha ya kila mja kuheshimiwa kwa tabia zake nzuri. Heshima huweza kudhihirika katika nyanja zifuatazo: Usemi, mavazi, mahusiano n.k.

## 5.2 Mwanamume na Mwanamke Kufurahiana na kutumia Lugha nzuri katika Ndoa

Wanandoa wanafaa kuishi pamoja kwa furaha huku wakitumia lugha nzuri katika mazungumzo. Kila mmoja aweze kufurahia uwepo wa mwenzake. Kicheko huwaleta wanandoa pamoja. Wanandoa wanaoweza kucheka pamoja wanaweza kulia pamoja pia. Wanandoa wahimizwa wasiwe wagumu na wenye msimamo mkali katika kila kitu. Wanapaswa kujiepusha na hasira katika ndoa yao. Vile vile wanashauriwa kutumia kicheko kama mlango wa kufurahiana ili wadumishe ndoa yao. Ikiwa watakuwa na mazoea kama haya watu wengine watawaiga kutokana na mfano wao mzuri.

Vile vile katika dini ya Kiislamu, Al Farsy (1942), anaeleza kuwa haki ya Uislamu ni kupendana na kutakiana kila la kheri bali siyo kuudhiana. Anasema kuwa Uislamu, unazuia watu kuachana na huwahimiza wanandoa kuchukuliana, kusameheana, kutoachana na kutokataana.

### 5.2.1 Mwanamke na Mwanamume Kufurahiana na Matumizi ya Lugha nzuri katika UWM

Katika UWM ubeti wa 24, mwandishi wa kazi hii ametoa maelezo muhimu yanayohusu kufurahiana na kutumia lugha ifaayo ili kudumisha ndoa husika. Katika *Utendi wa Mwanakupona* tunapata maelezo yafuatayo katika MF 95 hapo chini:

**MF 95**

Naawe radhi mumeo,
Siku zote mkaao,
Siku mukhitariwao,
Awe radhi mekuwiya
(UWM ubeti 24)

Katika MF 95 hapo juu, mama anamshauri bintiye ahakikishe kwamba mumewe anatabasamu na kuwa na furaha wakati wote. Mwanamke amepewa nafasi ya kuhakikisha kuwa mume wake anafurahi kila mara. Tunaelezwa kwamba: ***Naawe radhi mumeo, Siku zote mkaao.*** Mwanamume anapokumbana na matatizo ya maisha, mwanamke anafaa kuwa tayari kumliwaza. Tunayapata haya katika maelezo yafuatayo: ***awe radhi mekuwiya,*** na kumpa nguvu ya kustahimili.

Katika matini hii vile vile, mwanamke anapewa wosia wa kuwa na shukrani daima kuonyesha hali yake ya furaha. Hii inajitokeza kama sifa muhimu kwa mwanamke. Tazama MF 96 hapa chini:

**MF 96**

Akupacho mpokeye
Na moyo ufurahiye
Asilotenda kwa yeye
Huna haja kumwambiya
(UWM ubeti 49)

Katika MF 96 hapo juu, Mwanakupona amesawiriwa kama mwanamke mwenye furaha machoni pa mume wake. Kutokana na hekima yake, anamshauri bintiye kufanya vivyo hivyo mbele ya mume wake. Anamueleza binti yake kwamba anastahili kuwa na furaha kila mara. Anaendelea kumweleza kwamba anapaswa kukubali chochote anachopewa na mume wake. Hivi ndivyo mwanamke wa Kiislamu anapaswa kuishi akiwa kwenye ndoa.

Katika ubeti huu, mama anamshauri bintiye kupokea chochote anachopewa na mumewe kwa furaha. Suala hili linajitokeza wazi. Tunaelezwa kuwa: ***Akupacho mpokeye, na moyo ufurahiye***. Mwanamke anashauriwa awe wa shukrani kila mara anapopokea chochote kutoka kwa mumewe na chochote asichoweza kutekeleza basi siwajibu wake kumweleza. Tunaelezwa kuwa: ***Asilotenda kwa yeye, huna haja kumwambiya***. Mwanamke asimshurutishe mumewe katika kutoa asichoweza kufikia kwa uwezo wake. Achunguze uwezo wa mumewe kiuchumi na aombe anachotaka kwa kuangalia uwezo huo. Jambo hili huepusha mafarakano kati ya mume na mke katika ndoa.

### 5.2.2 Mwanamke na Mwanamume Kufurahiana na Matumizi ya Lugha nzuri katika UWA

Jambo hili pia limetiliwa mkazo katika WUB 5:16, ambapo tunasoma mambo muhimu yahusuyo furaha, upendo na matumaini katika ndoa. Yaani, mume na mke wanatakiwa kuishi kwa furaha kila wakati ili ndoa yao idhihirishe upendo na

matumaini. Kwa maneno mengine, hawatakiwi kuonyesha nyuso zilizosononeka, bali waonyeshe kwamba kuna matumaini katika maisha ya ndoa. Haya yanajitokeza katika MF 97 hapa chini:

**MF 97**

> Kinywa chake kimejaa maneno matamu,
> Ndiye mzuri sana pia pia,
> Ni huyu mpendwa wangu,
> Ni huyu rafiki yangu,
> Enyi binti za Yerusalemu.
> (WUB 5:16)

Katika MF 97 hapo juu, mwanamke anayependwa anamsifu mumewe. Tunaelezwa kuwa: ***Kinywa chake kimejaa maneno matamu***. Mwanamke huyu anadhihirisha sifa ya furaha kwa kuwa kinywa chake kimejaa maneno matamu tu bali si matusi na uchokozi. Tunaelezwa kwamba: ***Ndiye mzuri sana pia pia.*** Haya yote yanajaliza mapengo ya mahusiano mema yaliyopo kati ya wanandoa. Wazo kuu hapa ni kuwa ni vyema wanandoa waishi kwa furaha ili ndoa yao iwe ya kudumu na kwamba wote waweze kufurahia maisha yao. Tunaelezwa kuwa: ***Ni huyu mpendwa wangu, Ni huyu rafiki yangu.*** Mwanamke huyu anajivunia mume wake kwa kumtambua kuwa ni mpendwa wake na rafiki wa dhati.

Kutokana na maelezo ya MF 97, wanandoa wasipojishughulisha kwa lolote lile kwa ajili ya kuwafurahisha wapenzi wao, watasababisha chuki na hata kukasirikiana na mwishowe kuleta malumbano yanayoweza kusababisha vita na hata kutalakiana. Ni jukumu la kila mwanandoa kuhakikisha ametekeleza wajibu wake ili waendelee kuishi kwa furaha katika ndoa.

Ili kuepuka migogoro katika ndoa, wanandoa wahakikishe kuwa wanayapa kipaumbele mambo ambayo yanawafanya wajihisi maalumu kati yao. Njia rahisi, ya

kujishisi maalum ni kuwekeza katika matendo madogo madogo ya kimahaba kama kucheka, kucheza pamoja na kadhalika. Hivyo, badala ya kulaumiana, kila mmoja ajaribu awezavyo kuegemea sifa chanya za mwenziwe. Wahakikishe kuwa sifa hizi na kauli hizi za mahaba zinadhihirika kutoka moyoni, zisije kuwa kama mazoea tu. Iwapo watafanya hivi, ni rahisi sana kufurahishana na kuonyeshana nia njema. Wakumbuke mambo yao yalianza vivi hivi, pale walipokuwa bado wanachumbiana. Matendo madogo ya kimahaba hayapaswi kuwa na mwisho, maana ndiyo hudumisha msisimko wa wenza na basi kusababisha uhusiano mwema.

### 5.2.3 Mwanamke na Mwanamume Kufurahiana na Matumizi ya Lugha nzuri katika WUB

Solomoni ametumia lugha nzuri katika kumtaja mpenzi wake, na lugha hii nzuri inadhihirisha kuwa hawa wawili walifurahiana katika ndoa yao. Kwa mfano katika WUB 4: 9,

**MF 98**

Umenishangaza moyo,
Umbu langu,
Bibi arusi,
Umenishangaza moyo,
Kwa mtupo mmoja wa macho yako,
Kwa mkufu mmoja wa shingo yako.
(WUB 4: 9)

Katika mishororo hii, Solomoni anaeleza jinsi mke wake anavyomfurahisha na kumpendeza. Anamsifu mke wake kwa maumbile yake yanayomshangaza. Tunaelezwa kuwa: ***Kwa mtupo mmoja wa macho yako, Kwa mkufu mmoja wa shingo yako.*** Hii ndiyo lugha nzuri inayohitajika katika mazingira ya ndoa na ambayo huwafurahisha wanawake wengi. Mwanamume asiwe na mazoea ya kumwita mke wake kwa majina yake moja kwa moja au kumwita mama watoto, majina haya

hayaleti mahaba kwa ndoa. Majina kama *honey, sweetie, darling, my lolly pop, my pumpkin, my only bubble in my soda, the only bean in my githeri, the only mosquito in my mosguito net, my only tomato in my orange tree* n.k yanaongeza ladha kwa mapenzi ya ndoa.

Solomoni anaendelea kuonyesha furaha katika utumizi wa lugha nzuri katika ndoa yake.

**MF 99**

Jinsi zilivyo nzuri pambaja zako,
Umbu langu,
Bibi arusi,
Ni nzuri divai,
Na harufu ya marhamu yako yapita manukato ya kila namna,
Bibi arusi,
Midomo yako yadondoza asali,
Asali na maziwa vi chini ya ulimi wako,
Na harufu ya mavazi yako,
Ni kama harufu ya Lebanoni,
Wewe ndiwe chemchemi ya bustani yangu,
Kisima cha maji yaliyo hai,
Vijito vya Lebanoni viendavyo kasi.
(WUB 4:10,11,15)

Mishororo hii imeonyesha matumizi ya lugha nzuri ya mapenzi kwa wanandoa wanaofurahia uhusiano wao. Mwanamume anamsifu mkewe kwa uzuri wake na tabia yake nzuri. Mwanamke aliyewajibika katika ndoa na kumtimizia mahitaji yake mumewe hatakosa sifa kama hizi, kwa kuwa wanaume wanawapenda wanawake walionyenyekea na wanaowatii hata kwa maneno yao. Tunaelezwa kuwa: ***Midomo yako yadondoza asali, Asali na maziwa vi chini ya ulimi wako.***Wanawake wanaopenda kelele na kuwajibu waume zao ni chukizo kwa ndoa.

### 5.2.4 Mwanamke na Mwanamume Kufurahiana na Matumizi ya Lugha nzuri katika KCM

Mwanamke anaposimamia nafasi yake hasa ya kufurahisha mume wake, kulingana na Solomoni, matokeo yatakuwa kwenye Methali 31:28 katika MF 100 hapa chini:

**MF 100**

> Wanawe wamesima na kumtangaza
> kuwa mwenye furaha,
> mume wake naye humsifu
> (KCM 31:28)

Kulingana na MF 100 hapo juu, tunaelezwa kwamba iwapo mwanamke atazingatia nafasi yake kama msaidizi wa mumewe, basi watoto wake watamwita mbarikiwa. Maelezo yafuatayo yanajenga hoja hii: ***Wanawe wamesimama na kumtangaza kuwa mwenye furaha.*** Kwa upande mwingine katika ubeti uo huo, tunaelezwa kwamba mume wake vile vile atamsifu kwa kusema kuwa amewashinda wanawake wengine wote. Tunaelezwa maelezo yafuatayo: ***mume wake naye humsifu***. Solomoni anaendelea kufafanua hoja hii kwa kutoa maelezo muhimu katika Methali 31:29 kama inavyoelezwa kwenye MF 101 hapa chini:

**MF 101**

> Binti za watu wengi wamefanya mema,
> Lakini wewe umewapita wote.
> (KCM 31:29)

Kutokana na maelezo yanayotolewa katika MF 101 hapo juu, mwanamke anasifiwa na mume wake kwa kuwa ametenda mema na kumfurahisha mume wake. Solomoni anajaribu kumlinganisha na wanawake wengine lakini  mke wake amewashinda wote kwa kuwa na hulka za kipekee. Mwanamke anapotekeleza wajibu wake kama mke, mumewe hatakuwa na lingine zaidi ila kumpenda na kumtunza vyema.

Hali kadhalika ni muhimu kwa mwanamke kuwa na uhusiano mzuri na watu wengine kwa kujenga msingi ambao ni thabiti na ambao utakuwa bora kwake kwa maisha ya baadaye. Suala hili limetiliwa mkazo katika Kitabu cha Methali 31:25. Tazama MF 102 hapa chini:

**MF 102**

> Nguvu na fahari ndivyo mavazi yake naye
> anaucheka wakati ujao
> (KCM 31:25)

Kutokana na maelezo haya MF 102 hapo juu, mwanamke daima anapaswa kuwa na nguvu na majivuno huku akiwa na matumaini ya siku zijazo. Mwanamke pia, anatarajiwa kuelekeza familia yake kwa msingi wa kidini, upendo na tabia ya kipekee. Hivyo basi, mwanamke wa aina hii hujitia nguvu kama tunavyosoma hapa. Tunasoma kuwa: ***nguvu na fahari ndivyo mavazi yake***. Maelezo haya yanachangia katika kuhakikisha kuwa familia yake inabaki salama. Tazama MF 103:

**MF 103**

> Hufungua kinywa chake kwa hekima
> na sheria ya fadhili zenye upendo ziko katika ulimi wake
> (KCM 31:26)

Katika MF 103, kinachodhihirika ni kuwa mwanamke mzuri lazima awe na hekima. Tunasoma kuwa: ***hufungua kinywa chake kwa hekima,*** na apate kuwajibika kama mke, mama mzazi na mlezi katika familia. Hulka za mwanamke zijidhihirishe katika kazi na shughuli zake za kila siku. Tunasoma kuwa: ***sheria ya fadhili zenye upendo ziko katika ulimi wake.*** Katika kujishughulisha kila siku na kutumia maneno ya kinywa chake vizuri, mwanamke anaweza kushirikiana na wanajamii vizuri.

Katika kazi tulizozichagua za UWM, UWA, KCM na WUB, mwanamke anatakiwa kumheshimu mumewe hata katika kumuaga na kumkaribisha nyumbani anaporejea. Kwa mfano, katika UWM, mwanamke anapewa wosia kuhusiana na kutoka na kuingia kwa mume wake pale nyumbani kama inavyodhihirika katika MF 104 hapa chini:

**MF 104**

Kitoka agana naye,
Kingia mkongowee,
Kisa umtandikie,
Mahala pa kupumua
(UWM ubeti 30)

Katika MF 104, mwanamke anapewa maagizo kuwa kila mara mume anapotoka nyumbani lazima amuage. Tunaelezwa kuwa: ***kitoka agana naye.*** Pia mumewe anaporudi nyumbani lazima apokelewa vyema. Tunaelezwa: ***kingia mkongowee.*** Hali hii itawafanya wawili hawa waishi vizuri kwa amani na utulivu. Vile vile, mume akijua pindi arudipo nyumbani anapokelewa vyema, hatajihusisha na shughuli nyingi na wanaume wengine kule nje, atajitahidi kurudi nyumbani mapema ili apate muda mzuri na mkewe na wanawe. Mwanamke anahimizwa amwaandalie mahali pa kupumzika: ***mahala pa kupumua.*** Akifanya hivyo mumewe atafurahia kurudi nyumbani mapema.

### 5.3 Mahaba katika uhusiano wa Mke na Mume

Al-Amin (1936: 4), katika *Ndowa na Talaka katika Sharia ya Ki-islamu,* anaelezea kuwa katika sharia ya Kiyahudi ni lazima mtu yeyote kuowa, akiwa tajiri au maskini, mzima au mgonjwa, kijana au mtu mzima. Na lazima hii haitimii ila mtu apate watoto watatu, akiwa hakupata watoto kwa mke aliyenaye, ni lazima amuache aowe mke mwingine. Anaelezea kuwa katika sharia ya Kimasihiya, Paulo na Petro

wanafahamisha kuwa ujane ni bora zaidi kuliko kuowa (I Wakorintho 7: 8). Pia anaelezea kuwa sharia ya Kiislamu, kuowa si lazima kama sharia ya Kiyahudi, wala ujane si bora kama katika sharia ya Kimasihiya, lakini sharia ya Kiislamu yawahimiza sana kuowa wakiwa wanaweza kutimiza haki za uke na ume kwa hali zao. Iwapo mtu anaogopa kufanya mambo mabaya kwa ajili ya kuwa hana mke, basi wakati huo anafaa kuoa, kwa ajili ya kujihifadhi na mambo mabaya.

Nguvu ya mguso wa ukaribu kamwe haiwezi kulinganishwa na chochote. Lazima wanandoa wajifunze kujenga tabia ya kugusana mara wapatapo nafasi siyo tu wanapokuwa wamelala. Kugusana huku ni pamoja na kushikana mikono wakiongea au wakitembea, kukumbatiana mabega, kugusana au kuchezea nywele za mwenzake, kupapasana na njia nyingine zozote za kuonyesha ukaribu wa kimwili.

Wanandoa wengi hufanya baadhi ya mambo haya wanapokuwa peke yao na kamwe sio mbele ya watu. Mguso huu wa upendo haumaanishi mguso wa tendo la ndoa, ingawa pia ni vema kujifunza kuijenga lugha ya mguso wa tendo la ndoa katika mahusiano ya mume na mke.

### 5.3.1 Mahaba kati ya Mume na Mke katika UWM

Mahaba ni muhimu katika ndoa. Iwapo wawili wameoana punde au zamani lazima mahaba yawepo kudumisha ndoa ya furaha kama inavyoelezwa na Mwanakupona katika UWM. Kwa mfano katika UWM ubeti wa 29, mama anamweleza bintiye kuwa ni vyema aishi kwa imani na mumewe bila kumnyima chochote kama tunavyosoma katika MF 105:

**MF 105**

Enda naye kwa imani
Atakalo simukhini
We naye sikindaneni
Mkindani huumiya
(UWM ubeti 29)

Katika MF 105, Mwanakupona anamhimiza bintiye kuwa atakacho mumewe ampe na kutozua ugomvi wowote wanapokuwa na mumewe kwa sababu ugomvi wa kila mara hukera. Mwanakupona anamshauri bintiye kwamba kama mke, hapaswi kumyima mumewe chochote anachohitaji. Aidha, anamweleza kwamba anapaswa kumwonyesha mapenzi kwa kutumia maneno matamu wanapozungumza ili ugomvi wowote ule usizuke miongoni mwao. Tunaelezwa kuwa: ***We naye sikindaneni, Mkindani huumiya.*** Kutokana na maelezo haya mwanamke anapewa ushauri kuwa asishindane na mumewe na akifanya hivyo anaweza kujiumiza kama tunavyosoma katika MF 106 hapa chini:

**MF 106**

Kilala siikukuse
Mwegeme umpapase
Na upepo nasikose
Mtu wa kumpepeya
(UWM ubeti 31)

Kwa mujibu wa MF 106 hapo juu, Mwanakupona anamhimiza bintiye kuwa mumewe anapokuwa usingizini, binti asiondoke alipo bali aendelee kulala naye na kumpapasa. Tunaelezwa kuwa: ***Kilala siikukuse, Mwegeme umpapase.*** Hii ni hali ya kuonyesha mapenzi kwa mwenziwe kwa kumjali na kumfanyia analohitaji. Vile vile amhudumie kwa kumpepeya kila mara anapohisi joto. Tunaelezwa kwamba: ***Na upepo nasikose, Mtu wa kumpepeya.*** Hii ni njia mojawapo ya kuonyesha mahaba kwa unyenyekevu.

Mwanamke anahimizwa kumpepea mumewe, na kila mara anapomhitaji, basi ni sharti amtendee atakalo kama inavyodhihirika katika MF 107:

**MF 107**

Mpumbaze apumbae,
Amriye sikatae,
Maovu kieta yeye,
Mungu atakuteteya
(UWM ubeti 36)

Katika MF 107 hapo juu, mwanamke anapoonyesha mahaba yake kwa mumewe, ahakikishe kuwa ameyaondoa mambo yanayoweza kumletea mumewe mawazo au kero. Kwa hivyo, ni jukumu la mwanamke kumpumbaza mumewe kwa maneno matamu na vitendo vya mahaba. Tunaelezwa kuwa: ***Mpumbaze apumbae, Amriye sikatae.*** Anapoamriwa kufanya jambo fulani asikatae bali aheshimu na kumtii mumewe kwa lolote lile. Na anapoleta maovu huyo mume, basi Mungu atakuwa mtetezi wake.

### 5.3.2 Mahaba kati ya Mume na Mke katika UWA

Katika UWA beti 125-127, tumedhihirishiwa hali ya mahaba kwenye ndoa. Kupitia kwa beti hizi tunagundua utu alionao Rehema. Katika kuonyesha mahaba yake kwa mumewe, Rehema anaketi na kulala naye bila kujali ukoma wake kama tunavyosoma katika MF 108:

**MF 108**

Ayubu akasumbuka
kwa ndwee yalomshika
Rehema kusikitika
siku zote akilia
(UWA ubeti 126)

Katika MF 108, Rehema alishinda akilia kwa huruma anayomuonea mumewe kwa alivyoteseka na kusononeka kwa maumivu aliyoyapitia. Tunaelezwa kuwa: ***Rehema***

***kusikituka, siku zote akilia.*** Mapenzi yalimfanya Rehema kuhuzunika na kulia kila siku kwa vile alimpenda Ayubu kwa mapenzi ya dhati. Ayubu anapokuwa anaugua, tunaelezwa kwamba mkewe alikuwa karibu naye siku zote. Tunaelezwa kwamba alikula naye kila wakati walipopata chakula. Vile vile, tunaelezwa kwamba alikosa usingizi mara nyingi alipokuwa akimwaza na kumshughulikia mume wake kiafya na katika hali zote kama inavyodhihirika katika MF 109 hapa chini:

**MF 109**

Akawata masindizi
Rehema katenda kazi
ili kupata khubuzi
kumpa wake rijaa
(UWA ubeti 127)

Katika MF 109, Rehema aliacha usingizi ili aoke mkate wa kumpa mumewe. Tunasoma kuwa: ***ili kupata khubuzi, kumpa wake rijaa.*** Mwanamke anatakikana amuhudumie mumewe wakati ana shida au ni mgonjwa. Atafute chakula na kumuhudumia kama afanyavyo Rehema. Mahaba yanasababisha Rehema kumhudumia na kutafuta chakula. Hivi ndivyo itakikanavyo kwa wapendanao katika ndoa. Wosia huu ni mzuri kwa mwanamke wa hapo kale na hata wa leo. Wakionyeshana mahaba kama haya, ndoa zitakuwa imara.

### 5.3.3 Mahaba kati ya Mume na Mke katika WUB

Vile vile katika WUB, Solomoni anatoa wosia kuhusu mahaba katika uhusiano wa ndoa. Kupitia kwa kitabu hiki, bibi arusi anamtafuta bwana arusi, anaelezea juu ya mapenzi yake kama tunavyosoma katika MF 110 hapa chini:

**MF 110**

> Wimbo ulio bora, wa Sulemani.
> Kubusu na anibusu kwa kinywa chake. Maana pambaja zako zapita divai; Manukato yako yanukia vizuri; Jina lako ni kama marhamu iliyomiminwa;
> Kwa hiyo wanawali hukupenda.
> (WUB 1:1-3)

Kutokana na maelezo haya katika MF 110 hapo juu, Mfalme Solomoni anazungumzia tendo la kubusu katika ndoa kwamba ni muhimu katika kudumisha uhusiano mwema kati ya mume na mke. Anaeleza sifa za mwanamke mwema, kwamba pambaja zake zapita divai na kwamba manukato yake yananukia vizuri. Tunaelezwa kuwa: ***Manukato yako yanukia vizuri.*** Kutokana na maelezo haya, Solomoni hakumnyanyasa wala kumtusi mwanamke bali alimsifu kwa hulka na tabia zake nzuri hasa wanapokuwa na mumewe.

Hata hivyo, suala la mahaba katika KCM halipo, kwa kuwa Solomoni katika Kitabu cha Methali alizingatia sana mwanamke aliyewajibika katika nyumba yake kuhakikisha kuwa ndoa yake inadumu na familia yake kwa jumla imenawiri. Suala hili la mahaba halijadhihirishwa na Solomoni katika KCM bali amemchora mwanamke anayefanya kazi kuhakikisha familia yake imestawi. Mwandishi anasisitiza yale yanayofanywa na mwanamke kwa ajili ya mume wake na kuzingatia uthabiti wa ndoa.

### 5.4 Kuthaminiana katika Ndoa kati ya Mke na Mume

Wanandoa wanastahili kuthaminiana katika uhusiano wao na hata thamani hiyo ijulikane kwa watoto iwapo walijaliwa kuwapata. Kuthamiana ni muhimu mno katika jamii, ili kila mwanandoa aweze kuhisi kupendwa. Kuthaminiana katika hufanya ndoa kudumu kwa kuwa kila mmoja atahisi kuwa na usalama katika asasi hiyo. Katika *Ndoa na Maamrisho yake*, Al Farsy (1942: 49) Sahaba anayeitwa Bwana Muawiya

bin Hayda Al Qusheyry anaulizwa, 'Nini haki ya mke juu ya mumewe?' Anajibu, 'Umlishe unapokula na umvike unapovaa wala usimpige kabisa, uso wala usimtukane wala usimhujuru ila katika mahali pa kulala tu'. Katika dini ya Kiislamu, mume na mke wanatarajiwa kuthaminiana kama inavyodhihirika katika matini ya kifasihi na matini ya Kidini tulizozichagua.

### 5.4.1 Kuthaminiana katika UWM kati ya Mke na Mume

Mwanakupona alimpa wosia bintiye juu ya umuhimu wa kuthaminiana na mumewe katika ndoa. Kwa mfano, katika UWM beti za 33 na 34, Mwanakupona anamweleza bintiye kwamba punde tu mumewe anapoamka kutoka usingizini ampe chakula, amkandekande mwili wake na ahakikishe kuwa yu nadhifu. Tazama MF 111:

**MF 111**

Chamka siimuhuli,
Mwandikie maakuli,
Na kumtunda muili,
Kumsinga na kumowa
(UWM ubeti 33)

Mwanakupona anampatia wosia bintiye kuwa mumewe anapoamka awe tayari kumshughulikia kwa kumwandalia kiamsha kinywa na asijizuie kumhudumia. Tunaelezwa kuwa: ***Chamka siimuhuli, Mwandikie maakuli.*** Hii ni kuonyesha hali ya kuthaminiana bila malalamishi yoyote. Anashauriwa kumwosha mumewe na kumtunza ili mume ahisi vyema mikononi mwa mke wake. Tazama MF 112 hapa chini:

**MF 112**

Mnyoe umpalilize,
Sharafa umtengeze,
Na udi umfukize,
Burukata wa ashia
(UWM ubeti 34)

Mwanamke anahimizwa kumnyoa mumewe na kumchana ndevu zake vizuri. Anamwambia kwamba: ***Mnyoe umpalilize, Sharafa umtengeze.*** Kazi hii inamhitaji mwanamke aliyejitolea mhanga kumthamini mume wake na kuidumisha ndoa yake. Mwanakupona anaendelea kumweleza kuwa katika kuthaminiana, bintiye ampake mumewe manukato mazuri ili mume anapotembea, aheshimiwe na kupewa sifa kwamba alimpata mke anayemthamini, ***Na udi umfukize, Burukata wa ashia.***

Ikiwa wanandoa wanataka kuwaiga wale wanaofanya vyema katika ndoa zao, lazima wajikumbushe kanuni za kuidhibiti ndoa. Wakianza kupata ukaribu wa kweli baina yao hawatahitaji ukaribu huo na mwingine yeyote, na badala yake wataanza kuulinda ukaribu walionao. Wahakikishe kuwa kila mmoja wao, awe ndiye mtu muhimu maishani.

Ni jukumu la kila mwanamume au mwanamke aliye katika ndoa kuonyesha upendo wa dhati kwa mwenzake wa ndoa ili kufanya vitendo vya upendo vizae amani katika ndoa na mahusiano yao. Hisia hizi za mapenzi ni tendo linaloonyesha mapenzi ya dhati kati ya wanandoa. Hisia za mapenzi zaweza kuujenga undugu wa kudumu jinsi tunavyosoma katika UWM ubeti wa 30:

**MF 113**

Kitoka agana naye,
Kingia mkongowee,
Kisa umtandikie,
Mahala pa kupumua
(UWM ubeti 30)

Katika MF 113 hapo juu, mama anamweleza bintiye kwamba mumewe anapotoka, ni jukumu lake kumjalia mema kokote aendako. Tunaelezwa kuwa: ***kitoka agana naye***. Mume asitoke nyumbani iwapo wamekosana na mkewe bali wawe kwa nia moja na waagane. Arudipo mke ampokee vyema na amtayarishie mahala pa kupumzika.

Tunaelezwa kuwa: ***Kingia mkongowee, Kisa umtandikie, mahala pa kupumua.*** Ni jukumu la mke kuhakikisha kuwa mume wake anapata mahali patulivu kila mara anaporudi kutoka safarini au kwenye matembezi yake kama inavyobainika katika UWM.

Kutokana na UWM hivyo basi, ni dhahiri kwamba hisia za mapenzi hujengwa na vitendo vya upendo na huweza kutoweka na kuhamia mahali popote pale ambapo vitendo vya upendo hupatikana kwa urahisi.Vile vile hisia za mapenzi huweza kurudisha mapenzi yaliyoharibika kupitia vitendo vya upendo wa dhati. Hii ndiyo sababu wanandoa wanapaswa kuchunguza chanzo cha matatizo katika ndoa yao au uhusiano wao kabla ya kufanya uamuzi wowote. Wanandoa wafanye kwa vitendo mambo yanayodhihirisha hali ya kuthaminiana.

### 5.4.2 Kuthaminiana katika UWA kati ya Mke na Mume

Suala la kuthaminiana katika UWA limejitokeza vyema kati ya Ayubu na Rehema. Kwa mfano katika UWA ubeti wa 135 hapa chini:

**MF 114**

Kenda kwa wake rijali
Tumwe Ayubu rasuli
Akamshika muli
Kamzunguazungua
(UWA ubeti 135)

Katika MF 114 hapo juu, tunabaini kwamba Ayubu anaugua ukoma. Anapolala inakuwa vigumu yeye kupinduka. Tunaelezwa kuwa: ***tumwe Ayubu rasuli.*** Kwa upande mwingine, Rehema mkewe anamfaa pakubwa kwani anachukua muda wake na kumtimizia mumewe mahitaji yake. Tunaelezwa: ***akamshika muli kamzunguazungua.*** Katika nukuu hii, Rehema anajitokeza kama mkombozi wa

mumewe Ayubu. Matendo haya yanamtia Ayubu moyo na kumfanya awe na matumaini hata kama alikuwa anaugua kama tusomavyo katika MF 115 hapa chini:

**MF 115**

Ayubu halikiweza
Kilala kuigeuza
Kwa muiliwa kuoza
Shoti mtu kumwinua
(UWA ubeti 136)

Kutokana na maelezo ya MF 115 hapo juu, tunaelezwa kwamba Ayubu alishindwa kufanya lolote kwa mfano, kujigeuza alipokuwa mgonjwa, ikambidi Rehema amsaidie. Mwili wake Ayubu ulioza, lakini Rehema hakukata tamaa bali aliendelea kumvumilia na kumfariji kwa mateso na ugonjwa wake. Rehema anadhihirisha jinsi anavyomthamini mumewe. Kuthaminiana, kunadumisha ndoa. Vile vile katika UWA ubeti 190, tunaelezwa kuwa Rehema alikuwa na upendo wa hali ya juu kwa mumewe na hali hii ilimfanya amthamini mume wake kuliko nywele zake.

**MF 116**

Rehema akawajibu
Kuza nyee ni aibu
Waamma nina yawabu
Zaidi ya mambo pia
(UWA 190)

Katika MF 116 hapo juu, Rehema anawajibu kuwa kuuza nywele ni aibu lakini alikuwa na sababu kubwa kufanya hivyo. Tunaelezwa kuwa: ***Kuza nyee ni aibu, waamma nina yawabu***. Kisa cha kuuza nywele zake, ni shida za ulimwengu zilizowaangukia Rehema na mumewe. Hata hivyo, kwa kuwa Rehema alimthamini mumewe aliamua kuziuza nywele zake ili aweze kumshughulikia mume wake. Tunaendelea kusoma katika UWA ubeti wa 191:

**MF 117**

Ndipo kuza nyee
Zangu
Ni shida la ulimwengu
Ni imi la mume wangu
Limezotusikilia
(UWA 191)

Katika MF 117 hapo juu, tunapata kuwa ukakamavu na upendo aliyokuwa nao mkewe Ayubu ulimfanya ajitolea kwa moyo mmoja ili kupambana na majanga yanayoikumba familia yake. Tunaelezwa kuwa: ***Ni imi la mume wangu, limezotusikilia.*** Mwanamke huyu anamthamini mumewe sana na hata kudai kuwa shida zilizowaangukia zilisababisha kuuza nywele zake: ***Ndipo kuza nyee zangu.*** Tunaendelea kusoma katika UWA ubeti wa 192:

**MF 118**

Mkitaka mzipate
Nyee zangu mzikate
Ishrini kwa nkate
Tauza sitokataa
(UWA 192)

Katika MF 118 hapo juu, Rehema anawaeleza wanawake wenzake kuwa wakizihitaji nywele, wazikate ishirini kwa mkate mmoja. Tunaelezwa kuwa: ***Mkitaka mzipate, nyee zangu mzikate***. Umaskini na hali ngumu ya maisha ilimfanya Rehema kuamua kuuza nywele zake kwa fedha kidogo ili aweze kupata pato ambalo angetumia kuyakimu mahitaji ya familia yake hasa ya mumewe aliyekuwa anaugua ukoma. Tuanaelezwa kuwa: ***Ishrini kwa nkate, tauza sitokataa.*** Tunaendelea kusoma katika UWA ubeti wa 193:

**MF 119**

> Wanawake
> Wamwambie
> Khamsini tukatiye
> Kwa nkate tutwaziye
> Mmoya kutopungua
> (UWA 193)

Katika MF 119 hapo juu, Wanawake walimsihi Rehema wawakatie hamsini kwa mkate kwa kuwa alikuwa ameamua kuziuza nywele zake. Tunaelezwa kuwa: ***Wanawake, Wamwambie, Khamsini tukatiye***. Rehema akakata nywele zake singa hamsini, akazihesabu na kuwapa. Tunaelezwa kuwa: ***Kwa nkate tutwaziye, mmoya kutopungua.*** Wakazifunga nazo zikang'aa. Mume huhitaji sifa na heshima kama njia mojawapo ya kumthamini, na iwapo mke atashindwa kutekeleza mambo haya ndoa yake itakuwa hatarini.

### 5.4.3 Kuthaminiana katika WUB kati ya Mke na Mume

Katika WUB, tunampata mume na mke wanaothaminiana, kwa mfano katika WUB 5:9, Bibi arusi anatangaza kuwa bwana arusi ni wake wa dhati. Tazama MF 120 hapa chini:

**MF 120**

> Mpendwa wa namna gani ni mpendwa wako,
> Wewe uliye mzuri katika wanawake,
> Mpendwa wa namna gani ni mpendwa wako,
> Hata wewe utusihi hivyo?
> (WUB 5:9)

Kwa mujibu wa MF 120 hapo juu, Solomoni anamsifu mke wake kuwa hakuna anayefanana naye kwa umbo na wema wake. Katika kudhihirisha hayo anasema kwamba: ***Wewe uliye mzuri katika wanawake***. Kauli hii ni dhihirisho tosha kwa

mume anayempenda mkewe kuwa anamthamini. Kwa hivyo, wote wawili wanapaswa kuthaminiana kama tunavyoelezwa katika MF 121 hapa chini:

**MF 121**

> Kama mti wa mtofaa miongoni mwa miti ya msituni, ndivyo alivyo mpenzi wangu miongoni mwa wanaume vijana. Ninafurahia kuketi kivulini mwa Mwanamume huyu na tunda lake ni tamu kwangu. Amenichukua mpaka kwenye ukumbi wa karamu na bendera ya huyu Mwanamume juu yangu ni upendo. (WUB 2:2-4)

Katika kifungu MF 121 hapo juu, Tunaelezwa kwamba mwanamke anamsifu mumewe kwa kutambua hulka zake muhimu katika uhusiano wao. Mwanamke anamtaja mume wake kuwa wa kipekee na kwamba anamthamini. Tunaelezwa kuwa: ***Kama mti wa mtofaa miongoni mwa miti ya msituni, ndivyo alivyo mpenzi wangu miongoni mwa wanaume vijana.*** Tatizo kubwa la wanawake wa leo ni kwamba wana changamoto ya kumlinganisha mume wake na wanaume majirani ambapo kwa kufanya hivi, ndoa yake itapata mikosi. Kila mwanamume ana sifa zake mahususi. Ni jukumu la mwanamke kumpenda mume wake na kulifurahia tunda lake bila kulilinganisha na la mwingine kama tunavyoelezwa: ***Ninafurahia kuketi kivulini mwa Mwanamume huyu na tunda lake ni tamu kwangu.***

### 5.4.4 Kuthaminiana katika KCM kati ya Mke na Mume

Katika Kitabu cha Methali, Mfalme Solomoni anampa mwanawe wa kiume ushauri kuwa ni lazima ajitenge na wanawake makahaba, anapewa mawaidha haya ili asifuatane nao bali athamini ndoa yake na kutosheka. Solomoni anasema hivi kwa sababu anajua vinywa vya wanawake huota maneno ambayo daima huwa matamu na ambayo yana uwezo wa kuyeyusha nyoyo za wanaume. Vile vile anatoa ushauri kuwa

wanawake wenye tabia kama hii, maisha yao huwa mafupi mno, yanayoishia mautini kama tunavyosoma katika MF 122 hapa chini:

**MF 122**

> Mwanangu, sikiliza hekima yangu; Tega sikio lako, mzisikie akili zangu;
> Upate kuilinda busara, Na midomo yako iyahifadhi maarifa.
> Maana midomo ya malaya hudondoza asali, Na kinywa chake ni laini kuliko mafuta;
> Lakini mwisho wake ni mchungu kuliko pakanga; Ni mkali kama upanga wa makali kuwili.
> Miguu yake inatelemkia mauti; Hatua zake zinashikamana na kuzimu;
> Hata asiweze kuiona njia sawa ya uzima; Njia zake ni za kutanga-tanga wala hana habari.
> Basi, wanangu, nisikilizeni sasa, Wala msiache maneno ya kinywa changu.
> Itenge njia yako mbali naye, Wala usiukaribie mlango wa nyumba yake.
> (KCM 5:1-8)

Katika MF 122 hapo juu, tunaelezwa kwamba Solomoni anamshauri mwanawe kwamba wanawake ambao ni makahaba tabia zao si kamilifu na ni lazima awe mwenye hekima na kujitenga nao. Tunaelezwa kuwa: ***Tega sikio lako, mzisikie akili zangu; Upate kuilinda busara, Na midomo yako iyahifadhi maarifa. Maana midomo ya malaya hudondoza asali, Na kinywa chake ni laini kuliko mafuta.*** Anapotengana nao, yeye huishi maisha yanayotamanika na wengine naye huthaminika sana. Asikaribie nyumba zao, kujihusisha na shughuli zao au kujiingiza kwa mambo ambayo yanawahusu: ***Itenge njia yako mbali naye, Wala usiukaribie mlango wa nyumba yake.*** Kisa na maana, mienendo yao inaweza kufupisha maisha yake na kumkosesha heshima yake katika macho ya wanajamii.

### 5.5 Mwanamke kuwa Nadhifu ili kudumisha Mapenzi katika Ndoa

Imebainika wazi katika matini za kifasihi na za kidini kuwa wanaume wanapenda kuwa nadhifu, na kwa hivyo mwanamke anafaa kuzingatia usafi ili asipatikane matatani katika ndoa yake. Hii ni kwa kuwa kuna wanaume wataamua kuwachukua wasichana wadogo au waamue wawe na vimada ili kuepuka uchafu nyumbani.

#### 5.5.1 Unadhifu wa Mwanamke katika UWM

Tukirejelea UWM beti 37-41, ni dhahiri mama anamhimiza bintiye awe safi daima, ajirembeshe kila siku, na kuzipamba nywele zake. Pia mama anaendelea kusisitiza bintiye ahakikishe kuwa kidani kinabakia shingoni daima na mwili wake autie marashi yanayovutia. Vile vile, katika ubeti wa 41, mama amweleza bintiye kuwa asitoe pete kidoleni, hina aendelee kujipaka na lazima aweke nshini machoni ili abakie nadhifu. Mapambo haya yote ni ya kumvutia mumewe na kumtenga na fikra za kuvutiwa na wanawake wengine kama tunavyosoma katika MF 123-125 hapa chini:

**MF 123**

Mwanangu, siwe mkoo,
tenda kama uonao.
kupea na kuosha choo,
sidharau mama moya
(UWM ubeti wa 37)

**MF 124**

Na kowa na kuisinga,
na nyee zako kufunga,
na yasimini kutunga,
na furashani kutia
(UWM ubeti wa 38)

**MF 125**

Nawe ipambe libasi
Ukae kama arusi
Maguu itia kugesi
Na mikononi makoa
(UWM Ubeti wa 39)

Katika MF 123-125 hapo juu, tunaelezwa hapa kwamba mwanamke anashauriwa kuwa safi na nadhifu, anapokumbana na uchafu wa aina yoyote. Mwanamke anafaa awe tayari kufanya makazi yang'ae, anashauriwa hata kule chooni ahakikishe kuwa uchafu wote umetolewa. Tunaelezwa: ***kupea na kuosha choo, sidharau mama moya***. Mwanamke asiwe na roho ya kudharau kazi bali ajitolee kwa kuwa yeye ni mwanamke aliye na hulka za kutamanika.

Kwa jumla mwanamke anashauriwa kujiweka vizuri, kudumisha usafi na kuonekana mrembo na wa kuvutia kwa jinsi amesuka nywele zake na kujipaka marashi ili aweze kumvutia mume wake. Tunaelezwa kuwa: ***na nyee zako kufunga, na yasimini kutunga, na furashani kutia.*** Ni jukumu la mwanamke kujipamba kwa ajili ya mumewe, na kuhakikisha nyumba yake imetengenezwa vizuri. Ukweli ni kwamba mwanamke anatakiwa ajipambe akiwa nyumbani na awe mchangamfu kwa mume wake ili aweze kuvutia moyo wa mume wake. Hali hii husaidia kuziba ufa ambao unaweza kujazwa na wanawake wengine. Mwanakupona anamshauri bintiye ajipambe kila mara na abaki kama bi arusi. Tunaelezwa kuwa: ***Nawe ipambe libasi, Ukae kama arusi.*** Bi arusi huwa amejirembesha sana na kuwa kivutio cha watu wengi. Anashauriwa kuvalia bangili za urembo kwa miguu na hata mikononi ili abaki kuwa mrembo na kumvutia mume wake kama inavyoonyeshwa katika MF 126 hapa chini:

**MF 126**

Na kidani na kifungo.
Sitoe katika shingo.
Muili siwate mingo
Kwa marashi na dalia
(UWM Ubeti wa 40)

Kutokana na maelezo haya, tunaelezwa kwamba mwanamke hastahili kuonyesha uzuri wake kwa wanaume wengine kwa sababu hali kama hii inaweza kusababisha matatizo katika ndoa. Ni vyema atambue kuwa kuteka nyara moyo wa mumewe si jambo rahisi, hasa kwa uhusiano katika ndoa. Mwanakupona anamshauri bintiye asiondoe kidani na kifungo kwenye shingo lake. Tunaelezwa kuwa: ***Na kidani na kifungo, Sitoe katika shingo.*** Vile vile, mwili wake ushinde ukiwa na marashi na dalia, hali hii itamfanya mke huyu avutie sana kimwili jambo ambalo linapuuzwa na wengi. Tunaelezwa kuwa: ***Muili siwate mingo, Kwa marashi na dalia.*** Tazama MF 127 hapa chini:

**MF 127**

Pete sikose zandano
Hina sikome nyaani
Wanda sitowe matoni
Na nshini kutia
(UWM Ubeti wa 41)

Katika MF 127 hapo juu, tunaelezwa kwamba mwanamke anashauriwa asiondoe pete kwenye kidole chake wala hina kwenye makucha yake. Hii ni kwa sababu, mwanamke anastahili kurembeka kila mara. Tunaelezwa kuwa: ***Pete sikose zandano, Hina sikome nyaani.*** Vile vile aweze kupaka wanda kwenye macho yake kwa ajili ya urembo. Tunaelezwa: ***Wanda sitowe matoni.*** Jambo hili la kuwa mrembo litamfanya mumewe awe na furaha hata kama hawezi kutamka hisia zake. Kama mwanamke atashindwa kuridhisha matamanio ya moyo wa mume wake na anavaa nguo zisizovutia anapokuwa nyumbani, mumewe anaweza akawaona wanawake wazuri wenye kumvutia nje ya nyumba yake.

Mwanamke kama msaidizi wa mume, lazima azingatie mazingira yake kwa jumla. Inampasa ahakikishe kuwa kila jambo katika jamii limeimarika vilivyo. Tazama MF 128 hapa chini:

**MF 128**

Nyumba yako ii nadhifu
Mumeo umshaifu
Wakutanapo sufufu
Msifu na kumtaya
(UWM ubeti 42)

Kutokana na maelezo haya, mama anamwambia bintiye kuwa ni jukumu lake kuhakikisha kuwa nyumba yake ni nadhifu. Tunaelezwa kuwa: ***nyumba yako i nadhifu.*** Kwa hivyo, mwanamke anapaswa kumwonyesha mumewe upendo alionao kwake kwa kujitolea kunadhifisha wanakoishi. Pia, watu wanapotembelea mwanamke kwake, kila mara wao watamlimbikizia mumewe sifa. Tunaelezwa kuwa: ***wakutanapo sufufu, msifu na kumtaya.***

### 5.5.2 Unadhifu wa Mwanamke katika WUB

Kadhalika katika WUB 1: 9-11 na 14-15 ni wasifu wa bibi arusi unaotolewa na Mfalme Solomoni lakini mambo yanayozingatiwa hasa ni sifa ambazo Mfalme Solomoni anamlimbikizia bibi arusi kwa kuusifu urembo wake. Mahojiano haya yanatendekea mahali palipo wazi na kuna uwezekano kuwa watu wengi wanayashuhudia. Tazama MF 129 hapa chini:

**MF 129**

Mpenzi wangu, ninakufananisha na farasi jike aliyefungwa katika mojawapo ya magari ya vita ya Farao.
Mashavu yako yanapendeza yakiwa na vipuli, shingo yako ikiwa na mikufu ya vito.
Mpenzi wangu kwangu mimi ni kama kishada cha maua ya mhina yaliyochanua kutoka mashamba ya mizabibu ya En- Gedi.

> Tazama jinsi ulivyo mzuri, mpenzi wangu! Tazama jinsi ulivyo mzuri!Macho yako ni kama ya hua.
> (WUB 1: 9-15)

Kwa jumla kutokana na maelezo haya, uzuri ni suala muhimu kwa mwanamke na ni silaha muhimu katika mapambano ya kumpata mwanamume. Mwanamke mzuri anaweza kumshawishi kapera au mume wa mtu. Baada ya kufanikiwa kumteka mwanamume, uhusiano kati ya mwanamke na mwanamume unaweza kuwa wa kihawara au unaweza kuimarika zaidi na kuwa ndoa rasmi.

Vigezo vikubwa vya uzuri vinavyozingatiwa katika mipasho ni maumbile, urembo na mavazi. Kwa kawaida mwanamume anayelengwa ni yule mwenye sifa mbalimbali kama vile mwenye mali, mwenye umaarufu au sifa zingine zinazomvutia mwanamke. Kazi kubwa aliyonayo mwanamke ni kuhakikisha kuwa uzuri huo unatunzwa ili awe na nguvu na uwezo wa kumshindania mwanamume.

### 5.5.3 Unadhifu wa Mwanamke katika KCM

Katika KCM MF 130 kama inavyodhihirika hapa chini, Solomoni anabainisha unadhifu wa mwanamke katika ndoa:

**MF 130**

> Hujifanyia mazulia ya urembo;
> Mavazi yake ni kitani safi na urujuani.
> (KCM 31:22)

Katika MF 130 hapo juu, tunaelezwa kwamba mwanamke mzuri hudumisha usafi nyumbani mwake. Mwanamke huyu hujitengenezea mazulia ya urembo na kwamba mavazi yake ni safi na ya kupendeza macho. Tunasoma kuwa: ***Hujifanyia mazulia ya urembo.*** Hufanya hivi ili kumvutia mumewe na kuifanya nyumba yake makao maalum kwa mumewe. Mojawapo ya wajibu muhimu wa akina mama ni kudumisha

usafi ndani ya nyumba. Usafi ni ufunguo kwa elimusiha na afya. Huzuia maradhi mengi na huwavutia watu wa familia. Ni chanzo cha heshima kwa familia. Mwanamke lazima aweke nguo za familia yake mahala pazuri, safi na nadhifu. Ahakikishe kuwa vyakula ambavyo anaandalia familia viwe katika mazingira safi.

Nyumba nadhifu hupendwa zaidi kuliko nyumba chafu katika njia nyingi: unadhifu husaidia kuifanya nyumba ionekane safi, inavutia na ni mandhari ya kupendeza. Nyumba yenye mpangilio wa vitu, haimchoshi mtu, lakini itakuwa chanzo cha shangwe na furaha. Kazi ya utunzaji wa nyumba ingekuwa rahisi katika familia inayofuata maagizo ipasavyo, na mama mwenye nyumba angejua kwa usahihi mahali palipo vitu vya nyumbani, hangepoteza muda kuvitafuta.

Matokeo yake ni kwamba mwanamke hatachoshwa na kazi yake. Humvutia mwanamume kwa kuwa wanaume wengi hupenda usafi na unadhifu. Nyumba yenye mpangilio mzuri huwakilishi sifa chanya za mwanamke. Nyumba nadhifu ni chanzo cha majivuno ya familia yote. Yeyote anayeitembelea, atapendezwa nayo, na kuvutiwa na ubunifu na ladha ya mwanamke huyu kama inavyodhihirika katika MF 131 hapa chini:

**MF 131**

Mume wake hujulikana malangoni;
Aketipo pamoja na wazee wa nchi.
(KCM 31:23)

Katika MF 131, Mfalme Solomoni anaeleza kwamba. mwanamke ambaye anazingatia mambo ya nyumba yake husababisha mumewe kupewa heshima na watu wote. Hii ni kumaanisha kwamba kila mara mke akizingatia kanuni za ndoa na kuyatekeleza majukumu yake kama mwanamke, watu kule nje hujua na kwa hivyo mume wake

hushangiliwa na wenzake na kupewa heshima kila mara wanapoketi pamoja kwenye mazungumzo yao ya kila mara.

Hata hivyo, katika kipengele hiki cha 5.5, Unadhifu katika UWA ni suala ambalo halikujitokeza waziwazi kwa kuwa mwandishi wa *Utendi wa Ayubu* alijikita sana katika kubainisha mwanamke jasiri ambaye anaamua kujinyima kila kitu ili amshughulikie mume wake ambaye alikuwa anateseka kutokana na ugonjwa wa ukoma.

### 5.6 Mwanamume na Mwanamke Kuvumiliana katika Ndoa

Mwanamume na mwanamke ambao wamekula kiapo cha kuaminiana na kutia sahihi makubaliano ya ndoa, wanatakiwa kupita kwenye njia ya maisha kwa kuelewana. Makubaliano yanatakiwa kuwa imara sana wakati wowote, uwe wa maafa, maradhi, shida au raha. Katika kazi tulizozichagua, zinadhihirisha umuhimu wa mwanamke kuwa na ujasiri na jinsi ya kukabiliana na shida zinazoweza kutokezea.

#### 5.6.1 Mwanamume na Mwanamke Kuvumiliana katika UWM

Jinsi inavyobainika katika UWM, Mwanakupona alimpa bintiye wosia kwa kuwa alihitaji maelekezo katika ndoa jinsi ya kuvumiliana kama inavyodhihirika katika MF 132:

**MF 132**

Yalipokuya faradhi,
Kanikariria radhi,
Kashukuru kafawidhi,
Moyo wangu katushiya
(UWM ubeti 54)

Kutokana na MF 132 hapo juu, tunaelezwa kwamba katika Uislamu, mwanamke anatakikana apate radhi ya mumewe iwapo yeye anafariki au muume anapofariki. Kabla ya kufariki, mke apewe radhi ya mumewe yaani muume akubali mkewe

alimtendea mema katika maisha yao ya ndoa. Kwa hivyo, yeyote anayetangulia kufariki, jambo la radhi na kusameheana liwe limetokea.

Ubeti huu kwa hivyo unaeleza kwamba pindi wakati wa mauti (faradhi) umewadia, mumewe alimpa radhi yake. Tunasoma kuwa: ***Yalipokuya faradhi, Kanikariria radhi***, naye mwanamke akashukuru na moyo wake ukatulia kwa sababu amepata radhi ya mumewe kama dini inavyoagiza: ***Kashukuru kafawidhi, Moyo wangu katushiya.***

Kwa jumla, Mwanakupona alikubali hali yake ilivyo na kuendelea na maisha jinsi yalivyokuwa. Hii ni hali ya uhusiano mwema kati ya mume na mke ni sifa muhimu katika ndoa.

### 5.6.2 Mwanamume na Mwanamke Kuvumiliana katika UWA

Mfano wa uvumilivu ni ule wa Rehema mkewe Ayubu (UWA). Mwanamke huyu alivumilia maradhi ya Ayubu, shida za familia na akajaribu kwa jitihada zote kumsaidia Ayubu. Ayubu alivumilia kuwa na maradhi, alivumilia ufukara, na mkewe Rehema aliamua pia kuwa mke mvumilivu. Uhusiano wa mume na mke imeonyeshwa kuwa ya kuvumiliana mno kama inavyoelezwa katika MF 133 hapa chini:

**MF 133**

Ayubu akasumbuka
kwa ndwee yalomshika
Rehema kusikituka
siku zote akilia
(UWA ubeti 126)

Katika MF 133 tunasoma kwamba Ayubu anapougua ugonjwa wa ukoma, Rehema mkewe ndiye aliyekuwa karibu naye na hata alikuwa na huzuni alipogundua kuwa anaugua. Tunasoma kuwa: ***Ayubu akasumbuka, kwa ndwee yalomshika.*** Jamii yake na majirani walimtenga lakini yeye hakuwa tayari kuungana nao, alijizatiti kumtafutia

Ayubu chakula na kumfariji kwa mateso aliyokuwa nayo. Rehema alikuwa imara wakati huu wa shida na aliamua kuwa msaidizi wa kweli kwa mumewe Ayubu. Hoja hiyo inadhihirika katika MF 134 hapa chini:

**MF 134**

Rehema asikasiri
Akingia kulla dari
Kwambia ni tayari
Taka kuwatumikia
(UWA ubeti 128)

Kwa mujibu wa maelezo haya, umasikini unapoendelea kukita mizizi katika familia ya Ayubu na kusababisha ukosefu wa chakula, mkewe Rehema, alikuwa tayari kufanya lolote ili kuipatia familia yake lishe. Anazungukazunguka kwa nyumba za wenyewe akitafuta kazi hata ya kutupa taka ili apewe chakula. Tunasoma kuwa: ***akingia kulla dari, kwambia ni tayari, taka kuwatumikia.*** Hali kadhalika, hata anapofukuzwa na majirani anapoingia nyumbani mwao, anatoka na kwenda zake isipokuwa anaendelea kuwa na huzuni na kilio kama tunavyosoma katika MF 135 hapa chini:

**MF 135**

Kulla nyumba angiayo
Humfukuza kwa mbiyo
Kamba khabati tunayo
Yako tumeisikia
(UWA ubeti 151)

Kutokana na maelezo haya, ni dhahiri kwamba kila nyumba aliyoingia akafukuzwa mbio na kuambiwa tumekwisha sikia habari yote ikuhusuyo wewe. Tunaelezwa kuwa: ***Kulla nyumba angiayo, Humfukuza kwa mbiyo.*** Kutokana na usemi huu, inabainika kuwa Rehema hakukata tamaa bali aliendelea kumshughulia mumewe kwa moyo wake wote. Tunaonyeshwa hali yake ya kusosoneka jinsi inavyojitokeza katika MF 136 hapa chini:

**MF 136**

Karudi kisikitika
Matozi humdondoka
Katika ndia kifika
Awene ntu akiya
(UWA ubeti 155)

Kutokana na MF 136, Katika harakati za kumshughulikia mumewe, Rehema alijizatiti sana ili kuhakikisha kwamba mume wake alipata mahitaji yake ya kila siku hasa chakula. Katika ubeti huu tunaelezwa kwamba Rehema alipokuwa anarudi machozi yalikuwa yanamdondoka. Tunaelezwa kwamba: ***Karudi kisikitika, Matozi humdondoka.*** Yaani, ukosefu wa kazi pia ni ukosefu wa pato lake na kwa hivyo Ayubu angekosa chakula chake cha siku. Rehema alifika kiwango cha kuomba hata mabaki ya chakula yanayoanguka chini kama inavyobainika katika MF 137 hapa chini:

**MF 137**

Wala hamna masahaka
Kikitunda kichanguka
Kwani kitakula paka
Enyi hakitowafaa
(UWA ubeti 132)

Katika MF 137 tunasoma kuwa licha ya Rehema kutembeatembea na kuomba chakula kutoka kwa majirani, pia anatembea kutoka nyumba moja hadi nyingine na wazo la kuomba kazi. Wazo lake kuu la kuomba chakula na kazi lilikuwa ni kupata chakula cha kumlisha mumewe. Hata alikuwa tayari kuokota vipande vya mkate ambavyo anadai kuwa ni vya paka. Tunaelezwa kuwa: ***kikitunda kichanguka, kwani kitakula paka, enyi hakitowafaa***. Maneno haya yanamaanisha kuwa Rehema alikuwa amefika mwisho wake, na kwa hivyo aliomba chakula kilichoanguka. Wanawake wengi wa leo hawataweza kustahimili shida kama hii, lakini iwapo ndoa itadumu lazima wanawake waipiganie kwa nguvu zao zote.

Kipengele hiki cha 5.6 hata hivyo, kinaashiria kuwa uvumilivu katika ndoa ni suala ambalo halijadhihirika katika WUB na KCM kwa sababu Solomoni amemchora mwanamke ambaye anampenda kwelikweli, huyu mpenzi wake hajaona shida wala matatizo katika ndoa yao. Mpenziwe Solomoni amejitolea kutimiza mahitaji yote ya mume wake na kwa hivyo kumfanya Solomoni kumpenda kwa moyo wake wote. Tunampata mwanamke ambaye anafurahia mahusiano ya ndoa jinsi mwanamume wake anavyomsifu.

### 5.7 Dini kama Nyenzo muhimu katika Ndoa

Katika sehemu iliyotangulia (5.1-5.6), tulishughulikia uhusiano wa mwanamke na mwanamume katika ndoa. Katika sehemu hii, tumeshughulikia lengo la tatu ambalo ni, 'Kubainisha wosia kutoka dini kama kigezo muhimu katika uthabiti wa ndoa'. Dini ni dhana inayoashiria jumla ya mafundisho ya imani, itikadi na maadili, jinsi ya kuhusiana na Mungu muumba na kazi zake za uumbaji, binadamu na maisha kwa jumla.

Ndoa ni muungano wa hiari kati ya mwanamume na mwanamke wenye lengo la kuishi pamoja kama mume na mke kwa maisha yao yote. Muungano huu hukusudiwa kudumu kwa muda wa maisha yao. Kwa hivyo, ndoa ndio msingi wa familia, na familia ni tofali la kwanza la kujenga jamii na hatimaye kujenga umma. Ndoa ni hatua muhimu sana anayopitia binadamu maishani mwake, na ni hatua inayoathiri maisha ya mtu na maisha ya kizazi chake baadaye. Imani ni msingi wa maisha ya binadamu. Imani ni kile unachokiamini kimapokeo na ambacho ni mwongozo sahihi wa maisha yako ya baadaye. Al Farsy (1942: 7) katika *Ndoa na Maamrisho yake*, anawashauri wanaume wasiwaoe wanawake kwa ajili ya uzuri wao tu, huenda huo uzuri wao

ukawazamisha (katika mabaya) lakini wawaoe kwa ajili ya dini wanayofuata. Anasema:

> Kijakazi cheusi kisichokuwa na moja katika haya, lakini kina mwendo mzuri wa dini, ni bora zaidi kuliko wanawake wengine ambao hawajashika dini.

Sehemu hii imejadili; ndoa kama agizo kutoka kwa Mungu, suala la maombi katika ndoa, utimilifu wa ndoa katika dini, haki za wanandoa, kupendana katika ndoa, kuheshimiana, unyenyekevu katika ndoa kwa kurejelea lengo letu la dini kama kigezo muhimu katika uthabiti wa ndoa. Kwa jumla, haya ni masuala muhimu kuhusu dini yaliyojitokeza katika kazi zetu za kifasihi ambazo ni *Utendi wa Mwanakupona* na *Utendi wa Ayubu* na vile vile matini za kidini 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora'.

*Utendi wa Mwanakupona* unaanza kwa wosia kwa mwanawe kwamba ashike kanuni za Mwenyezi Mungu ili aweze kuwa na maisha ya furaha. *Utendi wa Ayubu* umeandikwa kwa msingi wa kidini ambapo Ayubu ni mtumishi wa Mungu aliyepatwa na matatizo mengi lakini akaamua kumtii na kumwabudu Mwenyezi Mungu. Vile vile, Solomoni mwandishi wa 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora' ni mcha Mungu aliyezitii na kuzishika kanuni za Mungu katika dini ya Kikristo.

### 5.7.1 Suala la Dini linavojidhihirisha Katika UWM

Katika UWM, mengi yameelezwa kuhusu imani, itikadi na maadili ya kidini kuhusiana na suala la ndoa. Mtunzi wa *Utendi wa Mwanakupona* alikuwa Muislamu aliyeshika amri za Mungu na kuyatekeleza na kumwomba bintiye vili vile azishike amri hizi. Al Farsy (1942) katika *Ndoa na Maamrisho yake* katika dini ya Kiislamu anasema kuwa Mwenyezi Mungu amebainisha mahala pengi katika *Kurani*, kwamba kuoa ni jambo la kheri sana na ni jambo ambalo wamelifanya Mitume wake.

Anaelezea kuwa kila mmoja ajitahidi kama awezavyo kufuata nyayo za Mabwana hao watukufu.

Katika *Biblia*, Musa katika kitabu cha Mwanzo anaelezea kuwa Mwenyezi Mungu alimwuumba mwanamke ili waishi na mume katika ndoa:

> Bwana Mungu akasema, Si vema huyo mtu awe peke yake,
> Nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye. (Mwanzo 2:18)
> Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake,
> naye ataambatana na mkewe ,
> Nao watakuwa mwili mmoja. (Mwanzo 2:24)

Kutokana na beti hizi, Mwenyezi Mungu ndiye mwanzilishi wa ndoa na anafurahia watu wanapooana na kuzaa kwa ajili ya ongezeko la binadamu.

#### 5.7.1.1 Sheria za Ndoa katika UWM

Mungu ndiye muumbaji na mwanzilishi wa mambo yote duniani. Aliyapanga mambo yote yaende kulingana na kanuni zake. Ndoa, kwa hivyo ina kanuni zake za kufuatwa na wanandoa, iwapo wangependa kudumisha uhusiano wao. Kwa mfano, katika *Utendi wa Mwanakupona*, Mwanakupona anamshauri bintiye ashikilie kanuni za Mwenyezi Mungu ili aweze kufanikiwa maishani kama inavyodhihirika katika MF 138 hapa chini:

**MF 138**

> La kwanda kamata dini,
> Faradhi usiikhini,
> Na sunna ikimkini,
> Ni wajibu kuitiya
> (UWM ubeti 12)

Katika MF 138 hapo juu, Mwanakupona anamsihi bintiye kuwa lazima ashike dini kwa kufuata maelekezo ya Mwenyezi Mungu. Katika maelekezo haya, lazima

azingatie maelekezi ya lazima (faradhi). Vile vile, maelekezo ya hiari ya Mwenyezi Mungu na maelekezo ya Mtume Muhammad (sunna) pia asiyaache, ayatekeleze kikamilifu. Katika dini ya kiislamu, kuna faradhi ( mambo ya lazima) na sunna (mambo ya hiari lakini ya heri). Maelekezi ya sunna, mtu anaweza kuyatenda au asiyatende. Akiyatenda maelekezi ya sunna anapata neema au thawabu kutoka kwa Maulana, asipotenda hapati chochote. Faradhi ni lazima Muislamu atende, asipotenda anapata dhambi. Kwa hivyo, Mwanakupona anamshauri bintiye atende faradhi na sunna kwa pamoja.

### 5.7.1.2 Suala la Sala katika UWM

Mwanakupona anaendeleza mawazo haya ya kanuni za dini katika ubeti wa nne kama inavyobainika katika MF 139 hapa chini:

**MF 139**

Kisake kutakarabu,
Bisumillahi kutubu,
Umtaye na Habibu,
Na sahabaze pamoya
(UWM ubeti 4)

Katika MF 139 hapo juu, tunaelezwa kwamba Mwanakupona anamweleza bintiye kuwa kabla ya kufanya lolote ataje jina la Mwenyezi Mungu. Tunaelezwa kuwa: ***Bisumillahi kutubu,*** nabii wake: ***Umtaye na Habibu,*** na malaika wote. Usemi huu unadhihirisha kuwa sala ni jambo muhimu katika ndoa na maisha kwa jumla. Mwanakupona anaendeleza mjadala huu katika MF 140 hapa chini:

**MF 140**

Ukisa kulitangaza,
Ina la Mola Muweza,
Basi tuombe majaza,
Mungu tatuwafikiya.
(UWM ubeti wa 5)

Katika MF 140 hapo juu, tunaelezwa kwamba baada ya kulitaja jina la Mwenyezi Mungu, basi waombe ili awajalie baraka na neema. Tunaelezwa kuwa: ***Basi tuombe majaza, Mungu tatuwafikiya.*** Mwanakupona anamshauri bintiye kuwa sala ni muhimu kwa kuwa Mungu husikia na hujibu maombi. Kuthibitisha haya, Mwanakupona alianza Utendi huu kwa dua na kumalizia kwa dua ubeti (4-7, 66-102). Falsafa ya mwandishi katika utenzi huu inaonekana kuwa sala ni suala muhimu sana katika maisha ya binadamu yeyote.

### 5.7.1.3 Suala la kupendana katika UWM

Katika MF 141 hapa chini tunaelezwa kwamba:

**MF 141**

Penda nikupe kifungo,
Kizuri kisicho ongo,
Uvae katika shingo,
Utaona manufaa
(UWM ubeti 10)

Katika MF 141 hapo juu, wosia wa Mwanakupona kwa bintiye unasisitiza umuhimu wa kufuata maelekezi ya Mwanakupona kwa kuwa yatamsaidia bintiye milele. Wosia huu utampa manufaa mengi ikilinganishwa na hasara. Mwanakupona anaona wosia huu kama kifungo kizuri cha kuvaliwa shingoni kwani wosia huu utamfaa maishani. Tunaelezwa kuwa: ***uvae katika shingo.*** Mwanakupona pia, anamweleza bintiye awe mtu wa upendo ili atapate faida za mapenzi. Tunaelezwa kuwa: ***Utaona manufaa.*** Mwanamke anapoyafuata maagizo mazuri ya ndoa na kanuni za ndoa, ataweza kupata faida na kuyafurahia maisha ya ndoa.

#### 5.7.1.4 Suala la Faida za dini katika UMW

Kusikilizana ni msingi muhimu katika dini, kwa kuwa watu wanaposikilizana wanaweza kukwepa shida na migogoro ambayo labda ingepatikana katika ndoa. Wanandoa kuwa wasikivu, waungwana na tayari kusikiza wanandoa wenzao wakati wa mzozo hufanya ndoa kuwa imara. Wanandoa wanafaa kuelekezana jinsi wanavyotaka wenzao wawe au watende. Mwanakupona anamshauri bintiye kama tunavyoelezwa katika MF 142 hapa chini:

**MF 142**

Pili uwa na adabu,
Na ulimi wa thawabu,
Uwe kitu mahabubu,
Kulla utakapongiya
(UWM ubeti 13)

Kutokana na MF 142 hapo juu, tunaelezwa kuwa Mwanakupona anamshauri bintiye awe mwenye adabu. Tunaelezwa kuwa: ***Pili uwa na adabu.*** Katika maelezo haya Mwanakupona anamshauri bintiye kuwa na adabu na matamshi yake yawe mazuri ndipo atapendwa popote anapoingia. Kinywa chake kisiwe chenye matusi kamwe na awe mtu wa matendo mema yatakayosababisha apendwe na jamii nzima. Tunaelezwa kuwa: ***Uwe kitu mahabubu.*** Kwa kufanya hivi, ataikwepa mizozo katika jamii na kwa hivyo ataishi kwa amani na mume wake. Mwanakupona anaendelea na mashauri yake kama tunavyosoma katika MF 143 hapa chini:

**MF 143**

La tatu uwa sadiki,
Ushikalo ulithiki,
Mtu asoshika haki,
Sandamane naye ndiya
(UWM ubeti 14)

Kutokana na maelezo haya ya MF 143 hapo juu, Mwanakupona anamhimiza bintiye awe mtu anayependa na kutenda mambo ya kweli daima. Tunaelezwa kuwa: ***La tatu uwa sadiki,*** yaani asiseme uongo bali atende mambo jinsi anavyoelekezwa na imani yake. Tunaelezwa kuwa: ***Ushikalo ulithiki.*** Awe mtu anayezingatia haki. Tunaelezwa kuwa: ***Mtu asoshika haki,sandamane naye ndiya.*** Hizi ni kanuni za dini ambazo zinaleta thawabu maishani.

**5.7.1.5 Suala la Unyenyekevu katika UWM**

Mwanakupona anaendelea kumshauri bintiye kuhusu unyenyekevu katika ndoa. Katika mfano ufuatao (MF 144) tunaelezwa kwamba:

**MF 144**

Yangu utakaposhika,
Mwanangu hutosumbuka,
Duniani utavuka,
Na akhera utakiya
(UWM ubeti 11)

Kutokana na maelezo MF 144 hapo juu, tunaelezwa kwamba Mwanakupona anamweleza bintiye afuate maagizo ya dini ili atapate furaha hapa duniani na baraka ya mbinguni. Anamsihi mwanawe kushika yote ambayo Mawanakupona amemfunza, kwamba mwanamke anafaa kunyenyekea na kumtii mumewe. Tunaelezwa kuwa: ***Yangu utakaposhika, Mwanangu hutosumbuka.***

Kumshukuru mume ni kudhihirisha unyenyekevu na ni tabia njema, kuwa na nidhamu, ni tendo la busara namna inavyosisitizwa katika dini. Wanandoa wanapaswa kuonyesha shukrani kwa kila jema wanalotendeana kama ishara ya kuthamini kazi, juhudi, na upendo wa mwenzake. Kusema ahsante kwa mwenzio wa ndoa ni ishara ya

kumpa nguvu na ari ya kuendelea kufanya makubwa zaidi, kwa uzuri zaidi na kwa moyo. Katika MF 145 tunaelezwa kwamba:

**MF 145**

Akupacho mpokeye,
Na moyo ufurahiye,
Asilotenda kwa yeye,
Huna haja kumwambiya
(UWM ubeti 49)

Kutokana na MF 145 hapo juu, tunaelezwa kwamba Mwanakupona anamhimiza bintiye awe tayari kupokea atakachopewa na mumewe: Tunaelezwa kuwa: ***Akupacho mpokeye,*** na wala asimlazimishe ampe kile ambacho hana uwezo wa kumpa. Pia tunaelezwa: ***Asilotenda kwa yeye, Huna haja kumwambiya.*** Mwanamke anahitaji kutosheka na kile amepata bali asilalamike kwa kuwa akifanya hivyo atakuwa anafungua mwanya wa migogoro katika ndoa.

### 5.7.2 Suala la Dini Katika UWA

Sehemu hii inahusu suala la dini katika UWA na hoja iliyoshughulikiwa ni kigezo cha maombi katika ndoa.

#### 5.7.2.1 Kigezo cha Sala katika UWA

Kwa mujibu wa *Utendi wa Ayubu,* suala muhimu ambalo limejitokeza katika dhana ya imani ni kusali au kuombeana katika ndoa. Wanandoa wanahitaji kusali siku zote pamoja ili wajaliwe neema ya kuwaimarisha na kuwadumisha katika maisha yao ya ndoa. Bila neema ya Mungu, shetani huwahangaisha na kuwavuruga wanandoa kila mara. Hivyo waliooana wanahitaji sana kuendeleza maisha ya sala. Kwa mfano, ubeti 328 wa *Utendi wa Ayubu* unawahimiza wanandoa wawe wakimwomba Mungu katika maisha yao ya kila siku kama inavyobainika katika MF 146 hapa chini:

**MF 146**

Tukala tikahilmili
tukimuomba wadudi
ili kazi ya abadi
wala nisikutukiwa
(UWA Ubeti 328)

Maelezo haya katika MF 146 hapo juu, yanadhihirisha wanandoa hawa baada ya kula humuomba Mola. Tunaelezwa kuwa: ***tukala tikahilmili tukimuomba Wadudi.*** Kwa hivyo, ni desturi ya wanandoa kuomba kila siku ili wasichukiwe na Mungu. Rehema katika kumheshimu Mungu na kuyafuata matakwa yake, anaonyesha umahiri, ujasiri, ukakamavu, kujitolea na kuyapinga mawazo ya shetani. Shetani anampa Rehema ahadi nyingi ili awachane na mumewe na kuenda kinyume na maagizo ya Mungu ila rehema anayapinga. Ayubu na Rehema wanashirikiana katika maombi ili Mungu amponye Ayubu na pia, awarejeshee mali na kumpinga shetani.

Rehema anakataa kushirikiana na shetani, ilhali alikuwa mwanamke maskini, hakuwa na chakula na wakati huo mumewe ni mgonjwa. Rehema anayashinda majaribu kutokana na imani thabiti aliyonayo. Kadhalika ubeti 329, unamchora Mola kama mpaji, kwa hivyo wanandoa wanastahili kumtumaini kila uchao kama tunavyosoma katika MF 147:

**MF 147**

Kikhudumu kwa furaha
na kumuombea siha
Mola  mpoaza jaraha
umpe ake afia
(UWA Ubeti 329)

Katika maelezo ya MF 147 hapo juu, tunaelezwa kwamba daima Rehema alimuomba Mungu ampe mumewe afya njema na kumponya majeraha aliyokuwa nayo. Rehema anadhihirisha kwamba maombi kwa Mola ni muhimu. Rehema na Ayubu wanadhihirisha kuwa ni Mungu anayetoa vyote, iwe ni afya, vyakula, mali, watoto au

chochote kile anachohitaji binadamu. Tunaelezwa kuwa: ***na kumuombea siha, Mola mpoaza jaraha.*** Mola hupoza jeraha na tatizo lolote hutatuliwa kwa uwezo wa Mungu. Kwa hivyo, wanandoa wanastahili kuwa na muda wa kuomba pamoja kama jamii ili Mwenyezi Mungu aweze kuwapa wanalolihitaji. Wanandoa huhangaika kwa mateso kutokana na kutengana katika ndoa au hata kutalakiana ilhali kupitia kwa maombi Mungu hutatua matatizo na changamoto katika ndoa.

#### 5.7.2.2 Suala la kupendana katika UWA

Katika *Utendi wa Ayubu*, Rehema alipendana na Ayubu kwa dhati kama inavyodhihirika katika MF 148 hapa chini:

**MF 148**

Imi ndiyo kuti angu
ya kula na mume wangu
tuyaaliwe na Mungu
haya kutusikilia
(UWA ubeti 133)

Katika mfano huu wa MF 148 hapo juu, mafunzo aliyoyapata Rehema kuhusu dini yalimsaidia kwa kuwa Rehema anadhihirisha upendo wa kweli. Anamwamini Mungu kuwa atamjalia mema na kuyasikia maombi yake. Rehema anajikaza kumtafutia Ayubu chakula. Tunaelezwa kuwa: ***ya kula na mume wangu, tuyaaliwe na Mungu.*** Maelezo haya yalitolewa na Rehema wakati Ayubu alipokuwa anaugua ugonjwa wa ukoma huku akimwamini Mungu atawajalia mema siku moja. Rehema anadhihirisha nafasi ya mwanamke aliyeshika mafunzo ya dini ambapo yuko tayari kuteseka kwa ajili ya mpenzi wake wa dhati.

#### 5.7.2.3 Suala la Kunyenyekea kama agizo la Kidini katika UWA

Katika *Utendi wa Ayubu* suala la unyenyekevu linasisitizwa kama agizo la kidini inavyojitokeza katika MF 149 hapa chini**:**

**MF 149**

Nikwambiao sadiqi
moya siitie dhidi
jalilu Mola khalaqi
mawi amenoondolea
(UWA ubeti 333)

Kutokana na MF 149 hapo juu, tunapata maelezo kuwa Mola ana uwezo wa kuondoa maovu. Tunaelezwa kuwa: ***jalilu Mola khalaqi, mawi amenoondolea.*** Hivyo basi, wanandoa wanapaswa kukuza na kujenga ushirikiano wao katika ndoa kwa misingi ya kidini ili kukabiliana na maovu na kuwapa ushirikiano mwema katika maisha yao ya ndoa.

### 5.7.3 Mafundisho ya Ndoa katika WUB

WUB na KCM ni dini kwa kuwa maagizo yote katika matini hizi mbili ni ya kidini na ni vifungu katika *Bibilia*. Kwa hivyo, katika sehemu hii, hoja zinazoshughulikiwa ni zile zinazowiana na matini za kifasihi tulizozijadili, yaani *Utendi wa Mwanakupona na Utendi wa Ayubu*.

#### 5.7.3.1 Suala la kupendana katika WUB

Solomoni katika Wimbo Ulio Bora 5:9, anaendeleza kigezo cha mapenzi katika ndoa kama inavyojitokeza katika MF 150:

**MF 150**

> Mpendwa wa namna gani ni mpendwa wako,
> Wewe uliye mzuri katika wanawake,
> Mpendwa wa namna gani ni mpendwa wako,
> Hata wewe utusihi hivyo?
> (WUB 5:9)

Solomoni anamchora mwanamke anayempenda kuliko wanawake wote. Tunaelezwa kuwa: ***Wewe uliye mzuri katika wanawake.*** Kutokana na maelezo haya, Mfalme Solomoni anamlinganisha mpenzi wake na wanawake wengine kisha anakiri kuwa mpenzi wake amewashinda wanawake wote. Solomoni anaendeleza mawazo yake katika Kitabu cha Wimbo Ulio Bora 7:1, bwana na bibi arusi wanaonyesha upendo na mapenzi yaliyo kati yao na pia wanaonyesha hali ya kuthaminiana, kila mmoja akimsifu mwenzake. Vile vile, katika WUB 8:7, bibi na bwana arusi wanatangaza kuwa mapenzi kati yao hayana kikomo. Haya yote yanaweka msingi thabiti kwa ndoa yao. Msingi wa kidini uliwasaidia kujiandaa kuhusu suala la ndoa na kwa hivyo kuwafanya kutokuwa na vizuizi bali furaha, upendo na mapenzi ya dhati kati yao.

### 5.7.4 Mafundisho ya Ndoa katika KCM

KCM pia ni dini kwa kuwa maagizo yote katika kitabu hiki ni dini. Kwa hivyo, katika sehemu hii, hoja zinazoshughulikiwa ni zile zinazoafikiana na *Utendi wa Mwanakupona na Utendi wa Ayubu* na hivyo nimefafanua vipengele vifuatavyo: Kanuni za dini katika ndoa, kusali pamoja katika ndoa, wosia faafu wa ndoa katika dini, agizo la kupendana katika dini, kunyenyekeana katika ndoa kama agizo la kidini na kuheshimiana katika Dini.

#### 5.7.4.1 Kanuni za dini katika KCM

Solomoni katika Kitabu cha Methali anasema (Tazama MF 151 hapa chini):

**MF 151**

Upendeleo hudanganya,
na uzuri ni ubatili;
Bali mwanamke amchaye Bwana,
ndiye atakayesifiwa
(KCM 31:30)

Solomoni anasema kuwa uzuri na urembo hudanganya na kumpa mwanamume picha isiyohalisi kuhusu mwanamke alivyo. Tunaelezwa kuwa: ***upendeleo hudanganya, na uzuri ni ubatili.*** Mwanamke anayemheshimu Mungu na kuzifuata kanuni za Mungu ni mwanamke bora. Tunaelezwa kuwa: ***bali mwanamke amchaye Bwana ndiye atakayesifiwa.*** Kwa hivyo, kinachosisitizwa hapa ni kuwa mwanamke mzuri lazima aishike dini wala si uzuri wa sura ya nje.

#### 5.7.4.2 Suala la Kusali Pamoja katika KCM kama Agizo la Kidini

Katika Kitabu cha Methali 25:2, Mfalme Solomoni anaendelea kubainisha umuhimu wa sala katika maisha ya binadamu kama tunavyosoma katika 152:

**MF 152**

Ni utukufu wa Mungu kuficha jambo
Bali ni utukufu wa mfalme
Kuchunguza jambo hilo
(KCM 25:2)

Kutokana na maelezo ya MF 152 hapo juu, Solomoni anazungumzia suala la maombi na kumtafuta Mungu kwa kumweleza yale ambayo ni magumu. Solomoni anatumia maombi kumfikia Mungu kwa kuwa Mungu haonekani. Tunaelezwa kuwa: ***Bali ni utukufu wa mfalme kuchunguza jambo hilo.***

#### 5.7.4.3 Wosia faafu wa Ndoa katika KCM kama Agizo la Kidini

Kulingana na utafiti wetu wa *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu*, ‘Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora’, imebainika kuwa maana na ufanisi wa ndoa hujengwa na imani za kidini. Mfalme Solomoni anabainisha uthabiti wa ndoa katika Kitabu cha Methali 5:1-14, kwa kumpa Mwanawe wa kiume ushauri kuwa ni lazima amsikilize na kutega masikio yake kwa makini kama tunavyosoma katika MF 153 hapa chini:

**MF 153**

> Mwanangu, sikiliza hekima yangu; Tega sikio lako, mzisikie akili zangu;
> Upate kuilinda busara, Na midomo yako iyahifadhi maarifa.
> Maana midomo ya malaya hudondoza asali, Na kinywa chake ni laini kuliko mafuta;
> Lakini mwisho wake ni mchungu kuliko pakanga; Ni mkali kama upanga wa makali kuwili.
> Miguu yake inatelemkia mauti; Hatua zake zinashikamana na kuzimu;
> Hata asiweze kuiona njia sawa ya uzima; Njia zake ni za kutanga-tanga wala hana habari.
> Basi, wanangu, nisikilizeni sasa, Wala msiache maneno ya kinywa changu.
> Itenge njia yako mbali naye, Wala usiukaribie mlango wa nyumba yake.
> Usije ukawapa wengine heshima yako, Na wakorofi miaka yako;
> (KCM 5:1-14)

Kupitia kwa maarifa ya Solomoni katika MF 153 hapo juu, mwanawe ataweza kuishi vyema na wengine. Anamshauri mwanawe, ajitenge na wanawake ambao ni makahaba. Tunaelezwa kuwa: ***Maana midomo ya malaya hudondoza asali, Na kinywa chake ni laini kuliko mafuta*** na hivyo vinywa vyao vinawaka kama moto na kutoa maneno ambayo daima ni matamu na yaliyo na uwezo wa kuyeyusha nyoyo za wanaume. Solomoni pia anamshauri kuwa wanawake wenye maneno matamu ya

kuwashawishi wanaume, maisha yao huwa mafupi mno, na mwishowe huishia mautini. Tunaelezwa kuwa: ***Miguu yake inatelemkia mauti; Hatua zake zinashikamana na kuzimu.***

Kadhalika, Solomoni anasisitiza kuwa wanawake ambao ni makahaba tabia zao si kamilifu na ni lazima mwanawe awe mwenye hekima na kujitenga nao. Tunaelezwa kuwa: ***Basi, wanangu, nisikilizeni sasa, Wala msiache maneno ya kinywa changu, Itenge njia yako mbali naye, Wala usiukaribie mlango wa nyumba yake.*** Solomoni anamwambia mwanawe kuwa asikaribie nyumba za wanawake wa aina hii, kujihusisha na shughuli zao au kujiingiza kwa mambo ambayo yanawahusu. Tunaelezwa kuwa: ***Wageni wasije wakashiba nguvu zako; Kazi zako zikawa ndani ya nyumba ya mgeni; Nawe ukaziombolea siku zako za mwisho, Nyama yako na mwili wako utakapoangamia***. Solomoni anataka mwanaye aepukane nao kwa kuwa mienendo ya wanawake hawa yaweza kufupisha maisha yake. Wosia wa mfalme Solomoni ni kuwa mwanawe ajiepushe na malaya. Ndoa nzuri ni ile iliyojengwa kwenye msingi wa kidini. Katika MF 154 tunasoma kwamba:

**MF 154**

Mwanamke mwema ni taji la mumewe
Bali aaibishaye ni kama kuoza mifupani mwake
(KCM 12:4)

Kutokana na MF 154 hapo juu, Mfalme Solomoni anatueleza kuwa mke mwema huwa taji la fahari kwa mumewe. Mwanamume hukuza na kumpenda mwanamke mwema lakini mwanamke mkorofi ni kama uozo kwa mumewe kwani humfanya mumewe kutawaliwa na huzuni na mashaka milele kama tusomavyo katika MF 155 hapa chini:

**MF 155**

> Mwanamke mwenye hekima huijenga nyumba yake,
> bali mpumbavu huibomoa nyumba yake
> kwa mikono yake mwenyewe.
> (KCM 14:1)

Katika kifungu MF 155 hapo juu, Solomoni anawashauri wanandoa wawe watu wa hekima, busara, na wacha Mungu na wajenge ndoa zao kwa msingi ambao ni thabiti katika dini. Tunaelezwa kuwa: ***Mwanamke mwenye hekima huijenga nyumba yake,*** Lakini wakiwa wapumbavu basi watazibomoa nyumba zao kwa mikono yao miwili, yaani kwa matendo ya wenyewe; ***Bali mpumbavu huibomoa nyumba yake kwa mikono yake mwenyewe.***

### 5.7.4.4 Suala la kupendana katika KCM kama Agizo la Kidini

Upendo ni kigezo muhimu katika dini. Mungu ni mwenye upendo na anasisitiza upendo kwa wanandoa ili waweze kuyatekeleza malengo yao ya ndoa. Upendo ni fadhila kuu inayowaunganisha watu wa ndoa. Maisha ya ndoa ni maisha ya uhusiano wa upendo kati ya mume na mke na sio uhusiano wa ubwana na utumwa. Kupendana si kati ya bwana na bibi tu pekee, bali kuwapenda wazazi na ndugu wa pande zote mbili. Kwa hivyo, ili upendo uwepo, lazima udhihirishwe na kuthibitika kwa njia ya fadhila zingine za hali na matendo. Msingi wa ushirikiano unatoka tu kwa kuwa na ufahamu wa ndoa kwa msingi wa kidini.

Tukirejelea mada yetu na data yetu tuliyokusanya kutoka *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi Wa Ayubu* , Wimbo Ulio Bora na Kitabu cha Methali, tunagundua kuwa suala la ndoa lilijengwa katika msingi wa mapenzi ya dhati, ushirikiano na upendo kama inavyoelezwa katika MF 156 hapa chini:

**MF 156**

> Mwanamke mwema ni taji la mumewe,
> Bali aaibishaye ni kama kuoza mifupani mwake
> (KCM 12:4)

Katika MF 156 hapo juu, Solomoni anatueleza kuwa mke mwema huwa taji la fahari kwa mumewe. Tunaelezwa kuwa: ***mwanamke mwema ni taji la mumewe.*** Mwanamke anapaswa kuwa na tabia njema na heshima nzuri, lakini mwanamke mkorofi ni kama dondandugu kwa mumewe kwani humfanya mumewe kutawaliwa na huzuni na mashaka milele. Tunaelezwa kuwa: ***bali aaibishaye ni kama kuoza mifupani mwake.***

**5.7.4.5 Kunyenyekeana katika KCM kama Agizo la Kidini**

Unyenyekevu ni sifa mojawapo katika zile kanuni za dini. Kuonyesha utiifu na upole, kuepuka kiburi, ujeuri, majigambo na matusi ni kanuni za dini. Kunyenyekea ni kufaana kila wakati kama tunavyosoma katika MF 157 hapa chini:

**MF 157**

> Ni afadhali kukaa katika pembe ya darini, kuliko katika nyumba pana pamoja na mwanamke mgomvi.
> Ni afadhali kukaa katika nchi ya nyika; Kuliko na mwanamke mgomvi, mchokozi.
> (KCM 21:9,19)

Katika MF 157 hapo juu, mfalme Solomoni anaeleza kwamba: ***afadhali kukaa katika pembe ya darini, kuliko nyumba pana pamoja na mwanamke mgomvi.*** Hii inatokana na sababu kwamba kuishi na mwanamke kama huyu kwenye nyumba moja ni sawa na kujichimbia kaburi. Mwanamke mgomvi pia huibomoa nyumba yake mwenyewe kwa mikono yake miwili.

Vile vile, anapozua ugomvi kila mara hakuna suluhisho ambalo hupatikana bali mambo huwekwa pamoja kwa muda na hatimaye ndoa hiyo hubomoka au husambaratika. Kutokana na maelezo haya, tunatambua kuwa ndoa nzuri ni ile ambayo mume na mke wanaheshimiana na kukaa kwa busara kuliko ugomvi, ukorofi na uchokozi. Tunasoma kwamba: ***ni afadhali kukaa katika nchi ya nyika, kuliko kuishi na mwanamke mchokozi.***

**5.7.4.6 Suala la Kuheshimiana katika KCM kama Agizo la Kidini**

Kanuni muhimu katika dini ni kuwa watu waheshimiane na kuthaminiana na kuepuka hali zinazozua machungu. Masuala yanayodhalilisha wenzako katika ndoa au yanayoweza kuvunja ndoa yanafaa kuepukwa kwa kudumisha heshima katika ndoa. Kulinda utu na hadhi ya mwenzio ni lazima ili kudumisha ndoa na kutomwona mwenzako kama mtumishi. Kutoonyesha dharau, kutomnyanyasa na kutomfinyilia chini kama inavyoelezwa katika MF 158 hapa chini:

**MF 158**

Mwanamke wa adabu
Huheshimiwa daima,
Na watu wakali hushika
Mali siku zote
(KCM 11:16)

Katika MF 158 hapo juu, Solomoni anatueleza kuwa mwanamke aliyena nidhamu, huwa na uhusiano mwema na watu, hali inayomfanya kuheshimiwa na wanawake wengine kuliko mwanamke aliyena kiburi, msaliti au anayekosa nidhamu. Kwa hivyo, ni jukumu la kila mwanamke kuwa na adabu, heshima na tabia njema ili naye pia apewe heshima. Tunaelezwa kuwa: ***mwanamke wa adabu, huheshimiwa daima.*** Mwanamume hupenda mke mwenye nidhamu.

Mwanamke akiwa na heshima ataishi na mumewe vyema huku wakiwa kielelezo chema kwa uzao wao. Nyumbani kulingana na Mwanakupona hakufai kuwa Jehanamu, mahali pa mateso, uwanja wa mapigano na shule ya matusi. Watoto huiga tabia za wazazi wao na hivyo amani na uelewano kati ya wazazi ni msingi imara kwa malezi na ujengaji wa tabia njema kwa watoto. Mke na mume lazima waheshimiane ndipo maisha ya ndoa yawe mazuri.

**5.8 Hitimisho**

Katika sura hii tumeshughulikia uhusiano wa mwanamke na mwanamume katika ndoa. Tulibainisha uhusiano wa mwanamke na mwanamume katika UWM, UWA, KCM, WUB. Tuligundua vigezo mbalimbali vinavyoweza kuujenga uhusiano mwema kati ya mume na mke katika ndoa. Kwa mfano, kufurahiana, kufarijiana, kuheshimiana, kusameheana, kufaana na kwamba uhusiano huu mwema humtegemea sana mwanamke. Ikiwa uhusiano wa wanandoa hauwezi kuzingatia yote tuliyoyataja katika sura hii, basi matarajio ya mahusiano katika ndoa yatakuwa kinyume na jinsi inavyoelezwa katika kazi zetu teule za *Utendi wa Mwanakupona* na *Utendi wa Ayubu* na pia matini za kidini; Methali na Wimbo Ulio Bora katika *Biblia*.

Kutokana na utafiti huu pia, imebainika wazi kuwa mwanzilishi wa ndoa ni Mungu, na kwamba inawapasa wanandoa wajizoeshe kusali pamoja. Ndoa itafana kutokana na mafunzo ya dini na kubainisha wazi haki za wanandoa katika ndoa. Wanandoa wanafaa kupendana, kuheshimiana, kuelewana, kunyenyekeana na kuungama makosa kila mara wanapokosa na kuwa tayari kusameheana. Mambo haya yote yanatokana na mafunzo ya dini, na kwamba ndiyo nguzo muhimu katika uthabiti wa ndoa yoyote. Tuna uhakika kutokana na utafiti wetu kuwa matatizo makubwa ya ndoa ni katika zile nyumba ambazo wanajamii hawamtegemei Mungu katika maisha yao ya kila siku.

Mwanamke mwenye asili ya dini ambaye hutambulika kama mwanamke shujaa mwenye maadili ya kuwa mke mwema, aliyechorwa katika *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu*, 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora'. Kwa kuegemea dini kama kigezo muhimu katika ndoa, mwanamke huwa mpenda maombi, mvumilivu, mnyenyekevu, na huwa na heshima, anaelewana na mume wake na pia anayaelewa majukumu yake ya ndoa. Wanandoa wakizifuata kanuni za dini juu ya ndoa, watayakwepa matatizo ya ndoa kama ugomvi, vita, utengano, talaka na hata mauaji, visa ambavyo tunavishuhudia kila mara katika jamii zetu hapa nchini Kenya. Katika sura inayofuata, tutatoa muhtasari, mahitimisho na mapendekezo ya utafiti huu.

# SURA YA SITA

# MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 6.0 Utangulizi

Katika sura ya tano tulizingatia uhusiano wa mwanamume na mwanamke katika ndoa kwa kurejelea kazi teule za fasihi ambazo ni *Utendi wa Mwanakupona* na *Utendi wa Ayubu* na matini za Kidini ambazo ni 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora' katika *Biblia*. Vile vile tulichunguza dini kama kigezo muhimu cha kuidhibiti ndoa. Katika sura hii, tumetoa muhtasari, mahitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Utafiti huu uliangazia usawiri wa mwanamke ndani ya ndoa katika *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu* na matini za kidini. Tulitoa muhtasari wa kila sura, mahitimisho ya kila lengo, mapendekezo ya utafiti na mapendekezo ya tafiti za baadaye.

## 6.1 Muhtasari wa Tasnifu

Katika utafiti wetu tuliangazia usawiri wa mwanamke katika ndoa kupitia *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu* na matini za Kidini. Katika sura ya kwanza, tuliangazia usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia-tete za utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka na umuhimu wa utafiti. Kila kipengele kilijadiliwa kwa kuzingatia mada yetu ya utafiti.

Katika sura ya pili, tulipitia maandishi na matini mbalimbali yanayohusiana na malengo ya utafiti huu. Nadharia zilizoongoza utafiti huu ni nadharia ya Ufeministi na nadharia ya Udenguzi. Tuliigawa kazi hii katika sehemu tatu kuu: yaliyoandikwa kuhusu taswira ya mwanamke katika ndoa, yaliyoandikwa kuhusu uhusiano wa mwanamke na mwanamume na yaliyoandikwa kuhusu dini kama kigezo muhimu katika uthabiti wa ndoa.

Katika sura ya tatu tulijadili mbinu za utafiti ambazo ni; eneo la utafiti, ukusanyaji wa data na uchanganuzi wa data iliyokusanywa. Tulikusanya data kutoka kwa kazi zetu teule za kifasihi ambazo ni UWM, UWA, WUB na KCM.

Katika sura ya nne, tuliangazia taswira ya mwanamke katika *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu,* 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora' na hali halisi ya maisha katika karne ya 21.Tulichanganua data tuliyokusanya kutokana na kazi zetu teule za kifasihi na matini za kidini.

Hatimaye katika sura ya tano, tulishughulikia uhusiano wa mwanamke na mwanamume katika ndoa. Tulibainisha uhusiano wa mwanamke na mwanamume katika UWM, UWA, KCM na WUB.

Kwa muhtasari, mapitio ya *Utendi wa Mwanakupona, Utendi wa Ayubu,* Wimbo Ulio Bora na Kitabu cha Methali yamebainisha wazi kwamba kazi hizi za kifasihi na matini hizi za kidini zimemsawiri mwanamke kama kiumbe cha thamani na kwamba hutekeleza majukumu yake kwa njia maalum.

## 6.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita hasa katika taswira ya mwanamke katika ndoa kwa kuangazia kazi teule za fasihi na matini maalum za kidini. Kutokana na utafiti huu, tuligundua kuwa mwanamke amesawiriwa kwa njia tofauti tofauti katika jamii. Kwanza, ana jukumu la kuilea familia kwa msingi wa dini, mila na desturi. Wanawake wanahimizwa kuwa ni vyema waambatane na watu ambao njia na mienendo yao ni nyoofu, haswa wakirejelea masuala ya kidini na Mungu na wanastahili kujiepusha na watu ambao njia zao zinaonekana kutokuwa na maadili.

Jambo lingine ambalo tumegundua katika utafiti wetu ni mapenzi. Imedhihirika kwamba hapo kale wanawake hawakujiingiza katika mapenzi kiholelaholela bali walilazimika kuweka mikakati kabambe na wale waliodai kuwa wanawapenda kabla ya kufanya uamuzi. Vile vile, mwanamke katika matini tulizozitafitia, amechorwa kama mwenye maadili, asiyefanya uasherati na mwaminifu katika ndoa yake.

Imedhihirika kuwa wanawake ni wakakamavu na jasiri na wenye kujitolea katika ndoa. Wanawake wamechorwa wakiwa na uwezo wa kudumisha ndoa zao na vile vile wale wazembe wanaweza wakazibomoa ndoa zao wenyewe. Wanawake wana uwezo wa kukabiliana na mengi katika ndoa zao kwa sababu ya ujasiri wao na kujitolea kwao. Tumebaini kuwa mwanamke ni msaidizi anayeweza kuipigania jamii yake kwa kila hali, iwe ni katika magonjwa, taabu na hata ukosefu wa mali.

Wanawake vile vile, imebainika kuwa ni watendaji na wala si washirika tu. Rehema katika *Utendi wa Ayubu* alijibidiisha kwa ukakamavu kuhakikisha kuwa familia yake inapata mahitaji yao, bila kumshirikisha mtu yeyote. Katika Kitabu cha Methali 31:10-31, vile vile tumelihakiki suala hili kwa upana. Wazo kuu ni kuwa ni vyema mwanamke awe mwenye bidii, awe tayari kuwalea wanawe na kuwasaidia wasiojiweza.

Suala lingine kuu kati ya wanandoa ni usafi wa kila siku. Kazi tulizozirejelea zimeangazia suala la usafi kwa undani kwani bila usafi wa mtu binafsi au mazingira wanamoishi, maisha katika ndoa yatakuwa magumu. Wanandoa wanapokuwa safi na nadhifu, kutakuwepo mahusiano mazuri, watapata baraka kutoka kwa Mola na mwisho mwanamke kwa sababu ndio nguzo kuu katika ndoa, ataweza kuzivutia fikira za mumewe na kufanya mume ampenda kikamilifu.

Katika utafiti huu, tuliyachunguza majukumu wanayoyatekeleza wanawake wa sasa katika ndoa na majukumu haya huchukuliwa na baadhi ya wataalamu kuwa ni mateso katika ndoa. Kwa kuangazia *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu*, 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora', tunagundua kuwa haya ni majukumu yaliyokusudiwa mwanamke tangu hapo jadi na ni kanuni ambazo haziwezi kuvunjwa iwapo tunataka kupata uthabiti wa ndoa katika jamii ya leo. Matokeo haya yadhihirisha kuwa wosia kutoka kwa UWM, UWA, KCM na WUB bado unafaa hadi leo. Iwapo tungependa ndoa thabiti basi mwanamke lazima amheshimu na kumtii mumewe.

Mwanamke katika kazi hizi ameelezwa kwa njia spesheli na ya kutosheleza majukumu ya mwanamke maishani mwake. Dini ni kigezo muhimu kwa jamii, kama ilivyojitokeza kupitia kazi tulizozichagua. Kwa hivyo, imani imejidhihirisha kama kiungo muhimu katika ndoa.

Kupitia utafiti huu, tuligundua kuwa hisia za mahaba ni muhimu sana kwa wapenzi ili kudumisha mahusiano yao. Mahaba ni njia mojawapo ya kumweka mpenzi wako tayari kwa kukupa kila kitu. Na changamoto moja hapa ni kuwa unaweza kusemwa na hata kuchekwa hasa katika nchi za ulimwengu wa tatu kwa mfano hapa Kenya, lakini la muhimu kwa wanandoa ni kwamba wanaonyeshana mahaba kwa ajili ya uhusiano wao. Kwa mfano, wanaposalimiana na wenzao wawapendao, wagusane mashavu yao, washikane mikono na hata kubusu. Wajikumbushe jinsi walivyokuwa wanagusana katika siku za kwanza, kabla hawajazoena, walikuwa wakigusana kwa huba na tamaa kubwa, kubusu inapowezekana na kadhalika. Ilidhihirika kuwa kugusana na kupapasana ni lugha muhimu ya mapenzi kwani kunadumisha mahusiano katika ndoa. Kwa muhtasari, tutaangazia matokeo ya kila lengo.

### 6.2.1 Taswira ya Mwanamke katika Ndoa

Lengo la kwanza katika utafiti huu lilikuwa ni kuchanganua taswira ya mwanamke katika ndoa, na tulilifikia lengo hili kwa kuangazia data tuliyokusanya kutokana na kazi zetu teule za kifasihi ambazo ni *Utendi za Mwanakupona* na *Utendi wa Ayubu*, na matini za Kidini ambazo ni 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora'. Mwanamke akizingatia taswira ya kuwa mpenda amani, mwanamke mwema, anayetekeleza wajibu wake, aliye na heshima, asiyenung'unika, mvumilivu na mwenye tabia nzuri kwa jumla, ataboresha ndoa yake na kuleta uthabiti katika nyumba yake huku akifurahia uamuzi wake wa kuolewa.

### 6.2.2 Uhusiano wa Mwanamke na Mwanamume katika Ndoa

Lengo la pili lilikuwa ni kutathmini uhusiano wa mwanamke na mwanamume katika ndoa. Tulibainisha uhusiano wa mwanamke na mwanamume katika UWM, UWA, KCM na WUB. Tulibainisha vigezo mbalimbali kutoka kwa UWM, UWA, KCM, WUB vinavyoweza kuujenga uhusiano mwema kati ya mume na mke kwenye ndoa. Kwa mfano, kufurahiana, kufarijiana, kuheshimiana, kusameheana, kufaana na kwamba uhusiano huu mwema humtegemea sana mwanamke.

Matokeo vile vile yanadhihirisha faida za sifa hizi muhimu za wanandoa kama vile, utumiaji wa lugha nzuri wakati wa maongezi, kuagana na mumewe kila mara anapoondoka kwenda kazini au katika shughuli zake za kila siku na kumkaribisha anaporejea, kupendana na kumjali mwenzako, kusameheana, kutimiza mahitaji ya kujamiiana kwa mwenzako, kutojihusisha na mpango wa kando, kuheshimiana, kumsaidia mkeo ama mumeo wakati wa majanga n.k. Wanandoa wakizifuata kanuni na sheria zinazostahili katika ndoa, basi watafurahiana, watasaidiana, wataaminiana na kufaana kila mara.

### 6.2.3 Dini kama Kigezo muhimu katika Ndoa

Kutokana na lengo letu la tatu, ilibainika wazi kuwa mwanzilishi wa ndoa ni Mungu, na kwamba inawapasa wanandoa wawe na mazoea ya kusali pamoja. Ufaafu wa ndoa unatokana na mafunzo ya dini na kubainisha wazi haki za wanandoa kwenye ndoa. Wanandoa wanafaa kufarijiana, kupendana, kuheshimiana,kuelewana, kunyenyekeana na kuungama makosa kila mara wanapokosa na kuwa tayari kusamehe mwenzake. Mambo haya yote yanatokana na mafunzo ya dini, na kwamba ndiyo nguzo muhimu katika uthabiti wa ndoa yoyote. Tuna uhakika kutokana na utafiti wetu kuwa matatizo makubwa ya ndoa ni katika zile nyumba ambazo wanajamii hawamtegemei Mwenyezi Mungu katika maisha yao ya kila siku.

Wanandoa wakizifuata kanuni za dini kwenye ndoa yao, watayakwepa matatizo ya ndoa kama ugomvi, vita, utengano, talaka na hata mauaji, visa ambavyo vimeshuhudiwa kila mara kwenye jamii zetu hapa nchini Kenya. Kwa hivyo, dini imebainika kuwa kigezo muhimu katika uthabiti wa ndoa.

## 6.3 Mahitimisho

Utafiti huu uliangazia usawiri wa mwanamke katika kazi teule za fasihi na matini za kidini. Yaani, *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu*, ‘Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora’. Kutokana na utafiti huu, tuligundua kuwa iwapo yaliyomo katika UWM, UWA, KCM na WUB yatazingatiwa na jamii ya leo, matatizo ya ndoa huenda yakapungua.

Nadharia ya Udenguzi ilitusaidia kubomoa na kuunda upya mielekeo mbalimbali inayohusiana na kazi yetu ya usawiri wa mwanamke katika ndoa. Kwa kusoma upya *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu* na matini za Kidini tulizozichanganua, tunagundua kwamba chuki, udhalilishaji, maonevu, unyanyasaji na ukandamizaji

uliodhaniwa kwa muda mrefu kufanyiwa mwanamke, ni majukumu yake yaliyokusudiwa tangu jadi. Kazi hizi zinampa mwanamke hulka nzuri katika jamii ili wanawake wachanga waweze kuwa na mwelekeo wa kijamii. Hizi ni kanuni ambazo lazima zifuatwe kwa minajili ya uimarishaji na uthabiti wa ndoa. Kwa kutumia nadharia hii ya Udenguzi, tumejaribu kuunda upya mtazamo wa mwanamke katika jamii na uhusiano wake na mwanamume. Hivyo basi, wanawake na wanaume hawakinzani bali wanasaidiana; lililo muhimu ni kwamba kila mmoja anasimamia nafasi yake kwa kuwajibika kama mume au mke katika kuyaendeleza maisha yao na ya jamii kwa jumla.

Ni dhahiri kuwa kazi tulizorejelea zinabainisha kwamba sanaa haiwezi kukadiriwa katika misingi ya ukale kama ilivyopendekezwa na wanafasihi wakongwe. Bali tunagundua kuwa fasihi faafu na iliyo hai ni ile inayotoa maudhui yanayoishi, yaani daima ni faafu katika jamii.

Kazi hizi kwa muhtasari zinawanasihi wasomaji wasilemazwe na fikra sawa na hizo ambazo, kwa hakika, ndizo adui wa maendeleo na kudumaza kukua kwa fasihi. Kupitia kwa utafiti huu, tumefahamu kuwa utamaduni, ndoa na dini, ndiyo masuala yanayomwelekeza mwanamke katika maisha yake ya kila siku. Katika utafiti huu, tulitumia mbinu tofauti tofauti zilizotuwezesha kuyachambua maisha ya wanawake kwa upana. Njia kuu tuliyoizingatia ni kurejelea tendi na vitabu vitakatifu kutoka *Agano la Kale*. Tuliyachambua mambo mengi ambayo yalitekelezwa na wanawake wa kale na tukagundua kuwa yanatofautiana na ya baadhi ya wanawake wa kisasa kwa mfano, kuwa na ndoa iliyojengwa katika msingi wa kidini, uhusiano mwema kati ya mume na mke na taswira inayodhihirisha hulka za mwanamke katika ndoa. Kwa mfano, mtunzi wa *Utendi wa Mwanakupona* anamwelekeza bintiye azingatie masuala

ya kidini. Pia *Utendi wa Ayubu* unamchora Rehema mkewe Ayubu kama mcha Mungu, jambo ambalo tunalipata pia katika 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora'.

**6.4 Mapendekezo ya Utafiti**

Katika utafiti huu tumeonyesha namna maisha na majukumu ya wanawake katika ndoa yalivyokuwa hapo jadi na umuhimu wa kuzingatia kanuni za ndoa zilizokuwepo kupitia fasihi na dini ili ndoa ziweze kudumu.

Kutokana na utafiti huu, kuna haja ya kuufanya utafiti zaidi. Tukizingatia jamii za kale tunaweza kusema kuwa wanawake walikuwa wanyenyekevu, wenye heshima, wenye imani thabiti na waliotekeleza majukumu yao kwa uzingatifu mkubwa. Wanawake wengi wa karne ya sasa wamekengeuka na kuathiriwa na kasumba ya kimagharibi katika viwango vyote vya maisha kwa sababu ya masomo na utandawazi. Wanaonekana kuwa katika hali na kiwango kimoja na waume wao.

Kutokana na matokeo ya utafiti wetu, tunapendekeza mambo yafuatayo: Kwanza, utafiti huu umejikita tu kwenye masuala machache ambayo kwayo kwa uzingatifu yanaonekana kuwakumba wanawake. Kazi yetu ni finyu kwa sababu tumeangazia tu masuala machache yanayohusiana na mwanamke katika nyanja zote za maisha. Basi ni tumaini letu kuwa watafiti wa baadaye watazingatia masuala yanaonekana kuwadhalilisha au kuwainua wanawake kwa jumla kama vile masomo, usawa katika nyanja zote za maisha wakirejelea wanawake wa karne tofauti tofauti. Kwa mfano uongozi usionekane tu kuwa wanaume ndio ambao wana uwezo wa kuongoza bali hata wanawake pia wanaweza kuonyesha ujasiri kupitia uongozi wao lakini wajikumbushe kuwa wao ni wanawake na kwa hivyo waendelee kuyatekeleza majukumu yao.

Pili, mabadiliko katika ndoa ya karne ya ishirini na moja na ndoa za jadi yachunguzwe. Kwa kuzingatia mapenzi ya kale, tunapata wanawake wa kale walifanya kila wawezalo kuhakikisha kuwa ndoa zao zinabaki imara. Jambo ambalo ni kinyume sana haswa tukilinganisha na ndoa za sasa. Pia mapenzi ya kale yanaonekana yalijengwa kwenye msingi wa kidini, na ngono kabla ya ndoa halikuwa jambo la kuzungumziwa. Tukilinganisha na maisha ya sasa, twaweza kusema kuwa dunia imebadilika kwa mwelekeo hasi. Tunapendekeza watafiti wengine waangalie sababu za tofauti hizi na ni kwa njia gani wanaweza kurekebisha tofauti hizi.

Tatu, wanaume wanapaswa kuepuka kasumba ya kuwapenda wanawake kwenye msingi wa maumbile bila kuzingatia imani yao ya kidini. Tumegundua kuwa swali hili halikuzingatiwa kamwe na wanaume wa kale. Pendekezo letu hapa ni kuwa wale watakaofanya utafiti wa baadaye, wajaribu kutafitia ni kwa nini wanaume wa sasa huzingatia maumbile ya wanawake haswa wakitaka kuchumbiana nao bila kuzingatia tabia zao kutokana na mafunzo ya kidini. Kwa nini wanaume wa kale hawakuzingatia jambo hili? Wao walizingatia mienendo na tabia za mwanamke mwanzo kabla ya mambo yanayoonekana.

Tunapendekeza pia, watafiti wa baadaye kutafitia sababu zinazopelekea ndoa za sasa kutodumu. Hapo kale kwa mfano, kupitia *Utendi wa Mwanakupona*, tunampata mama anamwambia bintiye kuwa atekeleze majukumu yote katika ndoa yake ndiposa ndoa yake idumu. Rehema, katika *Utendi wa Ayubu* hata kama alikuwa na changamoto nyingi katika ndoa yake na Ayubu, habanduki bali anafanya kila awezalo kuhakikisha ndoa yao iko imara, kwa nini si sasa?.

## 6.5 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu una mchango mkubwa katika taaluma ya Kiswahili na jamii kwa jumla. Tumeonyesha kwamba wosia katika *Utendi wa Mwanakupona*, *Utendi wa Ayubu* na matini za kidini ambazo ni 'Kitabu cha Methali na Wimbo Ulio Bora', si ukandamizaji wa mwanamke bali ni njia ya kujenga uhusiano mwema katika ndoa. Taswira ya mwanamke katika ndoa kwa kuegemea kazi hizi za kifasihi na kidini si udunishaji wa mwanamke bali ni wadhifa wake maalum katika jamii ili kuwe na uwiano na uimarishwaji wa ndoa. Iwapo tu wafuasi wa dini za Kiislamu na Kikristo watayazingatia maelekezo kutoka kwa kazi hizi, basi itakuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha ndoa zetu.

Utafiti huu vile vile ni mchango katika fasihi ya Kiswahili kwa wasomaji na wahakiki wa fasihi ya karne ya 21. Watafiti wanafaa kuziangalia kazi hizi upya, na kwamba zina wosia bora unaojikita katika misingi ya kidini. Kwa kuelekezwa na nadharia ya Udenguzi, kazi hizi zimepata sura mpya na kwamba mwanamke amesawiriwa vyema katika taasisi ya ndoa. Mwanamume amepewa majukumu yake maalum katika jamii jinsi alivyopewa mwanamke kwa ajili ya ustawi wa ndoa.

**MAREJELEO**

Al-Amin, A. (1936). *Ndowa na Talaka katika Sharia ya Ki-Islamu.* Mombasa: H.O Adam and Sons Publishers.

Al Farsy, A (1942). *Ndoa-Talaka na Maamrisho yake*. Zanzibar: Mulla Karimjee Mulla Mohamedbhai and Sons

Al Wolters, F. (2006). *Theological Wordbook of the Old Testament:* Moody Bible Institute, uk. 127.

Allen, J. W. T. (mha.) (1971). *Sanaa ya Utungo: Utendi wa Mwanakupona.* Nairobi: Heinemann Education Books (E.A) LTD.

____________(mha.) (1972). *Sanaa ya Utungo: Utendi wa Ayubu*. Nairobi: Heinemann Education Books (E.A) LTD.

Beauvoir, S. (1952*). The Second Sex.* London: Pan Books Publishers.

Biersteker, A. (1991). Language Poetry and Power: A Reconsideration of Utendi wa MwanaKupona katika *Faces of Islam in African Literature*. Heinemann Education Books. uk. 59-77.

Bitugi, M. (2001). *Mkasa wa Shujaa Fumo Liyongo;* Nairobi: Phoenix Publishers.

Bressler, M. (2003). *The Feminist Reader: Essays in Gender and Politics of Literary Cricitism 2nd Edition.* London: Macmillan ltd.

Camp, C. (2003). *Wisdom and the Feminine in the Book of Proverbs.* Decatur Press

Carter, D. (2006). *The Pocket Essential: Literary Theory.* Herts: Cox & Wyman Ltd.

Chodorow, N. J. (1989). *Feminism and Psychoanalytic Theory*. Cambridge, UK: Yale University Press.

Crook, M. B. (1954) "The Marriageable Maiden of Provo 61:10-31," *Journal of Near Eastern Studies* 13.

Derrida, J. (1981). *Deconstruction Theory: Gerd Zacher Encounter* Rotterdam. The Netherlands publishers.

Dworkin, A. (1979). *The New Womans Broken Heart*. Frog in the Well Press

Eagleton, M. (1991). *Feminine Literary Criticism*. London: Longman Group Limited.

El-Maawy, A. (2011). *Jawabu la Mwanakupona. Mausio ya Mke wa Kisasa na Wasiya wa Mwana Kupona.* Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Ellmann, M. (1968). *Thinking about Women.* New York, Harcourt, Brace & World. Harvest book Series.

Festinger, D. Marczyk, G. R., & DeMatteo, D. (2005). *Essentials of research design and methodology*. Hoboken, N.J.: John Wiley & Sons.

Fox, M. V. (1985). *The Song of Songs and Ancient Egyptian Love Songs.* USA:Yale University press.

Freud, S. (1950). *The Standard Edition of the Complete Psychological Works*. London: Hogarth.

Friedan, B. (1963). *The feminine mystique*. New York : Norton,

Friesen, L. J. (1990). 'Marriage: A Biblical model in historical perspective'. Tasnifu ya Uzamifu, Department of Theology, Talbot School of Theology:Biola University.(Tasnifu haijachapishwa)

Gideons International. (2010). *Biblia Takatifu*. India.

Greer, G. (1970): *The Female Eunuch.* London: Grafton Books.

Grey, M. & Selling, J. A.(2001). 'Marriage and sexuality in the Catholic Church', Katika J.A. Selling (ed.), *Embracing sexuality: Authority and experience in the Catholic Church*, Ashgate Publishing Company, Burlington. pp. 179–183.

Hermanson, M. R. (2001). "The Personification of Wisdom in Proverbs 31:10-31" http://www.textetc.com/modernist.html

Holcombe, J. (2007). *Modernist Poetry and the Contemporary Scene. http://www.textetc.com/modernist.html* (tarehe 21, mwezi wa Februari 2017)

Imbo, O. (2002). *Oral Traditions as Philosophy.* London: Rowman and Littlefield Publishers

Iribe, P., na Mukhwana, A. (2011). *Isimujamii*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2002). Nairobi: Oxford University Press.

Indede, F. (2011).'Mwanamke Angali Tata katika Ushairi wa Kisasa'.Swahili Forum 18163-197.

Katola, E. (2006), "Udhalimu Dhidi ya Wahusika wa Kike katika Tamthilia za Kiswahili". Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa).

Kemei, T. (2016). *Mumewe Marehemu Chelele Ashtakiwa* http://www.swahilihub.com. Imepakuliwa: Januari 14, 2016.

Kent, C. F. (1921). *The shorter Bible: the Old Testament.* New York: Scribner

Khatib, M. S. (1985). "Utenzi wa Mwanakupona" katika *Mulika* No.7. uk 46-52 Dar es salaam: TUKI

Kitali, H. N. (2011). *Fani na usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia ya Pango na Mama ee*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Kilonzo, E. (2016). *Battered Woman Says She Stayed on to Save Marriage.* http:www.nation.co.ke/news. Imepakuliwa - Alhamisi, Agosti 3, 2016

Knappert, J. (1967). *Traditional Swahili Poetry: An Investigation into the Concepts of East African Islam as reflected in the Utenzi Literature*. Leiden: E.J. Brill

Lawis, S., na wanzake (2003). *Research for Development*. New Delhi: Vistaar Publications.

Lugano, R. (1989). "Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi". Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Maingi, G. (2005). "The Kenyan Constitutional Reform Process" A Case Study on the Work of PI DA Kenya in Securing Women's Rights' *Feminist Africa 63, 66*

Matundura, E. (2007). *Taaluma ya Tafsiri katika vyombo vya Habari Nchini Kenya*: *Matatizo, Changamoto na Mustakabali Wake*,Twaweza Communications.

Mazrui, A. A., & Mazrui, A. M. (1995). *Swahili State and Society*. *The Political Economy of an African Language*. Nairobi: E.A. E. P.

Miller, J. B. (1976). *Toward a new psychology of women*. Boston: Beacon Press

Millet, K. (1979). *Sexual Politics*. New York: Garden City.

Mirikau, S. (2011). "Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia za Wamitila" Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Mnenuka, A. (2012).'Tofauti ya dhana ya mwanamke katika jamii'. *Swahili Forum* 19

Mohamed, M. A., na Mohamed, S. A. (2002). *Kamusi ya Visawe*.Nairobi. East African Educational Publishers Ltd: Nairobi.

Mohamed, S. A. (2010). *Nyuso za Mwanamke.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Mohamed, S. A. (2006). *Dunia Yao.* Nairobi: Oxford University Press.

Momanyi, C. (1998). "Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili". Tasnifu ya uzamifu. Nairobi. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki Wa Fasihi*. East African Educational Publishers Ltd.

Mulokozi, M. M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, TUKI.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Murphy, R. P. (2006). *Ecclesiastes, Song of Songs*. Grand Rapids. Dallas Theological Seminary

Mwamzandi, I. Y. (2013). "Riwaya teule za karne ya ishirini na moja na udurusu wa nadharia za fasihi". *Swahili Forum* 20: 48-66

Mwanakombo, M. H. (2011). "Tajriba za Uislamu Katika Utamaduni wa Mwanamke Mswahili: Ufasiri wa Ufeministi wa Kiislamu*".*Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret (Haijachapishwa).

Ndumbaro, E. (2013). *Dini.* Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Dar es Salaam: TUKI.

Ndungo, C. W. (1985). Mwanamke katika Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili. Haijachapishwa. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Njogu, K., na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njozi, H. (1990). 'Utendi wa Mwanakupona and Reception Aesthetics'. *Kiswahili* 57: 55-67. Dar-es-Salaam: TUKI.

Nkata, J. L., & Thody, A. M. (2001). *Who Is Allowed To Speak?* An Introductory Commentary on Ugandan and English Experiences of Community Involvement in the Control of Schools.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustana College. of Wisconsin Press, Madison, WI.

Ogudipe, L. (1987). *The Female Writer And Her Commitment*. London: Routledge.

Onyoni, J. K. (2012). Usawiri wa Wahusika wa Kike Katika Tamthlia za Natala na Mama Ee. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa).

Quayson, A. (1997). ''Protocols of Representation and the Problems of Constituting an African 'Gnosis': Achebe and Okri'', *Year book of English Studies* 27: 137-149.

Renate, P. (2008). 'Poem of the edge of differences; Mothering' Katika *New English Poetry by woman* (Gender Studies Woman) US: University of Akron.

Rorty, R (1996). Deconstruction and circumvention. *The university of Chicago press journals* 11, 1-23

Schmitz, T. A. (2007). *Modern LiteraryTheory and Ancient Texts*: *an Introduction.* Malden: Blackwell Publishing.

Senkoro, F. E. M. K. (1987). *Fashi na Jamii*. Dar es salaam: Press and Publishing Centre.

___________(1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar es salaam: Dar es salaam University Press.

Simala, I. K. (2000). 'Uhakiki wa Uana katika Ushairi wa Kiswahili'. Tasnifu ya Uzamifu. Eldoret: Chuo Kikuu cha Moi (Haijachapishwa).

Steady, A. (1981). *Reflecting on the Politics of Sisterhood*. New York: African Wordpress.

Swaleh, A. (1992). 'Maudhui katika Utenzi wa Mwanakupona'. Tasnifu ya Uzamifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Thatcher, A. (2002). *Living together and Christian Ethics*, Cambridge: Cambridge University Press.

Wafula, R. M., na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Walsh, C. E. (2000). *Exquisite Desire: Religion, the Erotic, and the Song of Songs* Minneapolis: Fortress Press.

Wamitila, K. W. (2003a). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus publication

____________(2003b). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*: Nairobi: Focus Publications Limited.

____________(2008a). *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

_______________ (2008b). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers Limited.

Wanjiku, K. na Akinyi, N. (1993). *Celebrating Women's resistance. A case study of Women Groups Movement in Kenya*. Nairobi: Africa Women Perspective.

Werner, A. (1971). 'Utendi wa Ayubu'. *Bulletin of the School of Oriental Studies*.

Wesley, J. (2014) *Wesley's Notes on the Bible*. Grand Rapids, MI: Christian Classics Ethereal Library, n.d. http://www.ccel.org/ccel/wesley/notes.pdf

Wollstonecraft, M. (1792). *A Vindication of the Rights of Woman*. Boston, Faust's statue, no. 45, Newbury-street.

Woolf, V. (1929). *A vindication, A Room of One's own*, London: Hogarth.

Yule, G. (1996). *The Study of Language*. Cambridge University Press, Cambridge.

## VIAMBATISHO

## TASWIRA YA MWANAMKE KATIKA NDOA

### Baadhi Ya Data Tulizozichanganua:

***Kiambatisho 1: Utendi wa Mwanakupona (UWM)***

| *Beti* | *Beti* |
|---|---|
| *1.Naawe* radhi mumeo,<br>2.Siku zot'e mkaao,<br>3.Siku mukhitariwao,<br>4.Awe radhi mekuwiya.(ubeti 24)* | *5.Keti naye kwa adabu,<br>6.Usimtie ghadhabu,<br>7.Akinena simjibu,<br>8.Itahidi kunyamaa(ubeti wa 28)* |
| *9.Enda naye kwa imani,<br>10.Atakalo simukhini,<br>11.We naye sikindaneni,<br>12.Mkindani huumiya (ubeti wa 29* | *13.Mwanangu siwe mkoo,<br>14.Tenda kama uonao,<br>15.Kupea na kuosha choo,<br>16.Sidharau marra moya(ubeti 37)* |
| *17.Na kowa na kuisinga,<br>18.Na nyee zako kufunga,<br>19.Na yasimini kutunga,<br>20.Na firashani kutiya(ubeti 38)<br><br>25.Na kidani na kifungo,<br>26.Sitoe katika shingo,<br>27.Muwili siwate mwengo,<br>28.Ya marashi na daliya(ubeti 40)* | *21.Nawe ipambe libasi,<br>22.Ukae kama 'arusi,<br>23.Maguu tia kugesi,<br>24.Na mikononi makowa(ubeti 39)<br><br>29.Pete sikose zandano,<br>30.Hina sikome nyaani,<br>31.Wanda siwate matoni,<br>32.Na nshini kuitiya(ubeti 41)* |
| *33.Nyumba yako i nadhifu,<br>34.Mumeo umsharifu,<br>35.Wakutanapo sufufu,<br>36.Msifu ukimweteya(ubeti 42)* | *37.Moyowe alipendalo,<br>38.Nawe ufuate lilo,<br>39.Yambo limtukialo,<br>40.Siwe mwenye kumweteya(ubeti 43)* |
| *41.Ukutiwapo kutoka,<br>42.Sharuti ruhusa taka,<br>43.Uonapo meudhika,<br>44.Rudi na kuiketiya(ubeti 44)* | *45.Fuata yake idhini,<br>46.Awe radhi kwa yakini,<br>47.Wala sikae ndiani,<br>48.Saa yane kasia ndiani(ubeti 45)* |
| *49.Wala sinene ndiani,<br>50.Sifunue shiraani,<br>51.Mato angalia tini,<br>52.Na uso utie haya(ubeti 46)* | *53.Rejea upesi kwako,<br>54.Ukakae na bwanako,<br>55.Utengeze matandiko,<br>56. Mupate kuilaliya(ubeti 47)* |
| *57.Na bwanako mtukuze,<br>58.Sifa zake uzeneze,<br>59.Wala simshurutize,<br>60.Asoweza kutukuwa(ubeti 48)* | *61.Akupacho mpokeye,<br>62.Na moyo ufurahiye,<br>63.Asilotenda kwa yeye,<br>64.Huna haja kumwambiya(ubeti 49)* |
| *65.Uonapo uso wake,<br>66.Funua meno uteke,<br>67.Akwambialo lishike,<br>68.Illa kuasi Jaliya(ubeti 50)* | *69.Mama sinoe ulimi,<br>70.Nioleza wako umi,<br>71.Naliowa nyaka kumi,<br>72.Tusitete siku moya(ubeti 51)* |
| *73.Naliowa na babako,<br>74.Kwa furaha na ziteko,<br>75.Tusondoleane mbeko,<br>76.Siku zot'e twalokaa(ubeti 52)* | *77.Siku moya tusitete,<br>78.Ovu langu asipate,<br>79.Na lake lisinikute,<br>80.Hatta akakhitariwa(ubeti 53)* |
| *81.Pili uwa na adabu,<br>82.Na ulimi wa thawabu,<br>83.Uwe kitu mahabubu,<br>84.Kulla utakapongiya (ubeti 13)* | *85.Mnyoe umpalilize,<br>86.Sharafa umtengeze,<br>87.Na udi umfukize,<br>88.Bukurata wa ashiya (ubeti wa 34)* |

| | |
|---|---|
| *89.Mpumbaze apumbae,*<br>*90.Amriye sikatae,*<br>*91. Maovu kieta yeye,*<br>*92.Mngu atakuteteya (ubeti 36)* | *93.Mwanangu siwe mkoo,*<br>*94.Tenda kama uonao,*<br>*95.Kupea na kuosha choo,*<br>*96.Sidharau marra moya(ubeti 35)* |
| *97.Negema wangu binti,*<br>*98.Mchachefu hasanati,*<br>*99.Upulike wasiati,*<br>*100.Asaa ukazingatiya (UWM ubeti 1)* | *101.Kilala siikukuse,*<br>*102.Mwegeme umpapase,*<br>*103.Na upepo nasikose,*<br>*104.Mtu wa kumpepeya (ubeti wa 31)* |

***Kiambatisho 2: Wimbo Ulio Bora (W U B)***

| *Maelezo* | *Sura* | *Mstari* |
|---|---|---|
| *9 Mpenzi wangu, nimekulinganisha Na farasi*<br>*katika magari ya Farao*<br>*10 Mashavu yako ni mazuri kwa mashada, Shingo yako kwa mikufu ya vito*<br><br>*14 Mpendwa wangu ni kama kishada cha hina, Katikamizabibu huko Engedi*<br>*15 Tazama, u mzuri, mpenzi wangu,U mzuri, macho yako ni kama ya*<br>*hua.* | *1*<br><br><br><br><br>*1* | *9-11*<br><br><br><br><br>*14-15* |

***Kiambatisho 3: Kitabu cha Methali (KCM)***

| | | |
|---|---|---|
| *9 Ni afadhali kukaa katika pembe ya darini, Kuliko katika nyumba pana pamoja na mwanamke mgomvi.*<br>*19Ni afadhali kukaa katika nchi ya nyika; Kuliko na mwanamke mgomvi, mchokozi.* | *21* | *9*<br><br>*19* |
| *10 Mke mwema, ni nani awezaye kumwona? Maana kima chake chapita kima cha marijani.* | *31* | *10* |
| *Moyo wa mumewe humwamini, Wala hatakosa kupata mapato.* | *31* | *11* |
| *Humtendea mema wala si mabaya, Siku zote za maisha yake* | *31* | *12* |
| *Hutafuta sufu na kitani; Hufanya kazi yake ya mikono kwa moyo.* | *31* | *13* |
| *Afanana na mserikebu za biashara; Huleta chakula chake kutoka mbali.* | *31* | *14* |
| *Tena huamka, kabla haujaisha usiku; Huwapa watu wa nyumbani mwake chakula; Na wajakazi wake sehemu zao.* | *31* | *15* |
| *Huangalia shamba, akalinunua; Kwa mapato ya mikono yake hupanda mizabibu.* | *31* | *16* |
| *Hujifunga nguvu viunoni kama mshipi; Hutia mikono yake nguvu.* | *31* | *17* |
| *18Huona kama bidhaa yake ina faida; Taa yake haizimiki usiku. 19Hutia mikono yake katika kusokota; Na mikono yake. huishika pia.* | *31* | *18 na 19* |
| *Huwakunjulia maskini mikono yake; Naam, huwanyoshea wahitaji mikono yake.* | *31* | *20* |
| *Hawahofii theluji watu wa nyumbani mwake; Maana wote wa nyumbani mwake huvikwa nguo nyekundu.* | *31* | *21* |
| *Hujifanyia mazulia ya urembo; Mavazi yake ni kitani safi na urujuani.* | *31* | *22* |
| *Mume wake hujulikana malangoni; Aketipo pamoja na wazee wa nchi.* | *31* | *23* |
| *Hufanya nguo za kitani na kuziuza; Huwapa wafanya biashara mishipi.* | *31* | *24* |
| *Nguvu na hadhi ndiyo mavazi yake; Anaucheka wakati ujao.* | *31* | *25* |
| *Hufumbua kinywa chake kwa hekima, Na sheria ya wema i katika ulimi wake.* | *31* | *26* |

| | | |
|---|---|---|
| ***Huangalia sana njia za watu wa nyumbani mwake; Wala hali chakula cha uvivu.*** | ***31*** | ***27*** |
| ***Wanawe huondoka na kumwita heri; Mumewe naye humsifu, na kusema,*** | ***31*** | ***28*** |
| ***Binti za watu wengi wamefanya mema, Lakini wewe umewapita wote.***<br>***Mke mgomvi ni kama***<br>***matone yasiyokoma ya siku ya mvua.***<br>***Kumzuia yeye ni kama kuuzuia upepo***<br>***au kukamata mafuta kwa kiganja cha***<br>***mkono*** | ***31***<br>***27*** | ***29***<br>***15-16*** |

*Kiambatisho 4: Utendi wa Ayubu (U W A)*

| *Beti* | *Beti* |
|---|---|
| *1.Wote wakamsukuma*<br>*2.pasiwe alomwegema*<br>*3.illaye mwana Rehema*<br>*4.mke wake mfadhaa (ubeti 121)*<br><br>*9.Mke soyo niwanbie*<br>*10.muumba umuumbiye*<br>*11.kana sura za babiye*<br>*12.za Yusufu Fahamia(ubeti 123)* | *5.Na yeye mwana Rehema*<br>*6.asiliye mbeu njema*<br>*7.ni binti furahimu*<br>*8.wa yusufu nisikie(ubeti 122)*<br><br>*13.Mwema mzawa na wema*<br>*14.yakamuelea tama*<br>*15.mumewe kumsukuma*<br>*16.kwa sababu ya kuwaa(ubeti 124)* |
| *17.Kaketi naye rijali*<br>*18.juzamu asiijali*<br>*19.walikilala wawili*<br>*20.na kuamka pamoya(ubeti 125)* | *21.Ayubu akasumbuka*<br>*22.Kwa ndwee yalomshika*<br>*23.Rehema kusikitika*<br>*24.Sikuzote akilia(ubeti 126)* |
| *25.Akawata masindizi*<br>*26.Rehema kitenda kazi*<br>*26.Ili kupata khubuzi*<br>*28.Kumpa wake rijaa(ubeti 127)* | *29.Rehema asikasiri*<br>*30.Akingia kulla dari*<br>*31.Kawambia ni tayari*<br>*32.Taka kuwatumikia(ubeti 128)* |
| *33.Nitumani kazi zenu*<br>*34.Zilo mayumbani mwenu*<br>*35.Kwamba ni kutwewa ngano*<br>*36.Mkinipa tawetea(ubeti 129)* | *37.Niwakatulie pete*<br>*38.Niwasinge niwapote*<br>*39.Mnipe name mkate*<br>*40.Mlapo ukisali(ubeti 130)* |
| *41.Na tena msinikinde*<br>*42.Niyapoona kipande*<br>*43.Cha mkate nikitunde*<br>*44.Tiati nichangukia(ubeti 131)* | *45.Wala hamna mashaka*<br>*46.Kikitunda kichanguka*<br>*47.Kwani kitakula paka*<br>*48.Enyi hakitowafaa(ubeti 132)* |
| *49.Sidhani takasirika*<br>*50.na nadhiri nimewewka*<br>*51.upoapo uchinuka*<br>*52.unipije mbati mia(ubeti 284)* | *53.Lo lote nikufuate*<br>*54.ili radhi niipate*<br>*55.bwana pokea nkate*<br>*56.usiiiudhi kwa ndaa(ubeti 286)* |
| *57.Ayubu katakalama*<br>*58.akamwambia Rehema*<br>*59.nawe ni asili njema*<br>*60.dhuria ya mursaa(ubeti 287)* | *61.Umekusa sumbuko*<br>*62.umezanya nywee zako*<br>*63.wala usiche ziteko*<br>*64.za wendo kukutekea(ubeti 288)* |
| *65.Asinyamae kusema*<br>*66.kunena akisa koma*<br>*67.akamshika hurama*<br>*68.Ayubu akashangaa(ubeti 355)* | |

**UHUSIANO WA MWANAMKE NA MWANAMUME KATIKA NDOA**

***Kiambatisho 5: Uhusiano wa Mwanamke na Mwanamume (UWM)***

| ***Beti*** | ***Beti*** |
|---|---|
| ***105. Naawe radhi mumeo,<br>106.Siku zote mkaao,<br>107.Siku mukhitariwao,<br>108.Awe radhi mekuwiya (ubeti 24)*** | ***109.Na ufapo wewe mbee<br>110.Radhi yake izengee<br>111.Wende uitukuzie<br>112.Ndipo upatapo ndizi (ubeti 25)*** |
| ***113.Siku ufufuliwao<br>114.Nadhari ni ya mumeo<br>115.Taulizwa atakao<br>116.Ndilo tutalotendewa (ubeti 26)*** | ***117.Kipenda wende peponi,<br>118.Utapekwa dalihini,<br>119.Kinena wende motoni,<br>120.Huna budi utatiwa(ubeti 27)*** |
| ***121.Keti naye kwa adabu,<br>122.Usimtie ghadhabu,<br>123.Akinena simjibu,<br>124.Itahidi kunyamaa(ubeti 28)*** | ***125.Enda naye kwa imani,<br>126.Atakalo simukhini,<br>127.We naye sikindaneni,<br>128.Mkindani huumiya(ubeti 29)*** |
| ***129.Kitoka agana naye,<br>130.Kingia mkongowee,<br>131.Kisa umtandikie,<br>132.Mahala pa kupumua(ubeti 30)*** | ***133.Kilala siikukuse,<br>134.Mwegeme umpapase,<br>135.Na upepo nasikose,<br>136.Mtu wa kumpepeya(ubeti 31)*** |
| ***137.Kivikia simwondoe,<br>138.Wala sinene kwa yowe,<br>139.Keti papo siinue,<br>140.Chamka kakuzengeya(ubeti 32)*** | ***141.Chamka siimuhuli,<br>142.Mwandikie maakuli,<br>143.Na kumtunda muili,<br>144.Kumsinga na kumowa(ubeti 33)*** |
| ***145.Mnyoe umpalilize,<br>146.Sharafa umtengeze,<br>147.Mkukize mfukize,<br>148.Bukurata wa ashiya(ubeti 34)*** | ***149.Mtunde kama kijana,<br>150.Asioyua kunena,<br>151.Kitu changalie sana,<br>152.Kitokacho na kungiya (ubeti 35)*** |
| ***153.Mpumbaze apumbae,<br>154.Amriye sikatae,<br>155.Maovu kieta yeye,<br>156.Mngu atakuteteya(ubeti 36)*** | ***157.Mwanangu, siwe mkoo,<br>158.tenda kama uonao.<br>159.kupea na kuosha choo,<br>160.sidharau mama moya (ubeti wa 37)*** |
| ***161.Na kowa na kuisinga,<br>162.na nyee zako kufunga,<br>163.na yasimini kutunga,<br>164.na furashani kutia (ubeti wa 38)*** | ***165.Nawe ipambe libasi<br>166.Ukae kama arusi<br>167.Maguuitia kugesi<br>168.Na mikononi makoa (Ubeti wa 39)*** |
| ***169.Na kidani na kifungo.<br>170.Sitoe katika shingo.<br>171.Muili siwate mingo<br>172.Kwa marashi na dalia (Ubeti wa 40)*** | ***173.Pete sikose zandano<br>174.Hina sikome nyaani<br>175.Wanda sitowematoni<br>176.Na nshini kutia (Ubeti wa 41)*** |
| ***177.Yalipokuya faradhi,<br>178.Kanikariria radhi,<br>179.Kashukuru kafawidhi,<br>180.Moyo wangu katushiya (ubeti 54)*** | ***181.Nyumba yako I nadhifu<br>182.Mumeo umshaifu<br>183.Wakutanapo sufufu<br>184.Msifu na kumtaya (ubeti 42)*** |

*Kiambatisho 6: Uhusiano wa Mwanamke na Mwanamume (WUB)*

| *Maelezo* | *Sura* | *Mstari* |
|---|---|---|
| *1Wimbo ulio bora, wa Sulemani.<br>2 Kubusu na anibusu kwa kinywa chake. Maana pambaja zako zapita divai;<br>3Manukato yako yanukia vizuri; Jina lako ni kama marhamu iliyomiminwa;Kwa hiyo wanawali hukupenda.* | *1* | *1-3* |
| *1 Tazama, u mzuri, mpenzi wangu, U mzuri, macho yako ni kama ya hua, Nyuma ya barakoa yako. Nywele zako ni kama kundi la mbuzi, Wakijilaza mbavuni pa mlima Gileadi.<br>2 Meno yako ni kama kundi waliokatwa manyoya, Wakipanda kutoka kuoshwa, Ambao kila mmoja amezaa mapacha, Wala hakuna aliyefiwa kati yao. 3 Midomo yako ni kama uzi mwekundu, Na kinywa chako ni kizuri; Mashavu yako ni kama kipande cha komamanga, Nyuma ya barakoa yako.<br>4 Shingo yako ni kama mnara wa Daudi, Uliojengwa pa kuwekea silaha; Ngao elfu zimetungikwa juu yake, Zote ni ngao za mashujaa. 5 Maziwa yako mawili ni kama wana-paa wawili, Nyuma ya barakoa yako. Ambao ni mapacha ya paa; Wakilisha penye nyinyoro.<br>6 Hata jua lipunge, na vivuli vikimbie, Nitakwenda kwenye mlima wa manemane, Na kwenye kilima cha ubani.<br>7 Mpenzi wangu, u mzuri pia pia, Wala ndani yako hamna ila.<br>8 Bibi arusi, njoo pamoja nami toka Lebanoni, Pamoja nami toka Lebanoni. Shuka kutoka kilele cha Amana, Kutoka vilele vya Seniri na Hermoni; Kutoka mapangoni mwa simba, Kutoka milimani mwa chui.<br>9 Umenishangaza moyo, umbu langu, Bibi arusi, umenishangaza moyo, Kwa mtupo mmoja wa macho yako, Kwa mkufu mmoja wa shingo yako. 10 Jinsi zilivyo nzuri pambaja zako, umbu langu, Bibi arusi, ni nzuri kupita divai; Na harufu ya marhamu yako Yapita manukato ya kila namna.<br>11 Bibi arusi, midomo yako yadondoza asali, Asali na maziwa vi chini ya ulimi wako; Na harufu ya mavazi yako Ni kama harufu ya Lebanoni.<br>12 Bustani iliyofungwa ni umbu langu, bibi arusi, Kijito kilichofungwa, chemchemi iliyotiwa muhuri.<br>13 Machipuko yako ni bustani ya komamanga, Yenye matunda mazuri, hina na nardo,<br>14 Nardo na zafarani, mchai na mdalasini, Na miti yote iletayo ubani, Manemane na udi, na kolezi kuu zote.<br>15 Wewe ndiwe chemchemi ya bustani yangu, Kisima cha maji yaliyo hai, Vijito vya Lebanoni viendavyo kasi.<br>16 Amka, kaskazi; nawe uje, kusi; Vumeni juu ya bustani yangu, Manukato ya bustani yatokee. Mpendwa wangu na aingie bustanini mwake, Akayale matunda yake mazuri.* | *4* | *1-16* |
| *1 Naingia bustanini mwangu, umbu langu, bibi arusi, Nachuma manemane yangu na rihani, Nala sega la asali na asali yangu, Nanywa divai yangu na maziwa. Kaleni, rafiki zangu, kanyweni, Naam, nyweni sana, wapendwa wangu.* | *5* | *1<br>.* |
| *9 Mpendwa wa namna gani ni mpendwa wako, Wewe uliye mzuri katika wanawake, Mpendwa wa namna gani ni mpendwa wako, Hata wewe utusihi hivyo?* | *5* | *9* |
| *4 Mpenzi wangu, u mzuri kama Tirza, Mwenye kupendeza kamaYerusalemu, Wa kutisha kama wenye bendera.<br>5 Uyageuzie macho yako mbali nami, Kwamaana yamenitisha sana. Nywele zako ni kama kundi la mbuzi,Wakijilaza mbavuni pa Gileadi.<br>6 Meno yako kama kundi la kondoo, Wakipanda kutoka kuoshwa; Ambao kila mmoja amezaa mapacha, Wala hakuna aliyefiwa kati yao.<br>7 Mashavuyako ni kama kipande cha komamanga, Nyuma ya barakoayako.* | *6* | *4-10* |

| | | |
|---|---|---|
| ***8 Wako malkia sitini, na masuria themanini, Na wanawali wasiohesabika;***<br>***9 Hua wangu,mkamilifu wangu, ni mmoja tu,Mtoto wa pekee wa mamaye.Ndiye kipenzi chake aliyemzaa,Binti wakamwona wakamwita heri; Malkia na masuria nao wakamwona, Wakamsifu, wakisema,***<br>***10 Ni nani huyu atazamaye kama alfajiri, Mzuri kama mwezi, safi kama jua, Wa kutisha kama wenye bendera?*** | | |
| ***1 Siti msharifu, jinsi zilivyo nzuri Hatua zako katika mitalawanda. Mapaja yako ya mviringo ni kama johari, Kazi ya mikono ya fundi mstadi;*** | ***7*** | ***1*** |
| ***14 Ukimbie, mpendwa wangu, Nawe uwe kama paa, au ayala, Juu ya milima ya manukato.*** | ***8*** | ***14*** |

*Kiambatisho 7: Uhusiano wa Mwanamke na Mwanamume (KCM)*

| *Maelezo* | **Sura** | **Mstari** |
|---|---|---|
| ***1 Mwanangu, sikiliza hekima yangu; Tega sikio lako, mzisikie akili zangu;*** | 5 | **1-14** |
| ***2 Upate kuilinda busara, Na midomo yako iyahifadhi maarifa.*** | | |
| ***3 Maana midomo ya malaya hudondoza asali, Na kinywa kchake ni laini kuliko mafuta;*** | | |
| ***4 Lakini mwisho wake ni mchungu kuliko pakanga; Ni mkali kama upanga wa makali kuwili.*** | | |
| ***5 Miguu yake inatelemkia mauti; Hatua zake zinashikamana na kuzimu;*** | | |
| ***6 Hata asiweze kuiona njia sawa ya uzima; Njia zake ni za kutanga-tanga wala hana habari.*** | | |
| ***7 Basi, wanangu, nisikilizeni sasa, Wala msiache maneno ya kinywa changu.*** | | |
| ***8 Itenge njia yako mbali naye, Wala usiukaribie mlango wa nyumba yake.*** <br> ***9 Usije ukawapa wengine heshima yako, Na wakorofi miaka yako;*** | | |
| ***10 Wageni wasije wakashiba nguvu zako; Kazi zako zikawa ndani ya nyumba ya mgeni;*** | | |
| ***11 Nawe ukaziombolea siku zako za mwisho, Nyama yako na mwili wako utakapoangamia;*** | | |
| ***12 Ukasema, Jinsi nilivyochukia maonyo, Na moyo wangu ukadharau kukemewa;*** <br> ***13 Wala sikuisikia sauti ya waalimu wangu, Wala sikuwategea sikio langu walionifundisha!*** <br> ***14 Nalikuwa karibu na kuingia katika maovu yote, Katikati ya mkutano na kusanyiko.*** | | |
| ***1 Mwanangu, yashike maneno yangu, Na kuziweka amri zangu akiba kwako.*** | | |
| ***2 Uzishike amri zangu ukaishi, Na sheria yangu kama mboni ya jicho lako.*** <br> ***3 Zifunge katika vidole vyako; Ziandike juu ya kibao cha moyo wako.*** | | |
| ***4 Mwambie hekima, Wewe ndiwe umbu langu; Mwite ufahamu jamaa yako mwanamke.*** | | |
| ***5 Wapate kukulinda na malaya, Na mgeni akubembelezaye kwa maneno yake.*** | | |
| ***6 Maana katika dirisha la nyumba yangu Nalichungulia katika shubaka yake;*** | | |
| ***7 Nikaona katikati ya wajinga, Nikamtambua miongoni mwa vijana, Kijana mmoja asiyekuwa na akili,*** | 7 | |
| ***8 Akipita njiani karibu na pembe yake, Akiishika njia iendayo nyumbani kwake,*** | | |
| ***9 Wakati wa magharibi, wakati wa jioni, Usiku wa manane, gizani.*** | | **1-27** |
| ***10 Na tazama, mwanamke akamkuta, Ana mavazi ya kikahaba, mwerevu wa moyo;*** | | |
| ***11 Ana kelele, na ukaidi; Miguu yake haikai nyumbani mwake.*** | | |
| ***12 Mara yu katika njia kuu, mara viwanjani, Naye huotea kwenye pembe za kila njia.*** | | |

| | | |
|---|---|---|
| ***13 Basi akamshika, akambusu, Akamwambia kwa uso usio na haya,***<br>***14 Kwangu ziko sadaka za amani; Leo hivi nimeziondoa nadhiri zangu;***<br><br>***15 Ndiyo maana nikatoka nikulaki, Nikutafute uso wako kwa bidii, nami nimekuona.***<br><br>***16 Nimetandika kitanda changu, magodoro mazuri, Kwa matandiko ya Kimisri yenye mistari.***<br><br>***17 Nimetia kitanda changu manukato, Manemane na udi na mdalasini.***<br><br>***18Haya, na tushibe upendo hata asubuhi, Tujifurahishe nafsi zetu kwa mahaba.***<br><br>***19 Maana mume wangu hayumo nyumbani, Amekwenda safari ya mbali;***<br><br>***20 Amechukua mfuko wa fedha mkononi; Atarudi wakati wa mwezi mpevu.***<br><br>***21 Kwa maneno yake mengi na ulaini akamshawishi, Kwa ubembelezi wamidomo yake akamshinda.***<br><br>***22 Huyo akafuatana naye mara hiyo, Kama vile ng'ombe aendavyo machinjoni; Au mpumbav kuadhibiwa katika pingu;***<br><br>***23 Hata mshale umchome maini; Kama ndege aendaye haraka mtegoni; Wala hajui ya kuwa ni hasara ya nafsi yake.***<br><br>***24 Basi, wanangu, nisikilizeni sasa, Mkayaangalie maneno ya kinywa changu.***<br>***25 Moyo wako usizielekee njia zake, Wala usipotee katika mapito yake.***<br><br>***26 Maana amewaangusha wengi waliojeruhi, Naam, jumla ya waliouawa naye ni jeshi kubwa.***<br><br>***27 Nyumba yake ni njia ya kwenda kuzimu, Hushuka mpaka vyumba vya mauti.*** | | |
| ***Mwanamke wa adabu huheshimiwa daima; Na watu wakali hushika mali siku zote.*** | 11 | **16** |
| ***Mwanamke mwema ni taji ya mumewe; Bali aaibishaye ni kamakuoza mifupani mwake.*** | 12 | **4** |
| ***Kila mwanamke aliye na hekima hujenga nyumba yake; Bali aliy mpumbavu huibomoa kwa mikono***<br><br>***yake mwenyewe.*** | 14 | **1** |

*Kiambatisho 8: Uhusiano wa Mwanamke na Mwanamume (UWA)*

| **Beti** | **Beti** |
|---|---|
| *69.Kaketi naye rijali<br>70. juzamu asijali<br>71.wakalia wawili<br>72.na kuamka pamoya (ubeti 125)* | *73.Ayubu akasumbuka<br>74.kwa ndwee yalomshika<br>75.Rehema kusikituka<br>76.siku zote akilia(ubeti 126)* |
| *77.Akawata masindizi<br>78.Rehema katenda kazi<br>79.ili kupata khubuzi<br>80.kumpa wake rijaa(ubeti 127)* | *81.Rehema asikasiri<br>82.akingia kulla dari<br>83.kwambia ni tayari<br>84.taka kuwatumikia(ubeti 128)* |
| *85.Nitumai kazi zenu<br>86.zilo mayumbani<br>87.kwambia ni kutwewa ngano<br>88.mkinipa taweta(ubeti 129)* | *89.Na tena msinikinde<br>90.niyapoona kipande<br>91.cha mkate nitunde<br>92.tiati nichangukia (ubeti 131)* |
| *93.Wala hamna masahaka<br>94.kikitunda kichanguka<br>95.kwani kitakula paka<br>96.enyi hakitowafaa(ubeti 132)<br><br>101.Alikahudumu kutwa<br>102.kwa kusi mbili za matwa<br>103.hata iyoni kukitwa<br>104.kondoka kandama ndia(ubeti 134)* | *97.Imi ndiyo kuti angu<br>98.ya kula na mume wangu<br>99.tuyaaliwe na Mungu<br>100.haya kutusikilia(ubeti 133)<br><br>105.Kenda kwa wake rijali<br>106.tumwe Ayubu rasuli<br>107.akamshika muli<br>108.kamzunguazungua(ubeti 135)* |
| *109.Ayubu halikiweza<br>110.kilala kuigeuza<br>111.kwa muiliwa kuoza<br>112.shoti mtu kumwinua(ubeti 136)* | *113.Mnagwana mwana Rehema<br>114.kwambiwakwe kainama<br>115.kayashika kwa huruma<br>116.mabombwe kayatundua(ubeti 139)* |
| *117.Kawatunda kiwaweka<br>118.mifupani kiwandika<br>119.hata wakakutanika<br>120.mwilinibwe wakakaa(ubeti 140)* | *121.Nawe usinihabisi<br>122.taka kwenenda upesi<br>123.moyo sioni nafasi<br>124.kutaka kulimatia(ubeti 164)* |
| *125.Akamweleza khabari<br>126.mumewe kamkhubiri<br>127.akamwomba nikhabari<br>128.kuti kwenda kuzengea(ubeti 182)* | *129.Akamwambia enenda<br>130.nami nipo takutunda<br>131.na samba kitonitunda<br>132.utanina ukiya(ubeti 183* |
| *133.Na kwamba Mola Mkwasi<br>134.ameiza yangu kasi<br>135.atanitukua basi<br>136.na mashumra na mbwa(ubeti 184)* | *137.Rehema akatamka<br>138.inshallah takudirika<br>139.na afia itashuka<br>140.Mola tashusha afua (ubeti 185)* |
| *141.Rehema akawajibu<br>142.kuza nyee ni aibu<br>143.wamma nina yawabu<br>144.zaidi ya mambo pia (ubeti 190)* | *145.Ndipo kuza nyee zangu<br>146.ni shida la ulimwengu<br>147.ni mimi na mume wangu<br>148.limezotusikilia(ubeti 191)* |
| *149.Mkitaka mzipate<br>150.nyee zangu mzikate<br>151.ishirini kwa mkate<br>152.tauza siokata(ubeti 192)* | *153.Wanawake wamwambia<br>154.khamsini tukatiye<br>155.kwa mkate tutwaziyen<br>156.mmoya kutopungua(ubeti 193)* |
| *157.Mwanamke wa rasuli<br>158.Rehema akaqubali* | *161.Akakata nyee singa<br>162.khamsini kaziwanga* |

| | |
|---|---|
| *159.naitaka mbalimbali*<br>*160.msinipe siku moya(ubeti 194)* | *163.kawapa wakazifunga*<br>*164.nuru zikawazagaa(ubeti 195)* |
| *165.Wakanena nisiwani*<br>*166.amba tuzinunueni*<br>*167.zote nyeeza kitwani*<br>*168.ni yambo tukimwondoa(ubeti 196)* | *169.Tuzikateni zisiye*<br>*170.nyee ziaimsalie*<br>*171.kwani hakuna kanaye*<br>*172.katika sute nisaa(ubeti 197)* |
| *173.Nyee zake atanapo*<br>*174.mikili aisukapo*<br>*175.kwa kulla mke alipo*<br>*176.shungie huwa king'aa(ubeti 198)* | *177.Wanawake wakazidi*<br>*178.kulifanyizia yuhudi*<br>*179.na nyinyoni maqusudi*<br>*180.hutaka kumuumbua (ubeti 199)* |
| *181.Wakuteneo huruma*<br>*182.wakamwambia rehema*<br>*183.kesho ndoo na mapema*<br>*184.singoye kupaza yua(ubeti 200)* | *185.Kurudi kwangundiani*<br>*186.kamkuta insane*<br>*187.naye umo sakarani*<br>*188.sura alokiongoa(ubeti 220)* |
| *189.Akaniambia mumeo*<br>*190.Hana mali hana cheo*<br>*191.Umeikusa upeo*<br>*192.Ntume atakuua(ubeti 221)* | *193.Nipoapo imi mja*<br>*194.Kwako usiweke huja*<br>*195.Sina shaka takupija*<br>*196.Mungu kinipa afia(ubeti 224)* |
| *197.Kulla nyumba angiayo*<br>*198.Humfukuza kwa mbiyo*<br>*199.Kamba khabati tunayo*<br>*200.Yako tumeisikia (ubeti 151)* | *201.Karudi kisikitika*<br>*202.Matozi humdondoka*<br>*203.Katika ndia kifika*<br>*204.Awene ntu akiya (ubeti 155)* |

*Kiambatisho 9: Dini Kama Kigezo Muhimu katika Ndoa (U W M)*

| Beti | Beti |
|---|---|
| *185. La kwanda kamata dini,<br>186.Faradhi usiikhini,<br>187.Na sunna ikimkini,<br>188.Ni wajibu kuitiya(ubeti 12)* | *189.Pili uwa na adabu,<br>190.Na ulimi wa thawabu,<br>191.Uwe kitu mahabubu,<br>192.Kulla utakapongiya(ubeti 13)* |
| *193.La tatu uwa sadiki,<br>194.Ushikalo ulithiki,<br>195.Mtu asoshika haki,<br>196.Sandamane naye ndiya(ubeti 14)* | *197.Tena mwanangu idhili<br>198.Mbee za maqabaili<br>199.Uwaonapo mahali<br>200.Anagusa kuwenukia(ubeti 15)* |
| *201.Keti naye kwa adabu,<br>202.Usimtie ghadhabu,<br>203.Akinena simjibu,<br>204.Itahidi kunyamaa(ubeti 28)* | *205.Yangu utakaposhika,<br>206. Mwanangu hutosumbuka,<br>207.Duniani utavuka,<br>208.Na akhera utakiya (ubeti 11)* |
| *209.Mpumbaze apumbae,<br>210.Amriye sikatae,<br>211.Maovu kieta yeye,<br>212.Mngu atakuteteya (ubeti 36)* | *213.Kivikia simwondoe,<br>214.Wala sinene kwa yowe,<br>215.Keti papo siinue,<br>216.Chamka kakuzengeya(ubeti 32)* |
| *217.Penda nikupe kifungo,<br>218.Kizuri kisicho ongo,<br>219.Uvae katika shingo,<br>220.Utaona manufaa (ubeti 10)* | *221.Chamka siimuhuli,<br>222.Mwandikie maakuli,<br>223.Na kumtunda muili,<br>224.Kumsinga na kumowa (ubeti 33)* |
| *225.Kilala siikukuse,<br>226.Mwegeme umpapase,<br>227.Na upepo nasikose,<br>228.Mtu wa kumpepeya (ubeti 31)* | *229.Kuchunguza jambo hilo<br>230.Mama, sione ulimi,<br>231.nioleza wako ulimi,<br>232.naliowa nyaka kumi,<br>233.tusitete siku moya.( ubeti 51)* |
| *234.Kisake kutakarabu,<br>235.Bisumillahi kutubu,<br>236.Umtaye na Habibu,<br>237.Na sahabaze pamoya (ubeti 4)* | *238.La kwanda kamata dini,<br>239.Faradhi usiikhini,<br>240.Na sunna ikimkini,<br>241.Ni wajibu kuitiya (ubeti 12)* |
| *242.Akupacho mpokeye,<br>243.Na moyo ufurahiye,<br>244.Asilotenda kwa yeye,<br>245.Huna haja kumwambiya(ubeti 49)* | *246. La tatu uwa sadiki,<br>247. Ushikalo ulithiki,<br>248. Mtu asoshika haki,<br>249. Sandamane naye ndiya (ubeti 14)* |
| *250. La kwanda kamata dini,<br>251.Faradhi usiikhini,<br>252.Na sunna ikimkini,<br>253.Ni wajibu kuitiya(ubeti 12)* | *254.Pili uwa na adabu,<br>255.Na ulimi wa thawabu,<br>256.Uwe kitu mahabubu,<br>257.Kulla utakapongiya(ubeti 13)* |
| *258.Ukisa kulitangaza,<br>259.Ina la Mola Muweza,<br>260.Basi tuombe majaza,<br>261.Mngu tatuwafikiya(ubeti 5)* | *262.Tena mwanangu idhili<br>263.Mbee za maqabaili<br>264.Uwaonapo mahali<br>265.Anagusa kuwenukia(ubeti 15)* |

***Kiambatisho 10: Dini Kama Kigezo Muhimu katika Ndoa (KCM)***

| | | |
|---|---|---|
| ***Upendeleo hudanganya, na uzuri ni ubatili; Bali mwanamke amchaye Bwana, ndiye atakayesifiwa.*** | **31** | **30** |
| ***Mpe mapato ya mikono yake, Na matendo yake yamsifu malangoni.*** | **31** | **31** |
| ***Ni utukufu wa Mungu kufichaJambo, bali ni utukufu wa mfalme Kuchunguza jambo hilo*** | ***31*** | ***25*** |
| ***Mwanamke wa adabuHuheshimiwa daima,Na watu wakali hushika Mali siku zote*** | **31** | ***11*** |
| ***9 Ni afadhali kukaa katika pembe ya darini, Kuliko katika nyumba pana pamoja na mwanamke mgomvi.*** | **31** | **9** |
| ***19Ni afadhali kukaa katika nchi ya nyika; Kuliko na mwanamke mgomvi, mchokozi.*** | **31** | **19** |

*Kiambatisho 11: Dini Kama Kigezo Muhimu katika Ndoa (U W A)*

| Beti | Beti |
|---|---|
| *205.Tukala tikahilmili*<br>*206.tukimuomba wadudi*<br>*207.ili kazi ya abadi*<br>*208.wala nisikutukiwa(ubeti 328)* | *209.Kikhudumu kwa furaha*<br>*210. na kumuombea siha*<br>*211.Mola mpoaza jaraha*<br>*212.umpe ake afia(ubeti 329)* |
| *213.Hakwamia MolaWako*<br>*214.timiza kiapo chako*<br>*215.ya ndhari mke wako*<br>*216.ipate kumwondokea (ubeti 358)* | *217.Unambizie wahabu*<br>*218.kwa hii kukudhurubu*<br>*219.moyo wako atiaba*<br>*220.shaka nafusi ondoa(ubeti 366)* |
| *221.watu wakakutanika*<br>*222.Maneno wakayashika*<br>*223.Kwa wote wakampeka*<br>*224.Pasiwe alosalia (ubeti 120)* | *225.wote wakamsukuma*<br>*226.Pasiwe alomwegema*<br>*227.Illaye Mwana Rehema*<br>*228.Mke wake mfadhaa (ubeti 121)* |
| *229.Ayubu akasumbuka*<br>*230.Kwa ndwee yalomshika*<br>*231.Rehema kusikitika*<br>*232. Sikuzote akilia (ubeti 126)* | *233.Imi ndiyo kuti angu*<br>*234.ya kula na mume wangu*<br>*235.tuyaaliwe na Mungu*<br>*236. haya kutusikilia(ubeti 133)* |
| *237.Nipoapo imi mja*<br>*238.Kwako usiweke huja*<br>*239.Sina shaka takupija*<br>*240.Mungu kinipa afia(ubeti 224)* | *241.Nihhimidie Mungu*<br>*242.mwenye kutandika mbingu*<br>*243.amewondoa utungu*<br>*244.moyoni haukusaa(ubeti 348)* |
| *245. Nikwambiao sadiqi*<br>*246. moya siitie dhidi*<br>*247. jalilu Mola khalaqi*<br>*248. mawi amenoondolea(ubeti 333)* | *249.Hakwamia Mola Wako*<br>*250.timiza kiapo chako*<br>*251.ya ndhari mke wako*<br>*252.ipate kumwondokea (ubeti 358)* |
| *253. Rehema asikasiri*<br>*254. Akingia kulla dari*<br>*255.Kawaambia ni tayari*<br>*256.Taka kuwatumikia(ubeti 128)* | *257.Tukala tikahilmili*<br>*258.tukimuomba wadudi*<br>*259.ili kazi ya abadi*<br>*260.wala nisikutukiwa (Ubeti 32)* |
| *261.Kikhudumu kwa furaha*<br>*262.na kumuombea siha*<br>*263.Mola mpoaza jaraha*<br>*264.umpe ake afia (Ubeti 329)* | *265.Rehema mwenye Saburi*<br>*266.Kusikiakwe khabari*<br>*267.Mno akatafakari*<br>*268.Akapeka na kupoa (ubeti 266)* |